**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 6 Februari, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019.

**MHE. ROSE C. TWEVE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimwite Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni miaka minne sasa tangu Serikali yenu imeweka zuio kwa vyama vya siasa kufanya wajibu wake kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Nchi. Na tunachozungumza leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ni siku 262 zimebaki kufika tarehe 24, 25 Oktoba siku ambayo nchi yetu itafanya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa busara zako

binafsi na ni Serikali ambayo wewe ni kiongozi mwandamizi, mnafikiri ni lini mtaruhusu vyama vya siasa vifanye wajibu wake wa uenezi kujiandaa kwa uchaguzi Mkuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Serikali ina mpango gani wa kuwezesha Taifa kupata Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itahakikisha kwamba uchaguzi huu unakuwa huru wa haki na wa halali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbowe Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza Mheshimiwa anaomba kujua ni lini vyama vya siasa vitaruhusiwa kufanya shughuli zake za kisiasa. Vyama vya siasa havijazuiwa kufanya shughuli zake, ila tumeweka taratibu muhimu unaowezesha vyama kufanya shughuli zake za kisiasa kama ambavyo tumetoa, kumekuwa na uhuru pia wale wote wanasiasa wote ambao waliomba ridhaa kwenye maeneo yao wakapata ridhaa hiyo kuendelea kufanya shughuli na maeneo yao ambayo wamepata ridhaa. Kama vile Madiwani, Wabunge wanaendelea kufanya shughuli zao za siasa kwenye maeneo yao kama ambavyo wao wanapaswa kufanya shughuli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumzia lini tunajiandaa kwa ajili ya uchaguzi, ratiba za uchaguzi zitatolewa na ratiba hizi zitaeleza kuanzia lini shughuli za kampeni zitaanza mpaka lini ili vyama viende sasa kama chama kikaeleze sera zake kwenye maeneo yote ili sasa wananchi waweze kupata fursa ya kuendelea kufanya maamuzi ya sera ipi ya chama gani, inafaa kutuletea maendeleo nchini. Kwa hiyo hilo linaendelea na wote mnajua hata kulipokuwa na chaguzi ndogo pale ratiba ilipokuwa inatolewa kila chama kilikuwa kinaendelea kushiriki na huo ndio utaratibu ambao unaifanya hata nchi kuwa imetulia na watu wote kufanya shughuli zao kama kawaida na tutaendelea kufanya hivyo kwa vyama vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu suala la Tume Huru. Jambo hili hata Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu juzi alitoa maelezo hapa, na mimi nataka nirudie tu; kwamba tume hii imeundwa kwa mujibu wa Katiba wa sheria, na kwa mujibu wa Katiba ya nchi kipengele 74 (7), (11), (12) inaeleza kwamba hiki ni chombo huru.

Kimeelezwa pia kwenye Katiba pale kinaundwaje; na chombo hiki hakipaswi kuingiliwa na chombo chochote; iwe Rais wa nchi, iwe chama chochote cha kisiasa au Mamlaka nyingine yoyote ile haipaswai kuiingilia. Kama ni chombo huru kwa mujibu wa Katiba ndiyo Tume huru. Sasa kunaweza kuwa kuna tofauti ya neno huru hili linataka litambulike vipi lakini chombo kipo kinajitegemea kinafanya kazi yake bila kuingiliwa na mtu yoyote, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Mwaka 1977. Hayo ndiyo maelezo sahihi na ndiyo ambayo yapo kupitia Katiba na sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Freeman Mbowe swali la nyongeza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu unajua vizuri sana, Serikali yako inajua vizuri sana, Watanzania wanajua vizuri sana kwamba vyama vya siasa vya upinzani vimezuiwa kwa miaka minne sasa kufanya kazi zake za siasa za uenezi. Na Mheshimiwa Waziri Mkuu unapotupa maelezo ndani ya Bunge ya kuhalalisha kilichofanyika na ukasema ni utaratibu ambao mmejiwekea mmejiwekea kwa sheria ipi. Najua yote hayo unajua vizuri sana, kwamba Tume ya Uchaguzi unayoiita ni huru kwa sababu imeandikwa kwenye

katibu si huru na watendaji wake vilevile wamekuwa ni *partisan* sana na masuala haya yamejitokeza wazi na yanaonekana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE.FREEMAN A. MBOWE:** Weweee!!!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Naomba muwe na adabu.

**MHE.FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu haya ni majibu mepesi ambayo kuna siku mtakuja kujuta katika nchi hii kwa majibu haya mepesi. Je…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Keleleni huko!

**MHE.FREEMAN A. MBOWE:…** Mheshimiwa Waziri Mkuu, narudia kwa mara nyingine hamuoni ni muda mwafaka sasa Serikali ikaona umuhimu wa wadau mbalimbali ambao wanahusika na masuala ya uchaguzi katika nchi hii kukaa na kutafuta njia bora zaidi ya kwenda kwenye uchagzui Oktoba kuliko kwenda kibabe kwa namna ambavyo tunataka kwenda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbowe Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nikanushe kwamba Serikali inaongoza kibabe, haiongozi kibabe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbowe ni kiongozi tunazungumza, tunabadilishana mawazo; sote tunapobadilishana mawazo tunalenga kulifanya Taifa hili liwe na usalama, liwe tulivu ili shughuli zetu ziweze kwenda lakini muhimu zaidi Watanzania wanahijtai maendeleo. Kwa maana hiyo tunapoweka utaratibu wa namna ya kuwafikia wananchi na kupata maendeleo jambo hili si la chama kimoja ni kwa nchi nzima. Hakuna Mbunge wala Diwani aliyezuiliwa kwenye eneo lake kufanya siasa na watu wake. Kunaweza kuwa labda kama kuna tatizo mahali fulani kwa utaratibu ule tunaozungumza tunakutana tuambizane wapi kuna shida. Kama wiki iliyopita Mheshimiwa Sugu alieza kwamba kule Mbeya anazuio na *OCD* na mimi nilimuita hapa tumezungumza. Mkuu wa Mkoa ameungana naye, Mkuu wa Polisi Mkoa ameungana naye. Shida kama ziko kwenye ngazi ndogondogo huko ni suala kuzungumza kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani; tunakuheshimu sana, tunatambua una majukumu kwa chama chako lakini Serikali yetu inaendelea kushirikiana na Viongozi wote kwa Mamlaka zao ili kufanya taifa hili liendelee kuwa salama na tulivu, pale ambako kuna shida ya namna hiyo tuendelee kuwasiliana Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi za Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili suala la Tume hii kuonwa kwamba si huru ni mtizamo wa mtu lakini Kikatiba na utendaji wake uiko huru. Pale ambako panaonekana kuna shida basi kwa utaratibu ule paelezwe kwamba hapa kuna shida lakini hatujawahi kuona Rais akiingilia, chama cha siasa kikiinglia ile Tume iko huru na inafanya kazi yake kama ambavyo imetakiwa kwa

mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kukiwa na jambo lolote lile unao uhuru wa kubadilishana mawazo ili tuone wapi tusaidie katika kufanya jambo hilo liweze kwenda sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Pius Chatanda swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu *TARURA* imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kutekeleza miradi ya barabara mijini na vijijini. Na kwa kuwa umuhimu wa barabara hizi ndizo zinazochangia kwa kiasi kikubwa uchumi katika usafirishaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bahati mbaya sana *TARURA* wanakumbwa na bajeti ndogo. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuiongezea bajeti *TARURA* ili iweze kutekeleza majukumu yake haya makubwa ambayo imekabidhiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chatanda Mbunge wa Korogwe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunacho chombo kinachosimamia ujenzi na ukarabati wa barabara vijijini; *TARURA* kwa sasa; ambacho tumekipa mamlaka ya kufanya kazi karibu kwa pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mtaa kwa maana ya halmashauri za wilaya.

Sasa kila *TARURA* iliyoko kwenye halmashauri hiyo jukumu lake ni kufanya mapitio ya barabara zote zilizopo ndani ya wWilaya hiyo kuona mahitaji ya ujenzi wake, ukarabati wake na matengenezo ya kila siku pale ambako panahitaji ukarabati huo na kutenga fedha na kuomba fedha kulingana na mahitaji yake. Kwa hiyo kila *TARURA* katika kila halmashauri inayo bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana pia *TARURA* Wilaya ya Korogwe haitoshelezi mahitaji ya ukarabati wa barabara zake. Si rahisi kupata bajeti yote kwa asilimia 100 kulingana na mahitaji hayo lakini bado kipindi tulichonacho sasa mwezi wa pili tukiwa tunaelekea kwenye Bunge la Bajeti kuanzia mwezi wa nne basi *TARURA* ile kwenye halmashauri husika ioneshe mahitaji ya fedha kulingana na mahitaji ya barabara zao ili sasa tuanze kuingiza kwenye mpango wa fedha kwa ajili ya matumizi ya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme Serikali iko tayari kupokea maombi ya *TARURA* zote nchini za mahitaji ya fedha halafu tutazigawa sote kwa pamoja; na kupitia Kamati yetu ya Miundombinu inaweza kusimamia pia *TARURA* kupata fedha ya kutosha ili iweze kujenga barabara zake kwenye maeneo yake kama ambavyo halmashauri inahitaji kuboresha barabara zake. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Ni sera na ni azma ya Serikali yetu kuwapatia wananchi maji salama lakini kwa bei nafuu pia kwa sababu maji ni huduma si biashara. Niipongeze Serikali yetu kwa kufikia azma hiyo hiyo mijini kwa zaidi ya asilimia 80 na vijijini kwa asilimia 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana *EWURA* walipandisha bili za maji kote nchini, jambo ambali limesababisha wananchi wengi kushindwa kulipa bili hizo. Serikali pamoja na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu mlituahidi hapa Bungeni kwamba *EWURA* wacheki upya mchakato wao ili waona kama hizi bili zinaweza zikashuka ili wananchi waweze kulipia. Naomba nifahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lini mchakato wa *EWURA* utakamilika ili hizi bili zishuke kwa sababu wananchi wengi wameshindwa kulipia; mfano wananchi wa Babati Mjini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gekul Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nimewahi kupokea malalamiko haya kutoka hapa Bungeni, kutoka kwenye mikutano ninayoifanya kwenye maeneo mbalimbali nchini juu ya upandaji wa bei za maji holela na kukwaza wananchi kumudu kupata huduma hiyo ya maji. Kwanza nataka niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali yetu imejipanga kutoa huduma za maji mpka kuingia vijijini kama ambavyo tumeeleza na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza. Kwamba tunahitaji sasa angalau kila kijiji kiwe na angalau kiwekwe kisima kama ni kifupi tupate maji ili wananchi wawe na uhakika wapi watapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo inaendelea vizuri na Wizara yetu ya maji inasimamia kuhakikisha kwamba huduma za maji zinapatikana kwa ujenzi wa miradi ya visima vifupi, vya kati lakini pia hata miradi mikubwa ambayo wakati wote tumekuwa tukiieleza. Maji haya Serikali hailengi kufanya biashara kwa wananchi wala hatuhitaji faida kutoka kwa wananchi, muhimu wa utoaji huduma ya maji kwa wananchi ni kufikisha maji kwa wananchi wayapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeunda Kamati zinazosimamia maji kwenye maeneo husika; na pia tumeunda mamlaka ya jumla ambayo inasimamia utoaji wa huduma ya maji kwenye ngazi ya Wilaya *RUWASA;* kwenye ngazi ya Kitaifa tuna zile mamlaka ambazo zinachukua unaweza ukawa ni Mikoa miwili au mitatu au Kanda kusimamia utoaji huduma lakini pia na ujenzi wa miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hizi tumezitaka zifanye mapitio ya huduma ndogondogo zinazohitaji kwa ajili ya ukarabati wa kuendesha mradi huo kwenye maeneo yao; kama vile kununua *tap* na kufanya mabadiliko ya bomba lililotoboka. Hiyo tumeiachia zile Kamati ziratibu na sasa Kamati hizi zinahitaji angalau wananchi wachangia huduma ya maji kwenye eneo lao. Huduma hii hatutarajii kusikia mwananchi analipa gharama kubwa inayomshinda na lile ndilo tuliloagiza kwa Wizara. Tumeweka utaratibu *EWURA* wafanye mapitio ya maeneo haya kuona kwamba gharama haziwi zaidi ya mapato ya mwananchi kwenye eneo lake ili kuongoa usumbufu au dhana ya kwamba tunatoa huduma ya maji kama vile biashara, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeweka utaratibu *EWURA* wafanye mapitio ya maeneo haya kuona kwamba, gharama haziwi zaidi ya mapato ya mwananchi kwenye eneo lake, ili kuondoa usumbufu au dhana ya kwamba, tunatoa huduma ya maji kama vile biashara, hapana. Agizo limeshatolewa na Wizara ya Maji imeshatekeleza. kwa hiyo nitamuagiza Waziri wa Maji atupe taarifa ya hatua waliyoifikia ili sasa tuone kuwa huduma hii inatolewa huko kwa namna ambazo mwananchi anaweza kupata maji akaendelea kuhudumiwa. Vilevile kama kijiji, kata, waendelee kufanya ukarabati mdogomdogo ili kufanya mradi huo kuendelea kutoa huduma kwa wananchi wake. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwea kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali; na nianze kwa kutoa pole kwa waathirika wote wa mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba; Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeshuhudia mvua zinazonyesha na zinazoendelea kunyesha. Tumeshuhudia maafa mbalimbali, vifo, watu kukosa maeneo ya kuishi, kupoteza mali zao, kuharibika kwa miundombinu, lakini pia watu wale hawana vyakula. Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuweza kuwasaidia watu hao ambao wameathirika na mafuriko hayo na pia, kuboresha miundombinu nchini kwetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu Vulu, Mbunge Mkoa wa Pwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami niungane na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa pole kwa waathirika wote a mafuriko nchini kwa maeneo yote ambayo yamekumbwa na tatizo hili la mafuriko. Pia Mheshimiwa Mbunge na yeye ametioa pole ni jambo zuri, jambo jema kwa sababu, wako Watanzania wamekumbwa na hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa bahati nzuri jana nilikuwa Mkoani Lindi, Wilaya ya Kilwa ambako kulikuwa na mafuriko pia. Nimetembelea kwenye maeneo yote nimeona hali ilivyo, ingawa angalao sasa maji yamepungua kwenye maeneo yale yamebaki tu yanayotiririka kwenye mito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uharibifu mkubwa umejitokeza, kwanza wenzetu wametangulia mbele za haki na kwa kweli tuungane na Watanzania wote, Mungu aweke roho zao mahali pema peponi, amina. Mbili, tumeona watu wamepoteza nyumba, vyakula na miundombinu mbalimbali imeharibika ikiwemo na barabara na njia nyingi zimejifunga. Nataka niwaambie Watanzania, kwamba mwaka huu mvua ni nyingi sana, na Taasisi yetu ya Hali ya Hewa imeendelea kutuhabarisha kwamba, mvua ndio zinaanza. Sasa kama ndio zinaanza kwa hali hii tutarajie tutakuwa na matukio mengi makubwa zaidi ya haya ambayo tumeyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapopata taarifa za wingi wa kiasi cha mvua mwaka huu sisi wenyewe tunatakiwa tuchukue tahadhari. Wale wote waliokaa kwenye maeneo hatarishi, na kwa kiwango hiki cha mvua na hali ambayo tumeiona na wanasema mvua bado inakuja; uko umuhimu na kweli nitoe wito; watu waondoke kwenye maeneo yale ya mabondeni. Kule iwe ni kazi za kilimo na kulishia mifugo, tusifanye maeneo hayo kuwa ni maeneo ya makazi kwa sababu kuna hatari tena ya kupoteza maisha ya wenzetu, nyumba, vyakula na athari nyingine inaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawa ambao tayari wamekumbwa kwenye maeneo yao kama vile huko Lindi, Kilwa, Liwale, Lindi Vijijini; pia Pawaga kule Iringa, Chikuyu Wilayani Manyoni, Magu Mwanza, Sengerema pamoja na Buchosa. Hayo maeneo yote ninayoyataja yana matatizo ya mafuriko. Kwa hiyo maeneo ni mengi na bado kuna mikoa sita ambayo mvua zitaanza kunyesha kwa wingi. Kamati za Maafa za Kata, Wilaya na Mikoa zipo zinafanya kazi yake na zinaendelea kutoa huduma kwa uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo Kamati ya Maafa Mkoa inapokuwa na jambo kubwa sana wanatoa taarifa kwa Kamati ya Maafa ya Taifa ambayo iko Ofisi ya Waziri Mkuu nayo pia itasadia katika kuratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya jambo hili ni la muda mfupi; muhimu zaidi tuanze kujiepusha kukaa kwenye maeneo hayo hatarishi ili kupunguza mzigo mkubwa ambao tutaupata. Haya yaliyotokea haya kamati za maafa zinafanya kazi nzuri, wakuu wa wilaya, viongozi wa kamati za wilaya, wakuu wa mikoa, kamati za mikoa, wameendelea kushirikiana na wale wote waathirika kuona mahitaji yao katika kipindi hiki kifupi na kazi inaendelea vizuri na taarifa tunaendelea kuzipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao pia mnatoka kwenye maeneo haya tunawapa pole na wananchi wetu tunawapa pole, lakini tuwahakikishie kwamba, kamati zetu za maafa zilizoko kwenye maeneo yale zinaendelea kushirikiana na wananchi huku tukiendelea kutoa wito wananchi wasirudi kwenye maeneo walikotoka ili kupunguza athari hii. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante. Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu swali:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, kila kijiji kinapelekewa umeme katika nchi yetu. na kwa kuwa, Serikali imejitahidi sana kupeleka nguzo nyingi na nyaya katika maeneo mengi ya nchi yetu, lakini bado nguzo hizo zimeendelea kulala chini na nyingine hazijafungiwa umeme. Na kwa kuwa mpango wa *REA* Awamu hii ya Tatu ni kwamba, lazima uishe mwezi wa sita, lakini katika mwenendo wa utekelezaji wa mradi wenyewe inaonekana mpaka mwezi wa sita kuna miradi ambayo itakuwa haijakamilika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, mradi huu wa utekelezaji wa *REA* katika vijiji vyetu unakamilika mwezi wa sita kama ambavyo Serikali ilipanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo miradi hii ya *REA* ambayo inapeleka umeme vijijini ambayo kwa kweli kazi zinaendelea vizuri. Tumeenda maeneo mengi; na sasa tumefikia zaidi ya asilimia 60 na kitu katika kuweka umeme kwenye vijiji vyetu vingi ambavyo vimekusudiwa. Mkakati huu unalenga kila kijiji huko kwenye maeneo yetu tunakotoka. Wizara ya Nishati imejipanga vizuri, imeshasambaza wakandarasi kila halmashauri, wakandarasi ambao wamesaini mkataba kukamilisha kazi hiyo kwa muda na kwa kuweka umeme katika kila kijiji kwa awamu hii ya tatu, awamu ya kwanza na kwenye awamu ya tatu kuna awamu ya kwanza na ya pili na zote hizi zitatekelezwa, ili kuhakikisha kwamba, umeme unapelekwa kwenye ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo ambayo nimeeleza kwamba inaendelea na ni nzuri inaanza sasa kupeleka umeme kwenye vijiji vyetu vingi; na vijiji vyote vilivyobaki viendelee kuwa na uhakika kwamba, umeme utafikishwa. Sasa suala la kufika mwezi wa Juni inategemea hapa katikati kama kunaweza kuwa na jambo lolote lile linaloweza kumfanya mkandarasi

akashindwa kukamilisha kazi yake vizuri. Sisi ndani ya Serikali tunahakikisha mtiririko wa fedha za malipo kwa mkandarasi unakwenda, tunahakikisha kwamba, vifaa anavipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa bahati nzuri sasa vifaa vya kutengenezea kazi hizo vinapatikana hapahapa nchini. Nguzo zinapatikana nchini, *transformer* zinapatikana hapa nchini, nyaya zinapatikana hapa nchini. Kwa hiyo tuna matumaini kwamba, tunaweza kukamilisha kazi hiyo kwa kipindi ambacho tunatarajia, na kwa kuwa, wakandarasi wako kazini na tumetoa pia mamlaka kwa *TANESCO* zetu maana *TANESCO* na *REA* ni taasisi mbili zilizo kwenye Wizara moja, ili *TANESCO* sasa wasimamie kazi za *REA* kuwa zinakamilika kwenye maeneo ambayo wanayasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumini yangu kwamba kazi za uwekaji umeme kwenye vijiji itakamilika. Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameelza hapa, kwamba sasa tunakwenda mbali zaidi mpaka kwenye vitongoji vikubwa navyo tunapeleka umeme. Kwa hiyo wananchi wawe na matumaini na wajiandae sasa kutumia fursa ya kuwa na umeme kwenye maeneo yao kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali zinazohitaji umeme, asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu muda wako wa maswali umekwisha. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Maswali ya Kawaida.

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Maswali ya Kawaida. Tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli sasa aulize swali lake.

Na. 96

### Tatizo la Miundombinu ya Barabara ya Mto wa Mbu

**MHE. JULIUS K. LAIZER** aliuliza:-

Mji wa Mto wa Mbu ni mji wa kitalii na unaingiza mapato mengi ya kitalii; lakini unakabiliwa na tatizo la miundombinu ya barabara;

(a) Je nini mkakati wa Serikali kuupatia Mji wa Mto wa Mbu angalau km 5 za lami?

(b) Je Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa barabara ya Mto wa Mbu mpaka Loliondo kwa kiwango cha lami ili kusaidia mradi wa kimkakati wa magadi Engaruka?

(c) Je ni lini Serikali itatimiza ahadi ya Mhe. Rais ya kuweka lami barabara ya Ngarasha mpaka Monduli Juu kwa Sokoine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini – *TARURA* imekamilisha usanifu wa barabara za Mji Mdogo wa Mto wa Mbu kwa kiwango cha lami zenye jumla ya urefu wa kilometa 9 ambazo ujenzi wake utagharimu jumla ya shilingi bilioni 7.32. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi ambao utafanyika kwa awamu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo ina urefu wa kilometa 247 na ipo chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Serikali imeanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2019/20 kiasi cha Shilingi bilioni 87 kimetolewa kwa ajili ya kujenga kipande chenye urefu wa kilometa 49 na ujenzi umefikia asilimia 43. Serikali itaendelea kujenga barabara hii kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Ngarasha mpaka Monduli Juu kwa Sokoine yenye urefu wa kilometa 11.66 iko chini ya Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Wakala wa Barabara unaendelea na usanifu wa barabara hiyo. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo unaotarajia kuanza pindi usanifu wa barabara hiyo utakapo kamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Julius Kalanga, swali la nyongeza.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza; na unipe ruhusa niwape pole wananchi wa Monduli, hasa wa Mto wa Mbu ambao wamekubwa na mafuriko kwa muda wa wiki moja sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Serikali imesema imetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa kilometa tisa; lakini bilioni saba hizo inawezekana zisipatikane kwa wakati. Nataka kujua *commitment* ya Serikali ya kuhakikisha kwamba walao barabara hii inawekwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Barabara hii ya Monduli Juu ambayo Waziri anasema ipo katika hali ya upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu umekamilika na *document* zote zipo tayari. Je, ni lini hasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Julius Kalanga yenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Mto wa Mbu unaufahamu vizuri. Na Mheshimiwa Mbunge amekuwa akipigania kwa sababu adha ambayo imekuwa ikipatikana kila wakati mvua zinaponyesha mafuriko yanakuwepo eneo lile. Kwanza kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akilipigania eneo hili kwa muda mrefu. Naomba nimhakikishie, katika bajeti ya mwaka 2020/2021 tutaanza na mifereji na ujenzi wa kilometa moja utaanza ili tupunguze adha kwa wananchi wa Mto wa Mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ameongelea barabara ya kwenda kwa Marehemu Sokoine. Kama anavyokiri hata yeye mwenyewe, kwamba usanifu ulishakamilika. Naomba nimhakikishie, kufanyika kwa usanifu tafsiri yake ni kwamba, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba fedha ikipatikana nako ujenzi utaanza. Aendelee kuiamini Serikali kama ambavyo tukiahidi daima tumekuwa tukitekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza; lakini uniruhusu niseme jambo moja dogo ambalo siku zote nimekuwa nikitafakari wahenga wakisema kua uyaone, lakini hatimaye nimeyaona jana goli kuwa kona kwa watani zangu wa Yanga; kwa kweli, nimestaajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba swali langu dogo la nyongeza lipate majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Serikali imedhamiria kuhakikisha barabara zote ambazo ziko kwenye ahadi zinajengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami ikiwemo Barabara ya kutoka Buhongwa – Lwanima – Kishiri mpaka Igoma. Sasa, ni lini Serikali itakuwa tayari kuhakikisha barabara hii inakamilika kwa kiwango cha lami kama ambavyo iliahidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge anaitaja ni barabara ambayo iko chini ya *TARURA*. Na kipekee Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiipigania barabara hii kwa muda mrefu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge; usanifu wa barabara hii umeshakamilika; na kitakachofuata katika bajeti ya mwaka 2020/2021 tutaanza kuijenga hatua kwa hatua, ili barabara yote iweze kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo huu wa Mto wa Mbu ni sawasawa na Mji Mdogo wa Karatu; kwa maana ni miji ambayo watalii wanapita kuingia katika Hifadhi ya Manyara na Hifadhi ya Ngorongoro.

Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kuwa na mpango mkakati wa kuendeleza miji hii kwa sababu ni kitovu cha kuingia katika Hifadhi zetu za Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mbunge ameongelea Mji Mdogo wa Mto wa Mbu na Mji wa Karatu; ni kweli ni miji ambayo ni ya pekee kwa sababu ni lango katika watalii wanapoenda kutembelea mbuga zetu. Kama ambavyo Serikali imekuwa na mpango kupitia *TSSP* tumekuwa tukiendeleza miji kwa kujenga barabara za kiwango ambacho ni kiwango kizuri. Naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuridhika na Serikali yetu hatua kwa hatua tunamaliza hiyo miji ambayo tulianzanayo nina hakika, katika mji ambao ameutaja kwa sababu ni jicho la kipekee kwa watalii nao hakika hatutauacha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Naibu Waziri, kwa nini Nyanghwale haitengewi pesa za maendeleo ya barabara ilhali kuna barabara ambazo zimeharibika vibaya yakiwemo madaraja kutoka Nyanghwale pale makao makuu kwenda Lushimba. Ni kwa nini Serikali haitutengei fedha za maendeleo ya barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya CCM ambayo na yeye Mheshimiwa Mbunge anatokana na CCM anajua kabisa kumekuwa hakuna upendeleo katika kupeleka maendeleo katika nchi yote kwa ujumla. Kwa kuwa yeye ni sehemu ya Madiwani ni vizuri basi wakahakikisha kwanza wanaanza kutenga wao na sisi Serikali Kuu tukapata taarifa. Kimsingi hakuna hata eneo moja ambalo hatutengi fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu.

Na. 97

**Mabaraza ya Ardhi ya Kata**

**MHE. WILLY Q. QAMBALO** aliuliza:-

Mabaraza ya Ardhi ya Kata ni chombo muhimu sana katika kutatua migogoro ya ardhi. Hata hivyo, changamoto kubwa ni uwezeshaji (chakula na nauli) na wajumbe wa mabaraza hayo ili wafanye kazi zao kwa weledi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wajumbe wanawezeshwa ili waweze kutoa haki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7 cha Sheria ya Mabaraza ya Ardhi ya Kata kinazipa Halmashauri wajibu wa kutengeneza utaratibu wa namna ya kuwezesha Mabaraza ya Ardhi na Kata kiutendaji na kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Mikoa na Wilaya

imeelekezwa kuzisimamia Halmashauri kuhakikisha Mabaraza hayo yanawezeshwa ili yaweze kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Kila Halmashauri inatakiwa kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia Mabaraza ya Ardhi ya Kata. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji ili kuhakikisha changamoto hiyo inapatiwa ufumbuzi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Qulwi Qambalo, Swali la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na maelekezo yaliyotolewa kwa Halmashauri kutenga fedha kwa ajili kuyawezesha Mabaraza haya, lakini ni ukweli usiopingika kwamba Halmashauri nyingi bado hazijaona umuhimu wa kutenga fedha ili Mabaraza haya yafanye kazi zao kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza; kwa kuwa suala kutoa maamuzi kwenye masuala ya ardhi ni suala muhimu sana: Kwa nini Serikali isichukue sasa jukumu hili kama ambavyo imechukua jukumu la kuyawezesha yale Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ili haki iweze kutendeka vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wajumbe wa Mabaraza haya wanapoteuliwa, wanapewa semina ya masaa kadhaa, baadaye wanaapishwa, lakini semina ya masaa kadhaa kwa mtazamo wangu haitoshi kwa watu wanaofanya kazi muhimu ya kutoa maamuzi kama haya: Kwa nini Serikali isije na mpango mahsusi wa mafunzo kwa Wajumbe hawa ili waweze kufanya kazi yao kwa weledi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni kweli kwamba mabaraza haya yanasimamiwa na Halmashauri na Mheshimiwa Mbunge anasema Serikali ichukue jukumu hili la kusimamia Mabaraza ya Kata. Katika mgawanyo wa kazi kwa maana ya Ugatuzi wa Madaraka *(D by D)* tumegawana kwamba Halmashauri itasimamia Mabaraza ya Kata ya Ardhi halafu na Serikali Kuu itaanzia ngazi ya Wilaya kwenda kule juu na Mheshimiwa Mbunge ni Diwani katika Halmashauri yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, Mabaraza haya hata baada ya kuwa yameteuliwa, usimamizi wake na uangalizi unasimamiwa na Halmashauri chini ya ulezi wa Mwanasheria wa Halmashauri zetu. Kwa hiyo kama kuna upungufu katika eneo hili ni muhimu kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema tuchukue hatua na kuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelekezo hapa kwa Wakurugenzi wote na Waheshimiwa Wabunge mtusaidie. Kwenye Bajeti ambayo inatengwa pale, mpaka wameelekezwa vikao vingapi wakae katika maeneo hayo ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka. Kwenye Bajeti ambayo inaendelea sasa tupitie: Je, kipengele hiki kimewekwa katika Bajeti yetu? Kama kuna tatizo, Bajeti ikifika hapa tuwasiliane ili tuweze kufanya marekebisho hayo. Wakurugenzi wana wajibu huo wa kusimamia, kutenga fedha na kuwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kwamba mafunzo yanatolewa kwa muda mfupi sana, lakini suala la mafunzo ni jambo endelevu. Kama kuna upungufu katika eneo lile Mwanasheria na Viongozi wa Halmashauri; na kama wanashindwa wataomba usaidizi katika ngazi ya Taifa, wanaweza kufanya mafunzo kadri inavyohitajika kutoka muda hadi muda mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo maelekezo ya Serikali, naomba wazingatie. Kama kuna upungufu tuwasiliane tuweze kuchukua hatua kwa maana ya *case by case.* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa bahati nzuri nimewahi kwenda mara kadhaa kwenye Mabaraza ya Kata. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Mwanasheria wa Halmashauri anasimamia Mabaraza hayo, lakini kiukweli kabisa hakuna usimamizi wa kisheria unaopatikana pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu: Je, Serikali iko tayari kuweka utaratibu mahsusi ili kusudi Mwanasheria apatikane wa kueleza na kuhakikisha wananchi wanatendewa haki kwa sababu unakuta Baraza la Kata linahukumu kesi ya shilingi milioni 10 wakati wao mwisho wao ni shilingi milioni tatu. Ni kwa sababu ya kukosa Mwanasheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua, Serikali imejipangaje kuhusu hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Siyo kweli kwamba Wanasheria hawasimamii haya Mabaraza ya Kata. Kama nilivyosema, kwenye majibu yangu yaliyotangulia hapa, kama kuna malalamiko kwenye eneo *specific,* Mheshimiwa Mbunge ni vizuri akataja ili tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano. Kule Kivule tulikuwa na shida kwenye Baraza la Kata, tulimwita Mwanasheria wa Halmashauri ile ya Manispaa ya Ilala akaja akasikiliza malalamiko yaliyokuwepo, gharama kubwa ya uendeshaji wa kesi, uonevu na kuvuka kiwango ambacho kimewekwa kwa mujibu wa sheria, tulivunja Baraza tukaweka viongozi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna malalamiko katika eneo mahsusi tupewe taarifa. Vilevile tujue kwamba Wanasheria wako kwa mujibu wa Sheria hii ili haya Mabaraza ya Kata na yanaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1985 na imeendelea kufanyiwa marekebisho kadri muda unavyoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama kuna malalamiko, lazima tuchukue hatua. Hata hivyo, Mwanasheria wa Halmashauri ana uwezo, kwa sababu hazungumzi mtu mmoja, Idara ya Sheria kwenye Halmashauri ina wajibu huo. Ila kama kuna Mwanasheria kwenye Halmashauri yoyote hapa Tanzania, ameshindwa kufanya wajibu wake na haendi kila siku, Mbunge umepeleka malalamiko, wananchi wamelalamika, wamehukumu kesi kinyume na utaratibu, tupe taarifa tuweze kuchukua hatua kwa Mwanasheria huyo wakati wowote kuanzia sasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza namshukuru Naibu Waziri, TAMISEMI kwa kujibu vizuri. Pia pamoja na hiyo aliyosema Naibu Waziri, changamoto hii kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pia tumeiona kwa sababu watu wale mashauri yao mengi yanahusiana na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Wizara yetu kwa kusaidiana na Msajili wa Mabaraza, akishirikiana na Wanasheria katika Halmashauri, tumeweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa zile Kamati zote za Mabaraza ya Ardhi ya Kata pamoja na Vijiji ili kuweza kuwapa elimu na ukomo wa namna wao wanavyotakiwa kusimamia. Kwa sababu wanapokwama, mashauri mengi yanaenda kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeona kwamba tujenge msingi kule chini ili watu waweze kufanya kazi zao vizuri kwa weledi ili kupunguza malalamiko ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayasema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na swali la msingi linalohusu Baraza la Kata, pia Mkoa wetu wa Songwe hauna Baraza la Ardhi la Wilaya. Nimekuwa nalalamika sana kwenye Bunge hili na Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba jambo hili watalishughulikia haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wananchi wangu wa Songwe wanakwenda Mbeya kusikiliza kesi zao na inasababisha gharama kubwa sana za kwenda kufika kule kusikiliza kesi na kurudi.

Je, ni lini Baraza la Kata litaanzishwa katika Mkoa wetu wa Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa mujibu wa Sheria, tunatakiwa kuwa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya kila Wilaya. Mpaka sasa Mabaraza yaliyoanzishwa kisheria yameshafikia 100, lakini yanayofanya kazi yako 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba tuko tayari kuanzisha Baraza katika Wilaya yoyote ili mradi pawepo na miundombinu ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Baraza hilo. Kwa sababu kama Wizara, hatujengi majengo kwa ajili ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Kwa hiyo, kama wakiwa tayari; na nilipokuwa kule mwezi uliopita, waliitoa hoja hiyo, nikasema tunachohitaji ni kuonyeshwa eneo ambalo litatosheleza kuweza kuwa na Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba ya Wilaya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Kuongezeka kwa Watoto wa Mitaani Jijini Dar es Salaam**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la Watoto wa Mitaani Jijini Dar es Salaam hali ambayo inakosesha Watoto hao haki zao za msingi kama elimu na malezi bora?

Je, Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kufiwa na wazazi, migogoro ya familia, kutengana kwa wazazi, vitendo vya unyanyasaji na ukatili na umasikini katika ngazi ya kaya, vimesababisha ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utafiti ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani iliyofanywa mwezi Mei mwaka 2018, inayohusisha mikoa sita nchini ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Arusha na Iringa, jumla ya watoto wapatao 6,393 wakiwemo wa kiume 4,865 na wa kike 1,528 wanaoishi na kufanya kazi mitaani, walitambuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 hadi mwezi Machi, 2019 jumla ya watoto 2,702 walipatiwa huduma mbalimbali katika mikoa ifuatayo: Arusha, watoto 330; Dar es Salaam 475, Dodoma 337, Iringa 313, Mwanza 770 na Mbeya 447. Huduma zilizotolewa ni pamoja na huduma za, chakula, afya, malazi, kurudishwa shuleni, stadi za ufundi, stadi za maisha, kuunganishwa na familia pamoja na msaada wa kisaikolojia na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa malezi na ulinzi wa watoto wakiwemo walio katika mazingira hatarishi. Pia itaendelea kuwajengea uwezo wazazi na walezi kwenye eneo la stadi za malezi na ulinzi wa watoto. Aidha, Serikali itaendelea kufanya tafiti ili kubaini kiini cha tatizo na kupanga mipango mahsusi ya kupambana na kutokomeza tatizo la watoto wa mitaani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa rai kwa jamii kuhakikisha kwamba jukumu la matunzo, malezi na ulinzi wa mtoto linatekelezwa ipasavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri ambayo yatasaidia wazazi waliokuwa hai na wanaoweza kuwatumia watoto isivyo kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya barabara wanapotembea, pembezoni mwa ile barabara utakuta mzazi na mtoto wake wanaomba ili waweze kujikimu kimaisha: Je, Wizara hii suala hili wanaliona? Kama wanaliona, wanamnusuru vipi yule mtoto ili aweze kuendelea na masomo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna baadhi ya watoto ni wadogo, wakati wa masomo utawakuta mitaani wanatembea na biashara, wengine za maandazi na matunda na wakati wazazi wao wanajulikana na sehemu wanazokaa: Je, Wizara hii itamnusuru vipi yule

mtoto ili aweze kwenda shuleni kwa wakati ule wa masomo badala ya kupita mitaani na biashara akitembeza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kutoa maelezo kuhusu haki za mtoto ni zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania tuliridhia Mikataba ya Kimataifa na tukatunga Sheria Na. 21 ya mwaka 2009 ambayo inatoa haki za msingi kwa mtoto. Naomba kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri Wabunge na hata vijana na watoto ambao wako kwenye *gallery* waweze kuzitambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto ana haki ya kuishi, mtoto ana haki ya kuendelezwa, mtoto ana haki ya kushirikishwa na mtoto ana haki ya kutofanyishwa kazi nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria hii, Kifungu cha 14 kimeeleza vizuri tu kwamba pale haki hizi zinapokiukwa, Serikali inaweza ikamshtaki mzazi na kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na faini isiyozidi shilingi milioni tano na kifungo kisichozidi miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ambacho sisi kama Serikali tumefanya? Kwanza kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, tumeanza kufanya tathmini ya kina katika maeneo ya majiji kuweza kuwabaini watoto wale ambao wako mitaani. Ukiangalia tumefanya katika njia mbili; moja, tumefanya mchana hili na kujua idadi yao, lakini vilevile tumefanya hili zoezi usiku. Tulichokibaini ni kwamba, watoto wengi wanakuwa mtaani mchana, lakini usiku wengine wanarudi majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Watoto hawa wanafanyishwa shughuli za ombaomba na nyingine hizi za kufanya biashara. Kwa hiyo, tumekuja na Kampeni inayokwenda kwa jina la "Twende Sawa" ambapo moja ya jambo tutakaloenda kulifanya katika kampeni hii, ni kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Vilevile tumejumuisha na hili suala la watoto ambao wanatumikishwa na kufanyishwa biashara mitaani, kwa lengo la kuanza kutoa elimu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Halmashauri kuweza kufanya zoezi hili la kufanya tathmini katika maeneo yao na kuanza kwenda kuchukua hatua kwa wale wazazi ambao wanakaidi na ambao hawasimamii majukumu yao ya msingi na kuwatumikisha watoto kama ombaomba na kufanya biashara mtaani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mpaka kufikia Desemba, 2019 Serikali mlikuwa mmesajili makao ya kulelea watoto kutoka 13 mpaka 213. Pamoja na mikakati mizuri ambayo meiwekwa, Serikali yetu mpaka sasa hivi ina Kituo kimoja tu cha makao maalum ya watoto na Mheshimiwa Naibu Waziri ameonesha kabisa changamoto ya watoto wa mitaani bado ni kubwa:-

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kuanzisha na wao badala ya kuachia Taasisi za Kidini na watu binafsi nayo ikaanzisha vituo maalum kwa ajili ya kulelea watoto hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rose Tweve kwa swali lake zuri. Sisi kama Serikali msimamo wetu ni kwamba watoto walelewe na wazazi, hilo ndiyo jukumu la kwanza. Endapo wazazi wameshindwa kutekeleza yale majukumu, basi jamii inayozunguka wale watoto iweze kuwalea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali kuwachukua watoto na kuanza kuwalea katika makazi ya watoto ni hatua ya mwisho sana. Ni kweli tuna hayo majengo ya kule Kurasini ambacho ni Kituo cha Kulelea Watoto lakini nikupe tu taarifa kwamba na hapa Dodoma kama Makao Makuu ya nchi tunakusudia kuanza ujenzi wa Kituo kingine cha watoto mwaka huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwanza niruhusu niishukuru Serikali kutujengea Hospitali kubwa ya Wilaya, Mbulu Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya mtoto inayosemwa hapa ni pamoja na kupata matibabu. Serikali ilituahidi kutupatia gari la wagonjwa: Je, lini inatimiza ahadi hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza; kwa kuwa tatizo hili ni kubwa kwa nchi nzima na kwa kuwa baadhi ya familia ambazo zina watoto hawa ni watu wenye uwezo, wametelekeza kutokana na matatizo mbalimbali ya kifamilia:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutafuta namna ya kutafuta msimamizi halisi wa sheria hii kwa ngazi ya Wilaya na Ofisi za Ustawi wa Jamii ili kuweza kuleta tija kwa kundi hili muhimu sana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi Serikali ya Tanzania imeridhia Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Mtoto na ndiyo maana tuna Sera ya Mtoto ya Mwaka 2008 na vilevile tuna Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009. Sheria hii imeainisha kwa kina sana haki hizi za mtoto. Niseme tu kwamba sheria ipo na imeainisha adhabu ambazo zinaweza zikatolewa endapo haki za mtoto zitakiukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo inatukabili ni idadi ndogo ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika maeneo mbalimbali katika Halmashauri zetu. Nasi kama Serikali tumeliona hilo, tunaendelea kuwajengea uwezo Maafisa Ustawi Jamii wetu katika Halmashauri ambapo wapo lakini vilevile dhamira ya Serikali ni kuongeza idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii ili waweze kusimamia jukumu hili la kuweza kuhakikisha kwamba haki za watoto zinalindwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 99

**Marekebisho ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kuondoa upungufu uliopo, hususan kwenye upande wa Uanachama na kuipa Serikali nguvu za Kisheria juu ya Vyama vya Ushirika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Msuha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa sote tunaelewa kuwa ushirika ni dhana ya hiari, lakini Serikali ni msimamizi mkuu wa vyama vya ushirika pale ambapo viongozi wake au vyama vyenyewe havitekelezi malengo yaliyokusudiwa na ushirika. Serikali inakiri vyama vinakabiliwa na changamoto za kiutendaji, usimamizi, viongozi kutokuwa waadilifu na upungufu wa kimfumo wa uendeshaji wa baadhi ya Vyama vya Ushirika hapa nchini. Hata hivyo, vipo baadhi ya Vyama vya Ushirika ambavyo vinafanya vizuri, mfano, Chama cha Ushirika cha Chai kilichopo Wilaya ya Mafinga kinachoitwa Chamkonge na Chama cha Ushirika cha Kahama (*KACU)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika ndicho chombo cha kuwaletea wananchi maendeleo ya kiuchumi kwa kuwaunganisha wakulima ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kutoa huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo na kutafuta masoko ya mazao. Aidha, Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020 Ibara ya 22(g) na 86(a) inaelekeza kuifanyia mapitio Sera ya Vyama vya Ushirika na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na upatikanaji wa takwimu zitakazosaidia kuandaa mipango na kuleta mageuzi katika sekta ya ushirika na kuimarisha uchumi wa taifa na kuviimarisha vyama vya ushirika kuwa na uwezo wa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ya ndani na nje kwa kuweka mfumo madhubuti wa ukusanyaji, uchambuzi na uenezaji wa taarifa za masoko na kutoa elimu juu ya uongezaji thamani na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ipo katika hatua za mwisho kuleta Bungeni mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Maendeleo ya Ushirika yatakayoendana na mahitaji ya sasa ambayo yatahusisha mabadiliko ya mfumo na muundo wa uongozi ili kuendana na mahitaji ya teknolojia na kuleta ushindani wa kibiashara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martin Msuha, swali la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya serikali; hata hivi nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa ambayo inavikabili vyama cha ushirikia kwa maana *AMCOS* wilayani Mbinga ni nikukosa mitaji kwa ajili ya undeshaji washughuli zake, jambo ambalo linasabisha kukopa kutoka kwenye benki za biashara kwa riba kubwa.

Je, serikali ina mpango gani wa kufungua tawi la Benki ya Kilimo Wilayani Mbinga ili kuziwezesha *AMCOS* hizo kukopa kwa riba naafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msuha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vyama vingi vya ushirika ama watanzania wengi walioko sekta ya kilimo walioko vijijini wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mitaji na hasa pale ambapo wamekuwa wakikopa katika benki za biashara. Serikali iliaangiza Tanzania *Agriculture Development Bank* kuingia akubaliano na benki za bishara kama NMB na CRDB; na benki zote hizi sasa hivi zina mahusiano ya moja kwa moja na Benki ya Kilimo. Umetengenezwa utaratibu ambapo mwananchi ama taasisi yoyote ambayo inajihusisha na kilimo iliyoko wilayani inaweza kwenda katika dawati lililopo katika NMB ama CRDB ambalo linaiwakisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni benki ambayo kimkakati hawezi kwenda kufungua matawi nchi nzima katika kila wilaya kwa sababu ya namna ambavyo imeundwa. Ni benki ya kimkakati ambayo ni ya uwekezaji wa muda mrefu katika sekta ya kilimo na haifanyi *commercial activities*. Kwa hiyo ningemshauri Mheshimiwa Mbunge awahamasishe vyama vyake vya msingi vya ushirika viende katika Benki za *NMB* ama *CRDB* zilizopo katika wilaya zetu ambazo zitayari zina madawati ya mahusiano ya kibiashara na Benki ya Maendeleo ya Kilimo, na huko watapata huduma wanazohitaji za muda mrefu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, naishukuru serikali kwa majibu mazuri, lakini pia naipongeza kwa kurejesha mali za ushirika mikononi kwa washirika wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu. Kwa kuwa elimu ya ushirika ni elimu ambayo inahitajika sana kwa wananchi na hasa tukizingatia ambavyo ushirika nchi hii umekuwa ukipata misukosuko hadi umefikia kutoka kwenye wizara mpaka hadi kwenda idara; na kwa kuwa nchi hii ina bahati sana kuwa na Chuo Kikuu cha Ushirikia pale Moshi, na wote washirika wanatakiwa kupata elimu.

Ni lini sasa serikali italeta muswada Bungeni kubadili mafunzo kwa wote wale ambao wanashiriki ushirika waende kwenye chuo kile kusomeshwa na kuelewa ushirika nini kama alivyoeleza Naibu Waziri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya elimu ya ushirika miongoni mwa viongozi wa ushirika vilevile na wanachama wa vyama vya ushikirika. Wakati tunapitia, na tutakapoleta sheria ambayo tunatarajia kuileta katika Bunge lango Tukufu. Wizara ya kilimo sasa hivi imeamua kuanzisha mkakati wa kutoa elimu ya ushirika kwa kukihusisha Chuo cha Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita tumeanza na vyama vikuu vya ushirika, viongozi wote walikuwa hapa Dodoma, na sasa hivi watalaamu kutoka Chuo cha Ushirika Moshi wamekatiwa *zones* kwenda kutoa elimu katika vyama vya msingi vilivyopo katika wilaya zetu na mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nitumie nafasi hii kusisitiza ofisi za serikali za wilaya na mikoa zitoe ushirikiano kwa Warajis wa Mikoa na walimu walioletwa katika mikoa kwa ajili ya kutoa elimu kwa vyama vikuu na vya msingi vilivyopo katika wilaya zetu. Tumewekeana *deadline* kufika mwezi wa Aprili wataalamu hawa waliogawana katika *zones* sita watakuwa wamefika katika wilaya zote na mikoa yote kuanza kutoa elimu ya ushirika kwa viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwia tunaendelea na swali la Mheshimiwa Azza Hilaly Hamad Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 100

**Kuboresha Mradi wa Umwagiliaji Kijiji cha Nyida**

**MHE. AZZA HILALY HAMAD** aliuliza:-

Je, lini Serikali itachimba bwawa kwa ajili ya kuboresha Mradi wa Umwagiliaji Nyida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hilaly Hamad Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo ikiwa ni pamoja na Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida. Katika kutekeleza Mradi huo, Kampuni ya Shekemu *Construction Ltd.* inafanya kazi ya ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuboresha mfumo wa usambazaji maji mashambani ambapo utekelezaji wa Mradi huu kulingana na Mkataba umefikia asilimia 68 ya kazi zote za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Disemba 2019 jumla ya Shilingi za Kitanzania 282,154,880.68 zimelipwa kwa Mkandarasi kati ya Shilingi za Kitanzania 466,594,981.81 zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza Skimu ya Nyida. Mradi huo kwa sasa umesimama kupisha msimu wa kilimo kwa wakulima na mvua zinazoendelea kunyesha. Hivyo, Mkandarasi ataendelea na kazi iliyobakia kulingana na Mkataba mara baada wakulima kuvuna mazao yao na msimu wa mvua kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya tabianchi na mvua zisizotabirika pamoja na wakulima kuwa na mwamko mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji kwa kutaka kuongeza tija na uzalishaji kwa kulima misimu miwili kwa mwaka; na kwa kuzingatia kuwa chanzo cha maji cha skimu hiyo ni Mto Manonga ambao ni wa msimu; na hivyo Serikali iliona umuhimu wa ujenzi wa Bwawa ili kuendeleza skimu hiyo.

Aidha, ili kutekeleza mradi huo, mwaka 2013 Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga na Nzega zilifanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa awali kwenye eneo linalokusudiwa kujengwa bwawa la Nyida eneo la Lyamalagwa

litakalokuwa na uwezo wa kumwagilia maji mita za ujazo 4,167,825 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.5 kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na mabadiliko ya kimuundo ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, na miradi mingi ya umwagiliaji kujengwa chini ya kiwango wakati huo, Serikali haikuweza kutekeleza mradi huo kwa wakati kutokana na kufanya tathmini ya kina ya ufanisi ya miradi hiyo na hivyo kushindwa kutekeleza mradi kwa wakati. Aidha, kwa kuwa muda mrefu umepita tangu tathmini hiyo ifanyike, Serikali itafanya mapitio upya ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kupata mahitaji na gharama halisi ya ujenzi wa bwawa na athari zake kwa sasa na itaanza kujenga ujenzi wa bwawa hilo baada ya tathmini hiyo kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Azza Hilaly Hamad, swali la nyongeza.

**MHE. AZZA H. HAMAD**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya serikali. Sasa naomba niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi ya umwagiliaji imekuwa haina tija kwa wakulima wetu, na hii ni kutokana na kwamba inategemea maji ya mvua za msimu.

(i) Je, serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuanza kujenga mabwawa badala ya kuanza kujenga mitaro ili tuweze kuvuna kwanza maji na baadaye kuweza kuyasambaza katika mashamba yetu?
(ii) Je, serikali imechukua hatua gani kwa miradi ya umwagiliaji ambayo imejengwa chini ya kiwango na imekuwa haina tija kwa wakulima wetu ukiwepo Mradi wa Masengwa na Mradi wa Ichololo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hilaly Hamad kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua je hatuoni umuhimu wa kuanza kabla ya miundo mbinu ya umwagiliaji. Nitake kwanza kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Azza Hilaly kwa uongozi wake kwa mfano, kwa sababu anatuunga mkono kwenye kilimo na amejenga bwawa la umwagiliaji eneo lake kwa kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama nilivyojibu swali la msingi, kwamba Serikali tupo tayari na tulishaanza kupitia Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa Mwaka 2012 tangu mwaka 2018. Kwa ajili sasa kwenda kuanza ujenzi wa miundo mbinu ya bwawa kabla ya hii miundo mbinu ya uwagiliaji kwa sababu tumeeona kwamba maji mengi wakati wa mvua yanakwenda baharini na kwenye mito na baadaye tunashindwa kupata maji ya umwagiliaji.

Kwa hiyo serikali tumeshaaza mpango huo na huo mpango umeshakamilikia ambao tumeugawa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza miaka mitano kuanzia mwaka huu mpaka mwaka 2025 na awamu ya pili itakuwa kuanzia mwaka 2025 mpaka mwaka 2035.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili; kwamba je, Serikali tumechukua hatua gani kwa miradi iliyojengwa chini ya kiwango. Kwanza, hatua tuliyoichukua kama Serikali ni kuhamisha Tume yenyewe ya Umwagiliaji kutoka kwenye Wizara ya Maji kuja Wizara ya Kilimo ili kukiweka pamoja kilimo pamoja na umwagiliaji. Pili ni kuimarisha Muundo wa Tume ya Umwagiliaji; kwamba badala ya kuwa na watalamu kwa ngazi ya kanda tu sasa tuna

wataalamu kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na kanda ili kuwe na usimaizi wa karibu sana katika miradi hii ya umwagiliaji siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tuko kwenye hatua za kufanya tathmini ya kina ili kujua mapungufu ya msingi yaliyosambisha miradi hiyo kujengwa chini ya kiwango na baada ya hapo hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wote ambao walitufikisha hapa ili tupate majibu sahihi ya nini cha kufanya kuendeleza miradi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika. Mradi wa *Ruafi Katongoro Irrigation* skimu serikali imetumia zaidi ya bilioni 1.8; Lakini hauna faida yoyote kwa wakulima zaidi ya 2000 wa Kata za Kilando, Kipili pamoja na Itete.

Je, ni lini Wizara kilimo na umwagiliaji itaenda kuimarisha mradi wa skim ya katongoro na ruafi ili wakulima wanufaike na kilimo cha mpunga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Ally Keissy kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa najibu swali la msingi, kwamba kuna miradi mingi ambayo imejengwa chini ya kiwango pamoja na Serikali kupeleka kiasi kikubwa sana cha fedha kwa ajili ya mahitaji ya wakati huo. Kwa sasa hivi serikali tutatuma timu ya wataalam kwenda kuangalia mapungufu yaliyofanyika katika mradi huo; na haraka iwezekanavyo baada tathimini hiyo tutaanza kupanga fedha kwa mujibu wa bajeti kwenda kuwahudumia watu hawa zaidi ya 2000 kwenye kilimo cha kisasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela, swali la nyongeza.

**MHE. RHODA E: KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mkoa wa Katavi bado una changamoto kubwa ya miradi ya umwagiliaji kuchukua muda mrefu na bila sababu ya msingi. Mradi wa mamba katika Jimbo la Kavuu ni miongoni mwa miradi, ambao imechukua muda mrefu na kuleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wa jimbo la kavuu. Serikali inasema nini kuhusiana na mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Kunchela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli miradi hii mingi ya umwagiliaji imechukua muda mrefu kumaliziwa. Kama nilivyozungumza hapo awali, ni kwamba changamoto kubwa ilikuwa ni kwamba miradi hii haikuleta gharama halisi wakati wa ujenzi wake. Kama tunavyofahamu wakati ule kulikuwa na miradi tuliyokuwa tunaitekeleza kwa ngazi mbili. Kuna miradi ambayo ilikuwa inatekelezwa kwenye ngazi ya wilaya ambao ni ya *DIDF* miradi ambayo ilikuwa inatekelezwa ngazi ya taifa. Miradi yote ambayo ilikuwa chini ya thamani ya milioni 500 ilikuwa ni ngazi ya wilaya na miradi ambayo ilikuwa ni zaidi ya milioni 500 tunatekeleza ngazi ya taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna baadhi ya halmashauri, mojawapo ikiwa yakwako, ilileta mradi huo chini ya thamani ya mradi ili kwamba wapate kigezo hela hizo ziende kwenye

wilaya yako wakatekeleza wao ilhali mradi ulikuwa unahitaji fedha nyingi. Sasa baada ya mapungufu hayo tumesema kwamba tunaunda kikosi kazi ili kupitia kujua gharama halisi ya kiasi gani kinachohitajika; na baada ya gharama hizo ndio tutaanza ujenzi wa mradi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafsi hii. Mvua zinazoendelea kunyesha katika Wilaya ya Lushoto zimefanya uharibifu mkubwa sana wa miundo mbinu ya skimu za umwagiliaji, Skimu ya Mng'alo Kitivo pamoja na skimu kiwani mwezae kwa Mgiriki Kata ya Lunguza nakufanya sasa kilimo cha mpunga kiwe shakani.

Je, serikali ina mpango gani mahususi wa haraka kwenda kuondoa mawe ambayo yamenasa katika kingo za mto umba ambao ndio unapeleka maji katika skimu hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba tumepata taarifa; kwanza kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge mwenyewe kwamba alishatuambua, lakini pia kutoka kwa katibu Mkuu wa Chama Chama Mapinduzi, anayesimamia ilani, Dkt. Bashiru Ally. Alifika mwenyewe kwenye skimu hiyo na alitupigia simu kujua namna gani tunakwenda kusimamia utekelezaji wa ilani katika Jimbo hilo la Mlalo huko Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali tupo tayari, na nichukue nafasi hii kuwaelekeza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kanda ya Kilimanjoro, viongozi wa mkoa na wilaya kwenda haraka iwezekanavyo katika skimu hii katika banio la Ng'alo Kitivo pamoja na Skimu ya Lunguza ili kuangalia mapungufu haya na uharibifu mkubwa wa mawe tuone namna gani tunaweza kuondoa haraka iwezekanavyo. Nami nikuahidi pia baada ya Bunge hili, kwa sababu nilishafika miezi miwili iliyopita, nitarudi tena huko ili kuona namna gani tunaweza kuwaidia watu wa Mlalo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara za Nishati Mheshimiwa Marry Pius Chatanda Mbunge wa Korogwe Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 101

**Tatizo la Kukatika Umeme – Korogwe**

**MHE. MARY P. CHATANDA** aliuliza:-

Umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara Korogwe na kufanya uharibifu wa mali za Wananchi:-

Je, ni lini tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na ukarabati wa miundombinu ya umeme unaoendelea kwa sasa Wilayani Korogwe, *TANESCO* hulazimika kukata umeme katika maeneo husika ya wilayani humo ikiwa ni pamoja na maeneo ya Mji wa Korogwe. Hali hiyo inasababishwa na kazi zinazoendelea za kukarabati wa miundombinu ikiwa ni pamoja na kubadilisha vikombe vibovu, nguzo mbovu, ukataji wa miti na matawi katika njia za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kazi za kukarabati miundombinu ya kusambaza umeme zifanyike hulazimika kuzima umeme katika maeneo yanayofanyiwa ukarabati. Kukamilika kwa ukarabati unaoendelea kutawezesha kuimarika kwa umeme na kurudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara zote kabla ya kuzima umeme taarifa zimekuwa zikitolewa katika vyombo mbalimbali vya habari katika Wilaya ya Korogwe na Mkoa wa Tanga. Hali ya kukatika umeme kwa ajili ya kupisha matengenezo kumeimarisha sana upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo. Aidha, tunaomba wananchi waendelee kuwa wavumilivu katika kipindi cha matengenezo ya miundombinu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda swali la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafas niulize swali la nyongeza. Nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara ya Nishati kupitia Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wa *TANESCO* Mkoa na Wilaya ya Korogwe kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya sasa ya kuhakikisha kwamba vijiji vinapata umeme wa *REA* katika maeneo yale ambayo yalikuwa yamekosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza ni kwamba; kwa kuwa adha hii imekuwa ni ya muda mrefu na majibu aliyoyatoa Naibu Waziri ni mazuri, yanaridhisha:

Je, ni lini sasa ukarabati huu utakamilika? Maana unaweza ukasema unaendelea kukarabati, halafu inaweza ikawa mwaka mzima unafanyika ukarabati. Ni lini sasa watakamilisha ukarabati huu ili kusudi wananchi waondokane na adha hii ambayo wanaipata sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimepokea kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri shukrani zake, lakini kipekee nampongeza Mheshimiwa Chatanda kwa kazi nzuri anayofanya kwenye Jimbo lake, lakini kwa ushirikiano wake pamoja na ofisi yetu ya *TANESCO* ya Mkoa na Wilaya ya Korogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi ni kwamba kwanza ukarabati huu ni mkubwa, unahusisha nguzo zaidi ya takriban 920 na unagharimu shilingi bilioni 1,400. Mpaka sasa zaidi ya nguzo 500 zimesharekebishwa, zimeondolewa zile mbovu na zimewekwa hizo mpya. Nataka nimwambie, matarajio yalikuwa tukamilishe mwezi huu Januari mwishoni na huu wa Pili unaoendelea, lakini kwa kuwa mvua zinaendelea, tumeongea na *TANESCO* tukiwaelekeza kwamba pamoja na changamoto ya mvua, lakini waendelee kufanya haraka kukamilisha nguzo takribani 400 zilizobaki ili wananchi wa Korogwe vijijini na mjini wapate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mama Chatanda amekuwa akiambatana na *TANESCO* Wilaya katika maeneo hayo na mwenyewe amejionea. Kwa hiyo,

niendelee tu kuwapa pole wananchi wa Korogwe, lakini dhamira ya Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* ni kuhakikisha umeme unapatikana wa uhakika na muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete swali la nyongeza.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza. Matatizo ya Korogwe Mjini yanafanana sana na matatizo ya Wilaya ya Rungwe hususan Busokelo kwa kukatika katika umeme. Kwa siku umeme unaweza kukatika zaidi ya mara 10 na tatizo kubwa lililokuwepo ni kwamba, nguzo za umeme chini yake kuna miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wizara pamoja na Waziri kwa maana ya kuleta timu maalum kwenda ku-*clear* ama kukata hiyo miti, lakini bado tatizo kubwa limeendelea kuwepo. Ni mikakati gani Serikali iko nayo kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Busokelo wanapata umeme masaa 24 kwa siku kuliko hivi ilivyo kwa sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika swali la msingi, lakini hata la nyongeza kwa Mheshimiwa Chatanda; na niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mwakibete kwa swali linalofafana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Shirika letu la umeme nchini na kwa niaba ya Serikali, napenda tu nisema mambo mawili kwamba ukarabati unaoendelea. Jambo la kwanza tumetenga kila Mkoa wa ki-*TANESCO* kwa nchi nzima takriban shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa.

Kwa hiyo, wananchi katika maeneo yote ya mikoa yetu ambayo kuna kero ya kukatika kwa umeme, kwanza haukatiki kwa sababu ya hali ya umeme, isipokuwa tunakata kufanya matengenezo. Kwa hiyo, naomba nitoe taarifa hiyo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumetoa muda mahususi wa miezi sita kukamilisha ukarabati wote kwa nchi nzima. Kwa hiyo, ni matumaini yetu Mheshimiwa Mwakibete katika eneo lake ambalo lilikuwa na kero kubwa sana ndani ya miezi sita ukarabati utakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tumeleta *transforma* kubwa, tunabadilisha *transformer* kutoka ndogo kwenda kubwa, kwa sababu shughuli za uchumi za wananchi zinaongezeka. Kwa hiyo, tunaomba radhi kwa wananchi wote ambako ukarabati unaendelea. Tunaomba mtuvumilie tukamilishe kazi hiyo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde sasa aulize swali lake.

Na. 102

**Kosa la Kutoa na Kusambaza Habari za Uongo**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Ni kosa la Jinai kwa Mtu au Vyombo vya Habari kutoa, kuandika, kusambaza au kutangaza habari za uongo. Je, Jeshi la Polisi linachukua hatua gani stahiki kwa watu au vyombo vya habari vinavyofanya makosa hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI YA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linao utaratibu unaotumika pindi mtu anapokuwa ametenda makosa ya jinai ambapo ushahidi hukusanywa kisha jalada huandaliwa kwenda kwa Mwanasheria wa Serikali; na ushahidi ukijitosheleza, mtuhumiwa hufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016 ambapo inaelekeza kuchukua hatua kwa chombo cha habari kilichotoa taarifa za uongo ikiwa ni pamoja na kufuta leseni au kusimamisha leseni kwa muda pale ambapo chombo cha habari kimekiuka masharti ya leseni hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji, swali la nyongeza.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba kila mtu anastahiki heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matukio ya vyombo vya habari kuwadhalilisha na kuwasingizia uongo baadhi ya watu na katika watu wanaosingiziwa wengine wana uwezo wa kwenda Mahakamani na wengine ni wanyonge ambao hawana uwezo wa kusimamia hizi kesi Mahakamani. Je, Serikali inatoa msaada gani wa kisheria kwa watu ambao wanadhalilika na kukosa haki za utu wao kutokana na kusingiziwa na makosa kama hayo na vyombo vya habari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mara kadhaa nimeshuhudia baadhi ya magazeti kama Mwanahalisi na Tanzania Daima yakipewa adhabu mara kwa mara ya kufungiwa kutokana na kuzua au kuonekana wamesema uongo, lakini sijawahi kuona magazeti ya Tanzanite, Jamvi la Habari na Fahari Yetu yakichukuliwa hatua yoyote wakati ni kinara wa kuzua na kudhalilisha watu katika nchi yetu: Kwa nini Serikali haichukui hatua kwa vyombo hivi vya habari na mmiliki wake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa ufafanuzi kwa maswali ambayo ameuliza Mheshimiwa Mbunge. Kwanza niseme kwamba kitu ambacho anazungumza siyo kweli kwa sababu sisi kama Serikali tunafanya kazi kwa kusimamia sheria pamoja na kanuni. Mara zote ndani ya hili Bunge tumekuwa tukitoa ufafanuzi kwamba sisi kama Wizara tumekuwa tukichukua

hatua kwa magazeti yote ambayo yanakiuka sheria ambazo sisi wenyewe Wabunge tumezitunga ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge ambapo amesema kwamba hatuchukulii hatua magazeti ya Tanzanite, siyo kweli kwa sababu tumeshajibu mara kadhaa humu ndani kwamba tumeshaandikia onyo gazeti la Tanzanite, vilevile hata gazeti la Tanzania Daima pamoja na kwamba mara nyingi limekuwa likikiuka hizo kanuni, lakini tumekuwa tukiliandikia onyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Sheria yetu ya Habari inazungumza kwamba kabla ya kuchukua hatua yoyote kwa chombo chochote cha habari, cha kwanza tunachokifanya, tunatoa onyo mara ya kwanza, tunatoa nafasi ya mara ya pili na pale ambapo tunaona sasa hali hiyo imezidi, ndipo ambapo tumekuwa tukichukua hatua ya kuweza kufungia hayo magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kweli kwamba tumekuwa tuna upendeleo. Sheria haina upendeleo, nasi kama Wizara tumekuwa tukichukua hatua pale ambapo tunaona tumeshaonya mara kadhaa lakini bado hawajajirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la nyongeza la kwanza.

**NAIBU WAZIRI YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida wananchi ambao wamekuwa hawana uwezo wa kifedha wa kupata huduma ya kisheria, wamekuwa wakisaidiwa kupewa huduma hiyo na Serikali kupitia Wanasheria wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pale ambapo kuna changamoto yoyote ambayo inahusu malalamiko ya kutotendewa haki katika eneo lolote linalohusu sheria, basi mamlaka ya Serikali kupitia Wizara ya Sheria na Katiba wamekuwa wakichukua hatua ya kuwasaidia, kuwasikiliza na kuwashauri wananchi ambao wamekuwa wakihitaji huduma hizo za kisheria kwa ajili ya kuweza kufanikisha mashauri yao ama kesi zao mbalimbali aidha iwe Mahakamani ama kesi za kawaida za upatanishi na usuluhishi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasilino, Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Abdallah Mtolea Mbunge wa Temeke.

Na. 103

**Ujenzi wa Barabara ya Kilwa – Rangitatu - Kongowe**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. ABDALLAH A. MTOLEA)** aliuliza

Eneo la kipande cha barabara ya Kilwa – Rangi Tatu – Kongowe limeharibika vibaya na kusababisha foleni na ajali nyingi.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kikamilifu kwa kiwango cha lami ili kuondoa kero hizo?

(b) Je, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kipande hicho kwa njia nne mpaka Kongowe itaanza lini?

(c) Daraja la Mto Mzinga katika kipande hicho lipo katika hali mbaya na hatarishi: Je, ni lini Serikali itajenga daraja jipya kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wakati akiwa Waziri wa Ujenzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, lenye sehemu (a),( b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara katika Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kushughulikia tatizo la msongamano wa magari katika Jiji hilo. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka kwa awamu ya pili, *(BRT Phase II)* ambao unahusisha barabara ya Kilwa kuanzia Gerezani hadi Mbagala Rangi Tatu. Kazi za ujenzi wa barabara na vituo vya mabasi ulianza mwezi Mei, 2019 na umepangwa kukamilika mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha usanifu kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Kilwa kuanzia sehemu ya Mbagala Rangi Tatu hadi Kongowe yenye urefu wa kilometa 3.8 kutoka njia mbili kuwa njia nne. Usanifu huo unahusisha Daraja la Mzinga. Baada ya kukamilika kwa usanifu huo, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naipongezs Serikali kwa kazi kubwa inayoendelea ya ukarabati na ujenzi wa barabara mbalimbali pale Wilayani Temeke. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara kutoka *Keko Furniture* mpaka kwenye geti la Chuo Kikuu cha *DUCE* imekuwa na mashimo makubwa na imekuwa ni usumbufu kwa wanaotumia barabara hiyo ikiwa ni sambamba na kipande cha barabara ya *Devis Corner, Jet corner* hasa kipande cha kutoka Lumo mwisho mpaka *Jet corner,* vimekuwa na mashimo mengi sana na barabara hizi ziko chini ya *TANROADS*: Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuiagiza *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam kwenda kuziba mashimo katika barabara hizi haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha, barabara nyingi zilizo chini ya *TANROADS* na *TARURA* hasa barabara ya kutoka *Temeke Veterinary* kupitia Mwembe Yanga mpaka Tandika na barabara zote zinazoingia Tandika barabara zote katika Kata ya Temeke 14, Kata ya Sandali na Kata ya Buza hazipitiki kabisa; na uwezo wa Halmashauri ya Temeke kuzikarabati barabara hizi zote kwa kipindi hiki umekuwa ni mgumu: Je, Wizara yako kama mdau mkubwa wa miundombinu, ina mpango gani wa dharura wa kuisaidia *TARURA* kukarabati barabara hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli baada ya mvua nyingi hizi kunyesha barabara zetu nyingi zimeharibika kwa kiasi kikubwa. Nianze tu kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anafanya kazi kwa ushirikiano. Na mimi nimetembelea barabara hizi ikiwemo hii barabara ya *Keko Furniture - DUCE* nimeipita tena ni wiki ya juzi tu kuona hali ilivyo mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwahidi Mheshimiwa Mbunge na kwa maelekezo yangu kama tulivyojipanga ni kwamba tutarejeshea miundombinu ya barabara hii mvua zitakapopungua. Inakuwa siyo rahisi wakati huu mvua nyingi zinaendelea kunyesha kufanya ujenzi wa kiwango cha lami kwa maana ya kurudishia sehemu zilizoharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira, tumejipanga vizuri, ndiyo maana tumeendelea kuyatambua maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa matengenezo na tutarudi kufanya matengenezo mvua zitakapopungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pia barabara hii ambayo ameitaja ya Tandika na kimsingi barabara ambazo ziko *TARURA*, niseme tu kwa ujumla kwamba tunao utaratibu wa kushirikiana kama Serikali kwa upande wa *TARURA* na *TANROAD*. Inapokuwa tumepata dharura *(emergency)* au shida kama wakati huu, tunafanya kazi kama timu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutashirikiana na wenzetu wa *TARURA* kuhakikisha kwamba mvua zikipungua tutafanya urejeshaji wa miundombinu muhimu katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofanya, nami namwahidi kumpa ushirikiano mkubwa; tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba tunawahudumia vizuri wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati ilifunguliwa mwaka 2018 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini katika baadhi ya maeneo ya barabara hii kumeshaonekana uharibifu wa kuwa na mashimo na hivyo kuhatarisha usalama wa raia pamoja na magari: Je, Serikali inatoa tamko gani kwenye hii barabara mpya ambayo imeshaanza kupata uharibifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yako maeneo ambayo yamekuwa dhaifu baada ya ujenzi wa barabara. Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara hii ya kutoka Dodoma - Kondoa – Babati ni kati ya barabara ambazo zipo kwenye kiwango kizuri na imejengwa kwa teknolojia mpya, hii ni *super pave* ukiilinganisha na barabara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kweli kwamba yako maeneo ambayo yamekuwa na upungufu. Vile vile uko utaratibu wa kimkataba kwamba kipindi cha matazamio barabara inafanyiwa urejeshaji. Kwa hiyo, tutaendelea kusimamia taratibu zilizokuwepo ili kuona maeneo ambayo yana upungufu yanafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mara baada ya miaka mitano ni utaratibu wetu wa kawaida kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na ubora wa barabara hii, maeneo yote ambayo yana upungufu tutaendelea kuyasimamia ili kuhakikisha kwamba barabara inakuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na wananchi wanapata huduma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Barabara ya Makurunge - Saadani - Pangani mpaka Tanga ni barabara ambayo inaunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga kwa njia ya mkato.

Pia barabara hii ni kichocheo kikubwa sana cha utalii hasa kwa hifadhi yetu maalum ya Saadani ambayo kwa sasa haipati watalii wa kutosha kwa sababu barabara hiyo ipo katika hali mbaya. Barabara hii pia imeahidiwa; au iko katika mipango ya Serikali kwa ujenzi wa kiwango cha lami kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali: Ni nini mkakati wa Serikali kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ikitokea Tanga – Pangani – Makurunge – Sadani, inakuja mpaka Bagamoyo, ni barabara ambayo iko kwenye mpango wa ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tumeshaanza ujenzi, tumeshapata mkandarasi ambaye anajenga barabara hii kutoka Tanga kwenda Pangani. Pia tuko kwenye mpango wa kujenga daraja katika Mto Pangani. Tunaamini kwamba baada ya ujenzi wa daraja hili katika Mto Pangani, italeta sasa mantiki ya kumalizia ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kuja Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bagamoyo na Watanzania kwa ujumla kwamba ni mpango wa Serikali kuikamilisha barabara hii kwenye kiwango cha lami na ujenzi umeshaanza, tuvute subira, tutakuja kumalizia kipande hiki kinachobaki kwa maana ya kutoka Bagamoyo kwenda Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuko kwenye mpango na itafupisha barabara hii ukitokea Tanga kwa sababu itakuwa na kama kilomitaa 240 hivi tu kutoka Tanga kuja bagamoyo. Kwa maana hiyo, pia itatusaidia sana kufanya watalii waende maeneo ya Sadani kwa maana ya kutuingizia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza na Naibu Waziri wa Maliasili kwamba tutaitembelea barabara hii kwa maeneo ambayo ni korofi kwa kipindi hiki baada ya mvua kupungua, tuhakikishe kwanza inapitika, inatupa huduma lakini wakati ule ule tutaendelea na utaratibu wa kuijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali letu la mwisho, Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalumu, sasa aulize swali lake.

Na. 104

**Kivuko Chenye Viwango Kyanyabasa – Bukoba**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Kivuko kilichopo Bukoba Vijijini Kyanyabasa hakikidhi viwango kabis:-

Je, ni lini Serikali itaweka kivuko au daraja litakalokidhi viwango?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kivuko cha MV Kyanyabasa kinachotoa huduma kati ya Buganguzi na Kasharu eneo la Kyanyabasa katika Mto Ngono kilinunuliwa mwaka 2005 na kina uwezo wa kubeba abiria 50 na magari madogo mawili kwa pamoja. Kivuko hiki kilifanyiwa ukarabati mkubwa mwaka 2016 na kinaendelea kutoa huduma kwa wananchi wa Bukoba bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kutoa huduma nzuri na zenye viwango, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021, imejipanga kukifanyia maboresho makubwa ikiwa ni pamoja na kuweka viti na paa kwa ajili ya abiria kujikinga na mvua na jua; kuweka taa kwa ajili ya kutumika kuvusha abiria kwa dharura nyakati za usiku na ukarabati utakaohusisha kubadilisha milango pamoja na kupaka rangi.

Mhehimiwa Naibu Spika, kivuko kilichopo kwa sasa kinatosheleza kutoa huduma inayohitajika kwa wananchi wa eneo hilo. Hivyo, hakuna haja ya kujenga daraja kwa sasa. Serikali itaangalia uwezekano wa kujenga daraja siku za usoni pale itakapohitajika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGULUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kivuko hiki cha Kyanyabasa wanafunga kazi saa 12.00 jioni ambapo inaleta adha kubwa kwa wananchi. Kwa mfano, imetokea umeuguliwa usiku, inakulazimu kuzunguka Kishogo – Nyakibimbili – Ibwela – Katelero kuja kwenye Hospitali ya Wilaya inayojengwa Kanazi eneo la Bujunangoma:-

Je, ni lini Serikali itatuondolea adha hiyo ya kufunga kivuko mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Tatizo lililopo katika kivuko cha Kyanyabasa ni sawa na kivuko kilichopo Kata ya Kashalu maarufu kwa jina Kansinda kinachounganisha Wilaya ya Bukoba na Misenyi:-

Sasa ni lini Serikali itaweka kivuko cha Uhakikika kuliko kuvuka na mitumbwi ambapo inahatarisha maisha ya wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayofanya, kwa sababu mara nyingi kwa kweli amekuwa akitusumbua kwa nia ya kuhakikisha wananchi wa eneo hili la Kagera wanapata huduma nzuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maswali yake mawili, niseme, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, ni kwamba tumedhamiria kufanya maboresho makubwa ya kivuko hiki. Nimesema kwamba pia tutaweka taa pale. Tukiweka taa za usalama pale na tutahakikisha kwamba tunatoa huduma vizuri usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu Mheshmiwa Oliver kwamba tumejipanga kuona tunatoa huduma usiku na mchana. Hata hivyo kwa sasa eneo lile tunavusha kwa kutumia dakika tano tu, tunafanya mivuko pale mara 35 hadi 40 ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri. Kwa hiyo tuendelee kuwasiliana tu na pale ambapo kuna dharura, kwa mfano tuna wagonjwa au misiba na hata wakati wa sherehe kama harusi, tuwasiliane. Tuko tayari kuwahudumia usiku na mchana wakati harakati za kufanya maboresho makubwa yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo eneo alilotaja la Kata ya kasharu umeita mwenyewe Kasinda, nielekeze tu wenzetu upande wa TAMESA waende wakaangalie kwa makini eneo hili tuone namna nzuri ya kuleta huduma hii ili tuwaokoe wananchi na hatari ambayo inaweza ikasababishwa na kuvuka kwa kutumia mitumbwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge, suala hili nitalisimamia ili tuone kwamba tunafanyaje wananchi hawa nao waendelee kunufaika na huduma nzuri ya vivuko kuliko kutumia mitumbwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa miradi mbalimbali: Ni lini ahadi za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa kwa kujengwa kwa kiwango cha lami katika Mji wa Makambako?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa jirani yangu, tumezungumza mambo mengi ya Makambako. Niseme tu, ahadi za Viongozi Wakuu zikiwemo ahadi za Mheshimiwa Rais tunaendelea kuzitekeleza. Ziko ahadi ambazo tumemaliza kuzitekeleza, ziko ambazo ziko na asilimia kadhaa na zipo nyingine ambazo bado. Naahidi tu Bunge lako kwamba ahadi zote ambazo zimetolewa na viongozi, tutaendelea kuzitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ambazo zilitolewa Makambako, ziko ahadi nyingi; iko ahadi ya ujenzi wa barabara kiwango cha lami, tunaendelea na ujenzi, Mheshimiwa Mbunge anafahamu, tumeshaanza kidogo kidogo, tutajitahidi tuweze kuweka kiasi kikubwa ili tuendelee kwa Mji wa Makambako uweze kukaa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu pia kwamba pale barabara kubwa tumeitengeneza vizuri, kulikuwa na foleni nyingi pale kwenye mizani, tumeziondoa kabisa; Mji wa Makambako unawaka taa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, waende wajifunze waone namna nzuri tu kuweka taa katika Mji wa Makambako. Ukienda Makambako, hali ni nzuri kabisa. Tunajua tena tuna ujenzi wa One Stop Station pale Idofi; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na yenyewe ni sehemu ya ahadi, tuko kwenye mpango wa kufanya ujenzi pale. Kwa hiyo, tunaendelea na hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu ahadi zote za viongozi tutaendelea kuzitekeleza na kwa ufundi mkubwa, Serikali imejipanga vizuri kuona ahadi hizi za viongozi wetu tunaweza kuzitekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Sasa nitaleta kwenu matangazo. Tutaanza na tangazo la wageni.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Balozi Mstaafu, Hemed Mgaza. Karibu sana Mheshimiwa Balozi.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, ambao ni kwanza ni Ndugu Masoud Juma ambaye ni Mtanzania Mfupi zaidi Duniani aliyeweka rekodi ya dunia kwa kupanda Mlima Kilimanjaro na kufika kileleni. *(Makofi)*

Haya, haya, ahsanteni sana na pongezi nyingi sana. Maana hiyo kazi ya kupanda mlima jamani siyo kazi nyepesi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasema siyo kazi nyepesi, lakini wale wanaoweza wajitahidi tu wakapande. Mimi mwenyewe nimepanda, ndiyo maana najua mambo mazito huko. Kwa hiyo, hongera sana. Pia ameongozana na Ndugu Samwel Malugu na Ndugu Edward Shirima. Karibuni sana. Sasa hawa hawajasemwa kama walimsindikiza kupanda mlima ama wao ameongozana nao hapa tu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walioko hapa. Wageni watano wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kutoka Jijini Tanga wakiongozwa na Mstahiki Meya, Mheshimiwa Mustafa Selebosi. Wamekaa upande gani hawa? Aah, karibuni sana. *(Makofi)*

Aah, sasa huyu bondia hajawekwa jina hapa? Hawa Makatibu wananiangusha. Haya, tutakutangaza vizuri bwana, naona umeshikilia na mkanda hapo. Kwa hiyo, tutakutangaza vizuri. Makatibu niletewe hilo jina la huyu mpiganaji wetu ambaye ameshikilia mkanda pale. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kutoka Pangani Mkoa wa Tanga ambaye ni kaka yake Ndugu Yusuf Zongo. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Stephen Masele ambaye ni Makamu Rais wa Bunge la Afrika *(PAP)*, ambao ni rafiki zake kutoka Afrika ya Kusini, Ndugu Dong Bocheng, Ndugu Qiao Guodong na Ndugu Chiruyi Walingo. Nadhani pengine wataingia baadaye, siwaoni. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Mhandisi Edwin Ngonyani ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wanaotoka Wilaya ya Namtumbo Mkoa wa Ruvuma, wakiongozwa na Ndugu Nyika Issa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Shaabani Shekilindi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndugu Kelly Rwekaza, Ndugu Charles Komba na Ndugu Dorica Mahonzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambao ni wanafunzi kutoka Jimbo la Longido wanaosoma katika Vyuo mbalimbali vya hapa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Lekishon Thomas. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Frank Mwakajoka kutoka Momba, Mkoa wa Songwe, ambao ni Mheshimiwa Diwani Ayubu Sikagonamo na Joseph Kasambala. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Joram Hongoli ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Njombe ambao ni Ndugu Getruda Monique, Ndugu Josephine Sapulla na Ndugu Keneth Swalle. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Haji Ameir kutoka Zanzibar, ambao ni mke wake Ndugu Saida Hassan na watoto wake Ndugu Mwanaisha Bakari na Ndugu Zulekha Suleiman. Sasa hapo nadhani wifi yetu asimame ili tujue watoto ni wepi na… eeeh, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao vile vile wageni wanne wa Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ambao ni Wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha *Park Nyigoti* kutoka Serengeti Mkoa wa Mara, wakiongozwa na Ndugu Mtiro Gekara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni Makatibu Kata wa CCM Wilaya ya Kilolo Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ndugu Barnabas Nyaupumbwe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni sita wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni wapiga kura wake kutoka Manonga Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Ndugu Thomas Manyonda. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jacquline Msongozi kutoka Songea Mkoa wa Ruvuma, nao ni Ndugu Veneranda Ngonyani na Ndugu Stambuli Ndimbo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, sasa sijawaona wanafunzi, pengine wapo. Ni wanafunzi 100 na Walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Mpirani iliyopo Moshi Mkoa wa Kilimanjaro. Haya, nadhani wataingia baadaye.

Wapo wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Jordan kilichopo Mkoa wa Morogoro, nao nadhani hawakupata nafasi. Wengine ni wanafunzi 100 na Walimu 10 kutoka Chuo cha *Black School of Linguistics and Literature* kilichopo Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 10 kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni Waandishi wa Habari za Utawala Bora wakiongozwa na Ndugu Elias Msuya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jumbe mbalimbali hapa zikimtaka bondia aonyeshe mkanda wake, lakini sasa asimame ili tumtangaze vizuri. Huyu ni bondia kutoka Tanga, anaitwa Mtango Salim; na wiki iliyopita ameshinda mkanda wa ubigwa wa dunia. Karibu sana Salim, karibu sana Bungeni. *(Makofi/Vigelegele)*

Pia Mheshimiwa Ummy, ahsante kwa kutuletea bondia humu ndani na ninamwona Mheshimiwa Sophia Mwakagenda bondia wetu humu Bungeni akiwa amefurahi kabisa. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Pia Wizara kwa ujumla tunawapongeza, mnafuatilia hii michezo kwa karibu sana. Sasa kijana wetu uendelee kujitahidi huo mkanda usije ukapotea tena hapa nchini, itakuwa mtihani. Sisi tumeshakuona wewe unao, kwa hiyo, uendelee kupigana uongeze mikanda mingine, lakini huo usiondoke hapa nchini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *TWPG,* yaani Umoja wa Wanawake wa Bunge Tanzania, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wabunge wanawake wote mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge saa 7.00 mchana wote waelekee Msekwa kutakuwa na semina. Kwa hiyo, wanawake wote mtatakiwa kuelekea huko. Maelezo hayajatoka vizuri kama na wale wanao-*support* wanawake ama vipi!

Sasa huo ndiyo mwisho wa matangazo yetu, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu, tunaendelea

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa kujielekeza katika Kanuni ya 47(1) kuomba kiti chako kitoe ridhaa ya kujadili jambo kubwa na janga linaloendelea kutokea katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilichangia hapa, kutokana na manyanyaso na ubaguzi na kupigwa faini holela pamoja na vifo vinavyoendelea kwa jamii ya wafugaji nchini, hususan katika Mkoa wa Katavi, ukienda Kagera, Kigoma, Tabora na Morogoro; katika taarifa zangu hapa nina baadhi ya majina ya baadhi wananchi ambao wamepata madhara hayo kwa kuuawa lakini pia kwa kutozwa faini zaidi ya shilingi milioni 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Morogoro, Katavi kwa ujumla wake pamoja na Geita kuna majina ya wafugaji, mmojawapo anaitwa Luhende Ndakama, alitozwa shilingi milioni 50, pia kuna Masanja Ngola ametwozwa shilingi milioni 36, vilevile kuna Bugadi Darushi ambaye ametozwa shilingi milioni 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako sambamba na Wabunge, Serikali inasema nini kuhusiana na mauaji, uonevu, manyanyaso na kutozwa faini holela zinazofanyika katika Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja na Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae Waheshimiwa Wabunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Rhoda Kunchela akiomba mwongozo wa hiki kiti kwa maelezo hayo aliyoyatoa, halafu akatupeleka kwenye kanuni ya 47 akitaka bado mwongozo huo huo kwenye matumizi ya kanuni hii ya 47 na akatoa maelezo kwamba alichangia juzi na leo tena anazungumza kwa hayo mambo yanayotokea.

Waheshimiwa Wabunge matumizi ya Kanuni ya Mwongozo yanataka jambo liwe limetokea hapa Bungeni mapema. Kwa hiyo, jambo hilo halijatokea hapa Bungeni. *(Makofi)*

Jambo la pili kuhusu matumizi ya Kanuni ya 47 inataka jambo liwe la dharura na limetokea kwa namna ambayo haliwezi kushughuliwa katika utaratibu wa kawaida. Masharti ya matumizi ya Kanuni ya 47 yako kwenye Kanuni ya 48.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge yeyote anayetaka kutumia Kanuni 47 lazima awe amesoma Kanuni 48 na aone jambo analolisema kama linakidhi masharti yaliyowekwa chini ya kanuni ya 48.

Jambo hili alilosema Mheshimiwa Rhoda kuhusu watu kuuawa na anasema anayo majina hapo, hajasema wanauwa na nani, lakini kwa sababu wanauwa maana yake siyo kifo cha kawaida. Lakini pia anazungumza watu wanapata manyanyaso ya faini, sasa sijajua ni zile faini ndiyo zinazowafanya wafariki pengine ama kuna tukio lingine linalowafanya hawa watu wafariki mpaka kuwaita wameuawa. Serikali iko hapa na imesikia na jambo hili pamoja na uzito wake wote si jambo la dharura, linaweza kufanyiwa kazi katika utaratibu wa kawaida uliopo. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea.

Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

**NA**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA YA MAENDELEO YA JAMII**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitamuita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, namuona Makamu Mwenyekiti karibu sana.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020. Kwa sababu ya suala

la muda naomba ripoti yangu yote iingezwe kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati, kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu taarifa ya mwaka kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Taarifa hii ya kipindi cha mwaka 2019 na mwaka 2020 ni kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliotumika kutekeleza majukumu ya Kamati; taratibu zifuatazo zimekuwa zikitumika katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake:-
(a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi mbalimbali ili kupata taarifa zake;

(b) Kufanya ziara ili kukagua shughuli zinazozekelezwa katika kipindi hicho; na

(c) Kushiriki semina na warsha mbalimbali zilizohusu masuala ya UKIMWI na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Kamati; Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania; katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI katika Halmashauri nyingi nchini. Hali hii inasababisha mkanganyiko katika matumizi ya takwimu hizo na hivyo kusababisha vikwazo kwa watumiaji na wafanya maamuzi katika kujenga hoja na kutekeleza wajibu wao.

(b) Ufinyu wa bajeti na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Serikalini ambapo kwa sasa zaidi ya asili 90 ya bajeti ya Tume inategemea fedha za wafadhili wa nje hali inayopunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI *(AIDS Trust Fund- ATF);* takwimu zinaonesha kuwa, zaidi ya asilimia 90 ya gharama za UKIMWI Kwa mwaka zinafadhiliwa na wadau wa maendeleo wa Serikali ya Marekani na Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria *(Global Fund).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua nzuri ya kuanzisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI tangu mwaka 2015 mpaka sasa serikali haijaweza kubainisha njia bora ya utatuzi ingawa Kamati imekuwa ikitoa taarifa mara kwa mara kuhusiana na suala hili.

Serikali kwa upande mwingine imekuwa ikitenga fedha katika bajeti kuu kwa ajili ya Bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 shilingi bilioni mbili zilitengwa kwa ajili hiyo. Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, bado kiwango kinachotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji na pia utekelezaji wa utoaji wa fedha hizo bado ni wa kiwango cha chini. Kwa sababau hiyo, Serikali inatakiwa kufanya uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato vya uhakika kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; katika utekelezaji majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti Kupambana na Dawa na Kulevya, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Kukosekana kabisa kwa fedha za miradi ya maendeleo ni tatizo kubwa ikizingatiwa kuwa ajenda ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyochukuliwa kwa sasa.

(b) Kutokuwa kwa Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya ni suala lenye uzito mkubwa na hivyo linahitaji msukumo wa ziada.

(c) kukosekana kwa mfuko maalum kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa dawa za kulevya. Kwa sababu hiyo kunakua na upungufu wa mwitikio wa Kitaifa wa kupambana na tatizo hilo, hii ni pamoja na kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevya kama ilivyofanyika kwa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za umma za kisekta zinazotekeleza sera za UKIMWI na dawa za kulevya:-

(a) Wizara ya Fedha na Mipango; Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu chanzo mahususi cha fedha kwa ajili ya kuwezesha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na mkakati wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ujumla kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI na uratibu wa msamaha wa kodi kwa miradi inayofadhiliwa na *Global Fund, PEPFAR* na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaona upo muhimu Serikali kuainisha na kutekeleza chanzo mahsusi cha upatikanaji wa fedha za ndani. Jambo hili litasaidia kutoa hamasa kwa sekta binafsi na wadau wengine wa ndani katika kuchangia mfuko wa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha taarifa kuhusu uratibu wa msamaha wa kodi kwa miradi inayofadhiliwa na *Global Fund, PEPFAR* na wadau wengine. Kamati imebaini kutokuwepo kwa mgongano wowote wa kisheria kuhusiana na msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, kumekuwa na tofauti ya uelewa wa sheria baina ya Wizara ya Fedha na wadau wa UKIMWI hivyo Kamati inashauri elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mkemia Mkuu wa Serikali; Kamati ilikutana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mkemia Mkuu wa Serikali ili kujadili utekelezaji wa kuhusu majukumu yao katika kupambana na madawa ya kulevya nchini, mafanikio, changamoto na hatua za kukabiliana nazo. Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni msimamizi wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani. Lengo kuu la sheria hii ni kusimamia uzalishaji, usafirishaji, uingizaji ndani ya nchi, utoaji nje ya nchi, uhifadhi na uteketezaji wa kemikali na usimamizi wa masuala yote yanayohusu kemikali. Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu inawajibu wa kusimamia utoaji wa huduma za maabara za sayansi jinai, vinasaba vya binadamu na kemia ikijumuisha usajili, ukaguzi, ufutaji wa usajili na kusimamisha huduma kwa muda wa maabara hizo kwa mujibu wa sheria. Mamlaka ya Mkemia Mkuu na Mamlaka ya Dawa za Kulevya zimeendelea kufanya kazi kwa kushirikiana ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi, usimimamizi na udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa za kulevya kwa kufanya operesheni za pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya zimeendelea kushirikiana na taasisi nyingine zikiwemo Jeshi la Polisi katika maeneo ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za kemikali bashirifu zinazoingia nchini kila mwezi kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Pamoja na mawasilisho mazuri ya taasisi hizo, Kamati imebaini ipo haja ya Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sheria Na.1 ya mwaka 2003 ya *TMDA* hususani kifungu cha 5(1) kuiwezesha *TMDA* kudhibiti kemikali ambazo zinatumika kama malighafi kwenye utengenezaji wa dawa zilizo na asili ya tiba pamoja na kuwianisha na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani. Kamati inaona kuwa marekebisho hayo yataziwezesha kutekeleza majukumu yake bila muingiliano na *TMDA* kama ilivyo sasa, pia ni vizuri mchakato huo ukaharakishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa usimamizi wa Sheria ya UKIMWI mahali pa kazi kwa Wizara na Idara zote za Serikali pamoja na magonjwa yasiyoambukiza; Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Watumishi wengi wa taasisi za umma hawajitokezi katika mazoezi ya upimaji pindi yanapoandaliwa. Kamati inaona ipo haja ya kuongeza msukumo katika suala hili.

(ii) Wizara zote za taasisi nyingine za umma zinatenga fedha za VVU katika *objective A* hii katika mpango wa muda wa kazi wa matumizi ya fedha. Hata hivyo Kamati imebaini kwamba fedha hizo hazitumiki kwa kazi iliyokusudiwa na inapofika mwisho wa mwaka zinabadilishwa matumizi.
(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Ufundi; Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu na Ufundi kuhusu mikakati ya kukabiliana na mapambano ya UKIMWI na dawa za kulevya katika vyuo vya elimu ya juu. Kamati ilibaini mambo yafuatayo; kwa mujibu wa utafiti wa *Tanzania HIV Impact Survey* ya 2017, takwimu zilionesha kuwa asilimia 40 ya maambukizi mapya yapo katika umri wa miaka 15 hadi 24 na asilimia 80 ya hao ni wasichana. Kwa kuwa kundi la vijana walio katika umri huu ni kubwa na kwa kiwango kikubwa wako katika shule za sekondari na vyuo, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuweka juhudi kubwa na kuanzisha mkakati mahsusi wa kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI katika taasisi za elimu. Kwa mfano, kwa ngazi ya shule za sekondari ipo haja ya kujumuisha afua ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike kama njia mojawapo ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; kwa mujibu wa taarifa za wizara pamoja na Shirika la Afya Duniani bado tatizo la *TB* ni kubwa hapa nchini na lina muingiliano mkubwa na maambukizi ya VVU. Kwa mujibu wa taarifa inakadiriwa kuwa watu 142,000 waliogundulika na *TB* mwaka 2018 hapa nchini.

Kamati inaishauri Serikali kwamba ni muhimu kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya *TB* sambamba na kuzishirikisha sekta binafsi na asasi za kijamii ili kupanua uhamasihaji. Aidha, ni muhimu kuweka msukumo zaidi katika suala la uwajibikaji wa kisiasa wa kuongeza mapambano ya *TB* kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi chini kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha *TB* inakuwa ni ajenda ya kudumu kwenye mikutano ya kisiasa na ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 wa mchakato wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020; Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa maoni na ushauri ilioutoa kuhusu bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya taasisi hizo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) Toleo la Januari, 2016, mnamo tarehe 30 na 31 Machi, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania; upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 Tume ilitengewa fedha kiasi cha shilingi 12,909,431,000; kati ya fedha hizo shilingi 2,609,431,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Februari 2019 Tume ilipokea kiasi cha shilingi 10,477,721,649.96 sawa na asilimia 81 ya fedha zote zilizotakiwa kutolewa na Serikali kwenda katika Tume hii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikisha upelekaji wa fedha kwa kiwango kinachoridhisha. Hata hivyo Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali kuongeza kiwango cha upelekaji wa fedha zilivyoidhinishwa na Bunge kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Kamati inaona kwamba utekelezaji wa shughuli za Tume kwa kiasi kikubwa unategemea sana fedha kutoka kwa wafadhili. Kutokana na hali hiyo ni dhahiri kuwa endapo ufadhili huu utakoma basi Tume itashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaiomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha hasa za ndani kwa Tume ili iweze kukamilisha utekelezaji wa shughuli zake kama zilivyopangwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* Fungu 92 iliomba jumla ya kiasi cha shilingi 8,767,193,747.000 ikiwa ni makadirio ya matumizi yake. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 5,956,634,747 sawa na asilimia 67 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi 2,812,559,000 sawa na asilimia 32 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI - Fungu 92 haikuwa na makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge kama unavyoona kwenye Jedwali Namba 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Fungu 91; uchambuzi wa makadirio ya matumizi; kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilikadiriwa kufanya matumizi ya kiasi cha shilingi 7,592,818,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, kati ya fedha hizo shilingi 4,948,552,000 sawa na asilimia 65 ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 2,644,266,000 sawa na asilimia 35 ni kwa ajili ya mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi 1,837,717,000 sawa na asilimia 32 ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haikutengewa kabisa fedha za miradi ya maendeleo. Kamati inasisitiza kwamba ajenda ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyotafsiriwa. Ni maoni ya Kamati kuwa miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika na fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha warahibu kiuchumi kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, stadi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya na kuikinga jamii ili isishiriki katika njia yoyote ya matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; kutokana na shughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari, 2019 hadi Januari, 2020, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania *(TACAIDS)*; upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI; kwa kuwa kamati imebaini kuwa mpaka sasa asilimia kubwa bajeti ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imekuwa ikitegemea fedha za wahisani.

Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni mbili tu sawa na asilimia 32 ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tume na hakuna fedha ambazo zimetolewa.

Na kwa kuwa kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI ikizingatiwa kwamba baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI kwa Tanzania. Kupunguzwa kwa fedha hizo kuna athari kubwa katika mipango iliyokuwa itekelezwa katika kupambana na UKIMWI nchini.

Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi wake. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vya kujiwezesha kutenga fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha tozo kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa *(ATF);* Kwa kuwa kamati imebaini kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, changamoto kubwa imekua ni kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za UKIMWI. Mfuko wa UKIMWI *(ATF)* lengo lake ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na janga hili.

Na kwa kuwa kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mapambano endelevu dhidi ya maambukizi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI ambayo yanahitaji rasilimali fedha za uhakika za kutosha.

Kwa hiyo basi, kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kuainisha na kutekeleza chanzo mahsusi cha upatikanaji wa fedha za ndani ili kuruhusu hamasa kwa Sekta binafsi na wadau wengine wa ndani katika kuchangia *ATF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali za UKIMWI; kwa kuwa afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana na ubora wa takwimu zinapatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali, na kwa kuwa kuna upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI; kwa hiyo basi, kamati inashauri Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS),* Wizara ya Afya na TAMISEMI kuimarisha usimamizi ikiwa wa ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya takwimu kwa ngazi za Halmashauri na vituo vya afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza mpango mkakati wa kimataifa wa kudhibiti na kupambana na UKIMWI wa 90-90-90.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI kuhusiana na umri wa mtu kuweza kupima vvu na upimaji wa mtu binafsi; kwa kuwa Serikali imefanya mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI kwa kuboresha suala la umri wa ridhaa ya kupima UKIMWI ikiwa ni hatua za kuboresha upatikanaji wa huduma za VVU; na kwa kuwa takwimu zinaonesaha kuwa umri unaochangia maambukizi ya VVU kiasi kikubwa ni vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 mpaka 24; kwa hiyo basi, kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zilizofanyika za mabadiliko katika Sheria ya UKIMWI ili kuzingatia mahitaji mapya kwa mujibu wa takwimu. Hata hivyo

Kamati inasisitiza utekelezaji wa haraka wa marekebisho hayo ya sheria sambamba na ufuatiliaji na tathimini ya uhakika juu ya matokeo ya mabadiliko hayo ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya UKIMWI ili kuimarisha Mapambano ya UKIMWI nchini ili yaendane na utekelezaji wa malengo ya kimataifa ya kutokomeza UKIMWI ya 90-90-90; kwa kuwa Tanzania inaendelea kutekeleza awamu ya kwanza ya malengo na mkakati wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na masuala ya UKIMWI *(UNAIDS)* ambalo limeweka malengo ya kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2020 ambayo yanajulikana kama 90-90-90. Malengo haya yanasisitiza kuwa ifikapo mwaka 2020 asilimia 90 ya waliokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU wajue hali zao kiafya, asilimia 90 ya watakaopima na kukutwa na maambukizi ya VVU wapate dawa na asilimia 90 wa waliopo kwenye tiba wawe na kiwango kidogo cha virusi kwenye damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa takwimu zinaonyesha utekelezaji wa mkakati huu wa 90/90/90 nchini hauna uwiano lingalifu, kati ya 90 ya kwanza Tanzania ina asilimia 61, 90 ya pili asilimia 93 na 90 ya tatu ina asilimia 87. Hivyo Tanzania ina alama za chini katika 90 ya kwanza ikizingatiwa kuwa 90 ya kwanza ndio msingi wa mafanikio na kutokemeza UKIMWI nchini. Kwa hiyo basi Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufanya mabadiliko ya kisera na sheria pale inapodhihirika kwamba kuna mahitaji hayo ili kuzingatia mahitaji mapya kwa mujibu wa takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afua za UKIMWI na Madawa ya Kulevya Shuleni. Kwa kuwa takwimu za Tanzania *HIV Impact Survey* ya mwaka 2017 zinaonesha kuwa asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 na asilimia 80 ya maambukizi hayo ni miongoni mwa wasichana; na kwa kuwa Kamati imebaini kutokuwepo mkakati wa uratibu na usimamizi wa mapambano dhidi ya UKIMWI na matumizi ya madawa ya kulevya shuleni na hakuna hatua madhubuti zinazoonekana kutekeleza kulingana na miongozo iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha suala la kutekeleza afua za kudhibiti dawa za kulevya na UKIMWI limebaki kuwa ni suala la ziada bila msukumo, mipango, bajeti na bila rasilimali fedha. Kwa hiyo basi Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka za kuhakikisha shule zote za msingi na sekondari zinaratibu, kutekeleza na kusimamia suala la elimu ya afya ya uzazi, jinsia, *VVU*, UKIMWI pamoja na dawa za kulevya ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Umma Kutokuzingatia Kikamilifu Mwongozo wa Utumishi wa Umma Kuhusu Masuala ya UKIMWI katika Kutekeleza Afua za UKIMWI Mahala pa Kazi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza. Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa baadhi ya taasisi za umma kutokuzingatia ipasavyo matakwa ya mwongozo wa utumishi wa umma kuhusu masuala ya UKIMWI katika utekelezaji wa afua za UKIMWI mahala pa kazi na magonjwa yasiyoambukiza katika wizara na taasisi za umma; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika wizara nyingi za umma hakuna mwamko wa watumishi kupima maambukizi ya VVU. Watumishi hawako tayari kuweka wazi hali ya afya zao ili kuweza kunufaika na huduma za walioathirika. Bajeti zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza afua za UKIMWI ni kiasi kidogo na hazitolewi kwa wakati na pale zinapotolewa hazitumiki. Na kwa kuwa mwenendo huu hukosekana chachu ya mapambano dhidi ya UKIMWI mahala pa kazi ni hatarishi kwa ustawi wa taifa.

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha wizara na Taasisi zote za Serikali zinaratibu na kutekeleza mwongozo wa utumishi wa umma kuhusu afua za UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza kama ilivyoainishwa katika mwongozo kwa kutenga bajeti ya kukidhi mipango na mikakati ya kupambana na UKIMWI mahala pa kazi na magonjwa sugu. Kuhamasisha watumishi kupima maambukizi ya VVU kubuni mbinu za kuwafanya watumishi

kuweka wazi hali zao za afya ili watakaoonekana wana maambukizi waweze kuanza kutumia dawa. Aidha Kamati inashauri Kamati za UKIMWI katika wizara na taasisi m,balimbali za umma ziimarishwe ili zitekeleze majukumu yake pamoja na kutakiwa kutoa taarifa kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na kitengo maalum ndani ya *TACAIDS* kinachoshughulikia na uratibu wa shughuli za UKIMWI ndani ya Wizara na Taasisi za umma kiimarishwe na kusimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Athari za Kutotenga Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Kwa kuwa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya imekuwa haitengewi bajeti kwa ajili ya maendeleo; mojawapo ya athari za kutotenga fedha za maendeleo ni kukosekana na maabara ya Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya kwa ajili ya uchunguzi.

Na kwa kuwa maabara inayotumika mpaka sasa ni maabara ya mkemia mkuu wa Serikali ambayo ina vipaumbele vingine katika utekelezaji wa shughuli zake si lazima vipaumbele vya Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya viwiane pamoja na kwamba ahadi ya wafadhili ya kujenga maabara kwa ajili ya mamlaka lakini utekelezaji wa ahadi umekuwa ukiahirishwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukosefu wa fedha za maendeleo umepelekea kasi ndogo au kukosekana kwa mfumo maalum kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa madawa ya kulevya na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia kumudu maisha na kuachana na biashara na matumizi ya madawa hayo.

Kwa hiyo basi; Kamati inashauri Serikali kwamba fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa mamlaka kuanza kujenga mifumo itakayojumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya na hivyo kuiwezesha Mamlaka kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa miradi ya maendeleo inayoweza kutekelezwa na fedha za maendeleo ni pamoja na kuwaweza waraibu kiuchumi kwa kuwaunganisha kuwapa mbinu za ujasiriamali mikopo nafuu ya biashara stadi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya kufanya urahabishi, elimu ya madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa wananchi; ili waweze kushiriki kikamilifu katika kupambana na kudhibiti dawa za kulevya kwani vita hii ni ngumu na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kujenga na Kuimarisha Mifumo ya Kitaasisi katika Utekelezaji wa Shughuli za Masuala ya Dawa za Kulevya. Kwa kuwa Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya udhibiti na upambanaji wa dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo taasisi zisizo za Serikali; na kwa kuwa Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya *NGOs* na taasisi zinazojihusisha na masuala ya dawa za kulevya nchini ambazo hazina muundo na mifumo rasmi ya jinsi gani zinawasaidia watumiaji wa dawa za kulevya kwenye jamii. Baadhi zikitekeleza shughuli zake kwa kuwabagua watumiaji wa dawa hizo mfano zinazowahudumia wamawake wale wanaojidunga kwa sindano na mara nyingine wale wanaotumia kwa kuvuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi Kamati inashauri kuwa kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo chake cha uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali waongeze kasi ya

kukamilisha zoezi la utambuzi na uratibu wa asasi zote zinazojishughulisha na dawa za kulevya. Hii itasaidia malengo yao pamoja na kazi zinazofanywa na asasi hizo na kuwekea mifumo rasmi na utekelezaji wa shughuli zao ili kuhakikisha kuwa walengwa wanafaidika na uwepo wa asasi hizi kwani fedha zinatolewa ni kwa jina la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokuwepo kwa Sera ya Dawa za Kulevya. Kwa kuwa mpaka sasa Tanzania haina sera ya taifa ya kupambana na dawa za kulevya ambayo kwa umuhimu wake ingeimarisha mapambano yaliyopo dhidi ya matumizi ya biashara ya dawa za kulevya; na kwa kuwa sera ina umuhimu mkubwa katika kuweka misingi na mwelekeo wa taifa katika vita dhidi ya madawa ya kulevya kwa ujumla wake; Kwa hiyo basi Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya mchakato wa kuandaa sera ya taifa ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya nchini. Suala la madawa ya kulevya kuwa ajenda ya Kamati za UKIMWI katika halmashauri na manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa halmashauri na manispaa nchini zimekuwa zikiratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika halmashauri na manispaa kwa ufanisi wa kutosha; na kwa kuwa Kamati katika ufatiliaji wa shughuli za mapambano dhidi ya madawa ya kulevya katika ngazi, halmashauri na manispaa umeonesha kutokuwepo utaratibu au mfumo rasmi wa namna ya kushughulikia suala la madawa ya kulevya;

Kwa hiyo basi Kamati inashauri kuwa ili kuwezesha utekelezaji wa jukumu hili kwa ufanisi Serikali ikamilishe mwongozo na hadidu rejea za namna Kamati hizi zitakavyotekeleza jukumu la kupambana na dawa za kulevya katika ngazi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Napenda kukushuru tena kwa kunipa fursa hii ili kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari 2020. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Pamoja na yeye namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi ndugu Gerald Magili, makatibu wa Kamati hii Ndugu Happiness Ndalu, Asia Msangi pamoja na msaidizi wa Kamati ndugu Paul Chima kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii k umpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb) na Mheshimiwa Naibu Waziri Anthony Mavunde na Stella Ikupa. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Dokta Leornard Maboko na Kaimu Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ndugu James Willbard Kaji na watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mar azote walipohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru na kuwapongea Waziri, Naibu Waziri, na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya sambamba na watendaji wao wote kwa kutoa ushirikiano mkubwa wakati wote wa shughuli za Kamati na namna wanavyoonesha dhamira ya kutatua matatizo yanayowakabili Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa pia napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote kwa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa sana katika kuhakiksiha Kamati inaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo mbele ya Bunge lako

Tukufu; sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kutoa hoja.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**
**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati, kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.Taaria hii ya kipindi cha mwaka 2019/2020 ni kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, hivyo imegawanyika katika sehemu kuu tatu (3). Sehemu ya Kwanza ni ya Utangulizi unaofafanua muundo, majukumu pamoja na maelezo ya jumla kuhusu utekelezaji shughuli za Kamati. Sehemu ya Pili ni Uchambuzi na Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Katika Sehemu ya Tatu Kamati imetoa mapendekezo na hitimisho.

1.1 **Muundo na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI inasimamia shughuli za Taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kusimamia majukumu ya Taasisi hizo, Kanuni hiyo pia imeipa Kamati jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya. Hivyo Kamati inatekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote Tanzania Bara;

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa Dawa za Kulevya;

c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti dawa za kulevya; na

d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

e) Hivi sasa Kamati imeongezewa jukumu jipya la kushughulikia Kifua Kikuu kwa kuwa ni mojawapo ya maradhi nyemelezi ambayo kwa mujibu wa takwimu ni ugonjwa pacha na Ugonjwa wa UKIMWI.

### 1.2 **Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** taratibu zifuatazo zimekuwa zikitumika katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake:-

(a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi kwa kuwaomba kufika mbele ya Kamati ili kutoa taarifa juu ya jambo au suala mahususi ambalo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa Watendaji wa Wizara na Taasisi hizo;

(b) Kufanya ziara ili kukagua shughuli zinazozekelezwa katika kushughulikia masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya

(c) Kushiriki semina, tamasha na warsha mbalimbali zilizohusu Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya; na

(d) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi hizo.

### 1.3 **Shughuli zilizotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilikuwa na shughuli zifuatazo:-

(a) Kufuatilia utekelezaji wa Afua mbalimbali za UKIMWI na Dawa za Kulevya katika Wizara na Taasisi balimbali;

(b) Kupata mafunzo mbalimbali kuhusiana na masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya;
(c) Kufanya ziara za Kamati katika sekta mbalimbali zinazojihusisha na mapambano ya UKIMWI na Dawa za Kulevya kwa lengo la kuona na kutoa ushauri kuhusiana na maeneo hayo.

(d) Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(e) Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 **UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inaelezea utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020 kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 hususan Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, Kamati iliandaa Mpango Kazi uliotekelezwa katika kipindi hicho ambao Matokeo ya utekelezaji wake yamefanyiwa uchambuzi katika Sehemu hii.

## 2.1 KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilianza utekelezaji wa majukumu yake kwa kufuatilia kwa ukaribu utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini yake pamoja na utekelezaji wa Sera na Mipango inayohusu Udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevya katika Wizara na Taasisi za Umma nchini kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

a) Upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI katika Halmashauri nyingi nchini. Halihii inasababisha mkanganyiko katika matumizi ya takwimu hizo na hivyo kusababisha vikwazo kwa watumiaji na wafanya maamuzi katika kujenga hoja na kutekeleza wajibu wao.

b) Ufinyu wa Bajeti na ucheleweshwaji wa fedha kutoka serikalini ambapo kwa sasa zaidi ya asili 90 ya bajeti ya Tume inategemea fedha za wafadhili wa nje hali inayopunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

### 2.1.2 MFUKO WA TAIFA WA KUDHIBITI UKIMWI (AIDS TRUST FUND (ATF)

(a) **Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa, zaidi ya asilimia 90 ya gharama za UKIMWI Kwa mwaka zinafadhiliwa na Wadau wa Maendeleo wa Serikali ya Marekani na Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria *(Global Fund)*. Pamoja na hatua nzuri ya kuanzisha mfuko wa udhamini wa UKIMWI (ATF) tangu mwaka 2015, mpaka sasa serikali haijaweza kubainisha njia bora ya utatuzi ingawa kamati imekuwa ikitoa taarifa mara kwa mara kuhusiana na wa suala hili

(b) **Mheshimiwa Spika**, serikali kwa upande mwingine, imekuwa ikitenga fedha katika bajeti kuu kwa ajili ya Bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 shilingi milioni 2,000 zilitengwa kwa ajili hiyo. Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, bado kiwango kinachotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji na pia utekelezaji wa utoaji wa fedha hizo bado ni wa kiwango cha chini. Kwa sababau hiyo Serikali inatakiwa kufanya uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato vya uhakika kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali iwekeze nia na jitihata katika kufanikisha jambo huli kwani uwepo wa vyanzo vya uhakika kwa ajili ya mfuko huu kutafungua milango kwa wadau wengine wenye nia na maslahi na suala husika kujitokeza na kuunga mkono jitiihada za serikali. Kwa mfano, ipo fursa kwa sekta binafsi ya kujumuisha nguvu za pamoja kwa ajili ya kuchangia katika mfuko wa udhamini wa UKIMWI kwa namna mbalimbali ikiwemo kuwekeza katika miradi ya pamoja ambayo sehemu ya faida itakuwa chanzo cha mapato kwa ajili ya Mfuko.

(c) Wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kunakuwa na maambukizi ya VVU kwa viwango tofauti kulingana na aina na ukubwa wa mradi husika. Aidha, kwa mujibu wa maelezo ya Wizara ya Fedha kwa Kamati wakati wa kikao cha pande hizo mbili, Kamati inazo taarifa za kuwepo chanzo chenye kuonesha **matumaini ya uwezekano** cha kutunisha mfuko wa udhamini wa UKIMWI. Chanzo hicho ni mfuko wa fedha za makampuni ambazo hazijadaiwa kwa zaidi ya miaka 15 zinazotokana na pesa za wateja waliojiunga ambazo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni fedha hizi huchukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania. Ni maoni ya

kamati kuwa ipo haja ya Serikali kufanya uchambuzi wa kina kwa chanzo hiki ili uamuzi stahiki ufanyike kwa haraka kuhusiana na uwezekano wa chanzo hiki kutumika kama moja ya vyanzo vya uhakika kwa ajili ya mfuko wa udhamini wa UKIMWI.

### 2.1.3 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti Kupambana na dawa na Kulevya, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Kukosekana kabisa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo ni tatizo kubwa ikizingatiwa kuwa ajenda ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyochukuliwa kwa sasa;

(b) Kutokuwepo kwa kwa Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya ni suala lenye uzito mkubwa na hivyo linahitaji msukumo wa ziada.;

(c) Kukosekana kwa Mfumo maalum kwa ngazi ya Jamii kwa ajili ya kuwatambua waraibu wa dawa za kulevya. Kwa sababu hiyo kunakua na upungufu wa mwitikio wa Kitaifa wa kupambana na tatizo hilo;hii ni pamoja na kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevya kama ilivyofanyika kwa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI;

(c) Kuwepo kwa baadhi ya NGOs na Taasisi zinazojihusisha na mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya nchini ambazo hazina muundo na mifumo rasmi kwa jinsi zinavyowasaidia waathirika wa dawa za kulevya.

### 2.1.4 TAASISI ZA UMMA ZA KISEKTA ZINAZOTEKELEZA SERA ZA UKIMWI NA DAWA ZA KULEVYA

#### (a) Wizara wa Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu chanzo mahususi cha fedha kwa ajili ya kuwezesha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) na mkakati wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ujumla kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI na uratibu wa msamaha wa kodi kwa Miradi inayofadhiliwa na Global Fund, PEPFAR na Wadau wengine. Waziri wa Fedha aliieleza Kamati kuwa, Serikali inaendelea kufanya juhudi za kutafuta vyanzo vya mapato endelevu kwa ajili ya kugharamia shughuli za Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF). Aidha, aliwajulisha kuwa suala hili limewasilishwa kwenye Kikosi Kazi cha Maboresho ya Mfumo wa Kodi *(Task Force on Tax Reforms)* ambacho kilifanyika mwaka 2019/2020. Kikao hicho kilipendekeza kutumia vyanzo vinne kama ifuatavyo:-

(i) Faida iliyopo kwenye Benki za Biashara kutokana na huduma za kibenki kupitia simu za mkononi. Hivyo, uamuzi wa kuzichukua ungekuwa kinyume cha taratibu za uendeshaji wa biashara na utunzaji wa amana za wateja katika soko la ushindani la fedha zitokanazo na miamala ya simu za mkononi. Hii ni kwa sababau uchambuzi wa kina umebaini kuwa fedha hizo ni mali ya wateja

(ii) Kutoza kodi ya zuio ya asilimia 10 kwenye faida na riba za miamala ya wateja wakati zinapohamishwa na kampuni za simu kutoka kwenye benki za biashara. Baada ya uchambuzi ilibainika kwamba, riba inayolipwa kwa benki za biashara kwenda kwa wadhamini wa makampuni tayari inatozwa kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 10. Hivyo, uamuzi wa kuongeza kodi ya zuio kwenye fedha hizo za riba wakati zinapokwenda kwenye akaunti za

wadhamini kwa ajili ya kugawanywa kwa wateja ni kinyume cha sheria kwa kuwa ingekuwa ni kutoza kodi ya aina moja mara mbili.

(iii) Fedha za makampuni ambazo hazijadaiwa kwa zaidi ya miaka 15 zinazotokana na pesa za wateja waliojiunga zinachukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha za Benki Kuu ya Tanzania. Uchambuzi wa kina ulibainisha uwepo wa uwezekano wa kukitumia chanzo hiki kwa ajili ya malengo yanayokusudiwa

(iv) Kuongeza viwango vya ada na tozo katika bidhaa na huduma mbalimbali vya mapato ikiwemo kuongeza ada na tozo katika bidhaa na huduma zinazoendeshwa nchini kwa ajili ya kuchangia kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI lakini bado haijafanikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona upo muhimu Serikali kuainisha na kutekeleza chanzo mahsusi cha upatikanaji wa fedha za ndani ili kuruhusu hamasa kwa Sekta binafsi na wadau wengine wa ndani katika kuchangia mfuko wa udhamini wa UKIMWI. Ushiriki wa wadau wengine ndani ya nchi ni jambo la muhimu kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa kuchelewa kufikia malengo husika endapo utekelezaji wa suala hili utaachwa kwa serikali pekee. Kwa upande mwingine kutokuwepo na chanzo mahsusi cha serikali hakutatoa fursa na hamasa kwa wadau wengine wa ndani ili kushiriki katika uchangiaji wa shuguli za UKIMWI hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Taarifa kuhusu Uratibu wa Msamaha wa Kodi kwa Miradi inayofadhiliwa na Global Fund, *PEPFAR* na Wadau wengine. Katika wasilisho hilo, aliainisha utaratibu wa msamaha wa kodi katika Miradi ya *PEPFAR* na *Global Fund* kama ifuatavyo:-

(i) Ununuzi wa bidhaa na huduma kwa Miradi inayofadhiliwa kupitia misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo, ikiwemo *Global Fund*, hunufaika na msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa njia ya Hati ya Msamaha (GN) kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 pamoja na marekebisho yake.

(ii) Sheria ya VAT, imempa Waziri wa Fedha na Mipango mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi hiyo kwa njia ya Hati ya Msamaha (GN) kwenye ununuzi wa bidhaa au huduma ndani ya nchi au bidhaa zinazoingizwa nchini na taasisi za Serikali *(Government Entities)*. Msamaha huo hutolewa katika utekelezaji wa Miradi kwa kutumia fedha za Serikali, mikopo au misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo pale mikataba husika baina ya Serikali na washirika hao inapokuwa na kifungu kinachoainisha utoaji wa msamaha wa VAT.

(iii) Mkataba baina ya Serikali na *Global Fund* umeainisha utoaji wa msamaha wa VAT, na hivyo hunufaika na msamaha wa VAT kupitia utaratibu ulipo. Aidha, dawa na bidhaa za afya zimesamehewa kodi kwa mujibu wa sheria kwa kuzingatia orodha inayoidhinishwa na Waziri mwenye dhamana wa Afya**.**

(iv) Kwa utaratibu unaotumika sasa miradi inayofadhiliwa na The U.S. President's Emergency Plan for AIDS Relief - PEPFAR haikidhi vigezo vya kupata msamaha wa VAT kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria hiyo kwa kuwa bidhaa/vifaa vinavyoingizwa nchini kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali huingizwa na Taasisi zisizo za Serikali (NGOs) na Taasisi za Kiraia (CSOs). Aidha, chini ya PERFAR kumekuwa na Taasisi nyingi zisizo za Kiserikali zenye mikataba na PERFAR isiyoainisha utoaji wa msamaha wa VAT.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kutokuwepo kwa mgongano wa kisheria na kimkataba kuhusiana na msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo kumekuwa na tofauti wa uwelewa wa sheria baina ya Wizara ya fedha na wadau wa UKIMWI,

hususani Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 2014 (*The Value Added Tax, 2014*) kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2017 (*The Written Laws* [*Miscellaneous Amendments*] Act,2017 tafsiri ya sheria hiyo ni kwamba inazuia mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGOs, CBOs etc) kupewa msamaha wa kodi, maombi ya msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani yamekuwa yakiwasilishwa na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofadhiliwa na *PEPFAR na Global Fund*. Hivyo basi utoaji wa msamaha huo umekuwa hautekelezeki.

Kwa upande mwingine kumekuwepo na kutokutolewa taarifa kwa ukamilifu au kwa uwazi kutoka Wizara ya Fedha kwenda kwa wadau wa masuala ya UKIMWI juu ya tafsiri hii ya sheria. Kwa sababu hiyo wadau wamekuwa wakikumbana na vikwazo mbalimbali vya kiutendaji kama mbadala wa matakwa ya kisheria yaliyoelezwa hapo juu na hivyo kumekuwepo na upoteaji mkubwa wa rasilimali muda, fedha na ufanisi kwa muda mrefu. Kamati inashauri elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wadau.

Aidha, Kamati imebaini kutokuwepo kwa majadiliano ya kutosha baina ya Wizara ya Afya na wadau wa UKIMWI na hivyo kusababisha uwepo na masuala mengi ambayo yanaibuavikwazo kutoka kwa kila upande baina ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii kwa upande mmoja na kwa wadau wanaotekeleza afua za UKIMWI kwa upande mwingine.

Vivyo hivyo yako masuala mengi yanayoleta vikwazo kwa kila upande baina ya Wizara ya fedha kwa upande mmoja na wadau wa UKIMWI kwa upande mwingine. Kamati imebaini kuwa kuna kukosekana kwa fursa ya kutosha na ya kiushirika ya kujadili masuala hayo na badala yake uchambuzi usiokwisha sambamba na kuvutana kwenye uendelevu kunapewa nafasi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, sio kazi ya Bunge kuingia katika ngazi hiyo ya utendaji lakini ni wajibu wa Kamati ya bunge kuisisitiza Serikali na wadau wa UKIMWI kwamba tija kwa watanzania itapatikana pale tu ambapo pande hizo mbili zitaweza kukaa kwenye meza ya mazungumzo kwa ushirika na kukubaliana namna sahihi ya kutatua matatizo yaliyopo. Kamati, inasikitishwa na hali inayoendelea na inatarajia kuwa ufumbuzi wa suala hili la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani utapatikana hivi karibuni. Kamati inaisisitiza Serikali hasa kupitia Wizara ya Fedha na Wizara ya Afya kuchukua nafasi ya uongozi katika suala hili na hivyo kuhakikisha sheria za nchi zinafuatwa na pia kulinda maslahi ya Taifa lakini kwa upande mwingine kutoa fursa ya kutosha ya mashauriano na wadau ili kutokuwa kikwazo kwa wadau hao wa masuala ya UKIMWI katika kutimiza wajibu wao, ambao upo kisheria pia.

### (b) **Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mkemia Mkuu wa Serikali (CGC)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mkemia Mkuu wa Serikali (CGC) ili kujadili Utekelezaji wa kuhusu majukumu yao katika kupambana na madawa ya kulevya nchini, mafanikio, changamoto na hatua za kukabiliana nazo. Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2017 ilianzisha Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ikiwa na lengo la kudhibiti na kupambana na matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya pamoja na jukumu la kufanya upelelezi unaohusisha sayansi jinai ambapo huenda sambamba na uchunguzi wa kimaabara kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Kuthibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kama ilivyofanyiwa marekebisho Mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni msimamizi wa Sheria ya Usimamizi na udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani. Lengo kuu la sheria hii ni kusimamia uzalishaji, usafirishaji, uingizaji ndani ya nchi, utoaji nje ya nchi, uhifadhi na uteketezaji wa kemikali na usimamizi wa masuala yote yanayohusu kemikali. Mkemia Mkuu inawajibu wa kusimamia Utoaji wa Huduma za Maabara za Sayansi Jinai, Vinasaba vya Binadamu na Kemia ikijumuisha usajili, ukaguzi, ufutaji wa usajili na kusimamisha huduma kwa muda wa maabara hizo kwa mujibu wa sheria. Mamlaka za Mkemia Mkuu na Mamlaka ya Kudibiti na Kupamba na Dawa za Kulevya zimeendelea kufanya kazi kwa kushirikiana ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi, usimimamizi na udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa za kulevya kwa kufanya operesheni za pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya zimeendelea kushirikiana na Taasisi nyingine zikiwemo Jeshi la Polisi katika maeneo ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za kemikali bashirifu zinazoingia nchini kila mwezi kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mkemia Mkuu zimekuwa zikishirikiana katika kufanya ukaguzi wa kemikali bandarini, viwanja vya ndege, mipakani, maghala yanayohifadhi kemikali na viwandani pamoja na kuvishirikisha vikosi kazi na vyombo vya ulinzi na usalama.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mawasilisho mazuri ya Taasisi hizo, Kamati imebaini ipo haja ya Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sheria Na.1 ya Mwaka 2003. ya TMDA hususani kifungu cha 5 (1) kuiwezesha TMDA kudhibiti kemikali ambazo zinatumika kama malighafi kwenye utengenezaji wa dawa zilizo na asili ya tiba (therapeutic effect) pamoja na kuwianisha na sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani. Kamati inaona kuwa, marekebisho hayo yataziwezesha Mamlaka ya Mkemia Mkuu kutekeleza majukumu yake bila muingiliano na TMDA kama ilivyo sasa. Pia ni vizuri mchakato wa kubadilisha sheria hii uharakishwe ili Taasisi hizi mbili ziweze kutekeleza wajibu wao kwa urahisi na kufanikisha malengo waliojiwekea katika kupamba na vita dhidi ya madawa ya kulevya. Aidha, mabadiliko haya yatakuwa chachu katika ukuzaji wa uchumi na kuboresha mazingira bora ya biashara kwa wadau wanaohusika na biashara za aina hiyo.

(c) **Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu Utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Sheria ya UKIMWI mahali pa kazi kwa Wizara na Idara zote za Serikali pamoja na Utekelezaji wa afua za UKIMWI mahala pa kazi pamoja na magonjwa yasiyoambukiza Mwongozo huo hutekelezwa kupitia Idara yake ya Utawala na Rasilimali Watu, na imekuwa ikitekeleza afua hizo kwa kuendesha zoezi la upimaji wa afya kwa watumishi wa Wizara zote. Vilevile idara hiyo inafanya uratibu wa uanzishwaji wa Kamati za UKIMWI mahali pa kazi katika Idara na Taasisi zake. Pamoja na hayo, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Asasi ya TAYOA, Idara pia inaendesha mafunzo kwa Kamati mbali katika Taasisi za Umma na uwekaji wa vifaa vya kuwekea mipira ya kiume (*Condom Dispenser*)

Wajumbe walijadili na kuibua hoja mbalimbali ambazo zilihitaji ufafanuzi, kisha kutoa Ushauri wa namna ya kuimarisha Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI kama ifuatavyo***:-***

Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Watumishi wengi wa taasisi za umma hawajajitokeza katika mazoezi ya upimaji pindi yanapoandaliwa. Kamati inaona zipo sababu ambazo zinazochangia watumishi wengi

kutojitokeza kupima ikiwa ni pamoja na kutokupata elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kupima.

(ii) Wizara zote na taasisi nyingine za umma zinatenga fedha za VVU katika *Objective A*" katika Mpango wa muda wa kati wa matumizi ya fedha (MTEF). Hata hivyo upo ushahidi kwamba fedha hizo hazitumiki kwa kazi iliyokusudiwa na inapofika mwisho wa mwaka fefdha hizo zinabadilishiwa matumizi.

(iii) Yako malalamiko kuhusiana na uwepo wa rushwa ya ngono inayotumika kuzuia baadhi ya haki katika utumishi wa umma.

(iv) Kamati imebaini hali ya utekelezaji hafifu wa uekelezaji wa Mwongozo wa masuala ya UKIMWI mahala pa kazi pamoja na magonjwa yasiyoambukiza. Hi ni pamoja na suala la utoaji wa fedha za kuhudumia watumishi waliojitokeza kuwa na VVU pamoja na uwasilishaji wa taarifa kuhusu namna Wizara hizo na taasisi walivyotekeleza afua za UKIMWI mahali pa kazi.

(v) Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa fedha ambazo zinazotolewa na Hazina kulinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Mikakati ya Afua za UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahali pa Kazi haikidhi mahitaji halisi ya Wizara.

(d) **Wizara ya Elimu na Ufundi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu na Ufundi kuhusu Mikakati ya Kukabiliana na Mapambano ya UKIMWI na Dawa za Kulevya katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Wasilisho lilieleza kwamba, katika kukabiliana na mapambano dhidi ya UKIMWI, Taasisi ya Elimu ya Juu imetoa elimu ya kuwajengea uwezo Waadili, Walezi na washauri nasaha kuhusu usimamizi na utoaji wa elimu ya afya ya uzazi, jinsia, VVU na UKIMWI pamoja na dawa za kulevya kwa wanafunzi. Lengo la elimu hiyo ni kuwajengea vijana uelewa kuhusu afya bora ili waweze kutoa mchango chanya katika maendeleo yao wenyewe na Taifa kwa ujumla. Aidha mikakati inayotekelezwa katika kukabiliana na maambukizi ya VVU na UKIMWI katika Taasisi za Elimu ya Juu ilielezwa.

Kufuatia Taarifa iliyowasilishwa hilo, Wajumbe walijadili na kuibua hoja mbalimbali ambazo zilihitaji ufafanunzi zaidi, kisha kutoa maoni Ushauri wa namna ya kuimarisha Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI kama ifuayavyo:-

(i) Kwa mujibu wa utafiti wa Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2017), takwimu zilionyesha kuwa **asilimia 40** ya maambukizi mapya yapo katika umri wa miaka 15-24, na **asilimia 80** ya hao ni wasichana. Kwa kuwa kundi la vijana walio katika umri huu ni kubwa na kwa kiwango kikubwa wako katika Shule za Sekondari na Vyuo, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuweka juhudi kubwa na kuanzisha mkakati mahsusi wa kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI katika Taasisi za Elimu. Ipo mifano katika baadhi ya nchi ambayo imeonesha mafanikio ya mkakati maalumu wa kukabiliana na tatizo la UKIMWI kwenye vyuo vya elimu ya juu ambapo Afrika ya Kusini ilitajwa kama moja ya mataifa yaliyofanya vizuri katika eneo hili. Kwa kuwa iko idadi ya kutosha ya wanafunzi wa shule za sekondari na hasa za kata ambao wanalazimika kuishi kwenye nyumba za kupanga karibu na maeneo yao ya shule kama mbadala wa kulazimika kusafiri mwendo mrefu, kila siku kwa ajili ya kuhudhuria masomo, na kwa kuwa hali hiyo inawaweka katika mazingira hatarishi kuhusiana na maambukizi yaVVU, Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa zilizopo za rasilimali fedha na utashi zinazoelekezwa katika masuala ya UKIMWI ambazo zinatolewa na wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi kukabiliana na ukosefu wa mabweni ya wanafunzi wa kike katika shule za kata. Suala la ukosefu wa mabweni hususani kwa wanafunzi wa kike lipewe mtazamo zaidi ya ule wa ndani ya Wizara

ya Elimu na kujumuisha masuala ya UKIMWI na mengineyo ili kukabiliana na tatizo hili kwa upana wake

(ii) Kamati inaona ili kupata takwimu sahihi za maambukizi ya VVU na UKIMWI katika shule za Sekondari na Vyuo, Wizara Elimu na Ufundi pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ziweke mikakati thabiti inayopimika kwa vitendo katika mapambano dhidi ya UKIMWI na Dawa za Kulevya katika Vyuo Vikuu na elimu ya Sekondari na Msingi.

(iii) Wizara ya Elimu na Taasisi zake ziboreshe ushirikiano na Taasisi za ndani na nje ya nchi katika kubadilisha uzoefu kuhusu mikakati ya kukabiliana na changamoto za masuala ya UKIMWI, afya ya uzazi, na Dawa za Kulevya. Adha, Wizara itafakari umuhimu wa kufanya tathmini ya uwezekano wa kuchukua uzoefu wa konga za watu wanaoishi na VVU na kuufanyia majaribio katika vyuo vya elimu ya juu. Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

(e) **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahala pa kazi pamoja na uratibu wa Asasi sizizo za Kiserikali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI kwenye ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji. Taarifa ya Wizara ilieleza Mikakati iliyopo na inayotekelezwa katika kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa jumla.Taarifa pia iliainisha malengo mahsusi ya Wizara, utekelezaji wake, mafanikio, pamoja na changamoto zilizopo katika kila hatua zinazochukuliwa. Aidha taarifa ilifafanua kuhusu uratibu wa asasi zisizo za kiserikali (NGOs) zinazotekeleza Afua za UKIMWI katika ngazi mbalimbai za Serikali za Mitaa.

Kufuatia Taarifa iliyowasilishwa, Wajumbe walijadili na kuibua hoja mbalimbali ambazo zilihitaji ufafanuzi, kisha kutoa Ushauri wa namna ya kuimarisha Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI kama ifuatavyo:-

i) Ni hatua gani zinachukuliwa na Wizara katika kuratibu na kusimamia upatikanaji wa lishe bora kwa wanafunzi walioathirika na VVU walio katika shule za sekondari, hususan za bweni.

ii) Ni vigezo gani vinatumika katika kugawa fedha za *Global Fund* katika Sekretarieti za Mikoa na Hamashauri. Kamati haikuweza kupata ufafanuzi kuhusu tofauti kubwa ya fedha za Global Fund zinazopelekwa katika Halmashauri mbalimbali. Ni muhimu kanuni za mgawanyo huo zikawa na uwazi zaidi kwa ajili ya ufanisi.

iii) Kamati inasisitiza kuwa ni vema Wizara ikaimarisha uratibu kwa kutambua Asasi gani inafanya nini, inafanya kazi wapi, kwa muda gani, kwa gharama kiasi gani na kwa matokeo gani. Aidha Wizara iwe na malengo na vipaumbele vya afua, kisha kuzitaka Asasi hizo kufuata Mpango wa Serikali katika kutekeleza Afua za UKIMWI, badala ya kila Asasi kutaka kutekeleza vile inavyojipangia yenyewe.

(f) **Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mpango wa Taifa wa Kudhitibi UKIMWI (NACP). Kamati ilibaini kuwa bado ipo changamoto ya ufuasi hafifu kwa matibabu kwa makundi machache ya wagonjwa hususani watoto. Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania haijafanikiwa kwa kiwango cha kutosha katika Mkakati wa 90 90 90 hususan kwenye 90 ya kwanza inayotaka asilimia 90 ya watanzania wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU wawe wamepima afya zao ifikapo Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Na Watoto kuhusu utekelezaji wa wa Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuuu na Ukoma Kwa ujumla,

Kamati ilibaini na kutoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

i) Kwa mujibu wa report ya WHO 2019 Tanzania inakadiliwa kuwa na watu **142,000** waliogundulika na TB mwaka 2018 ambapo ni sawa na watu **253** kwa kila Watanzania **100,000** wanakadiriwa kuwa waliougua ugonjwa wa TB mwaka huo. Katika kipindi hicho watanzania wapatao 22,000 walifariki dunia ambao kwa ugonjwa huo idadi ambayo ni sawa na vifo 60 vinavyosababishwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu pekee kwa siku. Aidha, Mikoa inayoonesha kuwa na ongozeko kubwa la wagonjwa wengi ni pamoja na Dar es Salaam, Iringa, Pwani, Arusha, Manyara, Njombe, Mtwara, Kilimanjaro, Shinyanga, Mbeya na Geita. Kamati inaishauri Serikali ni vizuri kuzishirikisha Sekta binafsi na Asasi za kijamii zote ili kupanua uhamasishaji kwa kuongeza wigo wa huduma hususani kwenye Mikoa yenye maambukizi makubwa kwa kutumia matangazo na jumbe za simu za mikononi. Aidha, ni muhimu kuweka msukumo zaidi katika suala la uwajibikaji wa kisiasa wa kuongeza mapambano ya TB kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi chini kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha TB inakuwa ni ajenda ya kudumu kwenye mikutano ya kisiasa na ya jamii.

ii) Tafiti za kisayansi zinabainisha kuwa, watu wanaoishi na VVU wapo katika hatari zaidi ya kuugua Kifua kikuu (TB), hali inayosababishwa na upungufu wa kinga mwilini. Katika kuthibitisha hili, tafiti zinaonesha kuwa asilimia **28** ya watu wanaoishi na VVU huugua pia kifua kikuu, ambapo asilimia **35** miongoni mwao huugua Kifua Kikuu sugu (MDRTB), ugonjwa ambao husababisha kifo kwa asilimia **5.6.** Kamati inashauri kuwa, ili kukabiliana na tatizo la kifua kikuu kwa WAVIU, Wizara iendelee kuongeza nguvu katika afua za mtangamano baina ya UKIMWI na kifua kikuu.

## 2.2 ZIARA ZILIZOFANYWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni 10 (b), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2016 10 (b), inayoitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, Kamati ilifanya ziara kati ya tarehe 4 – 9 Machi 2019, kutembelea na kukagua utekelezaji Afua na shughuli zinazotekelzwa na Wizara, Taasisi na Mmlaka za Serikali katika mwitikio dhidi ya mapambano ya UKIMWI na biashara na matumizi ya Madawa ya Kulevya katika Mikoa ya Morogoro, Dar es salaam na Pwani.

**Maeneo na Afua zilizokaguliwa na Kamati**
Kwa ujumla, ziara na ufuatiliaji ulilfanywa katika maeneo yafuatayo: -

a) Gereza la Kingolwira Mkoa wa Morogoro;

b) Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Kituo cha Huduma na Tiba- CTC Hospitali ya Sinza na Shule ya Sekondari Makoka;

c) Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Kituo cha Huduma na Tiba- CTC Tandale na Shule ya Sekondari Salma Kikwete;

d) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Kituo cha Huduma ya Methadone –Hospitali ya Temeke na Nyumba ya Upataji nafuu ya nafuu (MUKIKUTE-Temeke);

e) Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti-Pwani na Kituo cha huduma na tiba –CTC- Hospitali ya Songa –Mchukwi-Kibiti.

**Malengo ya Ziara katika maeneo yaliyotembelewa**

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa kutekeleza ratiba ya ziara, Kamati ilipokea kujadili taarifa za maeneo/ vituo ilivyotembelea, pamoja na kushuhudia utoaji wa huduma mbalimbali za masuala ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya.

Kwa ujumla malengo ya ziara, taarifa zilizowasilishwa na kujadiliwa na ukaguzi uliofanywa ulilenga kubaini mambo makubwa yafuatayo: -

a) Mwitikio wa UKIMWI kwa ujumla kwenye Halmashauri za Wilaya;

b) Hali ya maambukizi ya VVU na upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU pamoja na tiba ya magonjwa nyemelezi kwa muktadha wa malengo ya 90-90-90;

c) Utekelezaji wa afua za UKIMWI mahala pa kazi miongoni mwa Watumishi; mafanikio na changamoto;

d) Udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na huduma ya utoaji Methadon kwa watumiaji wa dawa za kulevya, Mafaniko na changamoto;

e) Ukusanyaji, Usimamizi na matumizi ya takwimu za Masuala ya UKIMWI katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya.

**Uchambuzi wa mambo yaliyobainishwa na Kamati wakati wa ziara**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika maeneo tajwa uliweza kubaini mambo ya msingi kuhusu mafanikio na changamoto zilizopo pamoja na hatua zinazochukuliwa. Aidha Kamati iliibua hoja pamoja na kutoa ushauri na mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI na adawa ya Kulevya.

Baadhi ya mambo ya msingi ambayo Kamati ilibaini ni pamoja na yafuatayo: -

(a) Katika ngazi mbalimbali, hususan baadhi ya Halmashauri na vituo vya afya, hakuna ufahamu wa kutosha juu ya utekelezaji wa shughuli za mwitikio wa UKIMWI katika muktadha wa 90-90-90. Jambo hili linapunguza uwezo wa Serikali na wadau kufanya tathmini ya matokeo ya hatua zinazochukuliwa.

(b) Kutokuwepo na takwimu za makadirio ya wanaokusudiwa kupimwa maambukizi ya VVU ni mojawapo ya mapungufu yaliyobainika katika Halmashauri na Manispaa zote zilizotembelewa. Jambo hili lina uzito mkubwa kwani ndio msingi wa wa takwimu zote za mkakati wa 90-90-90;

(c) Kuendelea kuwepo changamoto ya unyanyapaa miongono mwa watumishi, mahala pa kazi, ambapo katika Halmashauri zilizotembelewa kumekuwepo na idadi ndogo sana ya watumishi waliojitokeza kushiriki katika upimaji wa afya zao ukilinganisha na matarajio.

(d) Kuwepo takwimu za kutilia shaka kuhusu hali ya maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu katika magereza nchini. Kamati ilielezwa juu ya magereza nchi kuwa na idadi ndogo sana ya

wagonjwa wa Kifua Kikuu ikilinganishwa na wastani unaotarajiwa kulingana na takwimu za Kitaifa pamoja na takwimu za Kimataifa kwenye maeneo mahususi kama magereza

**Mheshimiwa Spika, endapo takwimu hizi zipo sahihi,** Kamati haitasita kulipongeza Jeshi la Magereza kwa mafanikio hayo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Jeshi la Magereza lishirikiane na Kitengo cha Taifa cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) ili kufanya ukaguzi na tathmini ya pamoja katika Magereza yote nchini ili kujihakikishia juu ya usahihi wa hali halisi ya Kifua Kikuu katika Magereza nchini.

(e) **Udhaifu katika uchambuzi na matumizi ya takwimu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini udhaifu mkubwa kwenye uwezo wa watendaji wa Halmashauri za Wilaya katika kuchachua na kutumia takwimu za UKIMWI katika ngazi husika. Hali hii imejitokeza kwenye Halmashauri zote zilizotembelewa kwenye idara ya afya (inayosimamia mwitikio wa UKIMWI kwa upande wa sekta ya afya) pamoja na ofisi ya mratibu wa UKIMWI ngazi ya Hlmashauri (Multisectoral HIV Response). Kwa mfano kwenye Halmashauri mojawapo mratibu wa takwimu wa idara ya afya aliitaarifu Kamati kwamba yeye binafsi hakushirikishwa kwenye maandalizi ya takwimu zilizowasilishwa mbele ya Kamati, licha ya kwamba yeye ndio mtunzaji wa takwimu hizi. Pia aliitaarifu Kamati kwamba huwa hafanyi uchambuzi wa takwimu kwa ajilia ya watumiaji kwenye Hlmashauri yake. Katika Halamashuri nyingine, takwimu za ngazi ya Hlmashauri ziliwasilishwa kwamba, **asilimia 50** ya WAVIU wanaotumia ARV hawafiki vituoni kwa ajili ya huduma kama inavyotakiwa (loss to follow up) na vivyo hivyo **asilimia 79** ya hali hiyo kenye ngazi ya kituo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii inaashiria aidha kuna udhaifu mkubwa kwenye uchambuzi na tafsiri ya takwimu au hali halisi ya matumizi ya ARV kwa WAVIU ni mbaya sana. Ni maoni ya Kamati kuwa serikali ifanyie kazi mapungufu haya ili taifa lisipate madhara ama kutokana na upungufu katika matumizi ya takwimu au hali halisi ya watu wanaoishi na VVU kutozingatia matumizi sahihi ya dawa za kufubaza vijidudu, kwauwa mojawapo kati ya hayo mambo mawili ni sahihi

(f) **Uelewa mdogo kuhusu Malengo ya Kimataifa ya Kupambana na UKIMWI ya 90-90-90**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na uelewa mdogo katika muktadha wa wa Malengo na mkakati wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI wa 90-90-90- ifikapo Mwaka 2020. Hii ni kutokana na kwamba, pamoja na takwimu nyingi zilizowasilishwa zililenga kuonyesha mafanikio katika kudhibiti maambukizi VVU/UKIMWI, mafanikio yanayoelezwa hayapimiki kutokana na takwimu kutoonyesha malengo yaliyowekwa ili kuweza kulinganisha na kiwango kilichofikiwa.Kwa mfano, taarifa nyingi hazionyeshi makadirio ya wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU, haioneshi wanapimwa wangapi kati ya walioakadiriwa, badala yake inaonyesha waliopatikana na maambukizi. Adha takwimu pia hazioneshi idadi ya WAVIU wanaotumia dawa na idadi ya waliofanikiwa kufubaza makali ya VVU. Hali hii, inaathiri kwa kiasi kikubwa maamuzi mbalimbali yanayohusu hatua za kuchukua katika kuimaraisha mapambano dhidi ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, ili kujenga uelewa wa kuondoa dosari zilizobainika katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI, Serikali **(TACAIDS)** iimarishe usimamizi katika ngazi zote kwa kuwezesha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi bora ya takwimu, ili ziweze kutumika ipasavyo katika kuongeza kasi ya kutekeleza mpango Mkakati wa Kimataifa wa kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90 90 90.

(g) **Afua za UKIMWI na madawa ya kulevya mashuleni.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2017) asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15-24 na asilimia 80 ya maambukizi hayo ni miongoni mwa wasichana. Hivyo basi afua za UKIMWI na madawa ya kulevya mashuleni ni muhimu. Kamati imebaini kutokuwepo mkakati wa uratibu na usimamizi wa mapmabano dhidi ya UKIMWI na matumizi ya madawa ya kulevya mashuleni. Kwa mfano, katika Shule zilizotembelewa na Kamati, wanafunzi waliiarifu Kamati kwamba hawajawahi kusikia kuhusu muktadha wa 90-90-90 kama mkakati wa mwitikio wa UKIMWI nchini na pia waratibu wa elimu ya afya mashuleni waliitaarifu Kamati kuwa hawajawahi kufika katika shule hizo. Kwa maana hiyo, hakuna hatua madhubuti zinazoonekana kutekelezwa kulingana na miongozo iliyopo. Aidha suala la kutekeleza afua kudhibiti dawa za kulevya na UKIMWI limebaki kuwa ni suala la ziada, bila msukumo, mipango, bajeti na bila raslimali fedha.

(h) **Kukosekana hatua mahsusi na za makusudi za kudhibiti maabukizi ya UKIMWI zinazoendana na kasi ya kukua kwa majiji**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Manispaa ya Kinondoni kuwa na idadi kubwa ya watu ambao wanashiriki kwenye shughuli za uchumi ikiwi ni pamoja na uwepo wa maeneo mengi ya starehe na viashiria vya ongezeko la maambukizi VVU kamati ilibaini kuwa hakuna mpango madhubuti unaolenga kudhibiti maambukizi mapya katka maeneo yao.. Aidha, takwimu zilizowasilishwa kuhusu hali ya mambukizi ya VVU/ UKIMWI hazijazingatia Makundi maalum, rika, jinsia, na umri. Hivyo kuzifanya kutoweza kutumika ipasavyo kufanya maamuzi madhubuti ya hatua za kuchukua katika kupambana na VVU/UKIMWI.

(i) **Mahusianisho ya madawa ya kulevya na maambukizi ya VVU**

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa maambukizi ya VVU kwa watumia dawa za kulevya yapo juu ya kiwago cha wastani wa maambukizi Kitaifa. Aidha kumekuwepo na ongezeko la maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu kwa warahibu wa madawa ya kulevya nchini kwa viwango tofauti kutegemeana na sababu mbalimbali. Hivyo Kamati inasisitiza kuwa, pamoja na huduma za methadone kwa warahibu ni muhimu kuimarisha utoaji huduma za upimaji UKIMNWI, magonjwa ya kifua kikuu na homa ya ini B na C.

**(j) Warahibu wa madawa ya kulevya kukosa namna ya kumudu maisha hasa baada ya kukamilisha matibabu**

Waraibu wengi wa madawa ya kulevya hawana ujuzi wa kuweza kujiajiri hali ambayo inawaweka katika hatari kubwa ya kurudia kuyatumia tena madawa hayo baada ya matibabu kutokana na kukosa makazi maalum, kukosa fursa za kufanhya shughuli za kuwapatia kipato ili kuweza kumudu maisha.

(j) **Malalmiko ya warahibu kukewa adhabu ya kusitishiwa dawa ya methadone kwa utovu wa nidhamu**

**Mheshimiwa Spika,** yamekuwepo malalamiko mengi kutoka kwa watumia dawa za kulevya katika Kliniki Methadone ya Temeke, ambapo wanaopata dawa wanalalmikia baadhi ya hatua za kinidhamu wanazochukiliwa pindi wakikiuka taratibu zilizowekwa, ikiwa ni pamoja na kunyinwa dawa ya methadone kwa kipindi maalum. Kwa kuwa kamati inaona uwezekano wa uwepo wa malalamiko kama hayo kwingineko, kamati inalichukulia suala hili kwa uzito mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa adhabu zinazotolewa zinaleta kuwataka wagonjwa kuzingatia masharti ya kupata matibabu ikiwa ni pamoja na kuwahi muda wa kupata dawa, kuepukana na matumizi ya kilevi chichote wakati wote wa kutumia dawa, kuwa na lugha nzuri, lugha ya staha na heshima kwa watu wote, kutozuzura maeneo ya Kituo baada ya kupata dawa, kutojihusiha na vitendo vya wizi, utovu wa nidhamu na baadhi yao kusitishiwa dawa kwa sababu moja au nyingine ikiwa ni pamoja na wanaofika wakiwa wametumia vilevi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Ina maoni kuwa kwa kuzingatia mazingira halisi ya warahibu, uchukuaji wa hatua za kinidhamu ni jambo la msingi. Hata hivyo adhabu ya kusitisha dawa ya methadone Kwa kipindi Fulani itekelezwe pale tu ambapo ni kwa mujibu wa sababu za kitaalam na si vinginevyo. Kwa mfano pale mrahibu anapobainika kuchanganya matumizi ya dawa ya methadone na dawa ya kulevya ni budi asitishiwe dawa ya methadone kwa sababu za kitaalamu. Lakini pale ambapo mrahibu anabainika kutenda kosa la kinidhamu kwa mfano kuchelewa au kupigana na mwenzake, Kamati inashauri utengenezwe utaratibu mwingine wa adhabu tofauti na usitishaji wa dawa. Msingi wa pendekezo hili ni kutokana na kwamba, adhabu kuwasitishia dawa ya methadone inawawaweka katika hatari ya kurudi kutumia dawa za kulevya, lakini pia inaisababishia Serikali hasara kwa kuhitaji kuendelea kumtumia dawa kwa muda mrefu zaidi.

## 2.3 **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019 NA MCHAKATO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri ilioutoa kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) Toleo la Januari, 2016, mnamo tarehe 30 na 31 Machi, 2019.

### 2.3.1 **Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

#### a) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ilitengewa Fedha kiasi cha shillingi **12,909,431,000.** Kati ya fedha hizo shillingi **2,609,431,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Februari 2019 Tume ilipokea kiasi cha shilingi **10,477,721,649.96,** sawa na asilimia **81** ya fedha zote zilizotakiwa kutolewa na Serikali kwenda katika Tume hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza serikali kwa kufikisha upeleakji wa fedha kwa kiwango kinachoridhisha. Hata hivyo Kamati inasisitiza umuhimu wa serikali kuongeza kiwango cha upelekaji wa fedha zilivyoidhinishwa na Bunge kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya kupelekewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kwamba utekelezaji wa shughuli za Tume kwa kiasi kikubwa unategemea sana fedha kutoka kwa wafadhili. Kutokana na hali hiyo ni dhahili kuwa endapo ufadhili huu utakoma basi Tume itashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaiomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji WA fedha hasa za ndani Kwa Tume Ili iweze kukamilisha utekelezaji wa shughuli zake kama zilivyopangwa kwa wakati.

**b) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) - **Fungu 92,** iliomba jumla ya kiasi cha shilingi **Bilioni 8,767,193,747.000** ikiwa ni makadirio ya matumizi yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi Bilioni 5,956,634,747** sawa **na asilimia 67** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **Bilioni 2,812,559,000** sawa na **asilimia 32** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi.

**c) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI - Fungu 92 haikuwa na makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge. **Rejea Jedwali Na 1**

Jedwali Na. 1: **Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana hadi Mwezi Februari, 2019 (FUNGU 92), hadi kufikia Mwezi Februari, 2019.**

| **BAJETI ILIYOIDHINISHWA** | | **UPATIKANAJI WA FEDHA** | |
|---|---|---|---|
| **MGAWANYO** | **KIASI KILICHOIDHINISHWA** | **Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2019** | **Asilimia %** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)** | | | |
| Mishahara | 1,696,685,000.00 | 960,769,000.00 | 56.6 |
| Kawaida (OC) | 912,746,000,00 | 518,013,662.52 | 56.8 |
| Mfuko wa UKIMWI (ATF) | 0.00 | **0.00** | 0 |
| **JUMLA NDOGO (PE &OC)** | **2,609,431,000.00** | **1,478,782,662.52** | 56.7 |
| **MAENDELEO (MFUKO WA UKIMWI) –ATF** | | | |
| **ATF** | **3,000,000,000.00** | **750,000,000.00** | 25 |
| **MAENDELEO (FEDHA ZA NJE)** | | | |
| DoD | 1,437,044,887.83 (Nje ya bajeti) | 871,592,411.00 | 60.7 |
| GGM Kill Challenge | 150,000,000.00 (Nje ya bajeti ) | 99,488,130.00 | 66. 3 |
| UNDAP | 948,062,277.00 | 711,394,980.00 | 75 |
| GLOBAL FUND | 6,551,937,723.00 | 5,950,499,119.61 | 90.8 |
| **JUMLA NDOGO (MAENDELEO)** | **12,087,044,889.83** | **8,382,974,640.61** | 69.4 |

**Chanzo.** ***Taarifa ya Tume (TACAIDS) ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2019/2020***

2.3.2 **Upatikanaji wa Fedha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA)- Fungu 91**

a) **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilikadiriwa kufanya matumizi ya kiasi cha Shilingi **Bilioni 7,592,818,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni **4.948,552,000 sawa na asilimia 65** ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (Jedwali namba 1) na Shilingi **2,644,266,000** sawa na **asilimia 35** ni kwa ajili ya Mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi **Bilioni 1,837,717,000** sawa na **asilimia 32** ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

b) **Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haikutengewa kabisa fedha za Miradi ya Maendeleo. Kamati inasisitiza kwamba, ajenda ya kupambana na Dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyotafsiriwa. Ni maoni ya Kamati kuwa miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika na fedha za maenedeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu kiuchumi kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriammali, mikopo nafuu ya biashara, studi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya zaidi ya kuikinga jamii ili isishiriki katika njia yoyote ya matumizi ya dawa za kulevya. **Rejea Jedwali Na. 2**

Jedwali Na. 2: **Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana 2018/2019 (FUNGU 91) hadi kufikia Mwezi Februari, 2019.**

| **BAJETI ILIYOIDHINISHWA** | | **UPATIKANAJI WA FEDHA** | |
|---|---|---|---|
| **MGAWANYO** | **KIASI KILICHOIDHINISHWA** | **Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2018** | **Asilimia** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)** | | | |
| Mishahara | 806,549,000.00 | 549,163,055.00 | 8.1 |
| Kawaida (OC) | 4,948,552,000 | 3,404,890,000 | 8.8 |
| Miradi ya Maendeleo | 0 | 0 | |
| **JUMLA** | **5,755,101,000.00** | **3,954,053,055.00** | 8.7 |

***Chanzo: Taarifa ya Mamlaka Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018***

2.4 **MAFUNZO NA SEMINA KWA WAJUMBE WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wajumbe wa Kamati wanajengewa uwezo katika maeneo mbalimbali lakini pia wanashirikiana na wadau katika kubadilishana mawazo na uzoefu, Kamati ilipata mafunzo kwa njia ya semina kutoka kwa Taasisi mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) **Semina kuhusu Takwimu za Maambukizi ya UKIMWI na mwitikio wa Kitaifa wa kukabiliana na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI (*JHPIEGO)***

Semina ilitolewa na Taasisi ya JHPIEGO chini ya Mradi wa Sauti Yetu kwa ajili ya kuwapa wajumbe uelewa kuhusu takwimu halisi za hali ya maambukizi ya UKIMWI Kitaifa na Kidunia pamoja na uhamasishaji wa wananchi kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari hususan wanaume.

Wajumbe walifahamishwa kuwa, takwimu za utafiti wa hali na viashiria vya UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2016/2017 zinaonesha kuwa idadi ya raia wa Tanzania inakisiwa kuwa ni **50.9** milioni. Ukubwa wa maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) kitaifa miongoni mwa jamii yenye umri wa miaka 15 – 49 ni wastani wa asilimia **4.7** Kitaifa; wanawake wakiwa asilimia **6.2** na wanaume ni asilimia **3.1.** Inakadiriwa kuwa jumla ya watanzania **milioni 1.4** wanaishi na Virusi vya UKIMWI na kwa vijana wa umri wa miaka kati ya 15 na 24 ni asilimia **1.4.** Wavulana asilimia **0.6** na wasichana ni asilimia **2.1**. Semina hii ilifanyika terehe 23 - 25 Aprili, 2019 katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge, Dodoma.

b) **Semina ya ICAP kuhusu Mapambano dhidi ya UKIMWI**

Semina hii iliendeshwa na Taasisi ya ICAP kwa ajili ya kukuza uelewa kwa Wajumbe wa Kamati kuhusu umuhimu wa mapambano ya UKIMWI pamoja na mikakati ya kufikia asilimia 90-90-90 na kuishauri Serikali kwa ajili ya kubadilisha Sera ya Taifa ya UKIMWI.Aidha Wajumbe walifahamu mahusiano baina ya ICAP chini ya mwanvuli wa CDC ikishirikiana Taasisi ya Taifa ya Takwimu walifanya Utafiti mkubwa wa kitaifa (THIS) wa kupima VVU kwa nchini nzima ili kupata takwimu sahihi za maambukizi kitaifa.Aidha, walijulishwa kuwa kuhusu matumizi ya PREP ambayo hutumika kwa ajili ya makundi maalum kama kinga ya maambukizi ya UKIMWI au kwa watu waliopata ajali. Kwa mujibu wa Tafiti za Viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania *(THIS)* ya Mwaka 2016/2017 vinaonesha kuwa vijana wenye umri wa miaka 15-24 wanapata maambuki ya ugonjwa wa UKIMWI kwa **asilimia 1.4.** Aidha wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 64 wana maambukizi ya juu kwa **asilimia 6.5.** Semina hii ilitolewa hapa Mjini Dodoma, tarehe 15 Mei, 2019 katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge, Dodoma .

c) **Semina ya Utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Na 22 na Marekebisho yake Na 6 ya Mwaka 2015**

Semina ilitolewa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa ajili ya kuwapa wajumbe uelewa wa umuhimu wa Sheria ya Kudhibiti ya Kudhibiti UKIMWI pamoja . Aidha, semina hii iliwawezesha Wajumbe kuelewa umuhimu wa marekebisho ya Sheria hii kwa kuzingatia hali ya maambukizi ilivyo sasa ongezeko kubwa la vijana husani wasichana ambao takwimu zinaonesha kuwa zaidi asilimia 40 ni wenye umri wa miaka 15-24 wasichana ni asilimia 8. Takwimu hizi zinaashiria kuwa ipo haja ya Serikali kutilia mkazo Suala la *Self Testing* kwa kuwa vina ndiyo ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Semina hii ilifanyika terehe 21 Agosti, 2019 katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge Dodoma.

d) **Semina ya Hali Halisi ya Kifua Kikuu (TB), pamoja na mwingiliano wake na UKIMWI, mafanikio na changamoto katika udhibiti wake hapa nchini. (Elizaberth Glaser Pediatric AIDS Foundation**

Semina hii iliendeshwa na Taasisi ya Elizaberth Glaser Pediatric AIDS Foundation kwa ajili ya kuwapatia Wajumbe uelewa kuhusu Hali ya Kifua Kikuu nchini pamoja na UKIMWI, Mafanikio na Changamoto zinazoikabili jamii katika utekelezaji wa shughuli za Kifua Kikuu. Wajumbe walifahamishwa kuwa Kifua Kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza na unaongoza kwa kusababisha vifo vingi Duniani na Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 zenye tatizo kubwa la Kifua Kikuu. Kila mwaka inakadiriwa kuwa watu 160,000 wanaugua Ugonjwa wa Kifua Kikuu hapa nchini. Aidha,

asilimia 40 yawagonjwa wenye maambukizi ya UKIMWI wanapata Kifua Kikuu. Semina hii ilifanyika mara mbili kuhakikisha Wajumbe wa Kamati wanapata fursa ya kuweza kujadili na kuishauri vizuri serikali katika mapambano ya Kifua Kikuu (TB). Semina hii ilifanyika terehe 20 Juni, 2019 katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge Dodoma.

e) **Semina kuhusu Umri wa Kupima kwa Vijana Na Changamoto wanazozipitia (Mwanza Youth and Children Network (MYCN)**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya MYCN iliendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe kuhusu umri wa kupima kwa vijana, changamoto wanazozipata na umuhimu wa kuruhusu watoto kupima afya zao mapema bila ridhaa ya wazazi au walezi ili kujua afya zao na kuanza tiba endapo wameathirika na VVU. Katika mafunzo haya ilibainika kwamba kuna baadhi ya watoto wanapitia changamoto nyingi sana ikiwemo kufanyiwa vitendo vya ukatili na wazazi au walezi; hali ambayo inasababisha kukosa mahali pa kushitaki. Vitendo hiki vya ukatili vimesababisha watoto wengine kufikia hatua ya kubakwa au kunajisiwa na kuambukizwa UKIMWI. Mzazi au mlezi aliyemtendea mtoto ukatili kama huu hawezi kuruhusu mtoto huyu akapimwe kwani anajua uovu wake utagundulika. Semina hii ilifanyika terehe 22 Juni, 2019 katika Ukumbi Namba 49 Jengo la Utawala Annex, Ofisi ya Bunge Dodoma.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na shughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari 2019 – Januari 2020, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao: -

### 3.1 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA (TACAIDS)

(a) **Upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI**

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa, mpaka sasa asilimia kubwa Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imekuwa ikitegemea fedha za wahisani. Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi **Bilioni 2** tu sawa na **asilimia 32** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tume. Kiasi kilichotolewa hakuna

**KWA KUWA** kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI ikizingatiwa kwamba baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI kwa Tanzania. Kupunguzwa kwa fedha hizo kuna athari katika mipango iliyokuwa itekelezwa katika kupambana na UKIMWI nchini**.**

**HIVYO BASI** Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi wake. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vya kujiwezesha kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(b) **Kuanzisha Tozo kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (ATF)**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, changamoto kubwa imekua ni kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia

shughuli za UKIMWI. Mfuko wa UKIMWI (Aids Trust Fund - ATF) lengo lake ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na janga hili.

**NA KWA KUWA,** kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mapambano endelevu dhidi ya maambukizi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI ambayo yanahitaji rasilimali fedha za uhakika za kutosha.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kuainisha na kutekeleza chanzo mahsusi cha upatikanaji wa fedha za ndani ili kuruhusu hamasa kwa Sekta binafsi na wadau wengine wa ndani katika kuchangia ATF. Hoja hii ni muhimu kwa kuwa kuiachia Serikali peke yake ibebe mzigo huu itachukua muda mrefu sana kufikia lengo tulilojiwekea na kwa upande mwingine kutokuwepo na chanzo mahsusi cha Serikali hakutatoa fursa kwa wadau wa ndani tofauti na Serikali kupata hamasa ya kushiriki katika uchangiaji wa shuguli za UKIMWI hapa nchini.

(c) **Kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali za UKIMWI**

**KWA KUWA**, afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana na ubora wa takwimu zinapatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali.

**NA KWA KUWA** kuna upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Wizara ya Afya na TAMISEMI kuimarisha usimamizi ikiwa wa ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya takwimu kwa ngazi za Halmashauri na Vituo vya Afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza mpango Mkakati wa Kimataifa wa kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90 90 90.

(d) **Uelewa mdogo kuhusu Malengo ya Kimataifa ya Kupambana na UKIMWI ya 90-90-90**

**KWA KUWA,** kumekuwepo na uelewa mdogo katika muktadha wa Malengo na mkakati wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI wa 90-90-90- ifikapo Mwaka 2020. Hii ni kutokana na kwamba, pamoja na takwimu nyingi zilizowasilishwa zililenga kuonyesha mafanikio katika kudhibiti maambukizi VVU/UKIMWI, mafanikio yanayoelezwa hayapimiki kutokana na takwimu kutoonesha malengo yaliyowekwa.

**NA KWA KUWA,** hazioneshi makadirio ya wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU, haioneshi wanapimwa wangapi kati ya walioakadiriwa, badala yake inaonesha waliopatikana na maambukizi tu

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri kuwa, ili kujenga uelewa wa kuondoa dosari zilizobainika katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI, Serikali **(TACAIDS)** iimarisha usimamizi katika ngazi zote kwa kuwezesha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi bora ya takwimu, ili ziweze kutumika ipasavyo katika kuongeza kasi ya kutekeleza mpango Mkakati wa Kimataifa wa kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90 90 90.

(e) **Mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI kuhusiana na Umri wa mtu Kuweza Kupima VVU na Upimaji wa mtu binafsi**

**KWA KUWA,** Serikali imefanya mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI kwa kuboresha suala la umri wa ridhaa ya kupima UKIMWI ikiwa ni hatua za kuboresha upatikanaji wa huduma za VVU.

**NA KWA KUWA,** takwimu zinaonesha kuwa umri unaochangia maambukizi ya VVU kiasi kikubwa ni vijana kuanzia miaka 15 mpaka 24.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zilizofanyika za mabadiliko katika Sheria ya UKIMWI ili kuzingatia mahitaji mapya kwa mujibu wa takwimu. Hata hivyo kamati inasisitiza utekelezaji wa haraka wa marekebisho hayo ya sheria sambamba na ufuatiliaji na tathimini ya uhakika juu ya matokeo ya mabadiliko hayo ya sheria.

(f) **Marekebisho ya sheria ya UKIMWI ili kuimarisha Mapambano ya UKIMWI Nchini ili yaendane na utekelezaji wa Malengo ya Kimataifa ya kutokomeza UKIMWI ya 90 90 90.**

**KWA KUWA,** Tanzania inaendelea kutekeleza awamu ya kwanza ya malengo na mkakati wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na masuala ya UKIMWI (UNAIDS), ambalo limeweka malengo ya kutokomeza ugonjwa huo ifikapo Mwaka 2020 ambayo yanajulikana kama 90-90-90. Malengo haya yanasisitiza kuwa, ifikapo mwaka 2020, asilimia 90 ya waliokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU wajue hali zao kiafya, asilimia 90 ya watakaopima na kukutwa na maambukizi ya VVU wapate dawa na asilimia 90 ya waliopo kwenye tiba wawe na kiwango kidogo cha virusi kwenye damu

**NA KWA KUWA,** takwimu zinaonesha utekelezaji wa mkakati huu wa 90-90-90 nchini hauna uwiano linganifu; katika 90 ya kwanza Tanzania ina **asilimia 61**, 90 ya pili asilimia 93 na 90 ya tatu ina asilimia 87. Hivyo Tanzania ina alama za chini katika 90 ya kwanza, ikizingatiwa kuwa 90 ya kwanza ndio msingi wa mafanikio ya kutokomeza UKIMWI nchini.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufanya mabadiliko ya kisera na ya Sheria pale inapodhihirika kwamba kuna mahitaji hayo ili kuzingatia mahitaji mapya kwa mujibu wa takwimu.

(g) **Afua za UKIMWI na madawa ya kulevya mashuleni**.

**KWA KUWA**, takwimu za Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2017) zinaonesha kuwa, asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15-24 na asilimia 80 ya maambukizi hayo ni miongoni mwa wasichana.

**NA KWA KUWA**, Kamati imebaini kutokuwepo mkakati wa uratibu na usimamizi wa mapamabano dhidi UKIMWI na matumizi ya madawa ya kulevya mashuleni na hakuna hatua madhubuti zinazoonekana kutekelezwa kulingana na miongozo iliyopo. Aidha suala la kutekeleza afua za kudhibiti dawa za kulevya na UKIMWI limebaki kuwa ni suala la ziada, bila msukumo, mipango, bajeti na bila raslimali fedha.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka za kuhakikisha shule zote za msingi na sekondari zinaratibu, kutekeleza na kusimamia suala la elimu ya afya ya uzazi, jinsia, VVU na UKIMWI pamoja na dawa za kulevya ipasavyo.

**(h)Taasisi za Umma kutozingatia kikamilifu Mwongozo wa Utumishi wa Umma kuhusu masuala ya UKIMWI katika utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahala pa kazi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza;**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Taasisi za umma kutozingatia ipasavyo matakwa ya Mwongozo wa Utumishi wa Umma kuhusu masuala ya UKIMWI katika utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahala pa kazi na Mgonjwa Yasiyoambukiza katika Wizara na Taasisi za Umma. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika Wizara nyingi za umma hakuna mwamko wa watumishi kupima maambukizi ya VVU, watumishi hawako tayari kuweka wazi hali ya afya zao ili kuweza kunufaika na huduma za walioathirika, bajeti zinazotengwa kwa ajili ya kutekeza afua za UKIMWI ni ndogo, hazitolewi kwa wakati, na pale zinapotolewa hazitumiki.

**NA KWA KUWA,** mwenendo huu hukosekana chachu ya mapambano dhidi ya UKIMWI mahala pa kazi ni hatarishi kwa ustawi wa Taifa,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kuhakikisha Wizara na Taasisi zote za Serikali zinaratibu na kutekeleza Mwongozo wa Utumishi wa Umma kuhusu Afua za UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kama ulivyoainisha katika Mwongozo kwa kutenga bajeti ya kukidhi mipango na mikakati ya kupambana na UKIMWI mahala pa kazi na Magonjwa Sugu, kuhamasisha watumishi kupima maambukizi ya VVU, kubuni mbinu za kuwafanya watumishi kuweka wazi hali zao za afya ili watakaoonekana wana maambukizi waweze kuanza kutumia dawa. Aidha Kamati inashauri Kamati za UKIMWI katika Wizara na Taasisi mbalimbali za umma, ziimarishwe ili zitekeleze majukumu yake pamoja na kutakiwa kutoa taarifa kwa Ofisi ya Rais, Managementi ya Utumishi wa Umma pamoja na Kitengo Maalum ndani ya TACAIDS kinachoshughulika na uratibu wa shughuli za UKIMWI ndani ya Wizara na Taasisi za Umma kiimarishwe na kusimamiwa ipasavyo.

**KWA KUWA** kumekuwepo na masuala yenye kuinua vikwazo baina ya Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha kwa upande mmoja na pia wadau wa UKIMWI kwa upande mwingine kuhusiana na msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa zinazoagizwa na wadau wa UKIMWI,

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa kuna kukosekana kwa fursa ya kutosha na ya kiushirika ya kujadili tofauti hizo na badala yake kumekuwepo na uchambuzi unaochukua muda mrefu sana sambamba na hali ya kuvutana zaidi kuliko kushauriana

**NA KWA KUWA** Kamati inasisitiza kuwa sio kazi yake kuingia katika ngazi hiyo ya utendaji lakini ni wajibu wa Kamati kusimamia ufanisi wa jambo hili kwa sababu maslahi kwa watanzania,

**HIVYO BASI** Kamati inasisitiza umuhimu wa Serkali na wadau wa UKIMWI kwenda hatua inayofuata ambayo ni kupata ufumbuzi wa pamoja wa suala hili. Kamati inaamini kuwa hatua ya uchambuzi imekamilika. Kamati inaisisitiza serikali hasa kupitia Wizara ya Fedha na Wizara ya Afya kuchukua nafasi ya uongozi wa kuhakikisha sheria za nchi zinafuatwa na pia kulinda maslahi ya Taifa lakini kwa upande mwingine kutoa fursa ya kutosha ya mashauriano na wadau husika ili kutokuwa na kikwazo kwa wadau hao kutimiza wajibu wao, wajibu ambao pia upo kisheria.

### 3.2 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

(a) **Athari za kutotenga Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**KWA KUWA,** Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya imekua haitengewi Bajeti kwa ajili ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotenga fedha za maendeleo ni kukosekana kwa maabara ya Mamlaka ya Kupambana na madawa ya kulevya kwa ajili ya uchunguzi.

**NA KWA KUWA**, maabara inayotumika mpaka sasa ni maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo ina vipaumbele vingine katika utekelezaji shughulia zake. Sio lazima vipaumbele vya Mamlaka ya kupambana na madawa ya kulevya viwiane. Pamoja na kwamba ipo ahadi ya Wafadhili ya kujenga maabara kwa ajili ya Mamlaka, lakini utekelezaji wa ahadi hiyo umekua ukiahirishwa kila mwaka. Vilevile ukosefu wa fedha za maendeleo umepelekea kasi ndogo au kukosekana kwa mfumo maalumu kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa madawa ya kulevya na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia kumudu maisha na kuachana na biashara na matumizi ya madawa hayo.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Seikali kwamba, fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa Mamlaka kuanza kujenga mifumo itakayo jumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya na hivyo kuiwezesha Mamlaka kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Kamati inaamini kuwa, miradi ya maendeleo inaweza kutekelezwa na fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu kiuchumi kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, studi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi, elimu ya madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kupambana na kudhibiti dawa za kulevya kwani vita hii ni ngumu na endelevu.

(b) **Kujenga na kuimarisha mifumo ya Kitaasisi katika utekelezaji wa shughuli za Masuala ya Dawa za Kulevya**

**KWA KUWA,** Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya udhibiti na upambanaji wa Dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo taasisi zisizo za kiserikali.

**NA KWA KUWA**, Kamati umebaini kuwa, zipo baadhi ya NGOs na Taasisi zinazojihusisha na masuala ya dawa za kulevya nchini ambazo hazina muundo na mifumo rasmi wa jinsi gani zinawasaidia watumiaji wa dawa za kulevya Kwenye jamii. Baadhi zikitekeleza shughuli zake kwa kuwabagua watumiaji wa dawa hizo, mfano zinazo wahudumia wanawake peke yake, wale wanaojidunga kwa sindano na mara nyingine wale wanaotumia kwa kuvuta.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri kuwa, kupitia Mamalaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo chake cha uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, waongeze kasi ya kukamilisha zoezi la utambuzi na uratibu wa asasi zote zinazojishughulisha na Dawa za Kulevya ili kuangalia malengo yao pamoja na kazi zinazofanywa na asasi hizo na kuwawekea mfumo rasmi wa utekelezaji wa shughuli zao ili kuhakikisha kuwa walengwa wanafaidika na uwepo wa asasi hizi kwani fedha zinazotolewa ni kwa jina la watanzania

(c) **Kutokuwepo kwa Sera ya Madawa ya Kulevya**

**KWA KUWA,** Mpaka sasa Tanzania haina Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya, ambayo kwa umuhimu wake ingeimaridha mapambano yaliyopo dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

**NA KWA KUWA,** Sera ina umuhimu mkubwa katika kuweka misingi na mwelekeo wa Taifa katika vita dhidi ya madawa ya kulevya kwa ujula wake.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na Madawa ya Kulevya Nchini.

(e) **Suala la madawa ya kulevya kuwa ajenda ya Kamati za UKIMWI katika Halmashauri na Manispaa.**

**KWA KUWA,** Halmashauri na Manispaa Nchini zimekua zikiratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika Halamshauri na Manispaa kwa ufanisi wa kutosha.

**NA KWA KUWA**, Kamati katika ufuatiliaji wa shughuli za mapambano dhidi ya madawa ya kulevya katika ngazi za Halmashari na Manispaa umeonesha kutokuwepo utaratibu au mfumo rasmi wa namna ya kushughulika na suala la madawa ya kulevya.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri kuwa, ili kuwezesha utekelezaji wa jukumu hili kwa ufanisi, Serikali ikamilishe muongozo na hadidu rejea za namna Kamati hizi zitakavyotekeleza jukumu la kupambana na dawa za kulevya katika ngazi husika.

**SEHEMU YA NNE**

4.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge – Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi – Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Happiness Ndalu na Asia Msangi pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Paul Chima, kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama, Mb na Naibu Waziri Antony Mavunde na Stella Ikupa, Mb. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kaimu Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndg James Wilbert Kaji na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

**Mheshimiwa spika,** naomba pia kuwashukuru na kuwapongeza waziri, naibu waziri na Katibu mku wa wizara ya afya sambamba na watendaji wao wote kwa kutoa ushirikiano mkubwa wakati waote wa shughuli za kaamti na namna wanavyoonesha dhamira ya katatua matatizo yanayowakabili watanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
14. Mhe.Oliver Daniel Semuguruka, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Susan Anselim Lyimo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amina Nassor Makilagi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Yussufu Haji Khamisi, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Ester Nicholas Matiko, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Fratei Gregory Massey, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Godfrey W. Mgimwa - Mjumbe
26. Mhe. Mwigulu L. Nchemba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu**,** sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

……………………………….
Oscar Rwegasira Mukasa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono asanteni sana Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na utaratibu wetu asante Mwenyekiti. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa ya Utekekelezaji wa Majukumu ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge za Kudumu Toleo la Januari 2016 napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji na majukumu ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *hansard* kama ilivyoletwa hapo mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu ya Kamati. Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni kama yalivyoainishwa kwenye nyongeza ya 7(1) (a) – (d) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari 2016 kuwa ni;

Mheshimiwa Naibu Spika, Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati. Kwa kipindi cha Mwaka 2019/2020 kamati ilitekeleza majukumu yake mbalimbali kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda nitaeleza baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati ambayo inapatikana kwenye vishukwambi vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Kwa mujibu wa kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 mnamo mwezi machi, 2019 kamati ilikagua miradi 7 ya maendeleo iliyotengewa fedha za mwaka 2018/2019 katikamikoa ya Dar es Salaam na Pwani na taarifa iliwasilishwa Bungeni Mwezi Mei 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kupokea na Kuchambua na Kujadili Taarifa za Utekelezaji na Maoni ya Kamati na Bajeti ya mwaka 2018/2019 mweleko wa bajeti ya mwaka 2019/2020 taarifa ya kina ni kama ilivyowasilishwa kwenye Bunge la Bajeti la Mei 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara na waasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto utekelezaji wa lengo Namba 3 la malengo ya maendeleo endelevu *(good health and wellbeing)*. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada wanazofanya katika kutekeleza lengo hili. Hata hivyo Kamati imebaini ukosefu wa fedha za kutosha unachangia kukwamisha utekelezaji mzuri wa lengo hili. Kamati inaamini kuwa afya ndio utajiri wa taifa lolote kama mwanazuoni kutoka Marekani Pinkerton F. J alivyowahi kusema "*The wealth of the nation depends upon the health of its people or the health of the people determines the wealth of the nation*". Hivyo Kamati inaendelea kusisitiza Serikali iendelee kuwekeza fedha za kutosha katika sekta ya afya ili kuweza kutekeleza lengo hili kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mloganzila. Katika kikao cha kupokea taarifa ya hospitali hii Kamati ilielezwa juu ya changamoto ya upungufu wa watumishi kwa asilimia 50, ukosefu wa nyumba za watumishi pamoja a wataalamu kwenye kutumia vifaa vya kisasa vilivyopo, hali inayoathiri utendaji bora wa hospitali hii ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa changamoto ya watumishi inaathiri utekelezaji mzuri wa majukumu. Hospitali hii ni moja ya Hospitali ambazo zimejengwa kisasa na ni Hospitali ya mfano. Serikali ione namna nzuri ya kuitumia hospitali hii kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Tengeru, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu Utendaji wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hiyo ilifafanua masuala mbalimbali yakiwemo utendaji kazi wa chuo; hali ya upatikanaji wa fedha na changamoto ambazo Chuo kinakumbana nazo kama zinavyoonekana kwenye Taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania *(TMDA)*. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TMDA* bado inakumbana na changamoto kuu mbili ambazo ni uhaba wa watumishi na ukosefu wa sheria moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya baadhi ya bidhaa ambazo nyingine si salama kwa matumizi ya binaadamu kuingizwa sokoni kutokana na uwepo wa mipaka isiyo rasmi. Kamati inaona kuna haja kuweka mifumo bora ya udhibiti kwenye mipaka hiyo maarufu kama njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*. Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya *NHIF* ambayo ilieleza masuala mbalimbali ya utendaji yenye kuonesha mafanikio mbalimbali kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu. Kamati inaona kuna haja ya kuongeza elimu ya namna ya kupambana na magonjwa haya yasiyoambukiza ili kupunguza mzigo wa kuyatibu kutokana na kuendelea kuongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kwa upande wa Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara pamoja na taasisi zilizo chini ya usimamizi wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto za Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Habari na Hususan Vyombo vya Kurusha Matangazo (visimbuzi) kwa Njia ya Televisheni. Kamati ilipokea taarifa hii ambapo kwa ujumla Kamati imebaini kuwa kuna changamoto za kisheria ambazo zinaathiri Sekta hii muhimu. Kamati inaendelea kushauri Wizara ya Habari pamoja na *TCRA* wakae waiangalie sheria na kushauri namna bora ya kufanya ili kukuza tasnia hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mkakati huu mzuri. Ni Imani ya Kamati kuwa Mkakati huu utasaidia katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili na kutoa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa upande wa Wizara hii, Kamati Ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji kama ifuatavyo: -

Utekelezaji wa Lengo Na. 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Quality Education*). Kamati inapongeza Serikali kwa mafanikio iliyopata kutokana na utekelezaji wa lengo hili. Aidha, inashauri nguvu zaidi kwa sasa ielekezwe kwenye ubora ili kuweza kutekeleza vyema lengo hili na kupambana na ujinga na umaskini kama ambavyo mwanazuoni Charles Rangel alivyowahi kusema "*A quality education grants us the ability to fight war on ignorance and poverty*"

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi na Teknolojia – Mbeya. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 Chuo kimetekeleza majukumu mbalimbali kama inavyooneshwa

kwenye Taarifa yetu. Kamati iliwahi kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Maktaba mwezi Machi, Mwaka 2018 na inatoa rai ujenzi huo ukamilike mapema ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata sehemu ya kujisomea na kufanya rejea ya vitabu na nyaraka mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka (2018/2019) kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu. Kupokea Maoni ya Wadau kuhusu Mafanikio na Changamoto za Mfumo wa Elimu katika Sekta ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wadau wa Elimu ambao ni pamoja na *TAPIE*, Haki Elimu, *Policy Forum*, *TENMET*, UWEZO na TWAWEZA walieleza changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika mafanikio ya Sekta ya Elimu nchini kama zinavyoonekana kwenye taarifa. Ni Imani ya Kamati kuwa Serikali itafanyia kazi changamoto zote zilizoainishwa na wadau kwa lengo la kuboresha mfumo wa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji (Fungu 46). Hadi kufikia mwezi Disemba, 2019 Wizara (Fungu 46) ilikuwa imekusanya shilingi Bilioni 255.3 sawa na asilimia 46.1 ya kiasi cha shilingi Bilioni 553.7 zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara (Fungu 46) ilikadiria kutumia Shilingi Trilioni 1.38. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 523.78 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 862.71ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Disemba 31, 2019 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni 610 sawa na asilimia 44 ya bajeti yote iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha za OC umezidi kiwango kutokana na nyongeza ya Shilingi bilioni 19.47 katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya taasisi ikiwa ni kwa ajili ya kulipa madeni ya stahili za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu ikijumuisha pango la nyumba na tuzo za mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuanza kufanya malipo hayo ambayo yalikuwa kero kubwa kwa Wahadhiri wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Fungu 46 imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka shilingi bilioni 799.02 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi trilioni 1.38 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 42.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kwa miaka yote hiyo, Serikali imetoa shilingi trilioni 7.4 kwa ajili ya elimu kupitia Fungu 46 kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014/2015 hadi 2019/2020 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 3. Ikumbukwe kuwa fedha hizi hazijajumuisha fedha zinazotengwa kupitia TAMISEMI kwa ajili ya Elimu. Kamati inaendelea kupongeza jitihada hizi za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendelea kuona umuhimu wa elimu nchini na kuongeza bajeti yake mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilieleza masuala mbalimbali yakiwemo ya hali ya upatikanaji wa fedha, urejeshaji wa mikopo na idadi ya wanafunzi ambao wamepata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imebainikuwa kuwa warejeshaji wa mikopo asilimia 70 wanatoka kwenye Sekta za Umma na asilimia 30 ni Sekta Binafsi. Kamati inaendelea kuhimizia Sekta Binafsi kushirikiana na Bodi ili kubaini wanufaika wa mikopo walipo kwenye Sekta hizo na hivyo kuanza kurejesha mikopo hiyo kwa faida ya Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhuus Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Fungu 52. Ili kutekeleza vipaumbele ambavyo Wizara ilijipangia, jumla ya shilingi bilioni 959.15 ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 415.01 sawa na asilimia 43.2 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha kwa ya ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 544.13 sawa na asilimia 56.8 ziliidhinishwa. Hadi kufikia Desemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 239.5 sawa na asilimia 25 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi na imebaini kuwa bajeti ya Wizara ya Afya kupitia Fungu 52 imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi bilioni 713.7 mwaka 2014/2015 hadi shilingi bilioni 959.1 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 31.4. Kwa ujumla, katika kipindi hicho cha miaka mitano, bajeti iliyotengwa na Wizara hii imefikia shilingi trilioni 5.2 bila kujumuisha fedha zilizotengwa kupitia TAMISEMI. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendelea kujali afya za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee Idara Kuu Maendeleo ya Jamii - Fungu 53. Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 31.53 kwa ajili ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 28.77 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2.76 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kufika Desemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 14.3 sawa na asilimia 45 ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na masuala mengine yaliyoelezwa, Kamati ilielezwa changamoto ya kuongezeka kwa magonjwa yasiyokuwa ya kuambukizwa (*Non-Communicable Diseases*) ni kubwa. Takwimu zinaonesha kuwa orodha ya magonjwa 20 yaliyoongoza kwa matumizi makubwa ya fedha kwa mwaka 2018/2019, magonjwa 11 yasiyoambukiza yaligharimu shilingi bilioni 57.6 sawa na asilimia 48 ya shilingi bilioni 120.6 zilizotumika kugharamia magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Dodoma ina changamoto ya upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali, uchakavu wa miundombinu na vifaa vya kutolea huduma pamoja na gharama kubwa katika kutoa huduma kwa makundi maalum ya msamaha, ambapo katika kipindi cha Julai mpaka Desemba, 2019, jumla ya wagonjwa 25,000 walipata msamaha wa matibabu wenye thamani ya shilingi milioni 867.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya *KCMC* ilianzishwa mnamo mwaka 1971 na Shirika la Msamaria Mwema la Tanzania ambalo kwa sasa limeingia makubaliano maalum na Serikali ya Tanzania, ambapo Serikali ndiyo inalipa mishahara ya wafanyakazi wote. Shirika la Msamaria Mwema linasimamia uendeshaji wa Hospitali na maendeleo yake. Hospitali hii ni muhimu sana. Hata hivyo ina changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa watumishi katika kada za afya na ukosefu wa tiba ya mionzi kwa wagonjwa wa saratani kutokana na kutokuwa na mashine na jengo la mionzi *(bunker)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara na Taasisi zake iliidhinishiwa shilingi bilioni 30.87. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 24.87 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni sita ni kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufika Desemba, 2019, Wizara hii ilikuwa imepokea shilingi

bilioni 11.87 sawa na asilimia 38.4 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7. Kamati ilijulishwa kuwa fedha za miradi ya maendeleo zinatarajiwa kupokelewa hivi karibuni**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Filamu ina fanya kazi nzuri lakini ina changamoto za upungufu wa rasilimali watu na ukosefu wa magari. Kamati inaona kuna haja kubwa ya Bodi hii kupatiwa magari ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama ambavyo ni jukumu lake kuendesha operesheni na hivyo kuhitaji vyombo vya usafiri kufanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* imefanya kazi kubwa, hata hivyo ina changamoto za uhaba wa wafanyakazi wapatao 100 kwa ajili ya kuendesha chaneli za *TBC,* ukosefu wa studio za televisheni na majengo ya utawala Makao Makuu hapa Dodoma. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa endapo *TBC* itawezeshwa kikamilifu katika Chaneli ya Utalii, basi itasaidia kwa kiwango kikubwa katika kuvutia watalii na kuongeza Pato la Taifa kama ambavyo Korea ya Kusini imekuwa ikifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote ambao wametoa mafunzo kwa Kamati na inapenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa *LSP II* ambayo mara zote imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Kamati inapata mbinu za kusaidia utekelezaji bora wa majukumu yake. Sambamba nao, napenda kuwashukuru kwa dhati Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC), The Maryland University, Jhpiego,* SIKIKA, *UNICEF*, HAKIELIMU, *Save the Children*, *CAMFED* na SHIVYAWATA kwa kuendelea kukutana na Kamati na kuipa mafunzo. Ni imani ya Kamati kuwa wadau hawa wataendelea kushirikiana na Kamati katika siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, naomba kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu uhaba wa watumishi:-

Kwa kuwa, Sekta ya Afya, Elimu na Habari zina changamoto ya uhaba wa watumishi wa kutosha, kwa mfano Wizara ya Afya takribani asilimia 50;

Na kwa kuwa, uhaba huo umekuwa ukiathiri utoaji wa huduma za afya, elimu na habari kwa wananchi wetu;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali iweke mkakati kuongeza watumishi hawa muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utekelezaji wa lengo Na. 3 la maendeleo endelevu linalohusu afya, unalenga kuhakikisha kuwa tunakuwa na Taifa bora na lenye afya:-

Kwa kuwa, utekelezaji huo unakwamishwa na upatikanaji wa fedha usioridhisha;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali iamue kwa dhati kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza lengo hili ambalo pia linaenda na malengo ya ajenda 2063.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mloganzila ina upungufu wa watumishi takribani asilimia 50, uhaba wa nyumba za wafanyakazi na ukosefu wataalam wanaoweza kutumia vifaa vya kisasa vilivyopo katika Hospitali hiyo:-

Na kwa kuwa, upungufu huo una athari kubwa katika utoaji wa huduma ilhali wapo madaktari wengi mtaani waliohitimu lakini hawana ajira;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

Serikali iamue kwa dhati kutafuta watumishi kwa kutoa ajira ili wasaidie kutoa huduma inayoendana na hadhi ya hospitali hiyo hasa ikizingatiwa kuwa hospitali hiyo ni ya mfano, imejengwa kwa gharama na kuwekwa vifaa vya kisasa na vyenye ubora wa hali ya juu; na

(a) Serikali itenge fedha zitakazowezesha ujenzi wa nyumba za watumishi pamoja na mafunzo ya namna ya kutumia vifaa hivyo vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Hospitali ya Mloganzila imejengwa kisasa na ina vifaa na vifaa tiba vya teknolojia kubwa**.**

Na kwa kuwa, hospitali zenye vigezo hivyo zimekuwa zikitumika kutoa huduma za kibingwa na kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi kuja kupata huduma na kuchangia katika kuongeza Pato la Taifa na nchi kujulikana duniani;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri hospitali hiyo itumike kutoa huduma za kibingwa ili kuvutia wagonjwa wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuwa sehemu ya utalii wa kimatibabu *(Medical Tourism)*. Hii pia itasaidia kuchangia katika kuongeza pato la Taifa na nchi kujulikana duniani kama ambavyo nchi ya India imefanya na kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kuwa namba moja katika utalii wa kimatibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wagonjwa wa kimsamaha:-

Kwa kuwa, Sera ya Afya inataka makundi maalum kama wazee wasiojiweza, watoto chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito kupata huduma za afya bure;

Na kwa kuwa, makundi haya ndiyo yenye idadi kubwa ya wagonjwa wanaotibiwa katika Hospitali zetu na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa Hospitali hizo, kwa mfano Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Dodoma katika kipindi cha Julai, 2019, jumla ya wagonjwa 25,000 walipata msamaha wa matibabu wenye thamani ya shilingi milioni 867.5;

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Serikali iweke utaratibu wa kutoa ruzuku katika Hospitali hizi ili ziweze kujiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TMBA*:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na tabia ya uingizwaji wa bidhaa nchini zisizo kidhi viwango kwa kutumia njia za panya;

Na kwa kuwa uingizwaji huo wa bidhaa zisizokidhi viwango kwa kutumia njia za panya unachangiwa pia na uhaba wa watumishi na hususan wakaguzi katika vituo vya forodha;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kutoa kipaumbele kwa ajili ya watumishi hawa ili wasaidie katika kudhibiti uingizwaji wa bidhaa hizo ambazo zimekuwa na madhara kwa wananchi, lakini pia iweke mifumo bora ya udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya:-

Kwa kuwa uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya ni haki ya kila raia kwa maendeleo ya Taifa;

Na kwa kuwa, wananchi wengi wamekuwa wakikosa huduma za afya kutokanana na kutokuwa na Bima za Afya;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kutekeleza ahadi yake ya kuleta Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote utakaowezesha wananchi wote kuwa na Bima za Afya na hivyo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya wakati wote wa Bunge hili la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika,

Kwa kuwa, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vina nafasi kubwa ya kuchangia katika maendeleo ya nchi na watu wake endapo vitawezeshwa kibajeti na kimitaala;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuzishauri Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa uhamasishaji wa namna bora ya kupunguza ukatili huo na hata kujikinga na kutoa taarifa katika vyombo husika ikiwemo Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, BAKITA:-

Kwa kuwa, lugha ya Kiswahili imeamuliwa kuanza kutumika katika nchi za *SADC;*

Na kwa kuwa, ili lugha hii iweze kutumika vizuri kunahitajika huduma za ukalimani na tafsiri mbalimbali, ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za *SADC,* pamoja na uandaaji wa mitaala ya kufundishia na kujifunza ambavyo vyote hivyo vinahitaji bajeti ya kutosha kuweza kutekelezwa;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa BAKITA ili iweze kutumia fursa hii na kuhakikisha huduma hizo za msingi zinapatikana ikiwa ni pamoja na kuandaa walimu wa kutosha wa kufundisha Kiswahili katika nchi ambazo zina uhitaji kama vile Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Visimbuzi:-

Kwa kuwa imebainika kuwa Sekta ya Habari na hususan vyombo vya kurusha matangazo (visimbuzi) kwa njia ya televisheni vinakumbana na changamoto nyingi;

Na kwa kuwa , changamoto hizo zimekuwa zikiathiri utoaji wa huduma kwa wananchi;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali ifanye mabadiliko ya Sheria ya *EPOCA* ili kuondoa utata wa utendaji kati ya wamiliki wa mitambo/visimbuzi na waandaaji maudhui na hatimaye kuwepo na mazingira mazuri ya kibiashara;

(ii) Serikali itafute namna ya kuunganisha teknolojia katika kisimbuzi kimoja ambacho kitawawezesha Watanzania kupata habari kwa urahisi badala ya kuwa navyo vingi kama ilivyo sasa; na

(iii) *TCRA* isimamie utitiri wa televisheni za mitandaoni kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja vya Michezo:-

Kwa kuwa mojawapo ya nyenzo muhimu katika mafanikio ya michezo ni uwepo wa viwanja bora na vya kutosha;

Na kwa kuwa, hali ya viwanja vyetu vya michezo hapa nchini siyo nzuri lakini pia ni vichache, hivyo kuathiri sekta ya michezo;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Wizara na *TFF* kwa kushirikiana na wadau wengine waone namna ya kuboresha viwanja vya michezo kuanzia kujenga vingine ili kuweza kufanya vizuri kwenye ligi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu:-

Kwa kuwa, changamoto za Sekta ya Elimu ni nyingi kama vile mitaala isiyoendana na soko la ajira, upungufu wa walimu wenye ubora, ukosefu wa vifaa vya kufundishia na vitabu, mkinzano wa sera na sheria ya elimu, kukosekana kwa chombo huru na jumuishi cha kusimamia na kuratibu Sekta ya Elimu Msingi nchini na ukosefu wa mikopo kwa wanafunzi wa *NACTE;*

Na kwa kuwa, changamoto hizi zimeendelea kudidimiza elimu yetu hali ambayo ni hatari kwa Taifa letu;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri iundwe Tume ya Elimu ambayo itapitia upya muundo na mfumo wa elimu ili kushauri namna bora ya kuenenda na kuwa na mfumo utakaoendana na mwelekeo wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *University Classification*:-

Kwa kuwa, msingi mkuu wa Taifa lililo bora ni elimu nzuri inayotolewa na vyuo mbalimbali vilivyobobea kwenye masuala mbalimbali;

Na kwa kuwa bado hatujaweza kuainisha vyuo hivi kulingana na ubora wa elimu inayotoa kama ambavyo nchi za wenzetu zinafanya kwa mfano kule Marekani;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Wizara ya Elimu ianze kuviainisha vyuo na hatimaye kuzalisha watoto wenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, msingi bora wa elimu unaanzia kwenye Elimu ya awali ambapo elimu ni nyenzo muhimu sana;

Na kwa kuwa, bado nchi yetu ina uhaba wa walimu hao wa elimu ya awali nchini hali inayowafanya watoto kuingia katika Elimu ya Msingi bila kuwa wameandaliwa vizuri;

Kwa hiyo basi, kama mwanazuoni kutoka Italia Bi. Maria Montessori alivyowahi kusema *"Early Childhood Education is the key to the betterment of society"* Kamati inashauri:-

(i) Serikali iandae mkakati maalum wa kutenga vyuo vya kufundisha walimu wa shule za awali;

(ii) Ikiwezekana Serikali iruhusu upatikanaji wa walimu wageni wenye taaluma ya elimu ya awali kutoka nje ya nchi ili wasaidie kufundisha watoto wetu na hivyo kuwapa msingi bora wa elimu kwa maendeleo ya jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine Kamati inatoa ushauri juu ya mitaala kuendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda:-

Kwa kuwa, dunia inaenda kuendeshwa kwa teknolojia ya hali ya juu ambapo roboti na mitambo ya kisasa itakuwa ikifanya kazi zaidi kuliko nguvu za binadamu na kwa ujumla mfumo wa maisha ya mwanadamu utabadilika;

Na kwa kuwa, kama nchi bado mitaala yetu haijielekezi katika kutoa elimu inayoendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Wizara kuanza kuboresha mitaala ya elimu ili ilenge zaidi katika kutoa elimu itakayosaidia kuendana na mapinduzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufundi:-

Kwa kuwa, mipango ya nchi yetu ni kwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda ambao unategemea sana uwepo wa mafundi ambao wanazalishwa na vyuo vya ufundi;

Na kwa kuwa, bado Vyuo vyetu vya Ufundi hajiwazeshwa vya kutosha kuweza kuzalisha wataalam hao kutokana na utamaduni uliojengeka wa wanafunzi kukimbilia masomo ya digrii katika Vyuo Vikuu;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri,

(i) Serikali iwekeze Vyuo vya Ufundi nchini ili viweze kuzalisha mafundi wa kutosha watakaosaidia katika kuendesha viwanda nchini; na

(ii) Serikali iangalie sera na sheria zetu na kuzifanyia maboresho pale itakapobidi ili mikopo ya elimu ianze kutolewa kwa wanafunzi wa Vyuo vya Ufundi ili wanafunzi wengi zaidi waweze kujiunga.

Wakati wa Kongamano la elimu huko China Naibu Waziri wa Elimu wa China, Liu Kim mnamo mwaka 2014 wakati wa Kongamano hilo la Viongozi wa Vyuo Vikuu alitangaza uamuzi uliofikiwa wa kubadili Vyuo Vikuu 600 ambavyo ni nusu ya Vyuo Vikuu vya China. Lengo ni kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi wenye *degree* ambao wanagombania ajira zinazofanana ili kuzalisha watalaam hao wa ngazi ya kati ambao ndiyo wanahitajika kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, *scholarship*:-

Kwa kuwa, kuna wanafunzi wengi wanaomaliza Kidato cha Sita na kufanya vizuri;

Na kwa kuwa, wanafunzi hao wengine wamekuwa hawana uwezo wa kwenda kusoma katika Vyuo Vikuu na hivyo kuishia mitaani au Vyuo vya kawaida tu hapa nchini;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali ione namna ya kuanzisha tuzo ya udhamini kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitaala yao ya Kidato cha Sita na kuwapeleka katika vyuo bora duniani kama Harvard. Hii itasaidia kuongeza morali kwa wanafunzi wengine, lakini pia kuwa na Taifa lenye watu wenye *exposure* na elimu bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa namna ya pekee naomba nikushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa hii ya Mwaka ya

Kamati. Napenda kukupongeza kwa uongozi wako shupavu ambao umeuonyesha katika Bunge hili. Aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Mawaziri tunaofanya nao kazi ambao ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile; Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Juliana Shonza; Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako na Naibu wake Mheshimiwa William Ole Nasha kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati. Pamoja nao, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara zote tatu na watendaji wote wa Wizara hizo kwa utendaji mzuri ambao umekuwa ukiwezesha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu Mheshimiwa Juma S. Nkamia, kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Kwa namna ya pekee kabisa, napenda sana kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa imani waliyokuwa nayo kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati na kunipa ushirikiano mzuri ambao umesaidia katika utendaji wangu wa kazi kwa Kamati ambao majina yao yameorodheshwa kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee zaidi napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao Kamati imekuwa ikiupata wakati wote.

Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara katika Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati Ndugu Gelard Magili, Katibu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Catherine Kitutu kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KWA MWAKA 2019/ 2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza ni

Utangulizi wenye kueleza Muundo, Majukumu ya Kamati na kuainisha shughuli zilizotekelezwa na Kamati; Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo; Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na mwisho kabisa ni Hitimsho la Taarifa.

**1.1 Muundo wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu kama ifuatavyo: -

a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**1.2 Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuwa ni: **-**

a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja Taasisi zilizo chini yake; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika Kipindi cha Mwaka 2019/2020, Kamati ilitekeleza majukumu yake mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na:-

a) Kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

b) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia;

d) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji na utekelezaji wa bajeti wa Wizara na Taasisi kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2019);
e) Kupokea Maoni ya Wadau kuhusu masuala mbalimbali; na

f) Kushiriki Semina za mafunzo.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyoelezwa awali, katika kipindi cha Mwaka 2019/2020 Kamati imetekeleza majukumu yake ya Kikanuni kwa kufanya yafuatayo: -

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, mnamo mwezi Machi, 2019 Kamati ilikagua baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua jumla ya Miradi 7 iliyopo katika Mkoa wa Dar Es Salaam na Pwani. Miradi hiyo ni pamoja na;-

i) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;

ii) Mradi wa Ukarabati wa Chuo Kikuu Ardhi;,

iii) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere- Kigamboni;

iv) Mradi wa Ukarabati wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama;

v) Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala -Dar es salaam;

vi) Mradi wa Uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani – Tumbi; na

vii) Mradi wa Ujenzi wa Eneo la Changamani la Michezo- Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za kina kuhusu utekelezaji wa Miradi hiyo ziliwasilishwa kwenye Taarifa za Bajeti zilizowasilishwa Bungeni mwezi Mei, 2019.

### 2.2 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji Maoni ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji Maoni ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Shughuli hii ilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 98(2) ya Kauni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa hiyo, yapo baadhi ya maoni ambayo Kamati ilibaini kuwa hayajafanyiwa kazi kikamilifu na iliendelea kuyasisitiza katika Taarifa yake. Aidha, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa maana ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020 taarifa ya kina ni kama ilivyowasilishwa kwenye Bunge la Bajeti Mwezi Mei, 2019.

### 2.3 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Mwaka 2019/2020 Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zake kama ifuatavyo: -

#### 2.3.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa zifuatazo:-

**a) Utekelezaji wa Lengo Namba 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Good Health and Well-Being*)**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Taifa ambayo inawajibika katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals* – SDGs). Kamati ya Huduma ikiwa na wajibu wa kuisimamia na kuishari Serikali hususan Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa Lengo Namba 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalohusu Afya.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Wizara ilieleza utekelezaji wa lengo hili umekuwa na mafanikio kutokana na yafuatayo:-

i) Kuendelea kupungua kwa vifo vya akina mama na watoto;

ii) Kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto;

iii) Kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI kutoka **asilimia 5.1** mwaka 2011/2012 hadi **asilimia 4.7** mwaka 2016/2017;

iv) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya afya vikiwemo vituo vya afya na Hospitali za Mikoa;

v) Ongezeko la vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; na

vi) Uboreshaji wa maslahi ya watumishi wa afya kama malengo (*Targets*) na viashiria (*Indicators*) zinavyoeleza.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto zinazoikabili Wizara katika kutekeleza Lengo hili, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Ukosefu wa huduma za dharura ikiwemo upasuaji kwenye vituo vya afya hususan kwa mama na mtoto;

ii) Wigo mdogo wa wananchi waliopo katika mfumo wa bima ya afya (**asilimia 33**) ikilinganishwa na Lengo 3.8 linalotaka watu wote wawe kwenye Bima (*Universal Health Coverage*);

iii) Upungufu wa watumishi na wataalamu wa afya kwa takribani asilimia 52;

iv) Ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza; na

v) Upatikanaji mdogo wa fedha ikilinganishwa na mahitaji ya mipango na mikakati ya afya.

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizi hata hivyo, Kamati imebaini ukosefu wa fedha za kutosha unachangia kukwamisha utekelezaji mzuri wa Lengo. Kamati inaamini kuwa afya ndiyo utajiri wa Taifa lolote*** kama Mwanazuoni kutoka Marekani Pinkerton FJ. Alivyowahi kusema "***The wealth of the nation depends upon the health of its people or the health of the people determines the wealth of the nation". Hivyo Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuendelea kuwekeza fedha za kutosha katika Sekta ya Afya ili kutekeleza lengo hili kikamilifu.***

**b) Hospitali ya Mloganzila**

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao cha Kamati kilichofanyika mwezi Agosti, 2019, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya Hospitali ya Mloganzila. Taarifa hiyo ilionesha kuwa tangu kuanzishwa kwake, kumekuwa na ongezeko la idadi ya wagonjwa wa ndani na nje kwa **asilimia 48**, wagonjwa wa upasuaji kwa **asilimia 107** na ongezeko la makusanyo ya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa juu ya changamoto ambazo Hospitali inakutana nazo, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa watumishi kwa **asilimia 50**, ukosefu wa nyumba za Watumishi na ukosefu wa utaalamu kwenye kutumia vifaa vya kisasa vilivyopo hali inayoathiri utendaji bora wa Hospitali hiyo ya kisasa.

**Mheshimiwa Spika, *uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa changamoto ya watumishi inaathiri utekelezaji mzuri wa majukumu. Hospitali hii ni moja ya Hospitali ambazo zimejengwa kisasa na ni Hospitali ya mfano. Serikali ione namna nzuri ya kuitumia Hospitali hii kwa manufaa ya Watanzania.***

**c) Chuo cha Maendeleo ya Jamii - Tengeru**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu Utendaji wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hiyo ilifafanua masuala mbalimbali yakiwemo utendaji kazi wa Chuo, hali ya upatikanaji wa fedha na changamoto ambazo Chuo kinakumbana nazo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Chuo kiliidhinishiwa jumla ya **shilingi Bilioni 4.7.** Kufikia Mwezi Juni, 2019 kiasi cha **shilingi Bilioni 3.5** sawa na **asilimia 74.4** ya kiasi cha **shilingi Bilioni 4.7** kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 kilikuwa kimepokelewa. Aidha, kuhusu ukukusanyaji wa Maduhuli Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2019 Chuo kilifanikiwa kukusanya kiasi cha **shilingi Bilioni 1.73** sawa na **asilimia 82 ya shilingi Bilioni 2.1** zilizokadiriwa kukusanywa katika mwaka huo wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji huo wa fedha uliwezesha Chuo kutekeleza baadhi ya majukumu iliyojipangia. Sambamba na majukumu hayo, Kamati pia ilielezwa juu ya changamoto mbalimbali ambazo Chuo inakumbana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na
i) Ukosefu wa Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo;

ii) Ukosefu wa Uwanja wa michezo na Hosteli kwa ajili ya wananchuo;

iii) Ukosefu wa Hati miliki ya eneo la Chuo; na

iv) Uchakavu wa Miundombinu zikiwemo kumbi za mihadhara.

**d) Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa kuhusu utendaji wa Mamlaka ya Chakula na Vifaa Tiba (TMDA) ambayo hapo awali ilikuwa ikiitwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). TMDA imeanza kutekeleza majukumu yake rasmi tarehe 1 Julai, 2019 baada ya Serikali kuhamisha majukumu ya Chakula na Vipodozi kutoka TFDA kwenda Shirika la viwango Tanzania (TBS) na hii ni kwa mujibu wa Sheria Na. 4 cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa majukumu ya TMDA ni pamoja na Kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa chakula, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi; Kutathmini na kusajili chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi; na Kusajili maeneo na kutoa vibali vya biashara ya chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi;

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, yapo baadhi ya mafanikio ambayo Mamlaka imeyapata tangu kuanzishwa kwake. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

i) Kuwa kitovu cha umahiri (*Centre of Excellence*) katika tathmini na usajili wa dawa barani Afrika;

ii) Kufikia hatua ya umahiri (*Maturity Level 3*) ya mifumo ya udhibiti wa dawa kwa mujibu wa viwango vya WHO na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Barani Afrika kufikia hatua hiyo;
iii) Kupata ithibati ya ISO katika mifumo ya uchunguzi wa kimaabara wa chakula ikiwa ni pamoja na maabara ya mikrobailojia; na

iv) Kulinda afya ya jamii kwa kupunguza kwa kiasi kikubwa uwepo wa bidhaa duni na bandia kwenye soko kwa kuweka mifumo mahiri ya udhibiti kutoka **asilimia 18** mwaka 2003 hadi **asilimia 1** mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa changamoto kuu mbili ambazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu ya TMDA. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

i) Ukosefu wa sheria moja ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kukidhi mahitaji ya sasa ya udhibiti kwa kuwa hata makosa na adhabu katika sheria iliyopo zimepitwa na wakati; na

ii) Uhaba wa watumishi na hususan wakaguzi katika vituo vya forodha, tathmini ya bidhaa na uchunguzi wa kimaabara.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na TMDA na changamoto wanazokumbana nazo lakini pia ***Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya baadhi ya bidhaa ambazo nyingine siyo salama kwa matumizi ya binaadamu kuingizwa nchini kutokana na uwepo wa mipaka isiyo rasmi. Kamati inaona kuna haja ya kuweka mifumo bora ya udhibiti kwenye mipaka hiyo maarufu kama Njia za Panya.***

**e) Utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuhusu changamoto na utatuzi wake katika mabadiliko ya huduma za vifurushi ya Bima ya Afya.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya NHIF ambayo ilieleza masuala mbalimbali ya utendaji yenye kuonyesha mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Kuendelea kujumuisha makundi mbalimbali ya wanachama katika Mfuko;

ii) Kuendelea kuongeza usajili wa vituo vya kutoa huduma katika ngazi zote; na

iii) Kuanzisha mpango wa kupelekea Madaktari Bingwa katika maeneo ya pembezoni;

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto ambazo NHIF inazokumbana nazo katika utoaji wa huduma. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Kupanda kwa bei za huduma za afya;

ii) Uhiari mdogo wa wananchi kujiunga na Mfuko; na

iii) Kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza kama sukari, presha n.k ambayo yanatumia fedha nyingi kuyatibu na hivyo kuongeza mzigo mkubwa kwa Mfuko.

**Mheshimiwa Spika, *Kamati inaona kuna haja ya kuongeza elimu ya namna ya kupambana na magonjwa haya yasiyoambukiza ili kupunguza mzigo wa kuyatibu.***

#### 2.3.2 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wizara hii**,** Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wake kama ifuatavyo:-

**a) Changamoto za usimamizi na udhibiti wa Sekta ya Habari na hususan vyombo vya kurusha matangazo (visimbuzi) kwa njia ya televisheni.**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ilieleza kuwa katika utekelezaji wa jukumu lake kuu la kusimamia vyombo vya habari kwa maana ya miundombinu ya kurusha matangazo kwa mujibu wa Sheria, TCRA ilitoa leseni za ujenzi wa Miundombinu ya utangazaji (DTT) na kuendelea kuzisimamia ili ziweze kufuata masharti ya ujenzi na usambazaji wa miundombinu husika.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu hayo, TCRA imeeleza uwepo wa changamoto zifuatazo;-

i) Waliopewa leseni hawakuweza kujenga na kusambaza miundombinu kulingana na makubaliano ya usambazaji;

ii) Wamiliki wa televisheni walikuwa wakiwalipisha fedha wateja ili kuweza kutazama maudhui yasiyopaswa kulipiwa; na

iii) Wenye leseni za maudhui ya nje ya kulipia nao walikuwa wakiwalipisha wateja maudhui ya ndani (FTA-Local) yasiyopaswa kulipiwa licha ya leseni zao kutoruhusu urushaji wa chaneli za ndani (*Local channels*) ambapo ni kinyume na kifungu Na. 13(4) cha EPOCA

**Mheshimiwa Spika *uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna changamoto za kisheria ambazo zinaathiri Sekta hii muhimu. Kamati inaendelea kushauri Wizara ya Habari pamoja na TCRA wakae kwa pamoja na waiangalie sheria hii na kushauri namna bora ya kufanya ili kukuza Tasnia hii muhimu.***

**b) Mkakati wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) wa kukuza Lugha ya Kiswahili**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya BAKITA ilieleza chimbuko la lugha ya Kiswahili kuanza kutumika katika nchi zilizo Kusini Mwa Jangwa la Sahara (SADC) kuwa ni Mkutano wa Wakuu wa Nchi

wanachama uliofanyika tarehe 18 Agosti, 2019 jijini Dar es salaam. Kamati ilielezwa kuwa pamoja na masuala ya Kiswahili kuwa ni moja ya fursa katika nchi za SADC, pia huduma zifuatazo zitahitajika katika mikutano hiyo. Huduma hizo ni pamoja na: - Ukalimani na tafsiri mbalimbali, Ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za SADC, Kutunga vitabu, mitaala ya kufundishia na kujifunza Kiswahili, Uandishi na utangazaji wa habari, na Kuimarika kwa utalii na utamaduni kwa wageni kuja kujifunza na kuifahamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mambo mengine yatakayopatikana kwa Kiswahili kuwa ni lugha ya mawasiliano, Wizara iliainisha Mikakati ya kutumia fursa hizo kama ifuatavyo: -
i) Kuratibu upatikanaji wa wakalimani wafasiri pamoja na vifaa vya ukalimani kwa ajili ya Mikutano ya SADC;

ii) Kutambua vijana wa kitanzania wenye uwezo wa kukalimani katika lugha rasmi za SADC;

iii) Kuandaa Kanzi data ya Wataalamu wa Kiswahili wenye uwezo wa kutoa huduma mbalimbali za Kiswahili katika nchi za SADC;

iv) Kuratibu ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za SADC nje ya mfumo rasmi wa elimu; na

v) Kuratibu utungaji wa mitaala ya kufundishia Kiswahili SADC nje ya mfumo rasmi wa elimu.

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mkakati huu mzuri ni imani Mkakati huu utasaidia katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili na kutoa ajira kwa Watanzania.***

### 2.3.3 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara hii, Kamati Ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa mbalimbali za utendaji kama ifuatavyo: -

**a) Utekelezaji wa Lengo Namba 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Quality Education*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu namna Wizara inavyotekeleza Lengo hili. Kamati imebaini kuwa kwa kiasi fulani Wizara imefanikiwa katika utekelezaji wa lengo hili. Baadhi ya mambo ambayo yanaonekana kuwa mafanikio ni pamoja na:-

i) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa (Wavulana na wasichana katika elimu ya awali, msingi na sekondari kwa wastani wa **asilimia 27.7**;

ii) Kutekeleza azma ya kuwa na elimu jumuishi kwa kuchapisha nakala 24,400 za vitabu nukta nundu kwa wanafunzi wa shule za msingi na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na

iii) Ongezeko la **asilimia 61.2** la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa katika Elimu ya Ufundi pamoja na uboreshaji wa vyuo vya ufundi.

**Mheshimiwa Spika,** mbali ya mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto katika utekelezaji wa lengo hili, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Ukosefu wa walimu wa kutosha kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa;

ii) Uhaba wa miundombinu kama madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu; na

iii) Ukosefu wa vifaa vya kufundishia.

***Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa mafanikio hayo. Aidha, inashauri nguvu zaidi kwa sasa ielekezwe kwenye ubora ili kuweza kutekeleza vyema lengo hili na kupambana na ujinga na umaskini kama ambavyo*** *mwanazuoni Charles Rangel alivyowahi kusema* ***"A quality education grants us the ability to fight war on ignorance and poverty"***

**b) Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi na Teknolojia – Mbeya.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Oktoba, 2019, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Chuo hiki. Katika Taarifa hiyo masuala mbalimbali yalielezwa yakiwemo ya shughuli kuu za Chuo ambazo ni kutoa mafunzo ya ngazi mbalimbali ikiwemo za stashahada; Kufanya tafiti mbalimbali kwa kuanzisha kurugenzi ya tafiti ili kuwapa wataalamu ujuzi mbalimbali na Kutoa ushauri wa kitaalamu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Chuo kimetekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya kutoa elimu, kutoa ushauri wa kitaalamu katika miradi 25 ya ujenzi wa miundombinu ya taasisi mbalimbali; kimetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Ujenzi wa Maktaba yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 2500 ambapo ujenzi wake umekamilika kwa **asilimia 93** kwa awamu ya kwanza. Aidha, Chuo kimekarabati vyumba vya ofisi kwa kiasi cha shilingi **milioni 62** ambazo zilitengwa na chuo na Wizara iliongeza kiasi cha shilingi **milioni 750** kutoka katika mradi wa ESPJ ambao mradi ukikamilika utaweza kutoa ofisi zipatazo 80 zenye kutosha watumishi 320.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri ambazo Chuo kinafanya, Makamu Mkuu wa Chuo alieleza kuhusu changamoto kuu mbili zinazokikabili Chuo kuwa ni Uchakavu na Upungufu wa miundombinu na Upungufu wa Watumishi katika kada mbalimbali.***Kamati iliwahi kutembelea Mradi huo wa Ujenzi wa Maktaba mwezi Machi, Mwaka 2018 na inatoa rai ujenzi huo ukamilike mapema ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata sehemu ya kujisomea na kufanya rejea ya vitabu na nyaraka mbalimbali.***

**2.4 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka (2018/2019) iliyowasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa Mwezi Januari, 2019**

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti, 2019 pamoja na majukumu mengine, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa na Bunge katika kipindi cha mwezi Februari, 2019 kwa Wizara zote tatu inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati** ***inaonesha kuwa yapo baadhi ya Maazimio ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu hususan suala la upatikanaji wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo na uhaba wa Watumishi. Kamati itaendelea kuyasisitiza masuala haya kwenye Taarifa hii.***

**2.5 Kupokea Maoni ya Wadau kuhusu Mafanikio na Changamoto za Mfumo wa Elimu katika Sekta ya Elimu Tanzania.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika shughuli za Kamati zilizofanyika mwezi Oktoba, 2019 Kamati ilijadili Mafanikio na Changamoto za Mfumo wa Elimu katika Sekta ya Elimu Tanzania. Ili kuweza kufanikisha shughuli hiyo, Kamati ilialika Wadau mbalimbali wa Sekta ya Elimu kwa ajili ya kupata maoni yao. Mwaliko huo ulitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (9) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Wadau mbalimbali waliweza kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao, Wadau hao ni pamoja na TAPIE, Haki Elimu, Policy Forum, TENMET, UWEZO na TWAWEZA. Wadau hao walieleza changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika mafanikio ya Sekta ya Elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** wadau walibainisha Changamoto mbalimbali zinazoikumba Sekta ya Elimu. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa walimu wenye sifa, ukosefu wa elimu ya awali, uhaba wa vifaa vya kufundishia, Mitaala isiyoendana na wakati, ukosefu wa vitabu, Mkinzano wa Sera ya Elimu na Sheria ya Elimu, Kukosekana kwa Chombo huru na Jumuishi cha kusimamia na kuratibu Sekta ya Elimu Msingi nchini, Kodi ya Ardhi na Mgawanyo wa Walimu. Kamati ilipokea maoni hayo na kuyawasilisha kwa Serikali (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI) kwa ajili ya kufanyiwa kazi. ***Ni Imani ya Kamati kuwa Serikali itafanyia kazi changamoto zote zilizoainishwa na wadau kwa lengo la kuboresha Mfumo wa Elimu nchini.***

### 2.6 Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2019)

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia tarehe 13 hadi 24 Januari, 2020, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa majukumu na Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2019). Lengo la vikao hivyo lilikuwa ni kupata picha na mwenendo wa utekelezaji wa majukumu, upatikanaji wa fedha, ukusanyaji wa maduhuli na changamoto ambazo Wizara na Taasisi zimekumbana nazo katika kipindi cha nusu mwaka wa bajeti.

#### 2.6.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia


**Mheshimiwa Spika**, katika Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara yenyewe, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)kama ifuatavyo:-

**a) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara (**Fungu 46)** kuhusu utekelezaji wa majukumu na Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba,2019) na masuala mbalimbali yalibainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Disemba, 2019 Wizara (**Fungu 46)** ilikuwa imekusanya jumla ya **shilingi 255,390,132,105.51** sawa na **asilimia 46.1** ya kiasi cha **shilingi 553,739,899,119.13** zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makusanyo ya Idara na Vitengo ni chini ya asilimia hamsini (**asilimia 32.62 ya lengo)**. Aidha, Kamati imebaini kuwa makusanyo ya **asilimia 50.8** yanatoka katika Taaasisi za Maendeleo ya Elimu Msingi kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1 **Kamati inazipongeza Taasisi za Maendeleo ya Elimu Msingi kwa ukusanyaji mzuri.**

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli - Fungu 46 (Julai - Disemba, 2019)**





***Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Elimu ya Tarehe 14 Januari 2020 na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Wizara (Fungu 46) ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 1,386,508,723,272.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 523,788,923,012.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (mishahara **Shilingi 450,356,645,012.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 73,432,278,000.00**) na **Shilingi 862,719,800,260.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo (fedha za ndani ni **Shilingi 583,415,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 279,304,800,260.00**).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba 31, 2019 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 610,909,534,090.76** sawa na **asilimia 44.** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 271,145,921,279.12** ni Matumizi ya Kawaida (**Shilingi 197,099,676,089.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 74,046,245,190.12** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo). Aidha, Shilingi **339,763,612,811.64** zimepokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha za OC umezidi kiwango kutokana na nyongeza ya **Shilingi 19,472,049,013.12** katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi ikiwa ni kwa ajili ya kulipa madeni ya stahili za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu ikijumuisha pango la nyumba na tuzo za mikataba. ***Kamati inapongeza sana Serikali kwa kuanza kufanya malipo hayo ambayo yalikuwa kero kubwa kwa Wahadhiri wetu.***

**Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha –Fungu 46 (Julai - Disemba, 2019)**





| | Kawaida | Maendeleo | JUMLA |
|---|---|---|---|
| KILICHOIDHINISHWA | 523,788,923,012 | 862,719,800,260 | 1,386,508,723,272 |
| KILICHOPATIKANA | 271,145,921,279 | 339,763,612,811 | 610,909,534,090 |
| ASILIMIA | 52 | 39 | 44 |

***Chanzo: Taaifa ya Wizara ya Elimu ya tarehe 14 Januari na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati pia inapongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake. uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Fungu 46 imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka shilingi Bilioni 799.02 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi Trilioni 1.38 Mwaka wa Fedha 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 42.3. Kwa ujumla shilingi Trilioni 7.4 zimetengwa kwa ajili ya Elimu kupitia Fungu 46 kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014/2015 hadi 2019/2020 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 3. Ikumbukwe kuwa fedha hizi hazijajumuisha fedha zinazotengwa kupitia TAMISEMI kwa ajili ya Elimu. Kamati inaendelea kupongeza jitihada hizi za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendelea kuona umuhimu wa Elimu nchini na kuongeza bajeti yake mwaka hadi mwaka.***

**Kielelezo Na 3 Bajeti ya Wizara ya Elimu (Fungu 46) kwa Miaka 5**




***Chanzo: Taarifa za Wizara ya Elimu (Fungu 46) kwa miaka 5 na Usanifu wa Kamati***

**b) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilieleza masuala mbalimbali yakiwemo ya hali ya upatikanaji wa fedha ambapo hadi kufikia mwezi Disemba 2019, Bodi ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi Bilioni 265.96** sawa na **asilimia 59.1** ya **shilingi Bilioni 450** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Fedha hizo zimewezesha Bodi kutoa Mikopo kwa **Wanafunzi wa mwaka wa kwanza 49,493** sawa na **asilimia 108.8** ya **wanafunzi 45,485** waliokadiriwa na **wale wanaoendela na masomo wapatao 80,579** sawa na **asilimia 97.3** ya **wanafunzi 82,800** waliokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu urejeshaji wa mikopo, kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2019, Bodi ilifanikiwa kukusanya jumla ya **shilingi Bilioni 95.13** sawa na **asilimia 43** ya **shilingi Bilioni 221** zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa warejeshaji wa mikopo **asilimia 70 wanatoka kwenye Sekta za Umma na asilimia 30 ni Sekta Binafsi.** ***Kamati inaendelea kuhimizia Sekta Binafsi kushirikiana na Bodi ili kubaini wanufaika wa mikopo walipo kwenye Sekta hizo na hivyo kuanza kurejesha mikopo hiyo kwa faida ya watanzania wengine.***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu hayo yaliyotekelezwa, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto mbalimbali ambazo zinaikumba Bodi zikiwemo za:-

i) Upungufu wa watendaji wenye ujuzi mahsusi kama ubunifu wa nyenzo za Ki –TEHAMA na umahiri katika takwimu mahsusi;

ii) Ukiukwaji wa sheria kwa baadhi ya waajiri na wanufaika; na

iii) Uwiano katiya uhitaji wa waombaji na mahitjai ya kitaifa ya rasilimali.

**c) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya NACTE ambayo ilijikita katika kueleza masuala mbalimbali yakiwemo ya utekelezaji wa majukumu, upatikanaji wa fedha na changamoto ambazo inakumbana nazo.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, NACTE iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 16,288,029,166.** Kati ya Fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yaliidhinishiwa **shilingi 11,888,029,166** na **shilingi 4,400,000,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 3 Disemba, 2019 NACTE lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi 4,283,868,903** sawa na **asilimia 26.3** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge**.**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli, hadi kufikia tarehe 3 Disemba 2019, Baraza lilikuwa limekusanya jumla ya **shilingi 2,709,043,571** sawa na **asilimia 31.3** ya Makadirio ya makusanyo ya **shilingi 8,661,662,500.** Kamati ilielezwa kuwa, Baraza halijafikia lengo la makusanyo yake ya ndani (asilimia 50) kutokana na vyuo vingi kuchelewa kuwasilisha malipo ya ada ya uhakiki ubora (*Quality Assuarance Fee*) kutoka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika dirisha la udahili wa mwezi Oktoba 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa upatikanaji huo wa fedha hizo umewezesha NACTE kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo:

i) Kutoa usajili kwa vyuo 24 katika bodi za masomo za mbalimbali pamoja na ithibati kwa Vyuo 19 katika fani hizo;

ii) Kuidhinisha kuanzishwa kwa idara/program saba (7) katika jumla ya vyuo saba (7) na vyuo 17 vimekaguliwa ili kuhakikisha elimu na mafunzo yanatolewa yanalingana na vigezo vilivyowekwa na Baraza;

iii) Kufuatilia vyuo 109 na kufanya tathmini ya ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivyo na kufuta usajili wa vyuo viwili (2), vyuo vinne (4) vilizuiliwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha upungufu uliobainika. Aidha, Vyuo 103 vilipatiwa ushauri kuhusu namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo;

iv) Kufanya tathmini ya vyeti vya wahitimu 16,549 vilivyopokelewa kwa ajili ya kutoa namba ya uthibitisho (*Award Verification Number* - AVN) ili kudhibiti uendeshaji wa mafunzo bila kufuata kanuni na sheria zilizowekwa na Baraza, Aidha, utoaji wa AVN umesaidia kuepusha udanganyifu wa wahitimu wanaoendelea na elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na majukumu hayo, Kamati ilielezwa juu ya changamoto zifuatazo ambazo NACTE inakumbana nazo: -

i) Upungufu wa majengo ya ofisi, kumbi za mikutano na sehemu za huduma unaotokana na kupanuka kwa shughuli za Baraza, hasa katika Ofisi za Kanda;

ii) Upungufu wa rasilimali watu;

iii) Upungufu wa vitendea kazi kama vile magari kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa kazi za Baraza; na

iv) Uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Miradi ya Maendeleo.

**d) Taasisi ya Teknolojia (DIT)**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya DIT iliyowasilishwa mbele ya Kamati mnamo tarehe 15 Januari 2015 na ilieleza masuala mbalimbali yakiwemo ya hali ya udahili wa wanafunzi, programu zinazotolewa na Taasisi, utekelezaji wa majukumu na hali ya upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, DIT ilikadiriwa kukusanya **shilingi 5,000,000,000.** Hadi kufikia Disemba 2019 ilifanikiwa kukusanya **shilingi 2,084,872,203** sawa na **asilimia 41.7** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa bajeti**,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, DIT iliidhinishwa kiasi cha **shilingi 22,373,227,478**. Kati ya fedha hizo Mishahara ilitengewa **shilingi 9,590,227,000,** matumizi mengineyo yalitengewa **shilingi 806,790,466** na Miradi ya Maendeleo **shilingi 11,976,210,012.** Hadi kufikia Disemba 2019, kiasi cha **shilingi 5,489,486,284** sawa na **asilimia 24.5** ya bajeti yote iliyoidhinishwa kilipokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji huo wa fedha umewezesha DIT kutekeleza majukumu mbalimbali iliyojipangia. Baadhi ya majukumu yaliyotekelezwa ni pamoja na: -

i) Kudahili jumla ya wanafunzi wapya 2045 (956 Diploma, 1027 Shahada ya kwanza na 42 shahada ya uzamili);

ii) Kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali kama afya, kilimo, elimu;

iii) Kukamilisha upanuzi wa jengo la Maktaba;

iv) Kukamilisha ujenzi wa jengo la *DIT Teaching Tower* awamu ya pili na ya mwisho inayohusu kusimika samani za ndani na miundombinu ya TEHAMA; na

v) Kufanya Mapitio ya Mitaala ambapo jumla ya Mitaala 14 imendelea kufanyiwa mapitio na kuboreshwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali ambazo DIT inakumbana nazo kama ifuatavyo:-

i) Idadi ndogo ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na mafunzo ya ufundi kutokana na uhaba wa Hosteli;

ii) Ufinyu wa nafasi na uchakavu wa majengo unaozuia uwezo wa Taasisi kuongeza udahili wa wanafunzi;

iii) Uhaba wa wakufunzi na wahadhiri waliobobea kwenye fani za sayansi; na

iv) Kushindwa kuhudumia vyema wanafunzi wa Stashahada ya Uhandisi wanaogharamiwa na Serikali kutokana na kutokuwa na bajeti yakutosha.

**2.6.2 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, katika Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Mafungu yote mawili (52 na 53), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na Hospitali ya KCMC kama ifuatavyo: -

**a) Idara Kuu Afya (Fungu 52)**


**Mheshimiwa Spika**, katika kikao cha Kamati cha tarehe 20 Januari 2020, Kamati Ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2019). Taarifa ya Wizara ilijikita katika masuala mbalimbali yakiwemo ya vipaumbele vilivyowekwa na Wizara kwa Mwaka 2019/2020, bajeti, makusanyo ya maduhuli na changamoto ambazo Wizara inakumbana nazo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza vipaumbele ambavyo Wizara ilijipangia, jumla ya **Shilingi 959,152,164,597.00** ziliidinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 415,014,262,000.00** sawa na **asilimia 43.2** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida (Shilingi **93,927,890,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 321,086,372,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake). Aidha, fedha kwa ya ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo jumla ya **Shilingi 544,137,902,597.00** sawa na **asilimia 56.8** ziliidhinishwa ambapo **Shilingi 270,600,000,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **273,537,902,597.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia 31 Disemba 2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 239,502,526,663.02** sawa na **asilimia 25** ya **Shilingi 959,152,164,597.00** zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 147,932,098,261.21** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 44,048,948,875.33** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Shilingi 47,521,479,526.48** (Fedha za ndani **Shilingi 16,276,131,290.48** na fedha za nje na **Shilingi 31,245,348,236**) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati imefanya uchambuzi na imebaini kuwa kwa bajeti ya Wizara ya Afya kupitia Fungu 52 imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi Bilioni 713.7 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi Bilioni 959.1 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 31.4 (Rejea Kielelezo Na. 4). Kwa ujumla katika kipindi hicho cha miaka mitano bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii (Fungu 52) imefikia shilingi Trilioni 5.2 bila kujumuisha fedha zilizotengwa kupitia TAMISEMI. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendelea kujali afya za watanzania.***

**Kielelezo Na 4: Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Miaka 5**




**Chanzo: Taarifa za Wizara ya Afya kwa miaka mitano na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, Kamati ilielezwa kuwa kiasi cha **shilingi 368,536,195,026** kilipangwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali katika Mwaka wa Fedha 209/2020. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 21,354,361,184.00 (asilimia 5.8)** kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 54,567,570,602** (**asilimia 14.9**) kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, na kutoka katika Mashirika yaliyo chini ya Wizara **Shilingi 292,614,263,240 (asilimia 79.3)** zilikadiriwa kiukusanywa**.** Hadi kufikia Disemba 2019, jumla ya **Shilingi 216.708.229.771** zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 59** ya lengo**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Hospitali za Rufaa na Mikoa zimeongoza kwa makusanyo kwani zimekusanya asilimia 61 ya lengo ikilinganishwa na Makao Makuu ya Wizara ambayo imekusanya asilimia 49 ya lengo (Rejea Kielelezo Na. 5). Kamati inapongeza sana Hospitali hizi na ina amini kuwa kufikia Juni 30 lengo la makusanyo litafikiwa au kuzidi kabisa.**

**Kielelezo Na. 5: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Fungu 52**
**Idara Kuu Afya (Fungu 52) : Makusanyo ya Maduhuli (Julai - Disemba 2019)**

| Idara Kuu Afya (Fungu 52) : Makusanyo ya Maduhuli (Julai - Disemba 2019) | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio** | **Makusanyo** | **Asilimia** |
| Wizara | 21.354.361.184 | 10.381.800.812 | 49 |
| Hospitali za Rufaa | 54.567.570.602 | 33.481.205.297 | 61 |
| Mashirika | 292.614.263.240 | 172.845.223.662 | 59 |
| **JUMLA** | **368.536.195.026** | **216.708.229.771** | **59** |

***Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Afya (Fungu 52) ya Tarehe 20 Januari, 2020***

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha kwa Fungu 52 umewezesha Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali iliyojiwekea, baadhi ya majukumu ambayo yametekelezwa ni pamoja na:-

i) Kutoa chanjo ya magonjwa surua, donda koo, ugonjwa wa kupooza na mengineyo kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kwa ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 10.6** kimetolewa kati ya shilingi **bilioni 15** zilizoombwa ambayo ni sawa na **asilimia 71** ya lengo;

ii) Kuteleleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira hapa nchini kwa kuhimiza matumizi ya vyoo bora katika kaya na taasisi kupitia Kampeni ya Nyumba ni Choo ambapo takribani matangazo ya runinga 1,400 na Redio 5,390 yalirushwa katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2019;

iii) Jumla ya wataalamu 204 walijengewa uwezo wa utayari wa kukabiliana na ugonjwa wa Ebola ambapo wadau 42 kutoka katika sekta ya usafiri na usalama walihamasishwa kuhusu udhibiti wa ugonjwa huo kupitia sekta ya usafiri. Vile vile miongozo ya kukabiliana na matukio ya dharura (*Public Health Emergence Contigency Plan*) kwa mipaka ya Murusagamba na Murongo mkoani Kagera iliandaliwa.; na
iv) Mikakati ya Afya na Usafi Mazingira na Udhibiti wa Mbu na Wadudu wadhurifu iliandaliwa ili kukabiliana na magonjwa ya milipuko kama vile Kipindupindu, Dengue, Malaria, kuhara na magonjwa mengine yatokanayo na uchafuzi wa mazingira

**Mheshimiwa Spika**, sambamba utekelezaji huo wa majukumu, Kamati ilielezwa juu ya Changamoto ambazo Wizara inakumba nazo kuwa ni pamoja na:-

i) Vituo vya kutolea huduma za Afya kutowasilisha mahitaji ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa wakati jambo linalosababisha kuchelewa kupata dawa kwa wakati;

ii) Wigo mdogo wa wananchi walio katika mifumo ya Bima za Afya;

iii) Upungufu wa watumishi wenye taaluma ya kutoa huduma za afya ikilinganishwa na mahitaji hususan katika ngazi za chini;

iv) Kuongezeka kwa watu wenye magonjwa yasiyo ya kuambukiza;

v) Upungufu wa rasimali fedha za kutekeleza majukumu ya sekta ya afya kulingana na mipango na mikakati ili kutoa huduma bora kwa wananchi; na

vi) Ongezeko kubwa la idadi ya watu lisiloendana na uwezo wa nchi katika kuwahudumia.


**b) Idara Kuu Maendeleo ya Jamii (Fungu 53)**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii (Fungu 53) kwa kipindi cha nusu (Julai – Disemba 2019) ilijikita katika kueleza hali ya upatikanaji wa fedha na namna ulivyowezesha kutekeleza baadhi ya majukumu ambayo Wizara ilikuwa imejipangia, hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli na changamoto ambazo Idara inakumbana nazo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii) iliidhinishwa na Bunge jumla ya **Shilingi 31,537,431,013.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 28,777,370,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 15,825,478,000.00** na Shilingi **12,951,892,000.00** kwa ajili ya Mishahara). Aidha, **Shilingi 2,760,061,013.00** zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo (Shilingi **1,000,000,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **1,760,061,013.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, kufikia Disemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 14,301,662,940.00** sawa na **asilimia 45** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa **Shilingi 8,001,505,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyodhinishwa kwa ajili hayo, **Shilingi 4,706,241,169.00** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 36** na **Shilingi 1,593,916,771.00** zimepokelewa kwa ajili Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 57**. (Rejea Kielelezo Na. 6)

### Kielelezo Na. 6 Upatikanaji wa Fedha - Fungu 53 (Julai - Disemba, 2019)




***Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Afya (Fungu 53) ya tarehe 21 Julai na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu maduhuli Wizara ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 4,763,596,000.00**. Hadi kufikia Disemba, 2019, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 2,103,170,107.11** sawa na **asilimia 44** ya makadirio ya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa upatikanaji wa fedha umewezesha Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali iliyojipangia. Baadhi ya majukumu ambayo Wizara imefanikiwa kuyatekeleza ni kama ifuatavyo:-

i) Vyuo vya Maendeleo ya jamii kama Monduli, Rungemba, Tengeru na Uyole vimeendelea kuamsha ari ya wanachi kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwemo kutoa mafunzo ya kuandaa chakula bora na unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa washiriki 50 na ujenzi wa vyoo bora katika maeneo yao;

ii) Vituo sita vya Kidigitali vya Ubunifu vimeanzishwa kwenye Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Monduli, Rungemba, Buhare, Ruaha na Misungwi Ili kuibua na kukuza mawazo na vipaji vya kibunifu miongoni mwa wanafunzi na jamii;

iii) Dawati la Jinsia na Watoto limeanzishwa katika Vituo vya Polisi vya Mbweni, Kimara na Mburahati na kufikia idadi ya madawati 420 yaliyoanzishwa katika Vituo vya Polisi;

iv) Wizara imezindua Kampeni ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ijulikanayo kama "**TWENDE PAMOJA: UKATILI TANZANIA SASA BASI** "; na Uanzishwaji wa madawati 26 ya kupinga ukatili dhidi ya watoto katika Shule za Msingi na Sekondari katika Halmashauri za Mkoa wa Rukwa;

v) Wizara pia imetoa mafunzo kwa watoa huduma 140 wa mahakama za watoto walio katika mkinzano na sheria kuhusu namna bora ya kuendesha mashauri ya watoto mahakamani. Lengo la mafunzo haya ni kuboresha uendeshaji wa mashauri ya watoto katika mahakama za watoto 134 zilizopo katika mikoa 23;

vi) Watoto 13 (wakike 7 na wakiume 6) walipata huduma ya kuasili na watoto 24 (wakike 12 na wakiume 12) walipata huduma ya malezi ya kambo;

vii) Leseni 35 za usajili wa Makao ya watoto zimetolewa. Usajili wa Makao ya watoto umeongezeka kutoka Makao ya watoto 13 mwaka 2015/16 na kufikia Makao ya watoto 213 Disemba, 2019 ambapo moja ni la Serikali (Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini);

viii) Serikali imeendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali kupitia Dirisha la Wanawake lililoanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania (TPB). Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2019, mikopo yenye thamani ya **Shilingi 3,586,400,000.00** imetolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,271; na

ix) Huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wakiwemo wazee wasiojiweza wapatoa 383 (Ke 179 na Me 204) zimetolewa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na shughuli hizo zilizotekelezwa, Kamati pia ilielezwa kuhusu changamoto ambazo Wizara inakumbana nazo kama ifuatavyo:-

i) Mashirika yasiyo ya Kiserikali kujijikita kufanya kazi zao maeneo ya mjini ambapo kiuhalisia hakuna changamoto kubwa kama ilivyo maeneo ya vijijini;

ii) Uwepo wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kuendelea kuongezeka;

iii) Uchakavu na upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii na miundombinu ya kutolea huduma katika vituo vya ustawi wa jamii; na
iv) Uwepo wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na mauaji dhidi ya wanawake, wazee na watoto.

**c) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mfuko wa Bima wa Afya ililenga katika kueleza masuala mbalimbali kama vile utekelezaji wa Kampeni za uhamasishaji wananchi kujiunga na mpango wa vifurushi vya bima ya afya na changamoto ambazo Mfuko unakumbana nazo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Disemba 2019, Mfuko umetekeleza yafuatayo: -

i) Imezindua rasmi Kampeni ya Uhamasishaji wananchi kujiunga katika vifurushi vya bima ya afya vya hiari ambapo tangu kuzinduliwa kwa mpango huo tarehe 28.11.2019, **wananchi 24,922** wamefika katika ofisi mbalimbali za Mfuko kupata elimu ya vifurushi na kuonesha nia ya kujiunga. Aidha, hadi tarehe 31/12/2019 Ofisi Saba (7) ambapo uzinduzi wa kampeni za uhamasishaji Wananchi ulifanyika awamu ya kwanza, jumla ya **wanachama 2,538** wamesajiliwa na kiasi cha **shilingi Bilioni 2.655** kimekusanywa. Kwa ujumla hadi kufikia tarehe 31.12.2019, jumla ya **wananchi 3,343** wamejiunga katika mfumo wa bima ya afya kupitia vifurushi vya bima ya afya na kiasi cha **shilingi Bilioni 3.46** zimekusanywa kutokana na michango. Kati ya wanachama hao waliojiunga, asilimia 60 wamechagua vifurushi vya WEKEZA na TIMIZA AFYA wakati asilimia 40 wamejiunga katika kifurushi cha NAJALI AFYA;

ii) Imefanya Malipo ya **shilingi Bilioni 232.67** sawa na **asilimia 95** ya madai ya **shilingi Bilioni 245.99** kwa Watoa Huduma;

iii) Imeboresha Mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha huduma;

iv) Imejumuisha makundi mbalimbali ya wanachama katika Mfuko ikiwa ni pamoja na wakulima kupitia vyama vya msingi (AMCOS), Wajasiriamali (Wamachinga, Bodaboda, Baba na Mama

Lishe na Madereva) kupitia Vyama au Umoja wao unaotambulika rasmi na Mamlaka za Serikali, Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, wanafunzi katika Vyuo vinginevyo, shule za msingi na sekondari, Watoto chini ya Miaka 18, Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wanachama binafsi na Makampuni binafsi n.k.;

v) Imeboresho ya Mafao yatolewayo ikiwemo idadi na aina za dawa, idadi na aina za vipimo, idadi na aina ya upasuaji pamoja na huduma za kibingwa kama vile huduma za Matibabu ya Moyo (*Cardiac Services*), Huduma za Saratani (*Anti cancer services*), Huduma za kusafisha damu (*Dialysis*), Huduma za upandikizi wa viungo (*Implants*), ugharamiaji wa vipimo vikubwa ikiwemo MRI na CT Scan pamoja na gharama za kuwaona madaktari;

vi) Imeongeza usajili wa Vituo vya huduma kwa ngazi zote na umiliki (Serikali, Binafsi na mashirika ya dini). Vituo hivi ni pamoja na Hospitali, Vituo vya afya, Zahanati, Kliniki maalum, Maduka ya Dawa pamoja na Maabara za uchunguzi zinazojitegemea

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi hizo zilizotekelezwa na Mfuko, kama ilielezwa juu ya changamoto zifuatazo:-

i) Uhiari mdogo wa kujiunga kwa wananchi hususani kutoka katika sekta isiyo rasmi;

ii) Kupanda kwa gharama za huduma za afya; na

iii) Kuongezeka kwa Magonjwa yasiyokuwa ya Kuambukizwa (*Non-Communicable Diseases)* na Gharama zake ambapo katika orodha ya magonjwa ishirini (20) yaliyoongoza kwa matumizi makubwa ya fedha kwa mwaka 2018/19, magonjwa Kumi na Moja (11) yasiyoambukiza yaligharimu kiasi cha shilingi **Bilioni 57.6** sawa **asilimia 48** ya shilingi **Bilioni 120.6** zilizotumika kugharamia magonjwa yote yasiyo ya kuambukiza.

**d) Hospitali ya Mkoa wa Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma ilianzishwa mwaka 1920, ikiwa ni Kituo cha Afya, na iliendelea kupandishwa hadhi na mwaka 2010 ilipandishwa na kuwa hospitali ya Rufaa ya Mkoa ikiwa na jukumu la kutoa huduma za tiba na kibingwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miezi sita (Julai – Disemba, 2019), Hospitali imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi **4,869,894,830.62** kutoka katika vyanzo vya ndani ambayo ni sawa na **asilimia 65** ya lengo ya kukusanya shilingi **7,471,000,000.00** zilizokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha hizo zilizopatikana zimewezesha Hospitali kutekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni kama ifuatayo:-

i) Imehudhumia jumla ya wagonjwa 172,311 sawa na wastani wa wagonjwa 28,719 kwa mwezi au 957 kwa siku;

ii) Jumla ya wajawazito 4,538 walipata huduma ya kujifungua na jumla ya watoto 4,471 walizaliwa hai;

iii) Jumla ya wagonjwa 22,801 walipata huduma mbalimbali za radiolojia, ambapo wagonjwa 14,230 walipatiwa huduma za X-ray, wagonjwa 5007 walipatiwa huduma ya "Ultrasound", na wagonjwa waliofanyiwa kipimo cha "ECHO" walikuwa 758;

iv) Jumla ya wagonjwa 46,565 wenye matatizo yanayohusiana na upasuaji walihudumiwa ambapo wagonjwa walionekana wanahitaji kufanyiwa upasuaji walikuwa 3,375, kati yao 2,583 walifanyiwa upasuaji mkubwa na wagonjwa 792 walifanyiwa upasuaji mdogo; na

v) Ukarabati mdogo wa Jengo Kuu la Upasuaji unaendelea. Aidha shughuli ya kupaka rangi kuta na mabati ya baadhi ya majengo ambayo yalikuwa yamechakaa na ukarabati mdogo wa kichomea taka ambacho kilikuwa kinapelekea uchafuzi wa hali ya hewa zinaendelea;

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu changamoto, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:-

i) Upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali wapatao 258 wakiwemo Madaktari wa kawaida, Madaktari bingwa wa Macho, Pua, Koo na Masikio;

ii) Uchakavu wa miundombinu na vifaa vya kutolea huduma kama vile Chumba cha upasuaji, chumba cha kuhifadhia maiti, x-ray na vifaa vingine vya kiuchunguzi;

iii) Gharama kubwa katika kutoa huduma kwa makundi maalumu ya misamaha, ambapo katika kipindi cha Julai mpaka Disemba 2019, jumla ya **wagonjwa 25,043** walipata msamaha wa matibabu wenye thamani ya **shilingi 867,492,300;**

iv) Utaratibu wa mfumo wa rufaa kutofuatwa kama inavyoelekezwa katika miongozo hivyo kusababisha msongamano mkubwa wa wagonjwa wanaoweza kutibiwa ngazi za chini; na

v) Kuchelewa kupatikana kwa vibali vya matumizi ya fedha.

**e) Hospitali ya KCMC.**

**Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya KCMC ilianzishwa mnamo mwaka 1971 na Shirika la Msamaria Mwema la Tanzania ambalo kwa sasa limeingia katika makubaliano maalumu (MoU) na Serikali ya Tanzania ambapo Serikali ndio inalipa mishahara ya wafanyakazi wote, na Shirika la Msamaria mwema linasimamia uendeshaji wa Hospitali na maendeleo yake.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2019, Hospitali ilipokea kiasi cha **shilingi 5,302,364,000.00** kutoka Serikalini kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Kwa upande wa Makusanyo ya Maduhuli, Hospitali ilikusanya jumla ya **shilingi 13,931,568,454** sawa na **asilimia 53** ya lengo la kukusanya **Shilingi 25,757,723,521.76**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, upatikanaji huo wa fedha umewezesha Hospitali kutoa huduma mbalimbali kama ifuatavyo:-

i) Huduma za Ngozi kwa wagonjwa wakiwemo Albino kwa kuwapatia *sunscreen lotion;*

ii) Jumla ya wagonjwa 1,297 walifanyiwa upasuaji na kupatiwa huduma mbalimbali za njia ya mkojo (*urology*);

iii) Jumla ya wagonjwa 65 walipatiwa huduma ya upasuaji kwa njia ya matundu (*Laparoscopic surgery);*

iv) Wagonjwa wenye matatizo ya figo, wapatao 1,333 walipatiwa huduma hiyo;

v) Upasuaji wa wagonjwa 96 katika kliniki ya magonjwa ya ngozi, ilitolewa;

vi) Ujenzi wa Wodi ya Wagonjwa wa Saratani unaendelea utakaokuwa na vitanda 60, Wodi, jengo la Mionzi ; na

vii) Kununua Mtambo wa kuzalisha Oksijeni na *Liquid Nitrogen* na hivyo kupunguza gharama ambazo Hospitali ilikuwa inaingia kununua

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji mzuri wa majukumu, Kamati ilielezwa baadhi ya changamoto kama ifuatavyo: -

i) Uhaba wa vitendea kazi kama vile; Mashine, vifaa, vitendanishi, na uchakavu wa majengo;

ii) Uhaba wa watumishi katika kada za Afya; ambapo ikama ya Hospitali ya KCMC ni kuwa na jumla ya wafanyakazi 1627 wakati kwa sasa kuna wafanyakazi 877 walio kwenye payroll ya serikali na 255 walioajiriwa na Hospitali;

iii) Ongezeko kubwa la wagonjwa, hasa wale ambao hawahitaji matibabu ya kibingwa; na
iv) Ukosefu wa tiba ya mionzi kwa wagonjwa wa saratani kutokana na kutokuwa na mashine na jengo la mionzi (*bunker*)

#### 2.6.3 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo


**Mheshimiwa Spika,** katika Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na Kujadili Taarifa ya Wizara (Fungu 96), Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) na Bodi ya Filamu kama ifuatavyo:-

**a) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96)**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Wizara (Fungu 96) ilibainisha mwelekeo wa upatikanaji wa fedha, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara na Taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 30,879,483,000.** Kati ya fedha hizo **shilingi 24,879,483,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara **shilingi 15,483,073,000** na Matumizi Mengineyo **shilingi 9,396,410,000**) na Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa **shilingi 6,000,000,000.** Hadi kufikia Disemba 2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 11,878,979,789** (Mishahara **shilingi 7,027,246,493** na matumizi mengineyo **shilingi 4,851,733,29**6) sawa na **asilimia 38.4** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7. Kamati ilijulishwa kuwa fedha za Miradi ya Maendeleo zinatarajiwa kupokelewa hivi karibuni**.**

**Kielelezo Na. 7 Upatikanaji wa fedha – Fungu 96 (Julai - Disemba 2019)**




***Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Habari ya tarehe 17 Januari 2020 na usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa maduhuli, jumla ya **shilingi 959,905,000** zilipangwa kukusanywa. Kufikia Disemba 2019, Jumla ya **shilingi 531,435,477** sawa na **asilimia 55.3** ya lengo zilikusanywa. **Kamati inapongeza Wizara kwa ukusanyaji huu mzuri.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa upatikanaji wa fedha umewezesha Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo: -

i) Kuchapa jumla ya habari 1,722 sawa na wastani wa habari 5 kwa siku na makala 574 sawa na wastani wa makala 2 kwa siku katika magazeti ya Chama, Serikali na Kampuni binafsi zikitoa taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali;

ii) Kuratibu jumla ya mikutano ya Waandishi wa Habari (*press conferences*) 145;

iii) Vipindi maalumu vya "TUNATEKELEZA" 64 vimeratibiwa na kurushwa hewani kupitia TBC1 ambapo Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi mbalimbali walipata fursa ya kuutaarifu Umma kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya Serikali;

iv) Kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, vikao mbalimbali viliratibiwa kwa lengo la kuandaa miongozo ya ufundishaji Kiswahili kwa Wageni na kubainisha mahitaji ya uandaaji wa mitaala ya kufundishia Kiswahili katika nchi za kigeni. Aidha, Andiko la kujenga hoja kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya kuridhia lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi za SADC liliandaliwa na lugha hiyo iliridhiwa kuwa miongoni mwa lugha rasmi za SADC katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya hiyo uliofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Agosti, 2019;

v) Kuratibu maandalizi ya Tamasha la Nne la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) lililofanyika nchini Tanzania kuanzia tarehe 21 - 28 Septemba, 2019 katika viwanja

vya Taifa Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Mwenyeji Tanzania;

vi) Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) iliratibu Tamasha la 38 la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo ambalo hufanyika kila mwaka katika taasisi hiyo;

vii) Kuratibu ushiriki wa Timu za Tanzania katika Michezo ya 12 ya Mataifa ya Afrika (All African Games) yaliyofanyika nchini Morocco tarehe 16 – 31 Agosti, 2019. Wachezaji wa Timu ya Riadha katika mbio za Kilometa 21 (Marathon) walishika nafasi ya Tano (5) na Saba (7). Aidha, Timu ya Walemavu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ilishiriki mashindano ya Walemavu yaliyofanyika kwa mara ya kwanza katika Bara la Afrika tarehe 04 – 11 Oktoba, 2019 nchini Angola. Timu hiyo iliweza kufuzu kushiriki katika Kombe la Dunia litakalofanyika kati ya mwezi Januari au Februari, 2021 nchini Uingereza au Poland;

viii) Kuratibu ushiriki wa Timu ya Riadha ya Wanawake katika michezo ya riadha iliyofanyikia Nagai City nchini Japan ambapo timu hiyo ilishinda Medali za dhahabu saba (7) na fedha moja (1);

**b) Bodi ya Filamu Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Bodi ya Filamu Tanzania kwa kipindi cha miezi sita (Julai-Disemba, 2019). Taarifa hiyo ilijikita katika kueleza majukumu ya ujumla ya Bodi, Dhima na Dira. Aidha, Taarifa ilieleza hali ya upatikanaji wa fedha kulingana na bajeti iliyopitishwa na Bunge na changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Bodi ya Filamu ilitengewa jumla ya **shilingi 1,117,140,000** ikijumuisha mishahara, matumizi mengineyo na mapato ya ndani. Kufikia Disemba 2019, Bodi ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 492,952,438** sawa na **asilimia 44.1.**

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji huo wa fedha umewezesha Bodi kufanya shughuli mbalimbali ilizojipangia kama ifuatavyo:-

i) Kuendelea na zoezi la kutunga Sera ya Filamu;

ii) Imechambua jumla ya maombi 70 ya vibali vya kutengeneza filamu (miswada);

iii) Imeendesha operesheni 18 dhidi ya kazi za filamu zinazoingia sokoni kinyume na taratibu kwenye maduka ya kuuza filamu, vyombo vya usafiri na mtandaoni, ambapo jumla ya filamu 20 ambazo hazikufuata Kanuni na Taratibu zilibainika;

iv) Imeratibu na kuendesha Tamasha la Filamu na Tuzo la Kimataifa (*Serengeti International Film Festival and Award*) ambalo lilifanyika Sambamba na Tamasha la JAMAFEST mwezi Septemba, 2019. Tamasha hilo lilijumuisha filamu kutoka Tanzania, Kenya na Rwanda, ambapo filamu mbili za Tanzania (T – Junction na Tunu ya Tanzania) zilishinda tuzo. Aidha, filamu mbili kutoka Kenya, na mbili kutoka Rwanda nazo zilishinda tuzo; na

v) Imepatiwa hati ya umiliki wa Kiwanja Na. 891 kitalu 'D', chenye ukubwa wa mita za mraba 46,080 kilichopo eneo la Chamwino, Jijini Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Eneo Changamani la Filamu (*Multipurpose Film Complex*) jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Bodi ya Filamu, changamoto zifuatazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji mzuri wa majukumu yake:-

i) Upungufu wa rasilimali watu;

ii) Kutokuwa na vyombo vya usafiri vya kutosha kwani Bodi ina gari moja tu; na

iii) Baadhi ya wadau kutokuwa tayari kuzingatia sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuna haja kubwa ya Bodi hii kupatiwa magari ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama ambavyo moja ya jukumu lake ni kuendesha operesheni hivyo kuhitaji vyombo vya usafiri kufanya shughuli hiyo.**

**c) Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)**

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 21 Januari, 2020 Kamati ilipokea,ilichambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya TBC kwa kipindi cha Nusu Mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi 27,781,038,000** kwa ajili ya Mishahara, Miradi ya Maendeleo na Matumizi Mengineyo ya TBC. Kati ya fedha hizo, bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani ni **shilingi 10,163,000,000**, Mishahara ni **shilingi 8,418,038,000**, Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 5,000,000,000** na Matumizi Mengineyo ni **shilingi 4,200,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, kufikia Disemba 2019, TBC ilifanikiiwa kukusanya **shilingi 4,954,485,819**. Aidha ilipokea kutoka Serikalini kiasi cha **shilingi 2,100,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na s**hilingi 4,127,694,960** kwa ajili ya mishahara
**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji huo wa fedha umewezesha TBC kutekeleza baadhi ya majukumu kama ifuatavyo: -

i) Imenunua magari mawili mapya na kuyafanyia marekebisho maalum (*modification)* kwa jumla ya **Shilingi 518,667,801.12** ili yaendane na matakwa ya uandaaji wa vipindi vya utalii maeneo ya hifadhi;

ii) Imenunua vifaa kwa ajili ya Chaneli ya Utalii zikiwemo kamera (12), *drones* (2), Kompyuta mpakato maalum (2), na vifaa vya kurushia matangazo mubashara *(transmitter* 2) kwa jumla ya Dola za Kimarekani 326,540. Vifaa hivyo vinatarajiwa kufika TBC Februari, 2020;

iii) Imefanya mchakato na kuwapata waandaaji vipindi wa kujitegemea wa kuandaa maudhui ya utalii katika maeneo ya vivutio vya utalii kama vile wanyamapori, malikale, utamaduni, viumbe wa baharini, misitu na vingine;

iv) Chaneli ya Tanzania Safari kwa sasa inaonekana kwenye kisimbuzi cha DSTV toka Septemba, 2019. Aidha, juhudi zinazoendelea ni kuwezesha kuonekana katika nchi zote za Afrika na nje ya Bara hili ambako visimbuzi vya hapa nchini havifiki; na

v) Chaneli ya Tanzania Safari inaandaa maudhui yatakayorushwa katika lugha mbalimbali za kimataifa (kama vile Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kijerumani, na Kiitaliano) ili kukidhi lengo la Serikali la kutangaza vivutio vya utalii.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu hayo yaliyotekelezwa na TBC, Kamati ilielezwa changamoto kuu mbili ambazo TBC inakumbana nazo kuwa ni:-

i) Uhaba wa wafanyakazi wapatao 100 kwa ajili ya kuendesha chaneli za TBC; na

ii) Ukosefu wa studio za Televisheni na majengo ya utawala Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa endapo TBC itawezesha kikamilifu hususan katika Chaneli ya Utalii basi itasaidia kwa kiwango kikubwa katika kuvutia watalii na kuongeza pato la Taifa kama ambavyo Korea ya Kusini imekuwa ikifanya.**

### 2.7 Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupatiwa mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujengewa uwezo. Katika kipindi cha Mwaka 2019/2020, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wadau mbalimbali kwa lengo la kujengewa uelewa katika masuala mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli ulio wazi kuwa mafunzo hayo yamesaidia sana Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuishauri vyema Serikali. Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote na inapenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa LSPII, (***Parliamentary Legislative Support Progamme* II) unaofadhiliwa na UNDP** ambapo mara zote imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Kamati inapata mbinu za kusaidia utekelezaji bora wa majukumu yake. Sambamba nao, napenda kuwashukuru kwa dhati Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), The Maryland University, Jhpiego, SIKIKA,UNICEF,HAKIELIMU,UN Women, Save the Children, CAMFED na SHIVYAWATA kwa kuendelea kukutana na Kamati ili kuipa mafunzo. Ni imani ya Kamati kuwa wadau hawa wataendelea kushirikiana na Kamati katika siku zijazo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, naomba kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatayo: -

### 3.1 Maoni ya Jumla

**a) Uhaba wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Sekta ya Afya, Elimu na Habari zina changamoto ya uhaba wa watumishi wa kutosha, kwa mfano Wizara ya Afya ni takribani asilimia 50,

**NA KWA KUWA** Uhaba huo umekuwa ukiathiri utoaji wa huduma za Afya, Elimu na habari kwa wananchi wetu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iweke mkakati wa kuongeza watumishi hawa muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

**3.2 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**a) Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** utekelezaji wa Lengo namba 3 la malengo ya maendeleo endelevu linalohusu afya unalenga katika kuhakikisha kuwa tunakuwa Taifa bora na lenye afya,

**NA KWA KUWA,** utekelezaji huo unakwamishwa na upatikanaji wa fedha usio ridhisha,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali iamue kwa dhati kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza lengo hili ambalo pia linaenda na malengo ya Agenda 2063.

**b) Hospitali ya Mloganzila**

**i) Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Hospitali ya Mloganzila ina upungufu wa watumishi kwa takribani asilimia 50, uhaba wa nyumba za walimu na ukosefu wataalam wanaoweza kutumia vifaa vya kisasa vilivyopo katika Hospitali hiyo,

**NA KWA KUWA** upungufu huo unaathari kubwa katika utoaji wa huduma ili hali wapo Madaktari wengi mtaani waliohitimu lakini hawana ajira,

**KWA HIYO BASI** Kamati inashauri yafuatayo:-

a. Serikali iamue kwa dhati kutafuta watumishi kwa kutoa ajira ili wasaidie kutoa huduma inayoendana na hadhi ya hospitali hasa ikizingatiwa kuwa hospitali hiyo ni ya mfano, imejengwa kwa gharama na kuwekwa vifaa vya kisasa na vyenye ubora wa hali ya juu; na

b. Serikali itenge fedha zitakazowezesha ujenzi wa nyumba za watumishi pamoja na mafunzo ya namna ya kutumia vifaa hivyo vya kisasa...

**ii) Mheshimiwa Spika KWA KUWA** Hospitali ya Mloganzila imejengwa kisasa na ina vifaa na vifaa tiba vya teknolojia kubwa**.**

**NA KWA KUWA** Hospitali zenye vigezo hivyo zimekuwa zikitumika kutoa huduma za kibingwa na kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi kwenda kupata huduma na kuchangia katika kuongeza pato la Taifa na nchi kujulikana duniani,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Hospitali hiyo itumike kutoa huduma za kibingwa ili kuvutia wagonjwa wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuwa sehemu ya utalii wa kimatibabu (*Medical Tourism*). Hii pia itasaidia kuchangia katika kuongeza pato la Taifa na nchi kujulikana duniani kama ambavyo nchi ya India imefanya na kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa namba 1 katika utalii wa Kimatibabu.

**c) Wagonjwa wa Msamaha**

**Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** Sera ya Afya inataka makundi maalum kama wazee wasiojiweza, watoto chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito kupata huduma za afya bure,

**NA KWA KUWA**, Makundi haya ndiyo yenye idadi kubwa ya wagonjwa wanaotibiwa katika Hospitali zetu na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa Hospitali hizo. Kwa mfano katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Dodoma katika kipindi cha Julai mpaka Disemba 2019, jumla ya wagonjwa 25,043 walipata msamaha wa matibabu wenye thamani ya **shilingi Milioni 867.5,**

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Serikali iweke utaratibu wa kutoa Ruzuku kwa Hospitali hizi ili ziweze kujiendesha.

**d) Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA)**

**Mheshimiwa Spika KWA KUWA,** kumekuwepo na tabia ya uingizwaji wa bidhaa nchini zisizo kidhi viwango kwa kutumia njia za panya,

**NA KWA KUWA** uingizwaji huo wa bidhaa zisizokidhi viwango kwa kutumia njia za panya unachangiwa pia na uhaba wa watumishi na hususan wakaguzi katika vituo vya forodha,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwa watumishi hawa ili wasaidie katika kudhibiti uingizwaji wa bidhaa hizo ambazo zimekuwa na madhara kwa wananchi lakini pia iweke mifumo bora ya udhibiti.

**e) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya ni haki ya kila raia kwa maendeleo ya Taifa,

**NA KWA KUWA**, wananchi wengi wamekuwa wakikosa huduma za afya kutokanana na kutokuwa na Bima za Afya

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kutekeleza ahadi yake ya kuleta Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote utakaowezesha wananchi wote kuwa na Bima za Afya na hivyo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya wakati wote kabla Bunge hili la 11 halijaisha.

**f) Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Vyuo vya maendeleo ya jamii vina nafasi kubwa ya kuchangia katika maendeleo ya nchi na watu wake endapo vitawezeshwa kibajeti na kimitaala,

**NA KWA KUWA**, Vyuo vingi vya Maendeleo ya jamii nchini kikiwemo Chuo cha Tengeru vinakumbana na changamoto ya bajeti ambayo inaathiri utekelezaji wa majukumu ikiwemo uhaba wa miundombinu ya madarasa, nyumba za walimu na hosteli za wanafunzi. Aidha, vyuo hivyo vimebainika kuendelea kufundisha mitalaa ambayo haiendani na kasi ya mabadiliko ya dunia,

**KWA HIYO BASI, Kamati inashauri: -**

i) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa vyuo vya maendeleo ya jamii vyote nchini itakayowezesha uboreshaji wa miundombinu ikiwemo madarasa, vyumba za walimu na hosteli za wanafunzi; na

ii) Wizara ione namna ya kuandaa mitaala inayoendana na wakati.

**g) Uhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii**

**Mheshimiwa Spika, KWAKUWA** Maafisa Maendeleo ya Jamii wana umuhimu sana katika kuzisaidia jamii katika masuala mbalimbali ikiwemo namna bora ya kuishi ili kuepuka magonjwa hasa yasiyoambukiza ambayo yana gharama kubwa,

**NA KWA KUWA,** Kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii hapa nchini,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iweke mkakati maalum wa kuongeza Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini.

**h) Ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA**, kumekuwa na ongezeko kubwa la Ukatili wa kijinsia nchini hususan kwa wanawake na watoto kutoka watu 31,996 mwaka 2016 hadi 43,487 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia **35.9**

**NA KWA KUWA**, madhara yanayotokana na ukatili huo ni makubwa ikiwemo kuumizwa vibaya, kupata ulemavu wa viungo, madhara ya kisaikolojia na hata kupoteza maisha kwa baadhi ya watu,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuzishauri Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa uhamasishaji wa namna bora ya kupunguza ukatili huo na hata kujikinga na kutoa taarifa katika vyombo husika ikiwemo polisi.

**3.3 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**a) Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Lugha ya Kiswahili imeamuliwa kuanza kutumika katika nchi za SADC,

**NA KWA KUWA** ili lugha hii iweze kutumika vizuri kunahitajika huduma za ukalimani na tafsiri mbalimbali, Ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za SADC, pamoja na uandaaji wa mitaala ya kufundishia na kujifunza ambavyo vyote hivi vinahitaji bajeti ya kutosha kuweza kutekelezwa,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa BAKITA ili iweze kutumia fursa hii na kuhakikisha huduma hizo za msingi zinapatikana ikiwa ni pamoja na kuandaa Walimu wa kutosha wa kufundisha Kiswahili katika nchi ambazo zina uhitaji kama vile Afrika ya Kusini.

**b) Changamoto za Usimamizi wa Sekta ya Habari na hususan vyombo vya kurusha matangazo (visimbuzi) kwa njia ya televisheni.**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** imebainika kuwa Sekta ya Habari na hususan vyombo vya kurusha Matangazo (Visimbuzi) kwa njia ya televisheni vinakumbana na changamoto nyingi,

**NA KWA KUWA** changamoto hizo zimekuwa zikiathiri utoaji wa huduma kwa wananchi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri yafuatayo: -

i) Serikali ifanye mabadiliko ya Sheria ya EPOCA ili kuondoa utata wa utendaji kati ya wamiliki wa mitambo/visimbuzi na waandaaji maudhui na hatimaye kuwepo na mazingira ya kibiashara;

ii) Serikali itafute namna ya kuunganisha teknolojia katika kisimbuzi kimoja ambacho kitawawezesha watanzania kupata habari kwa urahisi badala ya kuwa navyo vingi kama ilivyo sasa; na

iii) TCRA isimamie utitiri wa Televisheni za mitandaoni kwa mujibu wa Sheria

**c) Ubovu na uhaba wa Viwanja vya Michezo**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** mojawapo ya nyenzo muhimu katika mafanikio ya michezo ni uwepo wa viwanja bora na vya kutosha,

**NA KWA KUWA,** hali ya viwanja vyetu vya michezo hapa nchini siyo nzuri lakini pia ni vichache hivyo kuathiri sekta ya michezo,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Wizara na TFF kwa kushirikiana na wadau wengine waone namna ya kuboresha viwanja vya michezo na kuanza kujenga vingine ili kuweza kufanya vizuri kwenye ligi mbalimbali.

**3.4 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**a) Changamoto za Sekta ya Elimu**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** changamoto za Sekta ya Elimu ni nyingi kama vile Mitaala isiyoendana na soko la ajira, Upungufu wa Walimu wenye ubora, ukosefu wa vifaa vya kufundishia na vitabu, mkinzano wa sera na sheria ya elimu, kukosekana kwa Chombo huru na jumuishi cha kusimamia na kuratibi Sekta ya Elimu msingi nchini na ukosefu wa mikopo kwa wanafunzi wa NACTE,

**NA KWA KUWA**, Changamoto hizi zimeendelea kudidimiza Elimu yetu hali ambayo ni hatari kwa Taifa letu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri iundwe Tume ya Elimu ambayo itapitia upya muundo na mfumo wa Elimu illi kushauri namna bora ya kuenenda na kuwa na Mfumo utakaoendana na mwelekeo wa Dunia.

**b) Uanishiaji wa Vyuo (*University Classification*)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** msingi Mkuu wa Taifa lililo bora ni Elimu nzuri inayotolewa na vyuo mbalimbali vilivyobobea kwenye masuala mbalimbali,

**NA KWA KUWA** kama nchi bado hatujaweza kuianisha Vyuo hivi kulingana na ubora na elimu inayotoa kama ambavyo nchi za wenzetu zimefanya kwa mfano Marekani,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Wizara ya Elimu ianze kuviainisha vyuo na hatimae kuzalisha watoto wenye ubora unaotakiwa

**c) Uhaba wa Walimu wa Elimu ya Awali**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Msingi bora wa Elimu unaanzia kwenye Elimu ya Awali ambapo Walimu ni nyenzo muhimu sana;

**NA KWA KUWA,** bado nchini yetu ina uhaba wa Walimu hao wa Elimu ya Awali nchini hali inayofanya watoto kuingia katika Elimu ya Msingi bila kuwa wameandaliwa vizuri,

**KWA HIYO BASI,** kama Mwanazuoni kutoka Italia Bi. Maria Montesori alivyowahi kusema "***Early Childhood Education is the key to the betterment of society***" Kamati inashauri

i) Serikali iandae Mkakati Maalum wa kutenga vyuo vya kufundisha Walimu wa Shule za Awali; na

ii) Ikiwezekana Serikali iruhusu upatikanaji wa Walimu wageni wenye Taaluma ya elimu ya Awali kutoka Nje ya nchi ili wasaidie kufundisha watoto wetu na hivyo kuwapa msingi bora wa Elimu kwa maendeleo ya Jamii kwa ujumla.

**d) Mitaala kuendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine Kamati inatoa ushauri juu ya MItaala kuendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** dunia inaenda kuendeshwa kwa teknolojia ya hali ya juu ambapo roboti na mitambo ya kisasa itakuwa inafanya kazi zaidi kuliko nguvu ya binadamu na kwa ujumla mfumo wa maisha ya mwanadamu utabadilika,

**NA KWA KUWA** kama nchi bado mitaala yetu haijielekezi katika kutoa elimu inayoendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Wizara kuanza kuboresha mitaala yetu ya elimu ili ilenge zaidi katika kutoa elimu itakayosaidia kuendana na mapinduzi hayo.

**e) Vyuo vya Ufundi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mipango ya nchi yetu ni kwenda kwenye Uchumi wa Kati wa Viwanda ambao unategemea sana uwepo wa mafundi ambao wanazalishwa na vyuo vya ufundi,

**NA KWA KUWA** bado Vyuo vyetu vya ufundi hajiwazeshwa vya kutosha kuweza kuzalisha wataalamu hao kutokana na utamaduni uliojengeka wa wanafunzi kukimbilia masomo ya digrii katika Vyuo Vikuu,

**KWA HIYO BASI** Kamati inashauri,

i) Serikali iwekeze na kuboresha Vyuo vya Ufundi nchini ili viweze kuzalisha mafundi wa kutosha watakaosaidia katika kuendesha viwanda vyetu nchini; na

ii) Serikali iangalie Sera na Sheria zetu na kuzifanyia maboresho pale itakapobidi ili Mikopo ya Elimu ianze kutolewa kwa wanafunzi wa vyuo vya ufundi ili wanafunzi wengi zaidi waweze kujiunga. Naibu Waziri wa Elimu wa China Lu Xin mnamo mwaka 2014 wakati wa Kongamano la Viongozi wa Vyuo Vikuu alitangaza uamuzi uliofikiwa wa kubadili Vyuo vikuu (Universities) 600

ambavyo ni nusu ya vyuo vikuu walivyonavyo (1200)kuwa Vyuo vya Ufundi (Polytechnics). Lengo ni kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi wenye digrii ambao wanagombania ajira zinazofanana ili kuzalisha watalaam hao wa ngazi ya kati ambao ndiyo wanahitajika kwenye uchumi wa viwanda.

**f) Tuzo ya Udhamini wa masomo (Scholarship)**

**KWA KUWA** kuna wanafunzi wengi wanaomaliza kidato cha sita na kufanya vizuri,

**NA KWA KUWA** wanafunzi hao wengine wamekuwa hawana uwezo wa kwenda kusoma katika vyuo vizuri na hivyo kuishia mitaani au vyuo vya kawaida tu hapa nchini.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali ione namna ya kuanzisha tuzo ya udhamini kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha sita na kuwapeleka katika vyuo bora duniani kama Havard. Hii itasaidia kuongeza Morali kwa wanafunzi wengine lakini pia kuwa na Taifa lenye watu wenye *exposure* na elimu bora.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kipekee naomba nikushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa hii ya Mwaka ya Kamati ambayo ni ya mwisho katika Bunge hili la 11. Napenda kukupongeza kwa uongozi shupavu ambao umeuonyesha katika Bunge hili. Aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru Mawaziri tunaofanya nao kazi ambao ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy A. Mwalimu (Mb), Naibu Waziri Mhe. Dkt. Faustine E. Ndugulile (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Juliana D. Shonza (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Joyce L. Ndalichako (Mb) na Naibu wake Mhe. Wiiliam T. Ole Nasha (Mb) kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati. Pamoja nao, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara zote tatu na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa utendaji mzuri ambao umekuwa ukiwezesha pia utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Juma S. Nkamia, Mb kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu kwa imani waliyokuwa nayo kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati na kunipa ushirikiano mzuri ambao umesaidia katika utendaji kazi wangu na wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Peter J. Serukamba, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 5. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. John Peter Kadutu, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Selemani Said Bungara, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Maulid Said Mtulia, Mb | Mjumbe |
| 24. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kipekee zaidi napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao Kamati imekuwa ikiupata wakati wote. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati Ndg. Gelard Magili, Katibu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Catherine KItutu kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Peter Joseph Serukamba, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA**
**NA MAENDELEO YA JAMII**
6 Februari, 2020

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea sasa na uchangiaji, Mheshimiwa Mwenyekiti asante sana. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya awali ya kuweza kuchangia katika ripoti za kamati hizi mbili ambazo kwa bahati nzuri sana mimi ni Mjumbe wa kamati zote mbili. Niwapongeze sana Wenyeviti waliosoma, pia nipongeze na kukubaliana kabisa na maoni ya Kamati hizo kwa sababu hiyo ndio hali halisi. Nitaanza na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo linajitokeza katika Wizara hii ya Afya ni tatizo kubwa sana la watumishi. Tatizo la watumishi katika Wizara ya Afya ni *almost 50 percent*. Ukiangalia lile lengo namba tatu la kuhakikisha kwamba tunakuwa na taifa lenye afya na watu wenye siha njema si rahisi kabisa kufikiwa kwa jinsi ambavyo tunaenda na *trend* ya bajeti. Pamoja na kwamba Mwenyekiti wangu amesema bajeti ya Wizara ya Afya imekuwa ikiongezeka, ni kweli inaongezeka kwa fedha lakini ukiangalia kwa *percentage* inapungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu takwimu mwaka 2014/2015 tulikuwa na asilimia 9, na *that was the highest*. Mwaka jana ilikuwa asilimi 5.5 ilhali sisi kama nchi tumesaini *Abuja Declaration* ambayo inapaswa Wizara ya Afya walau Sekta ya Afya itengewe asilimia 15, lakini jambo hilo hatujaweza kulifikia. Kwa maana hiyo, pamoja na juhudi zote za Waziri, Naibu na watendaji wote unakuta kwamba tatizo kubwa linakuwa ni bajeti. Kwa hiyo, ni ombi langu kwamba ni muhimu sana bajeti ya afya ikaongezeka kwa *percentage* na sio kwa *figures.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kuzungumzia kwenye Wizara ya Afya na hili ni jambo kubwa sana, ni suala la bima ya afya. Waheshimiwa Wabunge mjue kwamba bima yetu ya afya inaisha Juni, kwa hiyo mjue kuanzia Julai mpaka Novemba hapo mtajijua wenyewe. Kwa hiyo, ni muhimu sana wakati tunajua sisi tuna bima, tuwaangalie wenzetu huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati imesema kwamba magonjwa yasiyoambukiza yameongezeka kwa kiasi kikubwa na magonjwa haya ni ya gharama kubwa sana. Jambo ambalo linasikitisha leo, wagonjwa wa figo ni wengi sana lakini *dialysis* ni *very expensive*. Ukiingia kwenye *dialysis* kipimo siku moja tu kusafishwa figo ni shilingi kuanzia 250,000 mpaka 350,000 lakini unatakiwa *process* hii ndani ya wiki moja mara tatu, kwa hiyo Mtanzania gani ataweza kujilipia kuanzia 750,000 mpaka 1,000,000 na? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachosikitisha naambiwa kuna ambao tayari walikuwa kwenye hiyo *package,* leo wameenda ku-*renew* bima zao wanaambiwa *dialysis* imeondolewa kwenye hiyo *package.* Kwa hiyo, kuna kilio kikubwa sana kwa wananchi ambao wana matatizo makubwa sana ya figo, lakini matatizo ya moyo na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali iangalie ni jinsi gani tumepiga kelele walete muswada ili kuhakikisha kwamba wananchi wote wanakuwa *covered* kwenye bima ya afya ili sasa gharama zipungue kwa wale ambao wanapata magonjwa haya makubwa, lakini jambo hilo bado hakijaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lishe; ni jambo la kusikitisha kuona kwamba kama nchi bado tuna watoto wenye udumavu wengi sana, takribani asilimia 32. Kinachosikitisha fedha iliyotolewa kwa ajili ya masuala haya ya lishe ilikuwa bilioni 289 lakini zilizopelekwa ni bilioni 123 sawa na asilimia 43 pekee. Kinachosikitisha zaidi, katika fedha hii asilimia 95 inatoka kwa wafadhili, yaani Tanzania kama nchi ni asilimia sita tu. Hivi kweli tunawategemea wafadhili hata kwenye lishe? Hili ni jambo ambalo halikubaliki. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo kama nchi lazima tuone kwamba tunajikomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la elimu; imezungumzwa vyema kwamba msingi wa elimu ni elimu ya awali *(nursery)* lakini kwa takwimu zinatisha; kwamba tuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa *nursery,* tunao walimu 9000 kati ya watoto takribani 1,000,000. Kwa hiyo, unakuta uwiano ambao unatakiwa katika *nursery* iwe mwalimu 1 kwa watoto 25 sasa hivi wastani ni mwalimu 1 kwa watoto 146 lakini inatisha zaidi kwa Jimbo la Serengeti peke yake wastani mwalimu 1 wanafunzi 3,300. Hizi ni data tulizozipata kutoka MCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama mtoto ametoka nyumbani anaenda kuanza shule, wakati huo ubongo wake hauna chochote zaidi ya kile anachokiona hivi kweli mtoto anaenda kwenye darasa la watoto 200/300, atakuwa na mapenzi au na *passion* na shule? hawezi kuwa na hiyo *passion.* Kwa hiyo, ni muhimu sana tunahitaji takribani walimu 43,000 wa shule za awali ili tuweze kuhakikisha kwamba tatizo hilo linaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri uone umuhimu wa kupata walimu katika shule za awali lakini vilevile katika shule za msingi. Leo tunavyoelekea kwenye shule za msingi tunajua elimu bure imekuja na mambo yake mengi na changamoto nyingi. Je, Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba watoto wanaoenda kumaliza darasa la saba mwaka 2022 ambao watakuwa *doubled;* sasa hivi wanamaliza takribani 900,000 – 1,000,000 wataenda mpaka 1,500,000; je, mmejipagaje watoto hawa sekondari? Kwa sababu kila siku ikifika mwezi wa kwanza ndipo tunaanza kusema/Waziri Mkuu na Wakuu wa Mikoa wanatoa matamko ya kujenga shule. Hivi hamna utaratibu wa kutenga tengeo kwa sababu kama tunahitaji leo bilioni 700 na kwa ajili ya kujenga madarasa, kwa nini msiyaweke kwa awamu kila mwaka mkatenga walau nusu au robo kwa miaka mitano ili mhakikishe kwamba tatizo hili linapungua au kuisha kabisa? Hawana mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba kuna kila sababu ya kuwa na mpango mahsusi wa kuhakikisha kwamba mnatenga kila baada ya muda fulani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watoto wanafaulu wanaenda kusubiri madarasa bali madarasa yawasubiri wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile bajeti ya Wizara ya Elimu Sekta ya Elimu nayo inapungua, hela inaongezeka lakini ukiangalia asilimia inazidi kupungua. Tulianza na trilioni 4.7 mwaka 2016/2017 leo tupo trilioni 4.5; kwa maana ya kwamba bilioni 255 zimeshapungua. Je, tunapunguza fedha wakati tumekuwa na changamoto kubwa lakini wanafunzi wameendelea kuongezeka, walimu hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwamba walau kwenye total budget ya Wizara ya Afya na Elimu 0.05 mtoe kwa ajili ya kuajiri watumishi wa afya na watumishi wa Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye UKIMWI; suala la UKIMWI ni suala mtambuka na kwa maana hiyo suala la Mfuko wa UKIMWI ninaomba sana, mfuko huu *about 90 percent* unategemea nje, lakini wagonjwa ni wetu na wagonjwa wakishaanza dawa hizi hawawezi kuziacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana Mheshimiwa Jenista muhakikishe kwamba Mfuko wa UKIMWI sasa tunakua tunautegemeza wenyewe na hatutegemei watu wa nje kwa kiasi kikubwa, *90 percent* leo wakikata maana yake wagonjwa wote waliopo kwenye dawa watakuwa hatarini kupoteza maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la UKIMWI kuna suala la *VAT exemption.* Kama Kamati tumekutana na wadau, hawa ambao ni *development partners* na hasa wale

wanaotoka Mfuko wa Rais wa Marekani ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa ukisaidia sana masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kumekuwa na mkinzano mkubwa sana wa kisheria kwa maana ya kwamba ile *VAT exemption* inasema kwamba *NGO* hazipata huo msamaha. Kikubwa ni kwamba tunaomba basi kuwe na utaratibu madhubuti ambao utawezesha hawa watu wapate *VAT* ili waweze kusaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, asante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nilimuita Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa nafasi hii, na mimi niweze kutoa mchango wangu katika kamati zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kipekee kabisa nianze na Kamati ya UKIMWI; na niwapongeze sana wewe pamoja Mheshimiwa Spika kwa ubunifu mkubwa wa kamati hii ambayo hapo mwanzoni Kamati hii wajumbe walikuwa wanaikimbia. Sasa hivi imekuwa ni kamati moja muhimu sana, tumepata semina za kutosha. Ni kamati ambayo imetoa madarasa mengi na imefanya mambo makubwa na kwa kweli Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oscar Mukasa anahitaji pongezi za ziada kabisa katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo kamati zimeeleza kwenye eneo hili la Kamati ya UKIMWI pamoja na madawa ya kulevya bado kuna changamoto hasa katika eneo zima la udhibiti wa madawa ya kulevya lakini pia tumeona katika kifua kikuu bado nguvu si kubwa kama ambavyo tunaiona katika UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie katika eneo hili, na haswa katika suala lile la Tume ya Madawa ya Kulevya, ili kuhakikisha kabisa kwamba tunaongeza ufanisi ili katika hali ambayo tumeona sasa hivi kwamba kumekuwa na udhibiti mkubwa wa madawa basi taifa letu liendelee kunusurika na hii hali ambayo tunaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningetamani nilichangie ni katika eneo hili la elimu haswa kwa kupitia Kamati ya Huduma za Jamii. Suala la elimu ni suala ambalo linahitaji tafakuri mpya kama taifa. Tumeona maoni na ushauri umekuwa ukitolewa, na mara ya mwisho Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais Mstaafu naye alitoa wazo hili la kupitia mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wetu wa elimu bado unazalisha watu ambao wanashindwa kushindana katika dunia hii ambayo *artificial intelligence* imechukua nafasi kubwa. Kwa hiyo, sisi kama taifa tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba tunaitizama upya elimu yetu. Na tunaposema hapa maana yake tuanzie katika Sera lakini pia katika sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo bado hatufanyi vizuri katika elimu na mara nyingi tunajificha katika kichaka cha Sera na sheria. Kwa mfano, hivi ninavyozungumza wanafunzi ambao wapo darasa la saba mwaka huu, Sera ya Elimu ilikuwa inatuelekeza vitabu mwisho ni darasa la sita lakini wapo darasa la saba; ina maana hakuna vitabu, sasa tunaweza tukaona kwamba wanapoteza mwaka mzima bure shuleni kwa kitu ambacho walishakisoma wakiwa katika darasa la sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni uzalishaji wa mitaala; Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala kwamba mitaala yetu sasa tuiboreshe zaidi ili iweze kuendana na dunia ya sasa. Kama ambavyo tumeona kupitia *SADC* tumepata fursa ya Kiswahili kuwa bidhaa katika nchi 16 za *SADC*. Ili Kiswahili kiwe bidhaa ni lazima sasa mitaala na yenyewe ilitamaze eneo hili; kwa maana huwezi ukaenda kufundisha nchi ambazo zinazungumza Kireno kama lugha ya asili bila hawa tunaowategemea wakafundishe Kiswahili katika nchi hizo bila kujua lugha ya Kireno ama lugha nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nata anitoe rai kwamba kwa kuwa ndio tunaelekea katika maandalizi ya bajeti basi eneo hili lionekane ni mahususi kabisa katika bajeti ili Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala iweze kuendana na soko hili la *SADC* ambalo tunakusudia kwenda kulifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni uhaba wa watumishi hasa katika kada ya elimu. Katika Halmashauri ya Lushoto tuna uhaba wa walimu 1,200. Utaona kabisa kwamba kule Lushoto mwalimu mmoja anafundisha vipindi 40 hadi 46 kwa wiki, tofauti kabisa na mapendekezo ambayo ni vipindi 24 hadi 26 kwa wiki. Kwa hiyo, utaona ni tatizo kubwa sana; lakini wakati Taasisi ya Mitihani inapotangaza matokeo huwa haiangalii maeneo ambayo hayana walimu, inatangazwa kwa usawa nchi nzima; wenye walimu na wasio na walimu wote mnawekwa katika kapu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningetaka pia tuangalie kwamba wakati wa kutangaza matokeo ya mitihani mbalimbali kuanzia shule za msingi, sekondari za kawaida na high school basi wazingatie pia kwamba kuna Halmashauri hazina walimu wa kutosha. Kama ambavyo umeona hapa kwamba kwa wiki moja mwalimu anafundisha vipindi 40 hadi 46 maana yake ni kwamba hapa huwezi ukatarajia kwamba utapata ufanisi wa kutosha sawa na shule za seminari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo hili ni muhimu sana tunapoelekea katika bajeti na Wizara ya Utumishi, na wametuahidi kwamba wanakusudia kuajiri watumishi wengi, basi eneo la elimu liwe ni eneo mahususi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine pia ni katika usimamizi katika elimu. Nitatoa mfano wa Halmashauri ya Lushoto ina shule za msingi 169, ni Halmashauri ya nne kwa kuwa na shule nyingi za msingi hapa nchini. Halmashauri inayoongoza ni ya Moshi Vijiji, hii pamoja na kwamba inaitwa vijijini lakini ipo mjini, zinazofuata ni Ubungo na Kinondoni, hizi zipo mijini; utaona hata miundombinu yake ya kufikia shule ni rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza Halmashauri ya Lushoto jiografia yake ya milima, mabonde, maporomoko na majabali ni ngumu sana kufikika kiasi kwamba hata ukaguzi hauwezi ukafanyika vile inavyopaswa, vilevile pia ndiyo maana unakuta hata upungufu huo wa walimu unachangiwa na kutokuwepo na miundombinu wezeshi ikiwemo ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe rai tu kwamba Wizara pamoja na TAMISEMI kuangalia maeneo fulani fulani ikiwezeka pia tutengenezewe kanda maalumu. Zisiwe tu zinatengenezwa kanda maalum za mambo ya uharifu lakini hata mambo haya ya elimu; kwa sababu Halmashauri yenye shule 169 maana yake ni kwamba kuna mwamko mkubwa sana wa kujenga hizi shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sitaki kuamini kwamba kwa mwamko huo wa kujenga shule kusiwe na mwamko wa kupata faida inayotokana na elimu. kwa hiyo, sisi kwetu shida sio vyumba madarasa, kwetu shida sisi ni ubora wa elimu ambayo inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala zima la *TBC*. *TBC* wanafanya kazi nzuri, tumeona maboresho mbalimbali yanaendelea upatikana lakini bado usikivu na upatikanaji wa *TBC* ni katika maeneo ya mjini; kiasi kwamba sasa *TBC* sasa hivi inashindana na redio hizi za kawaida. Kwa hiyo, tungetamani kuiona *TBC* ikienea nchi nzima hasa katika maeneo ya pembezoni. Hii itasaidia sana haswa katika vipindi vile ambavyo vinatoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kipindi kile cha lishe; sasa hivi vipindi vizuri kama hiki wananchi hawapati faida ya kuvisikia kwa sababu *TBC* haisikiki. Naamini kwa namna ambavyo Tanzania tunazalisha na vyakula vilivyo vingi, wananchi wakipata elimu hizi za lishe na mambo mengineyo kupitia *TBC* itasaidia sana kuhakikisha kwamba hata huu udumavu ambao tunausema utapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, pamoja na kazi kubwa ambayo anaifanya pale *TBC,* lakini tunaomba shirika letu hili lipate uboreshaji mkubwa. Tunaomba sana kuwa na Televisheni ya Taifa ambayo ndiyo msingi wa kulinda maadili, mila na desturi za Kitanzania, aweze kusaidia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naungana na walionitangulia kuwapongeza sana Wenyeviti hawa wawili; Mheshimiwa Serukamba pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI. Nimefurahi sana kwa taarifa zao nzuri sana, ushauri wao na maoni yao kuhusu maeneo ambayo wanayasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze upande wa elimu. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako, Waziri wa Elimu kwa kuja Sumve kwenye mahafali. Ujio wake Mheshimiwa Prof. Ndalichako umemuibua kijana mmoja wa kutoka shule zetu za Serikali anayeitwa Mayeka Ndaki aliyepata *Division* 1.7 shule za Serikali. Ujuo wake Mheshimiwa Waziri kwa kweli tunaufurahia sana; na wameniomba nimletee shukrani hizo ili akipata nafasi siyo vibaya, basi akapita tena kwa sababu aliwatia moyo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwa Wilaya yetu ya Kwimba kutupatia Chuo cha *VETA*. Chuo hicho sasa tayari kimeshaanza kujengwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maana yake siyo Kwimba tu peke yake, ni zaidi ya vyuo karibu 50 vinajengwa nchi nzima kupitia bajeti iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa huu utaratibu mzuri wa Elimu Bila Malipo kuanzia Chekechea mpaka Kidato cha Nne. Naleta ombi kama Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati itampendeza; kama tumeweza kulipia Chekechea mpaka

Kidato cha Nne, wanapofaulu hawa vijana kwenda Kidato cha Tano na Sita, mfuko unaweza ukawa mdogo lakini siku zijazo tunaweza tukawafikiria hawa vijana. Maana yake nao ni Watanzania. Kidato cha Tano na cha Sita, ikiwezekana nao waingie kwenye utaratibu huu wa Elimu Bila Malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nakuomba sana, ili tupate wanasayansi wengi na wazuri, tunazo maabara zetu huko kwenye maeneo yetu, tumeanzisha kwa nia nzuri tu. Namshauri Mheshimiwa Mwenyekiti na Waziri wa Elimu, tuone namna nzuri zaidi ya kukamilisha haya maboma ya maabara na kupeleka wataalam pia kwa maana ya Walimu wa Masomo ya Sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tunatengeneza maabara nzuri, tunapeleka na vifaa labda, lakini Walimu wa Masomo ya Sayansi hawapo, inakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu nzuri sana hii ya Maendeleo ya Jamii, angalau alione hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, nafikiri Mheshimiwa Waziri Jafo hayupo, lakini Serikali ipo; Mkoa wa Mwanza wakati wanafanya ukarabati katika ukamilishwaji wa maboma, Wilaya ya Kwimba peke yake ndiyo iliyosahaulika. Sijui ni kwa sababu gani? Hii kila siku nimekuwa nikiisema. Ni Wilaya peke yake iliyosahaulika, wilaya nyingine zote zilipewa fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha hayo maboma. Sisi tukaja baadaye tukaomba tupatiwe fedha za maboma 21, lakini mpaka leo, hazijapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije Wizara ya Afya. Nawapongeza wananchi wa Wilaya ya Kwimba na Mkoa wa Mwanza na Watanzania wote kwa ujumla. Wananchi wamejitolea kujenga Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya, cha ajabu ni kwamba hospitali zile ukienda baada ya kufunguliwa utakuta kuna mganga mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukiziimarisha hizi hospitali zetu kwa maana ya Zahanati, zikaimarika vizuri kukawa na wataalam wa kutosha, tukaviimarisha Vituo vya Afya vikawa na wataalam wa kutosha, madawa, *X-Ray, Ultrasound* na kadhalika, hutapata wagonjwa wa kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya au ya Mkoa, vinginevyo labda mgonjwa awe amezidiwa sana. Tukiwa na Zahanati na Vituo vya Afya vyenye vyombo vya kutibia na waganga wa kutosha, nina uhakika itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwa haina maana, zile nguvu za wananchi tunazipoteza bure. Tumejenga Zahanati, Vituo vya Afya kwa gharama kubwa, ambavyo kwa sasa inakaribia shilingi milioni 900, lakini ukienda unakuta wataalam hawapo. Inakuwa tu kama jitu liko pale, *white elephant* liko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado wanaweza kutumia utaratibu mzuri ambao naupendekeza kwa upande wa elimu na kwa upande wa afya. Kama hatuna wataalam wa masomo ya sayansi, hatuna waganga wa kutosha, hivi wale wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu katika vyuo vyetu upande wa elimu na afya, wakati tunasubiri ajira, ili kupunguza hii *gap* iliyopo ya upungufu wa wafanyakazi, ni jambo ambalo linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale mlioshiriki kwenye Mkutano wa *SADC* pale Dar es Salaam, Rais wa Afrika Kusini alikuja na familia yake inaitwa *YES (Youth Employment Service)*. Unawachukua hawa vijana waliomaliza vyuo wanakwenda kupata uzoefu kwenye maeneo hao. Wakati huo huo watakuwa wanafundisha au wanatoa huduma kuliko kuwaacha tu, wanapata uzoefu. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Waziri wa Afya, hebu tuangalie na hilo nalo mkiona linafaa basi tuweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nitakuwa simtendei haki Rais wangu kama sitampongeza kwa kazi nzuri sana za kizalendo anazozifanya nchi hii. Nawaomba sana Watanzania wenzangu wote, hata upande wa kule kwa rafiki yangu Mheshimiwa Mbowe, Rais anafanya kazi nzuri sana, nzuri mno na kila mtu anaona. Cha kufanya ni sisi Watanzania tuungane tumwombee ili aendelee na kasi ya kutuletelea maendeleo Watanzania wote. Haya mengine yatafuata baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme, Mheshimiwa Mbatia alisema maneno mazuri sana jana, nikawa nafikiria, Mwalimu Nyerere alikaribishwa pale *New York* na Mama Mongella, akamkuta Mganda mmoja, huyo Mganda akamwuliza Mwalimu, Mwalimu siku hizi kwenu sisikii neno ukabila, Mwalimu akamwambia, mama ilikuwa zamani, siyo leo; saa hizi wanasema!

Mheshimiwa Naibu Spika, nami namwambia Mheshimiwa Mbatia, ule utaratibu wa 1995 tulipoingia Bungeni na ustahimilivu wa namna ile na kuitetea Serikali ilikuwa wakati huo baba, siyo leo. Sasa Wabunge wote humu, hasa upande ule kule kuna mhemko! Uchaguzi kesho kutwa, wanafikiria, hivi viti kweli nitavirudia tena mwakani! Hiki ni kionjo tu, itakapofika kwenye Bunge la Bajeti ni mshike mshike! Kwa hiyo, tuvumiliane tu ndugu zangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo mimi ni *member*. Tuko vizuri chini ya Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Serukamba, ingawa kuna muda anakuwa *very partisan* badala ya kuwa *bipartisan* tunapokuwa kwenye vikao, anakuwa na mambo ya uchama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitagusia kwenye afya na habari. Kwenye afya tunajisifu kwa kujenga majengo mengi ya Zahanati, Vituo vya Afya na hata Hospitali. Hii lazima tuelewane, hata mimi najenga kupitia Mfuko wa Jimbo, na kadhalika; najenga Zahanati, natoa bati kwenye Vituo vya Afya na kadhalika, lakini tuna tatizo la madawa na vifaa tiba kwenye maboma tunayojenga. Kwa hiyo, yale maboma maana yake bila vifaa vya matibabu yanaweza yakawa hata *guest house*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajisifu kujenga majengo lakini hatuna watumishi wa kutosha wa afya. Kwa mujibu wa *study* pungufu ni takribani asilimia 52; tuna asilimia 48 tu ya Watumishi wa Afya wakiwemo Madaktari, kwa sababu hatuajiri kabisa. Kinachoshangaza, *graduates* wapo wengi sana kwenye kada ya afya wakiwemo Madaktari ambao wako mitaani hawana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yupo kijana mmoja Daktari, amemaliza Udaktari, amesajiliwa na Baraza la Madaktari, lakini yuko pale Uyole mpigakura wangu anauza vocha za kurusha. Daktari ambaye ame-*graduate,* amesajiliwa na Baraza yuko mtaani anauza vocha kwa sababu hakuna ajira. Kwa hiyo, hili ni tatizo sana. Inabidi tuangalie namna gani tunaongeza nguvu ya kuajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya sasa hata wale wachache waliopo, hiyo asilimia 48, maslahi yao ni duni sana bado, kama ilivyo kwa watumishi wengine wa Serikali au wa Umma.

Sasa hivi kwa takribani miaka mitano Madaktari na Watumishi wengine wa Umma hawajaongezewa mshahara hata shilingi mia ndani ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari walikuwa *vocal,* wanaongea na kugoma, sasa hivi hamsikii wanagoma mnafikiri kwamba wameridhika; sisi tunakutana nao kwenye Kamati, hawajaridhika. Ni kwamba sasa hivi kidogo mambo yako chini ya *iron fist, hard* kidogo! Hawawezi, wanaogopa kuishia kule ambako tunaishia wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu yote hawajaongezwa mshahara hata shilingi mia, hali inayosababisha tudhani labda hawa watu wanafanya kazi chini ya mgomo baridi. Kwa sababu haiwezekani, hata hili suala la kwenda kutibiwa nje, nafikiri hili suala tunasema kwamba hatuendi tena nje kisiasa, lakini kiuhalisia *(practically)* bado tunahitaji kupeleka baadhi ya wagonjwa nje kwa ajili ya matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni Mheshimiwa Lwakatare, *my brother* hapa, amekaa Hospitali ya Muhimbili, hospitali kuu kabisa ya Tanzania takribani miezi mitatu hajanyanyuka. Amepelekwa India, amekaa siku tano, siku ya sita amerudi, siku ya saba tuko naye Bungeni. Huu ni ushahidi kwamba bado kuna vitu tuna-*miss;* kama siyo vifaa, basi wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matibabu kwa wananchi masikini ni gharama mno. Ni gharama sana! Sasa nashauri, wakati tunajipanga vyema na masuala ya Bima ya Afya na kadhalika, tusiache watu wafe, tuwatibu. Uzuri ni kwamba ninyi mnajipambanua kama ni wajamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuko mlengo wa kati, huku ubepari huku nini, soko huria ndiyo msimamo wetu. Ninyi mnasema ni wajamaa; wajamaa gani mnaacha kutibu watu? Kwa sababu hata Uingereza ambao ni mabepari wanatibu watu bure chini ya mfumo wa *NHS (National Health Services).* Nashangaa sana, hivi mnawezaje kutoa elimu bure mshindwe kutoa matibabu bure? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi subiri kidogo. Mheshimiwa Ummy, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji. Kwanza Sera ya Serikali, lakini pia ndiyo uhalisia, hakuna Mtanzania anyehitaji matibabu ambaye amekosa kupata matibabu. Ndiyo maana taarifa ya Kamati imeonesha, tukichukua Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, zaidi ya shilingi milioni 800 zimetumika kuwalipia wagonjwa wasio na uwezo wa kulipia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Sugu anapotosha, hatujasema hatupeleki kabisa wagonjwa nje. Ninyi ni mashahidi, watu wa mafua, Malaria na magonjwa madogo madogo wote walikuwa wanakwenda nje. Tumewapunguza kutoka 600 mpaka 53. Kwa hiyo, ni kweli hatupeleki nje kwa magonjwa ambayo tuna uwezo wa kuyatibu ndani ya nchi na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumefanya vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana. Halafu asimwingize Rais, hapa tunaongea na ninyi ambao mmetumwa na Rais kufanya hizi kazi. Kwa hiyo, msimwingize Rais kwenye mijadala yetu humu, maana yake mnajificha kwenye kichaka cha Rais. Nini watu!

Wewe Mheshimiwa Waziri, ninyi mnasema kwamba hamjakosa fedha za kutibu Mtanzania, ninyi mnashikilia maiti za Watanzania kwa sababu wamekosa fedha za matibabu! Eeh! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hawalipi!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Watanzania; nenda Muhimbili, nenda Hospitali zote za Serikali, Mtanzania mwalimu mshahara wake shilingi 300,000/= au shilingi 400,000/=, anaumwa ugonjwa *serious,* analazwa miezi mitatu, minne, bili inakuja shilingi milioni saba, shilingi milioni nane, shilingi milioni tisa; anafariki dunia, hawa wanashikilia maiti. Mnashikilia maiti za Watanzania ninyi. Wanawanyima fursa Watanzania ya kwenda kufanya ibada za maziko. Wanawanyima Watanzania fursa...*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, kuna taarifa nyingine. Mheshimiwa Kandege.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naheshimu sana mchango wa Mheshimiwa Mbunge, lakini siyo vizuri akapotosha. Kwa sababu hakuna mtumishi wa Serikali hata mmoja ambaye hayuko kwenye *insurance*. Sasa anasema mwalimu ambaye ana mshahara wa shilingi 300,000/= anashindwa kutibiwa wakati yuko *fully covered* na *insurance!* Siyo sahihi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya basi, tufanye siyo walimu, tufanye Watanzania wa kawaida kama yule ambaye alimwomba Mheshimiwa Rais shilingi milioni tano ili agomboe maiti yake. Sasa ni wangapi ambao wanamwona Rais mpaka wapate huo msaada? Mpaka Watanzania wengine wachangie ili kumfanya Mheshimiwa Rais afanye shughuli zake. Ninyi, msimwingize Rais kwenye haya mambo ya humu Bungeni. Tukae na ninyi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo itakuwa taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Mbilinyi. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namheshimu sana Mheshimiwa Mbilinyi, ni rafiki yangu sana, lakini kwa kweli kile anachokisema hapa ni upotoshaji wa hali ya juu sana na akiwa ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ndani ya Wizara na kupitia hospitali zetu tumeweka utaratibu mzuri sana; na ni fursa hii ya kuwaelekeza Waheshimiwa Wabunge. Tuna Dawati la *Social Welfare* ambalo kama kuna mwananchi ambaye amepata matibabu ya aina yoyote ile na akashindwa kugharamia aidha amepona au mgonjwa wake amefariki anakwenda katika Dawati hili la *Social Welfare* pale, watamfanyia *assessment.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hatuna maiti ambayo tunaishikilia kama Serikali. Ndiyo maana lile ambalo alikuwa anasema Mheshimiwa Waziri hapa, tunatumia fedha nyingi sana, zaidi ya shilingi milioni 800 katika hospitali zetu nyingi kwa ajili ya kugharamia haya matibabu mengine ya watu ambao hawana uwezo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana. Ndiyo tunachosema, kwa sababu kama dawati lipo, halafu wananchi hawalijui na ninyi mpo, mpaka mwananchi anakurupuka kwenda kumwomba Mheshimiwa Rais shilingi milioni tano, tuna tatizo! Ndiyo maana tunasema hapa kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu ni gharama sana kwenye kila eneo. Twende kwa akina mama kwenye huduma za uzazi, kujifungua; hospitali za Serikali sasa gharama ni balaa. Ni gharama kubwa mno! Hospitali ya Wazazi Meta Mbeya kujifungua ni mpaka shilingi 300,000/= kwa *operation*, kujifungua kawaida mpaka shilingi 150,000/=, shilingi 200,000/=. Hii ni Hospitali ya Rufaa ya Wazazi Meta, *Maternity Hospital* pale Mbeya Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najiuliza, wakati wa Mheshimiwa Dkt. Kikwete na Mheshimiwa Mkapa huko nyuma wazazi walikuwa wanaambiwa waende hospitali na kanga, pamba, nyembe, sijui sindano na vitu vidogo vidogo, mambo mengine yote wanayakuta huko huko; inakuwaje? Ni nini kimesababisha Sera ile ya Afya Bure, Matibabu Bure kwa Wazazi Wajawazito Pamoja na Watoto Mpaka Miaka Mitano, ile sera imekwenda wapi? Au kama ndiyo matokeo ya *sanctions* ambazo tumeanza kuwekewa, basi mtuambie ili tufunge mkanda na tujiandae kwamba tuko katika *stage* gani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi kengele ya pili imeshagonga.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kweli!

**NAIBU SPIKA:** Sina saa mimi jamani, Makatibu wananiongoza hapa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wamekula sana dakika zangu!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukumbushane tu kidogo. Kaa Mheshimiwa Mbilinyi.

Tukumbushane tu kidogo, sisi wenyewe ndio tunatunga hizi sheria; na vile ambavyo sheria zetu zinaweka utaratibu fulani, pengine mchango uelekee kuonesha upungufu wa hiyo sheria kwenye utekelezaji wake. Kwa hiyo, ni kazi yetu kama Bunge kwa sababu kwenye hoja hii Serikali itakuwa ni mchangiaji, haitakuja kujibu hoja hapa.

Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati anataka Bunge liongozwe vizuri ili baadaye liazimie mambo ambayo linataka Serikali iweze kuyafanya. Kimsingi haya yote tunayochangia ni hoja za Kamati na Mwenyekiti ndio atakuja kujibu hapa. Kwa hiyo, tujitahidi kwenda kwa namna ambayo, wale Wabunge ambao sio Wajumbe wa hizi Kamati zetu waweze kupata ufafanuzi wa mambo mbalimbali yaliyoko kwenye hiyo taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe halafu kama muda wetu utakuwa bado upo, basi Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa atafuata.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujalia afya njema na kuweza kuendelea na shughuli zetu za Bunge. Vilevile nitoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kamati kwa taarifa zao walizowasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hii Wizara ni nyeti na imebeba au imeshikilia maisha ya Watanzania, lakini ukiangalia changamoto zilizokuwemo katika Wizara hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mzungumzaji aliyepita hapa amezungumza kwamba gharama za matibabu zimekuwa juu sana. Huu ni ukweli usiofichika. Ushahidi wa hili ni pale Mtanzania anapokuwa na maradhi kwa sababu ya ukali wa maisha, kwa sababu ya umasikini anakwenda katika vyombo vya habari kama *ITV Television* au *Channel Ten* anakwenda kujidharirisha kuomba, kwamba naomba wasamaria wema wanichangie. Mimi hili jambo linaniuma kweli kweli, kwa sababu huyu ni Mtanzania, tunajifaragua na kujidai kwamba tunakusanya *1.9 trillion* kwa mwezi, lakini kwa nini Mtanzania aende akajioneshe pengine ana maradhi ya aibu, anachukuliwa na *moving camera* anaonyeshwa namna hii yale maradhi yake. Huu ni udhalilishaji! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetembea katika baadhi ya nchi, najua hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu mmetembea, Naibu Spika, umetembea. Kwa mfano, nchi kama Qatar au Saudia, Denimak, Norway, Finland, kwa wenzetu matibabu hakuna mtu anayekufa kwa sababu hana fedha ya matibabu. Serikali imeweka utaratibu kwamba elimu ni bure na matibabu ni bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtanzania, hata mtoto mchanga, watoto waliozaliwa wameungana, bila aibu tunaenda kuwaonyesha kwenye *television* kwamba watoto hawa wanahitaji wasamaria wema wawachangie. Hili pato la Taifa tunalokusanya kupitia mamlaka ya mapato, shughuli yake ni ipi? Kazi yake ni kununua silaha peke yake? Kazi yake ni kutulipa mishahara sisi Wabunge na Watumishi wa Serikali peke yake? Hawa Watanzania wakimbilie wapi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali mambo mengine ni aibu!

**MHE. AMINA S. MOLELL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** …na kwa bahati mbaya sana, vyombo vyetu vya habari sasa hivi vinaonekana Kimataifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk, kuna taarifa. Mheshimiwa Amina Mollel.

**T A A R I F A**

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbarouk kwamba moja ya kazi za vyombo vya habari ni pamoja na kuihabarisha jamii. Katika kuihabarisha jamii ni pamoja na kuishirikisha katika mambo mbalimbali ikiwemo pia matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni utaratibu wa kawaida kabisa unaotumika na vyombo vya habari, anapokwenda mtu mwenye tatizo kuweza kutaka kuwasilisha tatizo lake kwa jamii na kwa sababu kwenye jamii wapo watu ambao wanaguswa na kuweza kusadia.

Kwa hiyo, asione kwamba ni aibu bali ni utaratibu uliopo katika vyombo vya habari. Ndiyo maana katika vipindi mbalimbali pia watu wanaweza kwenda na kushiriki katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa siipokei. Namwomba Amina Mollel aichukue mwenyewe taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia aibu maana yake, kwa mfano tangu majuzi inarushwa *clip,* kuna mtoto ana matatizo ya figo, tumbo lake limekuwa kubwa kabisa. Ukimtazama mama yake yupo kwenye *television* analia, maana yake hana uwezo wa kwenda kumtibu yule mtoto wake India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine labda niutoe, mimi na Waziri wangu wa Afya pale Mheshimiwa Ummy Mwalimu, sote ni watu wa Tanga, yupo dada mmoja wa Kwanjeka, ana maradhi ya mguu kama tende hivi. Tumejitahidi tukampatia Bima ya Afya, lakini Bima ya Afya kumbe nayo kuna baadhi ya *package* hazihusiki kwamba labda mtu kupelekwa nje. Sasa mtu anadhalilika na maradhi mpaka anakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ndugu yenu mnamwangalia huyu ndio anakwenda zake sasa, lakini hamna cha kumfanya. Mbona kwenye Serikali za wenzetu wanaweza? Kutibiwa na masuala ya elimu ni bure. Kwa nini sisi inashindikana wakati sisi Mwenyezi Mungu ametujalia rasilimali bila ya kumpa rushwa? Ametujalia madini, ametujalia bahari, ametujalia mazao, ametujalia wanyama, vyote hivyo Serikali inapata pesa, lakini inashindwa kuwatibu wananchi wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Hizi taarifa zinakula muda…

**T A A R I F A**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa msemaji ayezungumza kwamba yeye ni Mbunge. Kipindi cha kupitisha bajeti hapa mwezi Juni alikuwepo. Mambo anayoyazungumza alikuwa anayajua, lakini hajayaleta mbele ya Bunge lako ili kwamba bajeti iweze ku-*consider* jambo hilo. Sasa anakuja kusema kipindi hiki ambacho hata hatupangi mipango kama hiyo anayosema, sasa anayewahurumia watu hao ni yeye au anapenda tu kujisemea? Ahsante. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk, jitahidi utumie lugha ya Kibunge maana hapo umezungumza mambo mengine. Kwanza umemwambia Mheshimiwa Amina Mollel aichukue mwenyewe taarifa, hairuhusiwi kikanuni. Wewe unajibu kama unaipokea ama huipokei, unaendelea na utaratibu.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi taarifa siipokei.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia siipokei. Labda niseme, Mheshimiwa aliyesema kwamba eti tunapitisha bajeti; bajeti ndiyo tunapitisha, lakini kwa mfano jana mchangiaji mmoja alizungumza hapa, nami niliwahi kuzungumza huko nyuma, tunapitisha bajeti labda ya Wizara ya Kilimo kwamba wapewe asilimia 100 ya fedha, wanapewa asilimia 11, ni bajeti isiyotekelezeka. Hata mimi najua dada yangu Mheshimiwa Ummy hiyo bajeti tunayompelekea pia haimtoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naizungumzia Serikali kwa ujumla wake sasa kwa sababu ndiyo inayokusanya mapato yote ya Serikali. Ni wajibu wa Serikali kuwatibu wananchi wake hasa pale wanapokuwa katika maradhi ambayo hawayamudu kugharamia kwa matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niseme, kwa mfano Sera ya Taifa ni kwamba Wazee, Watoto na Akinamama Wajawazito Watibiwe Bure, lakini ukienda katika hospitali zetu hawa akina mama kwenye hizo *delivery kit* pia unakuta katika baadhi ya maeneo wanachangishwa, wanaambiwa walipie, siyo kwamba ni bure. Mtu anaambiwa alipie hiyo *delivery kit*, lakini pia kuna vitu vingine ambavyo anatakiwa alipie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama Wabunge humu ni mashahidi, labda kama watakuwa wanapendelewa kwa upendelo kwa hadhi waliyokuwa nayo, lakini akina mama wengi hususan maeneo ya vijijini, akienda kujifungua lazima *delivery kit* alipie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kusema, hata watoto ndiyo huo mfano ninaoutoa kwamba watoto chini ya umri wa miaka mitano wameambiwa watibiwe bure, sasa huyu mtoto ambaye anapelekwa kwenye *television* wakaombwa wasamaria wema, matibabu bure yako wapi hapo? Huyu ni Mtanzania, tena ni mtoto mchanga, malaika wa Mungu, basi sisi hata hatumwonei huruma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, tunaposema matibabu yawe bure, basi yawe bure; akina mama wapate *delivery kits* zile *free no charge,* wazee watibiwe bure. Tena kwa bahati mbaya, anakwenda mzee labda kutaka matibabu, anaambiwa wewe si una watoto? Sera ya Taifa haikusema kwamba mtu akiwa na watoto asitibiwe bure. Imesema "mzee." Au anafika hospitalini au Kituo cha Afya mzee anaambiwa, lete kitambulisho cha uzee. Sura yake ukimtazama, si unamwona ni mzee huyu, kitambulisho cha nini? Mtu unamwona kabisa huyu ni mzee, lakini anaambiwa atoe kitambulisho cha uzee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona huku ni kuwanyanyasa. Kama tumeshindwa kuwatibu bure watu wetu, naomba tuwaambie basi hakuna matibabu bure, kuliko tunawapa moyo, mtu anajua anaumwa anakwenda kutibiwa bure halafu akifika kule anakatishwa tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua umenilindia muda wangu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni watoto wa mitaani. Wizara inazungumza kwamba itahudumia maendeleo ya jamii, lakini watoto wa mitaani wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku kwa sababu hatushughuliki nao, hatuna *center* tunazowaweka tukawapatia labda elimu, tukawapa mafunzo; matokeo yake wale wale ndio wanaogeuka kuja kuwa vibaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, tukiachilia mbali watoto wa mitaani, hata vichaa; unakuta kichaa anatembea uchi sokoni au anapita maeneo ya shule; yaani watoto wadogo wanajua kumbe mtu akishakuwa mtu mzima, ana vitu hivi na hivi! Kichaa hana mtu wa kumwangalia, hana hata nguo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikari iweke vituo maalum kama baadhi ya nchi za wenzetu. Watu wenye kichaa tunawachukua, tuhakikishe na wao wanaoga, wanabadilishwa nguo na wanapewa chakula. Wengine wanakufa kwa njaa tu. Mtu ni kichaa, amekaa sehemu hana akili hata ya kujua kwamba muda huu natawakiwa nile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, watoto wa mitaani na vichaa lazima tuwawekee utaratibu, tuhakikishe kwamba kwanza watoto wa mitaani wanapata elimu, lakini hata hawa vichaa isiwe ni aibu sasa mitaani. Wawekewe maeneo maalum. Hebu fikiria wewe usipooga kwa muda wa siku moja tu unajisikiaje? Sasa kichaa miezi tisa hajaoga, unafikiri anajisikia vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, hawa nao ni Watanzania, wanahusika kabisa na pato la Taifa au keki ya Taifa ambayo inakusanywa na Serikali nao iwahudumie kwenye mavazi, chakula na hata hali ya kimazingira ya afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho labda nizungumzie kwenye masuala ya huduma; huduma ziko katika maeneo mengi sana. Sasa hivi tuzungumze hata kwenye huduma hizi kama za maji, labda na umeme, tunashukuru kwenye umeme wamejitahidi, lakini kwenye masuala ya maji bado wenzetu wa vijijini wana matatizo makubwa ya huduma hii ya maji. Maji wanayotumia kwa kweli yanawasababishia maradhi kwa sababu siyo safi na salama.

Tuishauri Serikali sasa, katika ile miradi ya vijiji kumi kila Halmashauri, wahakikishe wananchi wa Vijijini nao wanapata maji kwa usalama wa afya zao, lakini kwa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la maiti. Kumekuwa na tabia sasa maiti imekuwa ni dili au nacho ni chanzo cha mapato ya Serikali. Huyu mtu ameshatangulia mbele ya Mungu, amesamehewa. Kwa mfano sisi Waislamu, mtu akishakufa, amesamehewa kuswali, amesamehewa kufunga, maana yake huyu amerudi mikononi mwa Mwenyezi Mungu, lakini Serikali yetu ya Tanzania, maiti anachajiwa akikaa *mortuary*. Hii mimi nasema ni aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuhakikishe kwamba sasa hawa maiti isiwe dili, wasamehewe kama walivyosamehewa na Mwenyezi Mungu. Kuna baadhi ya familia hazina uwezo; mtu anaambiwa shilingi milioni tano, ndiyo hayo sasa aliyosema Mheshimiwa Sugu hapa, kwamba mtu anajitokeza mbele ya Mkutano wa Rais anaomba shilingi milioni tano akakomboe maiti. Hivi Rais huyu kwa nini tunamlundikia mizigo ya kazi nyingine ambazo hata hazimuhusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tena, maiti kwenye nchi yetu ya Tanzania wasichajiwe. Wakiwekwa *mortuary,* siku hizi kuna mawasiliano mengi tu, ifahamishwe familia yake waje wachukue maiti yao wakazike, lakini kumdhalisha maiti kumweka katika mortuary kwa muda mrefu, hilo nalo pia sio haki. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda tayari.
**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tukumbushane tu Waheshimiwa Wabunge, Serikali inaposema matibabu bure kwa wazee ni wazee wa zaidi miaka 60. Sasa kuna mtu anaweza akaonekana mzee kumbe miaka hajafikisha kwa sababu ya mazingira yake. Pia kuna wale ambao udongo

unatofautiana; na kuna watu wanaonekana wadogo, kumbe watu wazima. Kwa hiyo, huwezi kumwangalia mtu sura ukasema huyu ni mzee.

Pia ni wazee wasiojiweza. Asisimame Mbunge akasema mimi mzee wangu; wewe mzee wako mkatie bima, ndiyo maana tunasisitizwa tuwe na bima. Usianze, mimi mzee wangu naye amezidi miaka 60, aah, ni mzee asiyejiweza.

Kwa namna hiyo hiyo, hata wananchi wengine wanaojiweza lazima walipie hayo matibabu yao. Ni yule ambaye hajiwezi ndiye ambaye amewekewa lile dawati, maana sasa hata dawati hilo asije akaanza kwenda hata mtu mwenye uwezo.

Mheshimiwa Profesa Maghembe, dakika zimebaki chache sana, kwa hiyo, karibu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza naunga mkono hoja ambazo ziko mezani. Napenda sana kuzipongeza hizi Wizara ambazo tunazijadili hapa moja kwa moja na kuzilenga Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Afya. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na tuwapongeze wenzetu kwa sababu wanatumia muda mrefu na wanafanya kazi kubwa ambapo ni vizuri mtu akifanya vizuri tumwambie hongera, apate moyo zaidi wa kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda siyo rafiki sana, nitaongea na kukumbusha hapa Kamati zetu kwamba kwa miaka miwili hapa nimekuwa naongea na kupongeza juu elimu jinsi ambavyo inapata pesa nyingi. Nimesikia mtu mmoja anasema pesa hizo hazitoshi. Haziwezi kuja kutosha hata siku moja, lakini fedha ambazo zinatengwa na Serikali shilingi trilioni 4.4 ni sawa sawa dola bilioni 2.2. Dola bilioni 2.2 kwenye elimu peke yake, hebu angalieni nchi za Afrika, nchi ambayo inatumia dola bilioni mbili katika kutoa elimu ya watoto wake, ziko chache kweli kweli! Kwa hiyo, tuipongeze Serikali ya Tanzania kwa kazi nzuri hii ambayo inafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hiyo nzuri, napenda kukumbusha, bado kule Mwanga tuna walimu wachache sana. Walimu wa Shule za Msingi kule Mwanga ni wachache kweli kweli! Wastani wa walimu kwenye shule zetu za msingi kule Mwanga ni walimu wawili au watatu. Tuna madarasa nane kwenye shule moja ya msingi. Kwa hiyo, walimu watatu wakiingia kwenye madarasa matatu, watoto wengine waliobaki kwenye madarasa matano, wanaendesha soko huko na kucheza darasani. Kwa hiyo, kuomba tupate walimu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme pia kwamba kwa kweli Wizara ya Afya pamoja na kuipongeza, niipongeze tena, wamejenga Vituo vya Afya zaidi ya 300 katika kipindi kifupi hiki, wanastahili kupongezwa. Katika kazi hizi nzuri na watu tuko milioni 55 huwezi kudhani kwamba itakuwa kama maua, haiwezekani. Kutakuwa na shida shida kama hizi za wazee na hizi shida tutaendelea kuzitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuungana pamoja kama Wabunge na Serikali yetu tusaidie kutatua haya matatizo. Napenda nikumbushe kwamba huko nyuma tulikuwa tunajenga Vituo vya Afya sisi wenyewe; wananchi wenyewe na Serikali inatusaidia. Tunajenga Zahanati na Serikali inatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye Wilaya yangu ya Mwanga nina Vituo vya Afya vitatu ambavyo vimejengwa na karibu vimekwisha na vimejengwa na wananchi njia ya msaragambo. Hivi vituo tunaiomba Serikali na sasa wakati huu ndiyo mnapanga bajeti, mtusaidie kuvimaliza ili vile sawa sawa na hivi ambavyo vimeletwa na Serikali na kupigwa mara moja na kumalizika; sasa vile ambavyo wananchi wamejenga karibu wanamaliza na nguvu zao

zimetumika kiasi kikubwa sana, basi mtusaidie kuvimaliza. Tuna Kituo cha Afya cha Kileo na Kitu cha Afya cha Mwaniko ambavyo tunaomba Serikali itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tuna Zahanati sita ambazo tunaomba mtusaidie. Zahanati ya Kituri imekamilika na wananchi wamefanya juhudi kubwa, wamepaua na wamemalizia *almost complete,* lakini nasikia wametumia mabati *gauge* 30 na Injinia wa Wilaya anasema wang'oe mabati. Sasa nafikiri kwamba jambo hili tulifikishe kwenye Wizara ya Afya. Maana hata kama wananchi walikuwa hawana mabati, wana nyasi peke yake, basi wamejenga kituo chao ndiyo hicho, waruhusiwe kukitumia, wasiambiwe wang'oe mabati kwa sababu ni nyumba ya Serikali. Nyumba ya Serikali ingeng'oa mabati kama Serikali ingeleta hayo mabati mengine. Kwa hiyo, tunaomba wananchi wasaidiwe Zahanati ifunguliwe mapema, maana wametumia fedha nyingi sana kuijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna zahanati pia  Lembeni, Mlingeni, Vanua kule Ndorwe, Buchama, Ndambwe na Kitoghoto ambapo Zahanati hizo karibu zimekamilika, lakini wananchi wanahitaji msaada kidogo tu wa Serikali ili waweze kuzitumia Zahanati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nitoe mapendekezo hapa kwamba jamani tuna Shule za Sekondari sasa zinatosha, watoto wetu wa kutoka Shule za Msingi karibu wote niseme, wabaweza kwenda Sekondari, lakini kuna tatizo kubwa kwenye Sekondari zote hizi. Ni Sekondari chache tu ambazo wananchi wamemaliza ujenzi wa maabara. Ina maana kwamba wanafunzi wetu wanajifunza sayansi kwa nadharia tu, hakuna mahali ambapo wanajifunza *physics* kwa kufanya *practical;* hakuna mahali wanajifunza biolojia kwa kufanya *practical;* na hakuna mahali wanajifunza kemia kwa kufanya *practical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga maabara siyo kitu rahisi na kuwapa wananchi wa vijijini kazi ya kujenga maabara na hawajui maabara maana yake ni nini, ni kutaka vitu vingi sana kutoka kwa wananchi wa vijijini. Tunaomba sana jamani, katika bajeti hii inayokuja, Serikali itenge angalau shilingi bilioni 200 imalize hizi maabara zote ili watoto wetu wa shule hizi za Kata waweze kufaulu mtihani wa *Form Four* kama wale ambao wanasoma kwenye shule za *private,* kwa sababu watoto wetu hawa wanafanya sayansi kinadharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nimalize nalo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Profesa, ahsante sana.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** *Ooh, my goodness!*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Nitawataja Wabunge wachache watakaoanza kuchangia mchana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Profesa huyu; Mheshimiwa Said Maulid Mtulia, Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Grace Victor Tendega na Mheshimiwa Riziki Said Lulida.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.04 mchana Bunge lilisitishwa hadi 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

**NA**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA YA MAENDELEO YA JAMII**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NABI SPIKA:** Tutaanza na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Grace Victor Tendega ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii muhimu ya kuchangia taarifa mbili tulizonazo mbele yetu; taarifa ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Katika Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii katika ukurasa wa 44, Kamati imeshauri vizuri, kwamba kuna haja ya kuweka mikakati ya maksudi ya kuhakikisha tunakabili changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya afya na sekta ya elimu. Ushauri wa Kamati ni mzuri na mapendeklezo ya Kamati ni mazuri. Hii inadhihirisha maeneo mbalimbali kila mtu kwenye eneo lake atakubaliana nami kwamba Kamati inaposema kuna changamoto ya Wataalam katika sekta ya afya na elimu ni kweli, kwa mfano; kwangu kule Wilaya ya Misenyi tuna upungufu wa Walimu katika shule za msingi, upungufu wa Walimu 750; hiyo ni Wilaya moja; na ukienda kila Wilaya tatizo linafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lazima niipongeze Serikali; kwasababu tulikuwa na tatizo pia la upungufu wa walimu upande wa walimu wa sekondari, Tanzania nzima tulikuwa na upungufu mkubwa.Ambacho kimetokea kwa sasa ni kwamba tuna upungufu wa walimu tu wa masomo ya sayansi na hisabati, lakini sasa tuna walimu wa kutosha kwa masomo ya sanaa, wapo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo ndiyo maana nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya kuondoa tatizo la upungufu wa Walimuy wa sanaa. Naungana na Kamati kama ilivyoshauri kwamba mikakati itafutwe ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niikumbushe Serikali na niiombe Serikali kwamba kwa kuwa mmeweza kuondoa tatizo la upungufu w Walimu wa sanaa, mbinu mlizotumia hizo hizo mzihamishie kwenye kuondoa upungufu wa walimu wa sayansi na hisabati; nadhani tukifanmya hivyo tutaweza kupiga hatua kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimekuwa nikijiuliza, unakuta maeneo mengi hawa tunaowaita walimu wa sanaa, ukitembelea shule zetu hizi ukaenda ukazungumza utakuta wale walimu wa sanaa wengine watakwambia hapa hatuna mwalimu wa hisabati, hatuna mwalimu wa sayansi; sasa unauliza, kwamba wanafunzi hawafundishwi? Wanasema a’ a! hawa walimu

wengine hawa wa sanaa tunawaomba wanasaidia saidia kufundisha. kuna shule moja ambayo niliambiwa walimu wa sanaa wanaombwa, wanasidia kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana walikuwa wana A za hesabu, A za fizikia na A za masomo mengine ya sayansi. Maana yake ni kwamba walimu hawa ambao tunaowaita ni walimu wa sanaa kama wakiweza kuongezewa utaalam kidogo wanaweza pia wakawa walimu wazuri wa masomo ya sayansi. Kwahiyo, naungana na Kamati kama ilivyoshauri kwamba Serikali ifikirie nini kifanyike basi kimojawapo cha kufikiria ni jinsi gani wanaweza wakaandaa mafunzo maalum kwa hao walimu waliopo ili waweze kuwa walimu wa masomo ya hisabati na sayansi wakati tunaendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie pia suala la wagonjwa wa msamaha. Ni kweli kama ilivyoeleza Taarifa ya Kamati, ni kwamba unakuta akina mama wajawazito, wazee wasiojiweza na watoto wa chini ya miaka mitano wanakuwa ni wengi sana wanpokwenda hospitali; na kwa kuwa sera yetu iko wazi hospitali zinawajibika kuwahudumia hawa. Zikiwahudumia unakuta ndani ya muda mfupi fedha yote iliyotengwa imekwisha. Sasa nilikuwa nafikiria, kwamba kwa kuwa tunayo hoja ya kuanzisha ile bima ya afya kwa wote, basi hiyo sheria itakapoletwa pia izingatie umuhimu wa kutoa bima maalum kwa haya makundi ambayo tulishasema kwamba yapate huduma. Mimi nadhani tukifanya hivyo tutaweza kupata ufumbuzi wa kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika ukurasa wa 53 Kamati imeshauri kwamba ni vizuri Serikali iwekeze na kuboresha vyuo vya ufundi nchini ili viweze kuzalisha mafundi wa kutosha watakjaosaidia katika kuendesha viwanda. Nakubaliana na Kamati kwa mapendekezo hayo, ni mazuri; na nipnde kuchukua nafasi hii kuishukuru Wizara ya Elimu kwa jinsi ambavyo imewekeza vya kutosha. Kule kwangu kwa kweli sina cha kulalamika, wamewekeza zaidi ya milioni 700 kwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi-Gera.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa napita pale rafiki yangu mmoja akasema hicho ni Chuo Kikuu kipya, nikasema hiki si Chuo Kikuu, hiki ni Chuo cha Maendeleo ya Wannachi; na nashukuru sana na serikali imefanya hivyo maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo tulilonalo maeneo mengi vyuo hivi havitumiwi vizuri. Ukivitembelea vyuo hivi maeneo mengi unakuta hatuvitumii vizuri. Kwahiyo nitoe wito kwa wenzangu Waheshimiwa Wabunge tuliopo hapa kwamba vyuo hivi tuvitumie vizuri, kwasababu tukivitumia vizuri vitatusaidia kutoa mafunzo ya kuweza kupambana na ukosefu wa ajira, kuwawezesha vijana kuweza kujiajiri pamoja na kuwaandaa na vijana ambao wanaweza wakatusaidia katika kuendesha hii Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna eneo moja ambalo ningependa kulizungumzia kidogo, ni upande wa mikopo ya elimu inayotolewa kwa ajili ya vijana wetu; tunatoa mikopo kwa vijana wanaosoma shahada mbalimbali, lakini kuna kada ambazo tumezisahau. Kwa mfano mimi najiuliza, tuna Chuo chetu cha *IJA (Institute of Judicial Administration)* kule Lushoto; vijana wanaosoma pale wanasoma mafunzo muhimu sana ya sheria kwa *Diploma, Certificate* na hawa tunawahitaji sana ili watusaidie lakini wao hawapewi mikopo.

Sasa mimi najiuliza, hivi, hawa tunawahitaji na tunafikiri kwamba watatusaidia katika kutoa haki ndani ya nchi lakini kwanini inapokuja kwenye mikopo tunasema hao wasipewe? Na kwamba wapewe wa *Degree* peke yake? Mimi nadhani wakati umefika wa kuangalia ni kwa jinsi gani tunaweza tukapanua wigo ili vijna wengi zaidi waweze kupata mikopo ya kuwasaidia kupata elimu kila mtu kadri ya hatua ambayo anasoma. Kwasababu kusoma *Certificate* au *Diploma* siyo dhambi wkamba usimpe mkopo kwasababu anasoma Kada ndogo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekwisha au bado kidogo?

**NAIBU SPIKA:** Umekwisha Mheshimiwa, umeshamaliza dakika zako ahsante sana.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Said Maulid Mtulia atafuatiwa an Mheshimiwa Grace Voctor Tendega, Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mimi pamoja na Wabunge wenzangu leo kupata fursa ya kujadili hoja zote mbili zilizotolewa na Wenyeviti wetu wa Kamati; pili nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wangu mimi naunga mkono hoja zote mbili na Maoni ya Kamati. Hata hivyo nilikuwa nataka niseme hapa, kama kuna Kamati amabzo zinaonyesha namna gani Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ilivyotekeleza Ilani na inavyojali maendeleo ya watu, basi hoja za leo zinathibitisha kwa wazi kabisa kwamba Serikali si tu inajali maendeleo ya vitu bali pia imezingatia sana maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii adhimu kabisa kumpongeza Rais wetu mpendwa, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kusimamia kwa dhati, kwa umahiri mkubwa kabisa, kujenga na kuleta maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo ukizingatia kwamba hivi sasa pesa za elimu bure kila mwezi Serikali inatoa bilioni 23. Ukipiga hesabu kwa Mwaka unapata biloni 276, na ukizidisha miaka mitano ya Awamu hii unapata trilioni 1.38

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo; ukienda kwenye mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, tumetoka katika bilioni 337 mpaka bilioni 450; na kama nayo utaizidisha mara miaka mitano unapata trilioni 1.7

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya, haya matrilioni nayataja kwasababu ukienda kwa lile jambo ambalo linasemwa sana la ndege si zaidi ya trilioni 1.2. Kwahiyo utaona kwa haya mambo mawili niliyoyataja ya Wizara hii ya Elimu imezidi gharama tulizoziweka kwenye ndege kwasababu tu Serikali inajali maendeleo ya watu na inahakikisha watu wentu wanapata maendeleo sambamba na maendeleo ya vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukija kwenye afya huko ndiko hatari kabisa. Utakumbuka huko nyuma iliwahi kutokea Mtu alifanyiwa *operation* ya kichwa badala ya *operation* ya goti; lakini leo Serikali yetu imenunua vifaa vikubwa kabisa. Kuna *angle-suit* inanunuliwa pale *MOI* kwa ajili ya kufanya *operation* ya Ubongo kwa kutumia mshipa wa paja. Kwahiyo leo Mtu unaweza kumkuta anafanyiwa *operation* kwa kutumia mshipa wa paja lakini *operation* ya kichwa, mambo ya kwenda kufumua ubongo sasa hayapo tena. Haya yanapatikana Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia gharama za vifaatiba na dawa za Wizara ya Afya inafika trilioni 1.35. Sasa wakati mwingine wenzetu wengine wanaweza wakasema hatufanyi

hiki, hatufanyi kile, hatufanyi vile lakini lazima tuwaoneshe Serikali inafanya vitu gnai ambavyo vinaleta maendeleo kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye michezo; leo tu umemtambulisha yule kijana bondia amekuja na mkanda wake hapa; lakini najua kuna Bondoa Mwakinyo amekuja na mkanda hapa. Mwaka jana tumekwenda kule Misri kwenda kuipeleka timu yetu; ambapo tangu miaka ya 1980 hatujawahi kwenda katika Mashindano ya Afrika, lakini tumeenda katika Utawala huu. Mimi nasema kwamba Utawala huu umekuja na mavumba, umekuja na kismati unafanyakazi kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Simba mambo waliyoyafanya ni makubwa. Wewe unajua kwamba tumefika robo fainali kwenye robo fainali kwenye Mashindano ya Afrika. Hivi tunavyozungumza, Bwana Ally Samatta yuko Uingereza; kwa mara ya kwanza tumepeleka mchezaji kule anapiga *soccer* katika *Premier League* ya Uingereza. Mtu mwingine anaweza akayaona haya yanatokea kama uyoga. Wakati wenzetu wengine wanasema hatuhajafanya huki, hatujafanya hiki sisi tunaenleza tumefanya hili, tumefanya hili, kazi inapigwa kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda wkenye Maoni ya Kamati; Kamati inaitaka serikali sasa kwenye michezo waje na uboreshaji wa viwanja vyetu vya michezo; lakini si uboreshaji peke yake na kuongeza idadi ya viwanja vya michezo pale Dar es salaam na Mafia, lazima Mafia tupeleke viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili, tunataka sasa tuje na Kampuni, viwanda ambavyo vitaleta nafuu katika gharama za vifaa vya michezo *(Sports industry)*. Tukifanya hivi kwenye michezo tutafika mbali sana. Nchi nyingine zote, katika idara ya michezo, idara ya sanaa, idara ya mambo ya *music* ni miongoni mwa idara tajiri sana, lakini kwetu bado inaonekana kuna umasikini. Serikali ikiongeza nguvu kwenye michezo hapa tunaweza kupoata ajira nyingi sana kwa vijana wetu na vijana wetu wakapata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesisitiza umuhimu wa Baraza letu la Kiswahili kushirikiana na Wizara ya Elimu kutengeneza vyuo vingi vya kufundisha walimu wa Kiswahili kwenda kuwafundisha Kiswahili wasiokuwa Waswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakumbuka Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amejaribu kukimiliki Kiswahili na kuuonesha ulimwengu kwamba Kiswahili wenyewe ni Watanzania, na amefanya juhudi kubwa sana. Vilevile kuna soko kubwa sana *East Africa,* kuna soko kubwa sana *SADC,* kuna soko kubwa sana Afrika nzima na ulimwenguni. Tunapokuwa hatuna vyuo vingivya kutoa walimu wengi wa kufundisha Kiswahili kwa wasio waswahili, soko hili litachukuliwa na watu wengine na sisi tutakosa fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumefika mahali, tunakwenda kwenye uchumi wa kati, lakini uchumi wa kati una utamaduni wake. Ifike mahali Wizara yetu ya Elimu na Serikali kwa ujumla itengeneze chombo kitakachopitia mitaala yetu yote ili tuje na kitu ambacho kitatupeleka latika uchumi wa kati. Uchumi wa kati hauwezi kwenda kwamba wanaume wako wanawakata masikio wake zao, uchumi wa kati hauwezi kwenda wanaume wako wanawabaka watoto wadogo, wanawalawiti, uchumi wa kati una ustaarabu wake. Ili tuingie kwenye ustaarabu wa uchumi wa kati lazima na mitaala yetu iwa-shape watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya zamani tulikuwa tunafundisha sayansi kimu watu wapige mswaki, watu wafanye hivi lakini leo lazima tuwafundishe watu utamaduni huu wa kiulimwengu wa watu kuwa wastaarabu, kwasababu uchumi wa kati unataka watu wafanyakazi, wawe wastaarabu, wawe wavumilivu, wawe hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunazungumza hapa kwamba kuna watu wanazidai hospitali maiti, hospitali watu wapate matibabu, wazee na vijana; suluhisho ni kuja na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote; isiwe leo Watanzania mtu akijijua ana tatizo la figo ndipo anakwenda kukata bima. Tunapokuwa na watu wa bima ambao tayari wameshajijua wagonjwa, na ni wengi ndipo wanakwenda kukata bima, hapana. Tuje na nima ya watu wote kwasababu watu wengi watachangia na wachache wenye matatizo ndio tutakaowatatulia matatizo yao. Leo unamkuta mtu anasema hapa tupeleke watu nje, Serikali haijakosa kupeleka watu nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa tunapeleka watu zaiid ya 600 kwenda kutibiwa nje, leo tunapeleka watu 65 sasa ukipiga mahesabu ya kipesa hapa, pesa tunazookoa ni zaidi ya trilioni 1.835. Haya ni mambo ya fedha. Uthibitisho kwamba watu wanapelekwa nje Mheshimiwa Lwakatare yule pale amepelekwa nje, na uthibitisho wa kwamba watu wanafanyiwa *opetation* za figo, siku hizi *operation* za figo ziko hapa Dodoma. Mtu akipata tatizo la figo, wala Wanyamwezi hawaji tena Dar es salaam, wanaishia Dodoma hapa hapa, wanafanyiwa operation ya figo, hayo Mabusha ndiyo usiseme wanamaliza kabisa, kule kwetu hakuna fujo siku hizi mambo yanakwenda vizuri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaj)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umeksiaha, ahsante sana.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja zote mbili za Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Victor Tendega atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Vedastus Mthayo Manyinyi ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Taarifa za Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Taarifa ya Ukimwi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Maoni ambayo ametoa Mwenyekiti wetu ndiyo tumeyafanyiakazi na nina hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia katika sekta ya afya pamoja na elimu. Katika sekta ya afya, ninapozunguma sasa, kwa takwimu za *UNICEF* tuna watoto chini ya miaka mitano ambao wanafariki kila siku kwa idadi ya watoto 312 kwa siku. Ninapozungumza hapa, watoto 312 kila siku wanafariki. Hii ina maana gani? Tukiona kuna ajali inatokea ya basi kwa mfano lenye abiria 65 na tunasikitika watu hawa wamefariki basi moja, kwa watoto 312 ambayo yanaangusha abiria kila siku. Kwa hiyo watoto hawa wanapoteza uhai, na hii ni kwa sababu ya changamoto kubwa tunazozipata katika utoaji wa huduma na ukosefu wa huduma za afya zikiwemo huduma za dharura za upasuaji kwa wakina mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ni masuala ambayo tunapaswa tuyaone na tuyaangalie kwa mapana kwa sababu tunapoteza watoto wengi wakati huo huo sisi tunasema kwamba tuna makusanyo makubwa ya fedha; haya makusanyo makubwa yanakwenda wapi? Hatuna watumishi wa kutosha takribani asilimia zaidi ya 50, hawapo. Sasa kama Serikali hatuna watumishi zaidi ya asilimia 50 kwa Sekta ya afya tunatarajia nini? Hawa Watanzania wengi tunaowapoteza matarajio ni yapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ijipime, ijiangalie, wapi ambako wanatakiwa waweke mkazo tumesema tunakusanya fedha nyingi za mafisadi sawa japokuwa mimi sijaona hao mafisadi wameweza kuhukumiwa wapi tukapata hizo pesa, lakini hatujaajiri wafanyakazi ni miaka mwaka wa nne unakwenda wa sekta ya afya hawapo, hii inaleta adha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda katika sekta hiyo ya afya watumishi wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Sekta hii ni muhimu, ndiyo kinga. Tunapata semina mbalimbali hapa Wabunge viribatumbo, sijui kuna hiki, kuna kile; yote haya ni kwa sababu sekta hii hajaajiri, tuna upungufu takribani asilimia 95 ya watumishi wa maendeleo ya jamii katika sehemu zetu kwenye kata na vijiji ambao walikuwa wakipita zamani wakielimisha jamii, kuleni kuku, mayai, mboga, samaki, maziwa havipo tena sasa hivi ambao walikuwa wanaelimisha, wanawaelekeza wakina mama na wananchi kwa ujumla wapate hiyo elimu, haipo. Sasa kama hatuwezi kuwekeza kwa watumishi hawa ambao ndio kinga matarajio yetu ndio hii kuongeza bajeti ya dawa ambayo inatu-*cost* kama Serikali. Kwa hiyo Serikali lazima iangalie, kinga ni bora kuliko tiba; tuwekeze kwenye sekta hii na tupeleke wafanyakazi ili waweze kuhudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za wenzetu unakuta watu wana-*volunteer,* wanajitolea. Serikali haiamasishi hicho, hamasisheni wananchi wajitolee wakiwa shuleni, wanapotoka shuleni waende wajitolee. Tunaona *volunteers* wengi wanatoka nje wanakuja hapa sisi wa kwetu tunapelekea wapi? Hatuna huo mkakati, Serikali iweke mkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika sekta ya elimu, ninapozungumza *ratio* ya mwalimu wa elimu ya awali ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 146; inayotakiwa ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25, na pale ndipo tunapojenga msingi wa elimu, tunapowakuza watoto wetu wakuzwe vipi, wawe na *study* zipi , wafanye nini, baadae waweje hapa ndio tunapokuza. Lakini sasa tuna uhaba wa walimu 44,273, ni zaidi ya mara nne ya walimu tulionao, miaka 50; miaka 50. Ina maana tutatumia zaidi ya miaka 200 kupata walimu ambao watatosheleza katika nchi yetu, halafu mnasema mtaendelea kuchaguliwa katika awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye suala la wasichana kurudi shuleni wapatapo ujauzito; hiyo ni haki yao ya kielimu. Katika Ilani yenu ya Chama Cha Mapinduzi Kifungu 52 ukurasa 99 kipengele cha elimu (i) *roman*(ii), naomba ninukuuu, kinasema;

*"Wasichana wote wa elimu ya msingi wanaoacha shule kwa sababu ya kupata ujauzito wataendelea na masomo"*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo imenukuliwa, na hii mliipeleka kwenye mpango na ikawa mpango mzima wa utekelezaji; hata tunavyotafuta fedha kwa wafadhili tunatumia kifungu hicho. Niwaulize imetekelezwa wapi? Hawa wanafunzi wengi; mimi siwezi kutetea kwamba mwanafunzi apate ujauzito lakini wale kwa bahati mbaya ambao wanapata ujauzito hakuna mkakati mzima wa kutengenezea utaratibu wa kwenda kwenye masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Zambia wameweka utaratibu, huyu mtoto anatokaje shule, atafanyaje, ataendelezwaje mpaka atarudije shule kuwa-*formal education;* sisi tunataka tumpeleke kwa upeo mwingine aende akatengeneze sijui vitambaa, kufanya hivi. Huyu alikuwa na ndoto zake pengine awe *Pilot*, awe *engineer*, awe mtu ambaye ana mtazamo wake alikuwa anautaka sisi….*(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega kuna taarifa Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa mzungumzaji kama alikuwa na ndoto zake kwa nini alipata mimba ungemzuia asipate mimba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega endelea na mchango wako.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei ninasema hivi kama tendo hilo hilo ambalo linafanya watoto wapate ujauzito na tendo hilo hilo linafanya watu wapate UKIMWI mbona kwenye UKIMWI hatusemi chochote na tunapeleka fedha wanahudumiwa? Kwa nini kwa upande huu tunasema haipo? Ama kwa sababu kwenye UKIMWI na wanaume wanakuwemo? Lazima tuliangalie hili na tupigie kelele hawa watoto wa kike wapate elimu, wapate ndoto zao ambazo wanazitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Afrika Mashariki wameweza kuingiza hilo ukiangalia Kenya, ukiangalia Uganda na soko la ajira ni moja. Sisi tunapokuja kuwa hatuna soko la pamoja tunasema tuko nyuma ni kwa sababu hatuweki mkakati madhubuti watoto wa kike kwenda shule na kuendelea na shule zao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyenyi, Mheshimiwa Mboni Mohamed Muhita ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu anayenijalia afya njema na mimi kuwepo hapa na kuchangia hoja iliyokuwepo mezani. Kwanza napenda nitoe pole kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi ambao wamekutana na mafuriko makubwa ambayo hayajawahi kutokea katika kipindi cha zaidi ya miaka 50. Mafuriko haya yalitokea mwaka 1952; lakini mwaka huu wananchi wa Lindi wamekutana na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikwenda kuona eneo la tukio; lakini kuna watu ambao hawajaona hayo matukio. Lazima Mwenyezi Mungu tuwaombee wale wenzetu ambao wako katika mazingira magumu. Kitu ambacho hujakiona ni sawasawa na usingizi wa giza au usiku wa giza. Wenzetu wako katika mazingira magumu ambayo ukienda lazima utalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilwa peke yake ni zaidi ya watu 15,000, Lindi takriban watu 8000 wako nje hawana mahali pa kulala, hawana kitanda, hawana godoro, hawana maji, hawana nguo, hawana chandarua. Sisi Wabunge Mungu ametupenda tumekaa humu ndani, tuko vyumbani tumelala, tumepumzika, tunashiba ndiyo maana kuna wengine wanabeza wakati mwenzangu kaka yangu Mheshimiwa Bungara anazungumza watu walibeza, msibeze, na ukibeza Mungu hataleta furaha katika nafsi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna methali inasema kitu kimoja ukimkuta mtu masikini akikuomba pesa kama hauna pesa nyamaza, lakini kama unayo mpe kwa kuwa yeye naye anahangaika anataka kunusuru maisha ili apate rizki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka hapa kwenda Lindi na Nanjime nimekwenda Nanjilinji nimeshindwa kufika. Ina maana leo hivi kwenda Liwale huwezi watu wako katika kisiwa, kwenda Luwangwa watu wako katika kisiwa, kwenda Kilwa ndani vijijini watu wako katika visiwa, watu wanaokolewa na helkopta. Nimesikitika kuna mtoto anaitwa Derick Masanja huyo mtoto ana miezi 11; maana haya mafuriko hayakutokea wakati wa mvua yametokea wakati jua linawaka; maporomoko yametoka huko yamewakuta watu wakiwa mashambani, wakiwa na mifugo. Leo ninavyozungumza jamaa zangu Wasukuma ambao wametoka Ihefu hawana

ng'ombe, hawana mifugo yao, maisha yao ni magumu, hivyo tusibeze wakati wenzetu wakikuona kwanza wanaanza kulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalimba Bunge langu Tukufu kwa umoja tulio nao na huruma tuliyo nayo watakaokuwa tayari tuanze kuchangia tuwasaidie wenzetu. Huu ndio umoja ninauona mimi utatusaidia angalau kunusuru tuonekana na sisi Bunge tunaonekana tuna umoja na tunafarijika kwa kuwafariji wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaingia katika hoja iliyokuwa mezani, nitazungumzia suala la maralia. Ukiachilia mbali UKIMWI malaria gonjwa ambalo linamaliza watu Tanzania, na bahati nzuri mwaka jana mwezi wa 12 nilihudhuria mkutano wa mabadiliko ya tabianchi *(climate change meeting)* ambao ilifanyika Madrid. Haya tunayoyaona walishayazungumza wenzetu mwezi wa 12. Walisema hivi; Afrika Mashariki kutatokea na maangamizi matatu; la kwanza mafuriko ambayo hayajawahi kutokea katika miaka mingi ndio haya tunayaona sasa hivi; lakini la pili kutokana na mafuriko haya na mvua za holelaholela mazalia ya mbu yatakuwa maradufu. Hivyo tutegemee ugonjwa wa Maralia ambao tulisema tunataka kuutokomeza bado tuna mkakati rasmi wa kuhakikisha maralia yamnatokomezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu tuko naye beneti katika suala la maralia, mimi ni Mwenyekiti wa Maralia; tuko nae kila siku yeye yuko kwenye kipaumbele kuhakikisha Tanzania yenye *zero* maralia inaanza na yeye na mimi nikifuatia na nyinyi vilevile mfuatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kimoja nataka nimuambie ndugu yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Waziri, mikoa mitano mikubwa ambayo ina maralia ambayo ni *high burden* maralia ni Lindi, Mtwara, Geita, Kigoma na Kagera; lakini baadhi ya watendaji wanataka kuvuruga. Wametoa ajira ya kwenda kusaidia hiyo mikoa basi wameandika mikoa 10 ambayo imepewa kipaumbele, nataka nitaje kwa majina, Dodoma ambayo ina *only one percent*, Singida, Geita, Shinyanga, Kigoma, Katavi, Kagera na Mara; lakini Lindi na Mtwara hamna ilhali Lindi ina 24 *percent*. Sasa tujisikieje? Tujisikie sisi tuendelee kufa kwa ajili ya watendaji wachache wanaotuharibia *program* zetu za maendeleo ya kutokomeza maralia wanaiacha Lindi na Mtwara hamna? Kwa bahati nzuri mimi gazeti ninalo na nitakupa ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba kitu kimoja, tu sitaki kubishana, naomba uiingize Lindi na Mtwara iwepo katika kundi la watu ambao ajira ipelekwe kwa watu kwenda kusaidia maralia hasa sasa hivi. Kutokana na mafuriko haya mimi nimekwenda *site* watoto wanatapika wanatisha. Ina maana wamekaa wanaumwa na mbu, hali ya maralia Lindi na Mtwara ni kubwa; na mafuriko yale kwa Lindi ina maana maralia kwao itakuwa ni maangamizo na vifo vitakuwa vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaizungumzia suala la walemavu; Wizara hii ndio Wizara ya Walemavu. Tumepitisha sheria ya haki za walemavu lakini hakuna ajira ya walamavu. Walemavu wanaonekana ni kama kundi ambalo halistahili kupata ajira katika nchi hii. Tuna asilimia tatu ya walemavu tujiulize, Bunge lenyewe limeajiri walemavu kwa asilimia hiyo? Hapa ndani je, asilimia hizo zimetimia ina maana kwanza tujinyooshee sisi wenyewe ndani ya Bunge tunalitekelezaje suala la walemavu na ajira? Tunahitaji alama za *sign language,* hakuna Bunge. Watu wanakaa wanataka kuangalia Bunge linazungumzia nini, hakuna. Ina maana bado Bunge hawajajipanga kuhusu suala la walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge kama Bunge tunaporidhia tuwe namba *one* kuhakikisha haki za walemavu zinaanza ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapo tutasema kweli Bunge tumejisafisha ndipo tutake kusafisha maeneo mengine ya walemavu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele imegonga ya pili.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia tena kuhusu hao walemavu kwanza nishukuru Serikali….

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haaa haijatimia!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, shukrani. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Mboni Mohamed Muhita, Mheshimiwa Said Kubenea ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hizi hoja zetu mbili za Kamati ya Afya pamoja na Huduma za Jamii. Mimi binafsi naendelea kuipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo wameendelea kuboresha katika haya maeneo mawili. Nilishazungumzia maeneo mengine lakini leo kwa sababu tuko kwenye elimu pamoja na afya naomba nijikite upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakumbuka katika mafanikio mengi tuliyoyapata, na naomba nijielekeze zaidi katika Jimbo langu la Musoma. Hata kwenye upande wa elimu peke yake nakumbuka hata kwa mwaka jana tu tumepata shilingi milioni 700 kwa ajili ya Shule ya Msingi Mwisenge, shule aliyosoma Hayati Baba wa Taifa. Shule hii haikuwa kwenye bajeti lakini kwa sababu Mheshimiwa Rais alikuja kule basi akaitembelea na akaweza kutupatia fedha hizo, kwa hiyo pongezi hizo ziweze kumfikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile hata kwenye zile shule zetu kongwe tulipata 1.2 bilioni kwenye shule yetu ya Musoma Teki. Tumeendelea kupata mafanikio mengi katika nyanja mbalimbali kwenye upande wa elimu. Walimu wameongezeka pamoja na kwamba bado kuna upungufu mkubwa wa walimu kutokana na wingi wa wanafunzi; maana ukiangalia kwenye taarifa ya Kamati wamesema wanafunzi tu wameongezeka kwa asilimia 27.7, kwa hiyo inaonesha dhahiri kwamba baada ya kuwa tumepata mfumo wa elimu bure au elimu bila malipo sasa haya haya ndiyo matokeo yake, kwamba wanafunzi wengi zaidi wameendelea kujiunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ungeangalia kwenye elimu ya juu bado kwa mwaka huu peke yake imetolewa mikopo ya thamani zaidi ya bilioni 49. Hii ni kwa sababu ya wale watoto, wale watoto wasiokuwa na uwezo waweze kuwa na uhakika wa kusoma. Kwa hiyo naipongeza sana Serikali kwa kazi hiyo nzuri

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi hata ukizungumzia kwenye idara ya afya yako mambo mengi ambayo yemefanyika. Uilinganisha sasa na kipindi cha nyuma utakubaliana na mimi kwamba hata upungufu wa dawa katika vituo vyetu vya afya pamoja na kwenye zahanati umepungua ukilinganisha na kipindi cha nyuma. Kwa pale Musoma Mjini kwa mwaka jana peke yake tuliweza kupata fedha isiyopungua milioni 400 kwa ajili ya kituo chetu

cha afya cha Makoko naipongeza sana SerikaliPamoja na fedha za bajeti jambo ambalo limetufurahisha sana wananchi wa Musoma na wananchi wa Mkoa wa Mara tumekuwa na hospitali ya Rufaa ambayo tumehangaika nayo kwa zaidi ya miaka 20. Kwa mwaka huu peke yake tumepata bilioni 15 kwa ajili ya ile hospitali na tunategemea wakati wowote ule ile hospitali itaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya si maendeleo ya kubeza, ni maendeleo ambayo ni maendeleo makubwa ambayo tunadhani kwamba kwa kadri tunavyoenda hivi basi kusema kweli tunaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe tu kusema kwamba pamoja na hayo maendeleo ambayo yameendelea kupatikana; lakini liko suala moja ambalo bado ninategemea Kamati iweze kuli-*address*, kwamba kutokana na ongezeko kubwa la watu mimi nilitegemea Kamati ya Huduma za Afya iweze kulizungumzia hili suala la uzazi wa mpango. Maana kama hatuwezi kulizungumza kila leo huduma zitakuwa zinaongezeka lakini baada ya miaka miwili, mitatu zile huduma zinaonekana tena hazitoshi kwa sababu ongezeko letu la watu bado ni kubwa sana. Sasa hilo nalitegemea, kama hatuwezi kulizungumza na tunaendelea kulikalia kimya kwa hiyo tuendelee kutambua kwamba kazi kubwa ambayo itakuwa inafanyika bado tutakuwa tunaonekana tu bado tuko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hayo ningependa kufahamu Kamati ilivyojipanga hasa kwenye mapungufu ya kuondoa tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, tuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi katika shule zetu. Hii hata kwenye vile vyuo vyetu vya ufundi, *VETA;* kati ya matatizo mengine tuliyonayo, mfano tuna Chuo cha *VETA* pale kinachukua wanafunzi 280. Ukiangalia kile ni chuo ambacho mwanafunzi wa Darasa la Saba anaweza kwenda, wa Kidato cha Nne anaweza kwenda, wa Kidato cha Sita anaenda. Sasa kwa sababu wanachukuliwa wachache, matokeo yake ni kwamba tunapeleka wanafunzi wengi mpaka Vyuo Vikuu, lakini wakifika kule matokeo yake ni kwamba wanakosa ajira. Kumbe tungeweza kuboresha na kuongeza zaidi kwenye hivi vyuo vya ufundi kama *VETA* vingeweza kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Serikali ilianza na utaratibu wa kupeleka wanafunzi JKT na wengine wamekaa huko miaka mpaka mitatu. Nadhani ilikuwa ni nafasi nzuri ya kutumia mafunzo ya JKT katika kuwafundisha vijana wetu stadi mbalimbali. Mambo ya kilimo wangeweza kujifunza kule, mambo ya ufundi wangeweza kujifunza kule. Kwa sababu JKT ni mahali pekee ambapo mwanafunzi anaweza kuishi kwa gharama nafuu, lakini akajifunza mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwamba baada ya kuwa wamejifunza kule, badala ya kuwaacha tu kwamba sasa hebu rudini majumbani, nilitegemea kabisa kwamba ni mahali ambapo wangeweza kujifunza stadi mbalimbali, mafunzo mbalimbali na baada ya hapo, wale vijana wakapewa mitaji wakaingia wakaja huku kwenye ujasiriamali wakaweza kujiajiri katika ajira mbalimbali. Kile kitendo cha kuwaweka pale halafu baada ya muda tukawaondoa, kusema kweli sioni kama inawasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea na Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi ajiandae.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Wizara hizi nyeti. Naomba nitumie fursa hii kwanza nikiwa Mbunge mwanamke, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ya kipekee na jinsi ambavyo amejitoa kuweza kuimarisha na kudumisha sekta ya afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Ummy na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa namna ya kipekee kwa jinsi ambavyo wanatumikia Wizara hii kwa weledi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amechukua *initiatives* za kipekee kabisa katika kuhakikisha kwamba, anamaliza changamoto kwenye Sekta ya Afya. Ushahidi wa kwanza ambao wengi ulituonyesha dhahiri kwamba Mheshimiwa ameamua kujitoa ili kuweza kumaliza changamoto hizi, ni pale alipoelekeza gawio la fedha zinazopatikana kutoka kwenye Kampuni ya Simu ya *Airtel* kuja na kujenga hospitali katika Makao Makuu ya Nchi hapa Dodoma. Ni Rais wa kizalendo sana anayeweza kufanya maamuzi hayo ya kishujaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumeshuhudia katika kipindi hiki cha miaka minne ya utekelezaji Vituo vya Afya 352 vimejengwa Tanzania. Nasi wananchi wa Handeni Vijijini tulibahatika kupata shilingi milioni 800 ambazo tukazigawa kwenye Kituo cha Afya cha Kabuku pamoja na Kituo cha Afya cha Mkata. Hakuishia hapo, tumeshuhudia Hospitali za Wilaya 67 zikijengwa katika kipindi cha miaka minne tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kwa haraka haraka mtu anaweza akaona ni chache, lakini tujikumbushe huko nyuma; toka tumepata uhuru tulikuwa na Hospitali za Wilaya 77 tu. Sasa sisi wenyewe tufanye hesabu hiyo, yaani toka tumepata uhuru tuna hospitali 77 dhidi ya miaka minne tu ambayo zimeongezeka hospitali za ziada 67. Kwa hesabu za haraka haraka hapo mtu unaweza ukajiongeza na ukaona. Hospitali 77 kwa miaka yote tangu uhuru *versus* miaka minne na upatikanaji wa Hospitali za Wilaya 67. Hiyo ni takriban amepiga jiwe kwa asilimia 70 ndani ya miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naendelea hapo. Katika kipindi hiki cha miaka minne tumeshuhudia ujenzi wa hospitali tano za mikoa; Njombe, Songwe, Katavi, Simiyu, Geita na Hospitali ya Kikanda Mtwara. Nadhani habari hii itamfurahisha sana mama yetu Mheshimiwa Riziki Lulida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kugusia kidogo kwenye mpango wa kidunia wa 90, 90, 90, ambapo mpango huu unasema asilimia 90 ya wale ambao ni *suspects* wa maambukizi ya UKIMWI wafikike na wapimwe. Asilimia 90 ya wale waliopimwa waweze kuanza kupata huduma ya dawa, lakini 90 ya mwisho ni wale ambao wameanza dawa, zile dawa ziweze ku-*suppress* yale maambukizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Wizara ya Afya. Dada yangu Mheshimiwa Ummy na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Faustine, Tanzania tuko mbali. Katika 90 ya mwanzo tuko kwenye *85%* tunakwenda juu; 90 ya pili tuko kwenye asilimia 90; na tisini ya tatu tuko kwenye asilimia 90. Pongezi nyingi sana kwa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sehemu ambako kunakosekana changamoto. Changamoto ambayo tunaipata na ninaamini kwamba Wizara iko katika hatua za mwisho kabisa kutatua changamoto hii ni changamoto ya watumishi. Naomba nigusie Jimbo la Handeni Vijijini. Handeni Vijijini tuna changamoto kubwa ya watumishi kwenye Sekta ya Afya.

Katika hitaji la watumishi asilimia 100, sisi tuna *access* ya watumishi asilimia 25 tu. Kwa lugha nyingine ni kwamba, tuna uhaba wa asilimia 75, yaani katika hitaji la watumishi 896 sisi tuna watumishi 226.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kushauri Wizara, naelewa wazi kwamba Wizara iko kwenye hatua za mwisho kabisa kuweza kutatua changamoto hii ya kuajiri. Ushauri wangu na wito wangu, namwomba sana dada yangu na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Faustine basi mpango huu waweze kuufanya kwa uharaka, ili kuweza kumaliza changamoto hii ya uhaba wa watumishi kwenye Sekta ya Afya katika maeneo mbalimbali, hususan Jimbo la Handeni Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saed Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie jioni ya leo. Kwanza nianze mchango wangu kwa kunukuu maneno ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tisa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, liyoyatoa kwenye Bunge hili tarehe 7 Februari, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lowassa alisema, "Bunge hili ndio chombo kikuu cha kusimamia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba hapa ndipo mahali pekee ambapo tunapaswa kuonesha umahiri wetu na utayari wetu wa kudumisha kwa vitendo demokrasia ya hali ya juu katika Taifa letu." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mijadala yetu ndani ya Bunge na ukiangalia kazi yetu sisi kama Wabunge unapata shida kwamba Mbunge anasimama ndani ya Bunge anapongeza kwa asilimia mia moja halafu analaumu kwa asilimia mia moja. Anasema tokea mwaka 1967 nchi hii ilikuwa haijawahi kujenga hospitali, lakini imejenga baada ya mwaka 1977. Sasa unauliza hicho chama kilichokuwa kinaongoza hiyo Serikali ni kipi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapata shida ukiangalia, mtu anajaribu kuweka ushabiki wa vyama badala ya kuweka maslahi ya nchi mbele. Kwa hiyo, ni rai yangu tu kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge tujikite zaidi kuangalia Taifa letu na maslahi yake badala ya kuangalia ushabiki wa vyama vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 ya Katiba yetu ambayo ni mchango wangu katika Kamati ya Huduma za Jamii, inaeleza wazi kwamba kila mtu anayo haki ya kupata habari na kutoa habari na ni wajibu wa Kikatiba wa kila raia. Sasa Kamati imeleta mapendekezo juu ya uboreshaji wa Kituo cha *Television* ya Taifa cha *TBC*. Walisema *TBC* iboreshwe ili iweze kutoa matangazo yake vizuri na iweze kusikika vizuri. Ni jambo zuri sana na tunaliunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* ya sasa hivi siyo chombo cha Umma tena. Kimejaa ushabiki na hakiendeshi mambo yake kwa weledi ambapo upande wa pili wa watu wengine ambao wako ndani ya Bunge hili au wanaunda vyama ambavyo viko ndani ya Bunge hili au kwenye Taifa hili, hawapewi nafasi ya kutosha ya kutoa maoni yao. Sheria zilizopo, Kamati inapendekeza *TCRA* wasimamie leseni za *TV* za *online* na *television* za kawaida. Ni jambo ambalo binafsi silipingi. Ila kuna shida kidogo. Ukienda upande wa magazeti; na katika hili naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mwandishi wa Habari na mmiliki wa chombo cha habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, magazeti katika nchi hii sasa hivi yanapewa leseni ya kuendesha kwa kila mwaka, jambo ambalo limeondoa uwezekano wa wawekezaji wakubwa wenye fedha kuja kuwekeza kwenye nchi, kwa sababu mtu hana uhakika kwamba baada ya leseni yake kumalizika atapata muda wa kupewa leseni nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yalikuwepo magazeti, yaliyumba kwenye uchumi, lakini wawekezaji wa ndani na nje walikuja kuyachukua wakayanunua, wakayaendesha na sasa yametoa ajira kubwa, yameleta mitambo ya kuchapisha magazeti, yameajiri watu wengi sana Watanzania wako hapa, wamepata kazi. Kwa hiyo, nitoe ushauri kwa Kamati na Serikali kwamba, ile sheria ambayo inatumika angalau kwenye *television* wanapewa leseni ya miaka mitano. Angalau basi kwenye magazeti wangeweka kipindi cha miaka mitano mpaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ardhi kuna miaka 33 mpaka miaka 99. Sasa tuangalie kwenye madini sheria zimebadilishwa, mambo haya yamebadilika; ili sasa tuweze kufungua uwanja mpana sana wa watu kupata habari kwa uwazi, kupata habari sahihi na kwa wakati sahihi, ili haki ya kila raia isivurugwe kwa sababu ya sheria tunazotunga hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haki hii ya Kikatiba ni haki ambayo mtu haiombi ni yake amepewa kwa mujibu wa Katiba yetu. Ni muhimu sana haki hiyo ambayo tumepewa kwa msingi wa Katiba yetu ikalindwa na kudumishwa. Tunapata shida leo, tunalaumiwa dunia nzima kwamba Taifa letu haliheshimu uhuru wa watu kujieleza, haliheshimu uhuru wa watu kutoa maoni, haliheshimu uhuru wa watu kutoa habari. Sasa baadaye sisi tunakimbizwa na tuko porini…

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, kuna taarifa.

Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**T A A R I F A**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuokoa muda sitaisoma kanuni husika, lakini nataka nimpe Taarifa mzungumzaji kwamba suala la uhuru wa kujieleza ni suala ambalo liko wazi; na kwa sababu, Serikali ya Awamu ya Tano inasimamia jambo hilo, ndiyo maana rafiki yangu Mheshimiwa Kubenea pamoja na wenzake wakiwemo akina Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Komu na wengine ambao sitawataja kwa majina, wameukosa uhuru huo wa kujieleza ndani ya chama chao kufikia hatua ya kusema; na wameambiwa sumu haionjwi kwa kulamba na ulimi. Sasa ni haki ipi ya kujieleza anayoitaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu nimpe taarifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni majungu tu. Kwa hiyo, taarifa kama hiyo nimemwachia yeye mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haki hizi ambazo tumezizungumza ni haki za kisheria, kama zipo basi zinawezekana zipo kwa pande zote katika nchi. Hata kwenye chama ambacho naye anatoka hizo haki inawezekana zikawa zinavurugwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo la muhimu ni kwamba tumekubaliana kwa mujibu wa sheria zetu na Katiba yetu. Mnalaumiwa sana na yeye anajua kwamba leo ukienda kwenye mitandao ya kijamii, ukienda kwenye ripoti mbalimbali za *Amnesty International, World Bank, IMF,* wanatulaumu na tunanyimwa misaada kwa sababu ya kuzuia hizi haki. Sasa hili jambo siyo geni, linafahamika na kila mmoja. Rai yangu, kwa nini tunakaa kwenye pori tunakimbizwa na simba, badala ya kurukia faru anaweza kukuokoa unaenda kurukia swala, anakuua? Simba anachukua wewe na swala pamoja. Tusifike huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari Tanzania vinapita katika wakati mgumu sana. Vyombo vya habari havipati matangazo kutoka Serikalini, vinabaguliwa hasa vile vya binafsi, kuna urasimu mkubwa wa kutoa habari hata ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi kwamba baadhi ya mijadala inayofanyika humu ndani haichukuliwi na vyombo vya habari. Kwa hiyo, sisi badala ya kwenda mbele sana, miaka 100 mbele, tunarudi nyuma miaka 50 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakushukuru sana. Ahsante sana, Mungu akubariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Edward Francis Mwalongo ajiandae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye juu Mbinguni kwa kunipa nafasi ya kusimama na kuweza kuchangia hoja hii muhimu ya Sekta ya Huduma za Jamii na Masuala ya UKIMWI ambayo mimi Amina Nassoro Makilagi ni Mjumbe wa Kamati zote hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya shukrani, naomba nianze kwa kuleta salamu za wanawake na wananchi wa Tanzania walionipigia kura za kishindo wakanileta hapa Bungeni. Wamenituma nije niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, wanamshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi kwa kuboresha huduma za afya, kwa kutenga fedha za kutosha za kuhakikisha tunapata dawa, vifaa tiba na vilevile tunaboresha miundombinu. Wenzangu wameshasema, sitataka kurudia; na kama alivyosema Mbunge wa Mkoa wa Mara, Mheshimiwa Vedastus Mathayo, kwa miaka hii ya hivi karibuni tunashuhudia Hospitali za Rufaa zaidi ya 10 zinajengwa katika nchi hii. Mkoa wa Mara peke yake tumepata zaidi ya shilingi bilioni 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nianzie hapo kuleta salamu za wananchi wa Simiyu, wanashukuru sana kwa Hospitali ya Rufaa na pia ninaleta salamu za wananchi wa Geita, wanashukuru sana na ninaleta salamu za wananchi wa Katavi, wanashukuru sana, wananchi wa Songwe na wananchi wa Geita na Mkoa wa Mara wanashukuru sana na hata Mkoa wa Mtwara. Wanaomba Serikali iendelee kuleta fedha za kutosha ili Hospitali za Rufaa ziweze kukamilika, hasa kwa kuzingatia kwamba Kanda ya Ziwa mfano Hospitali ya Rufaa ya Bugando imezidiwa, Hospitali ya *Mwalimu Nyerere Memorial Centre* itasaidia kukabiliana na ile changamoto ya watu *(population)* ya zaidi 15,000 ambao wanahudumiwa katika Hospitali ya Bugando.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ule Ukanda wa Mtwara hapakuwa na Hospitali ya Rufaa, kwa hiyo, wamekuwa wakipata adha ya kuja Muhimbili. Nina imani sasa changamoto inaenda kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali na wanawake wa Tanzania wamenituma nije kuleta ahsante kwa kujenga hospitali 67. Wanawake wanasema ahsante sana, Mungu amjalie Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aendelee kutenga fedha kwa zile Halmashauri ambazo hazijafikia mpango huu kwa mwaka wa fedha ujao 2020/2021, nao waweze kupata fedha na hospitali zijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala zima la kupunguza vifo vya wanawake na watoto; wanawake wamenituma, wanasema wanaishukuru sana Serikali ya CCM kwa kujenga vituo zaidi ya 350 jambo ambalo limepunguza kasi ya vifo vya wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayezungumza, nimetembea ziara kabla ya kuja hapa, kwenye Mkoa wa Mara nimetembelea vituo vyote na mikoa ya jirani nimekwenda, kwa kweli hali ni nzuri, tunashukuru sana na wanawake wamenituma nije niseme ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ushauri ninaoutoa kwa Mheshimiwa Spika, tumefanya kazi nzuri ya kujenga vituo, tumefanya vizuri kuboresha huduma, lakini naungana na wachangiaji wenzangu kwamba Serikali itafute fedha kwa ajili ya kuajiri wataalam. Maana tusipoangalia, tumejenga vituo, lakini havifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niwashauri pia kwamba ni vizuri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na TAMISEMI, wafanye hizo tathmini kuona tangu tumejenga hivi Vituo vya Afya ni vingapi vinafanya kazi? Kwa sababu, mfano nimetembelea Kituo cha Kinesi, Kituo kimeshajengwa, kimekamilika lakini pale hakuna Mtaalam wa Usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea Kituo cha Nata Isenye Serengeti Kituo kiko vizuri na huduma zimetolewa lakini yupo daktari mmoja; nimekwenda kule Butiama hakuna mtaalamu wa mionzi lakini pia hakuna *x-ray*. Kwa kweli tunaweza tukajenga baadaye tukabaki na Majengo nilikuwa naomba sasa Mheshimiwa Waziri na timu yake hebu sasa tujielekeze kwenye wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa ushauri ninaoutoa kama alivyosema Mheshimiwa Tendega ambaye ni mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii tumekuwa tukitoa ushauri chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Peter Serukamba; kwamba sasa ifike wakati Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iwatambue wataalamu wa sekta ya afya iongee nao, izungumze nao iwaombe wajitolee. Sisi wenzenu tulianza kujitolea; hata mimi hapa nilipo sikufika hapa leo nikawa Mbunge, sikufika hapa nikawa Katibu Mkuu, nilianza kujitolea. Mimi nilijitolea miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wataalamu ambao wako tayari wanasubiri ajira, wapo wataalamu ambao wanasubiri kupewa ajira Serikalini ni vizuri tukazungumza nao halafu kupitia vyanzo vya ndani wakalipwa fedha kidogo kwa ajili ya kujikimu ili waweze kutoa mchango wao katika taifa. Vilevile kuna watu waliostaafu kazi, wako huko wamestaafu na bado wana nguvu kabisa; miaka 60, miaka 55, ni wataalamu wetu wanaweza wakashirikishwa ili waweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshauri tena katika mwaka wa fedha ujao 2020/2021 tuje na bajeti nzuri itakayotoa fursa kwa Serikali kuweza kuajiri Wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu naleta shukrani nyingi sana kwa wananchi na wanawake wa Tanzania kwa kazi nzuri sana inayoendelea ya kuhakikisha vijana wetu waliopata fursa ya kupata elimu ya juu wanapata mikopo. Ni ukweli usiopingika kwanza kwa kipindi hiki kifupi zaidi ya shilingi bilioni mia nne zimeweza kutoka kwaajili ya vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kwenye sekta hii ya kutoa mikopo kwa elimu ya juu hebu tufanye uwiano ulio sawa kwa upande wa vijana wa kike ili na nao waende sambasamba kwa sababu takwimu zinaonesha kwamba watoto wa kike wamebaki nyuma kidogo. Vilevile nataka nitoe tena ushauri kwenye kupeleka watoto wa elimu ya juu katika vyuo vikuu; hata ukiangalia takwimu pia uwiano hauendi kati ya wanawake na wanaume bado wanawake wako chini. Nilikuwa nashauri hebu tupandishe hii na wanawake wapate hii fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niache salamu za wananchi; wanashukuru sana jinsi ambavyo Serikali imeendelea kutoka mikopo. Ni hivi karibuni tu kupitia takwimu tulizozipata kupitia huduma za jamii ni zaidi ya shilingi milioni mia nne na themanini zimetolewa kwa ajili ya mikopo. Tumetoka mbali kazi ni nzuri tunaomba fedha ziendelee kutengwa ili akina mama vijana wetu waendelee kupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu ya dekondari tumefanya kazi nzuri, vijana wetu sasa wanakwenda wengi, na hata kwenye shule za awali wanakwenda, wenzangu wamezungumza, nisirudie. Hata hivyo hapa ushauri wangu, tujitahidi sasa kwenye walimu wa sayansi. Kusema ukweli kuna changamoto ya sayansi katika elimu ya sekondari na msingi. Kama nilivyoshauri kwenye sekta ya afya, tutafute fedha ili tuwapate na walimu wa sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la. Kadri tunavyoongeza watoto; majengo ni yale yale; na bahati nzuri wananchi wanafanya kazi nzuri ya kujenga maboma. Nitatolea Mkoa wa Mara ninakotoka; sisi Mkoa wa Mara hatusubiri Serikali ijenge kuanzia msingi, sisi tunajenga mpaka renta. Wananchi wanahitaji haya maboma sasa yatengewe fedha kwa ajili ya kukamilika. Tunashukuru sana Serikali kwa kutuletea fedha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu awabariki, naunga Mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa ajiandae. Wakati huo huo wajumbe wa Kamati ya Uongozi itakapofika saa 12:30 kutakuwa na kikao *speaker's lounge* hapa nyuma; saa 12:30 Wajumbe wa Kamati ya Uongozi. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kuniwezesha kusimama hapa. Awali ya yote ninaunga mkono Kamati zote mbili Kamati ya Masuala ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu nitaanza moja kwa moja na Kamati Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kuzungumzia kutoa ushauri kwa Shirika la Utangazaji Tanzania *TBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni-*decrare interest* kwamba mimi ni Mwanahabari na kabla ya hapo pia nilikuwa *TBC*. Kwa hiyo ninapozungumzia *TBC* naizungumzia *TBC* kwa upendo kwa kutambua changamoto zilizopo katika Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitakuwa mchoyo wa fadhili endapo sitaipongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa wanayoifanya; Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza lote la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwakyembe ninakupongeza sana hasa baada ya kuona jitihada kubwa unazozifanya katika kukagua mitambo ya *TBC* na kuweza kuiboresha pale ambapo ina changamoto. Kwa kiasi kikubwa sana Mheshimiwa Waziri hii itasaidia katika kutatua changamoto hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote ile inajivunia Chombo chake cha Habari na *TBC* ndilo Shirika la Umma. Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumzia uhuru wa kupata habari, lakini vilevile inaendelea mpaka kuzungumzia katika uhuru wa kutoa mawazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo hakuna uhuru usiokuwa na mipaka; hivyo nipongeze sana Serikali pale ambapo inasimamia kikamilifu kuhakikisha kwamba Vyombo vya habari vinafuata maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* ni Shirika kongwe, na tunafahamu Shirika hili la Utangazaji Tanzania *(TBC)* liliendelea kutumia majengo ambayo yalikuwa ni majengo ya filamu kwa miaka hiyo; na kwa muda mrefu kwa kweli limekuwa likihitaji marekebisho na mabadiliko makubwa hasa katika mitambo pamoja na mazingira yenyewe kwa ujumla, lakini hasa mitambo. *TBC* bado inahitaji uboreshwaji mkubwa wa mitambo ili basi kiweze kuwafikia wananchi kwa ukaribu zaidi pasipo kuwa na hizo changamoto, na hata kama zitakuwepo basi changamoto ziwe ni chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi najivunia Shirika hili la Utangazaji Tanzania na pamoja Mkurugenzi wa *TBC*, Bwana Ayoub Ryoba kwa jitihada kubwa wanazozifanya. Wafanyakazi hawa wa *TBC* ni Wafanyakazi ambao kwa kweli wanahitaji pongezi hasa kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi maeneo yote katika ziara zote za Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Jemedari Dkt. John Joseph Pombe Magufuli *TBC* tumekuwa tukiwaona wakituhabarisha kile kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kweli nimpongeze aliyekuwa Msemaji wa Serikali Dkt. Hassan Abass kwa kazi kubwa aliyokuwa anaifanya katika kuwahabarisha wananchi nini ambacho Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Serikali, inayoongozwa na Dkt. John Joseph Pombe Magufuli inachokifanya na tumeshuhudia kwa kweli hata wananchi sasa hivi wanamwelewa vizuri sana Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kutokana na kazi kubwa ya Dkt. Abass.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii basi wanasema pengine ndiyo ambayo imempendezesha Rais na kumpa nafasi hiyo. Mimi ninampongeza akaendeleze jitihada hizo hizo katika kuhakikisha kwamba anasimamia misingi ya taaluma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali, na nimpongeze Spika wetu kwa sababu hivi sasa katika Bunge letu kipindi cha maswali na majibu watu wanafatilia, hata wenzangu viziwi wanafatilia kwa sababu wapo Wakalimali wanaotafsiri lugha ya alama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hao tu, tumeanza vizuri katika taarifa zetu za habari televisheni mbalimbali nazo pia wanafanya kazi hiyo kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma. Mheshimiwa Waziri na Naibu wako nakupongeza sana kwa hili jambo unalolifanya katika kuhakikisha kwamba tunazingatia na mikataba yote ambayo nchi yetu imeiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* hivi sasa wana *channel* ambayo inatangaza utalii ninaiomba Serikali kuhakikisha kwamba inawawezesha TBC kwa kiasi kikubwa na hata ikibidi kuongeza bajeti ili basi wao ndio wawe wa kwanza katika kutangaza utalii wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia ni mjumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, TB bado ni tatizo kubwa hapa nchini; kwa mwaka watu zaidi ya 75,000 wanakufa kutokana na ugonjwa huu wa kifuu kikuu. Niiombe Serikali kuhakikisha kwamba jitihada zinaongezwa ili kuweza kunusuru wananchi wa Tanzania wengi wasiangamie na ugonjwa huu wa *TB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia elimu iendelee kutolewa na tulishirikishe Shirika letu la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kutoa elimu juu ya madhara gani au nini basi hasa chanzo cha ugonjwa huu ili wananchi waweze kufahamu na vilevile kuchukua tahadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulipitisha sheria kuhusiana na upimaji kwa watoto chini ya miaka kumi na nane mpaka kumi tano; ninaiomba Wizara iharakishe kanuni na pia kutoa elimu ili wazazi watambue umuhimu wa kuwapima watoto wao hasa chini ya miaka kumi na nane mpaka kumi na tano ili basi malengo ya 90 90 90 yaweze kukamilika na kufanyiwa kazi kwa jitihada kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumekuwa tukitegemea sana vyanzo au wafadhili kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI; sasa ni wakati wa Serikali; naishauri Serikali kuhakikisha kwamba tunapata vyanzo vya uhakika vya kuweza kutunisha mfuko wa UKIMWI ili basi tuweze kujitegemea angalau kupunguza misaada mikubwa ambayo kwa wakati mwingine kwa kweli tunapata misaada hiyo kutokana na masharti magumu. Kwa hali ilivyo kwa sasa hivi kwa kweli tuharakishe mfuko huu na kwa kupata vyanzo katika bajeti ya mwaka huu ili basi tuweze kupunguza misaada kutoka kwa wafadhili wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda umekwisha ninakushukuru sana kwa kweli, naipongeza Serikali tena Mheshimiwa Harisson Mwakyembe na Naibu wako hongereni sana. Vilevile Mheshimiwa Ummy Mwalimu Mungu akubariki sana, *A luta continua* mapambano yanaendelea, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga ajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hizi mbili zilizopo mezani kwa siku ya leo. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa fursa ya kuendelea kuwa uhai, lakini pia niwapongeze sana wenyeviti wote wawili Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii lakini pia Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI Dkt. Tiisekwa;

nawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyofanya. Kwanza wanatusimamia vizuri kwenye Kamati zetu lakini leo wamewasilisha vizuri sana Taarifa za Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze na jambo moja, nianze na suala la elimu. Kwenye elimu tunahangaika sana juu ya suala la walimu, hali ya walimu ni mbaya sana, na sielewi kabisa kwamba sasa Serikali inajipangaje kwa sababu shule zetu hazina walimu, ni tatizo la Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia ni mjumbe wa Kamati ya *LAAC* ukiangalia Taarifa za Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali unaona kabisa kwamba anaonesha mapungufu kwamba katika kila Halmashauri kuna upungufu mkubwa sana wa walimu na tatizo likishakuwa kubwa sana halafu ukawa huwezi kulitatua inafika mahali unaliona hili huliwezi unaamua kuliacha tu liendelee kama lilivyo na unalizoea unaona kama ni hali ya kawaida. Ni hali mbaya sana. Kwa mfano tu kwenye Halmashauri yangu ya Mji Njombe ina upungufu wa walimu mia nne. Niombe sana Serikali iangalie ni kwa namna gani itafanya iajiri walimu wa kutosha ili kusudi shule zetu pamoja na kwamba wananchi wanachangia ujenzi wa shule, Serikali inachangia nguvu za wananchi pia lakini kama hakuna walimu katika shule za msingi kama hakuna walimu wa sayansi itakuwa ni tatizo kubwa sana kwa maana watoto hawa hawatapa elimu iliyokusudiwa *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine tunahitaji vijana wetu wapate ujuzi; hawa vijana hawawezi kupata ujuzi kwa namna yoyote ile kwa sababu leo hii katika nchi yetu hakuna chuo kinachotoa walimu wa ufundi; hatuna chuo hata kimoja kinachotoa walimu wa ufundi. Watu wengi tunapenda vijana wapate elimu ya ufundi lakini ni ukweli usifichika kwamba hakuna chuo hata kimoja. Kuna chuo kidogo sana cha *VETA* pale Morogoro na hakina uwezo hata kidogo wa kutoa walimu wa ufundi; lakini vilevile mitaala ya ufundi inayofundishwa ni mitaala ya zamani sana. Mimi ni fundi, kwa hiyo ninajua nini kinafundishwa huko. Kwa kweli ufundi ulipofikia leo na ufundi wanaofundishwa vijana ni vitu viwili tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niishauri Serikali ijitahidi sana kuhakikisha kwamba sasa inajenga vyuo na inafundisha walimu wa ufundi wa kutosha ili kusudi tutakapotaka kuwa na mafundi walimu wa kuwafundisha wawepo. Tutakaa tunasema tunahitaji ufundi *VETA* zianzishwe lakini walimu wako wapi? Walimu hakuna. Nchi hii hakuna vitabu vya ufundi vinavyoandikwa, havipo. Sisi tunataka mafundi lakini nchi hii vilevile hakuna mitaala ya ufundi ya kisasa, yaani hakuna; mitaala iliyopo ni ya kizamani sana. Kwa hiyo niombe sana Serikali iangalie kadri inavyowezekana na hasa hasa Wizara ya Elimu ijikite kuliona hilo; ni jambo gumu zito lakini ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake Mama Jenista, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa. Katika Wizara yao wameweka utaratibu wa kutoa ujuzi; ni utaratibu mzuri na vijana wengi wanapelekwa maeneo mbalimbali ili kupata ujuzi. Wengi hatuyajui hayo lakini kwa kweli ukiuona ule mpango umeinua vijana wengi na umewawezesha vijana wengi kupata ujuzi. Ni mpango mzuri unaosaidia sana katika kuhakikisha kwamba sasa Vijana wengi wanapata fursa kupata ujuzi. Niwaombe muendelee na kazi hiyo muimarishe zaidi lakini mpanue, msiende tu kwenye fani zile zile za useremala, ujenzi, ushonaji. Haiwezekani nchi nzima ikawa ya mafundi seremala na washonaji, tuweke na fani nyingine, twende kwenye fani za kilimo, uvuvi na mifugo ili sasa vijana hawa watawanyike sehemu pana zaidi ili wakatumie ujuzi huu na hivyo uweze kuwasaidia kuweza kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la elimu liko jambo moja baya sana. Serikali imetoa mitaala mipya, Serikali ina ruzuku ambazo zinatakiwa ziende shuleni; haipeleki zile ruzuku

badala yake inapeleka ku-*print* vitabu Taasisi ya Elimu iki-print vile vitabu inaviandika kitabu hiki hakiuzwi na vile vitabu vinapelekwa moja kwa moja shuleni na kwa hiyo shule zisizo za Serikali zote hazipati vitabu. Sasa unajiuliza, hivi hawa wanaosoma shule zisizo za Serikali ni watoto wa nani? Hawa si Watanzania? Hakuna fursa hata chembe ya shule isiyo ya umma kupata kitabu kilichoko kwenye mtaala wa kisasa. Kwa hiyo niombe sana hilo Serikali ilione na ilitatue hilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tulipitisha hapa Sheria ya fedha, kwamba tozo kwenye shule zisizo za umma inayofanana ya *fire* isiwepo; lakini mpaka leo *fire* bado wanatoza; hivi mimi najiuliza sheria na waraka ni nini kikubwa? Maana wao wanadai hawajapelekewa waraka. Niwaombe wahusika, watu wa Wizara ya Elimu, wati wa Wizara ya Mambo ya Ndani waambieni hawa Askari wa Zimamoto sheria inasema usitoze *fire* kwenye Shule zisizo za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie suala la UKIMWI. Tunalo tatizo kubwa la UKIMWI katika nchi yetu lakini tatizo tunavyoliendelea ni kama vile si letu. Hatuna mfuko imara kama nchi kwa ajili ya kukabiliana na UKIMWI tunategemea fedha za wafadhili; na fedha hizi za wafadhili zina masharti mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, MheshimiwaWaziri wa Fedha yupo, niombe sana sasa hivi ndiyo tunaandaa bajeti kwa ajili ya mwaka ujao tuhakikishe tunaweka kifungu cha Mfuko kwa ajili ya UKIMWI ili kusudi kama nchi tuweze kuwa na fedha yetu kwa ajili ya matatizo ya suala la UKIMWI; vinginevyo hawa wafadhili wakiondoka, na wanavyotuyumbisha itafika mahala tutashindwa kabisa kuhudumia wagonjwa wa UKIMWI. Hawa wafadhili muda wanaokatiza shughuli, kwa mfano kuna taasisi moja ilikuwa inafanya huduma ya UKIMWI katika Mkoa wa Njombe *JHPIEGO* mkataba umekwisha.

Sasa katika kipindi kile ambacho mkataba umeisha na wenyewe hawana fedha za kuendelea kuhudumia, wale wanufaika wa ile huduma sasa hawapati; na kwa sababu hakuna fedha ya Serikali ya kufidia pale kwa hiyo wale watu wanakuwa hawapati huduma inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Serikali, kwa kuwa sasa tunakwenda kwenye kikao kijacho ambacho kitakuwa ni cha bajeti; na sasa hivi ndiyo maandalizi yanafanyika tuanzishe Mfuko wa Nchi kwa ajili ya huduma ya UKIMWI kwa wananchi. Vilevile niombe sana wananchi wote wajitahidi kupima na Serikali ihamasishe upimaji. Watu wengi wanaogopa kupima ni uoga tu lakini tuhamasishane tupime ili kusudi tuweze kupata tiba ya UKIMWI kwa maana ya kupata tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo na Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala huu unaoendelea wa Kamati za Huduma ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya Ukimwi. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inaendelea kuifanya. Tumeona Vituo vya Afya vingi vikijengwa, tumeona Hospitali zikijengwa na tumeona Zahanati zikijengwa. Kwa kweli mambo yanaenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite kwenye eneo la kinga. Tuna tiba na kinga. Ukiangalia Wizara ya Afya imejikita sana kwenye eneo la kitabibu, lakini ni Wizara hii ambayo inashughulika pia na kinga. Kwa hiyo, napenda sasa kuishauri Serikali, ifike mahala tuweke *concentration*

kubwa kwenye maeneo ya kinga ambayo yatazuia gharama kubwa kutumika katika maeneo ambayo ni ya tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mifano ya nchi kama Rwanda ambako tumeenda. Wapo Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao kazi yao kubwa ni kuelimisha watu wale vyakula vya namna gani kwa maana ya lishe na kutoa elimu mbalimbali za kinga dhidi ya mimba, dhidi ya ujauzito na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, naamini kwamba tukijikita kwa kiasi kikubwa kwenye kinga, tutaokoa gharama kubwa zinazotumika maeneo ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile; wametengeneza *concentration* kubwa kwenye hivyo vitu. Sasa naomba nguvu ile ile ambayo imetumika sana kwenye afya, tumeona Serikali ikiwa imeokoa hela nyingi sana za kupeleka wagonjwa nje ya nchi, kutoka 600 mpaka watu 50 kwenda nje, siyo jambo dogo. Hilo ni jambo kubwa sana nami nasema kwamba endeleeni kukomaa kwenye hilo ili mwisho wa siku ikiwezekana tupeleke watu sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza, kazi mnayoifanya ni kubwa na Watanzania wanaiona. Pia tuwaimarishe watumishi wa ya Maendeleo ya Jamii ili waweze kutoa huduma kule vijijini ya namna ya Lishe na namna ya kujikinga na magonjwa mbalimbali ili tuweze kuokoa gharama kubwa inayotumika kwenye afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala ya maboma ya Vituo vya Afya, Zahanati na Shule. Maeneo mengi ya Majimbo ambako tunatoka, wananchi wametumia nguvu zao nyingi na kubwa katika kuhakikisha kwamba wanaisaidia Serikali yao kujenga Zahanati na Vituo vya Afya. Sasa umeshafika wakati wa Serikali angalau kuwasaidia hawa wananchi kwa ajili ya kuezeka na baadaye kukamilisha. Wananchi wetu wakielimishwa wala hawana shida yoyote. Ludewa ninakotoka kuna zaidi ya maboma ya Vituo vya Afya 14 na mengine yameshaezekwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, kinachoitajika tu pale ni kuwa-*support* ili kuweza kumalizia na baada ya hapo, utekelezaji wa Ilani wa Chama cha Mapinduzi kwamba Kila Kijiji kiwe na Zahanati na Kila Kata iwe na Kituo cha Afya, tutakuwa tumetekeleza kwa kiasi kikubwa sana, zaidi ya asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunajenga shule nyingi, kwa sababu tumeshasema kwenye kila kijiji tunatakiwa shule. Kwa hiyo, nadhani kuwekwe mpango madhubuti wa timu maalum ya kwenda kupitia maeneo hayo, yaje na taarifa ili tuweze kupata takwimu sahihi za kuweza kusaidia hiyo kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kwamba Mheshimiwa Waziri na Watendaji huko Serikalini wana uwezo wa kuifanya hiyo kazi na mwisho wa siku tukaitekeleza ilani kwa asilimia 100, hiyo inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uhaba na watumishi kwenye maeneo ya afya. Uhaba huu umekuwa ni mkubwa sana. Kama wenzangu walivyokuwa wamezungumza huko mwanzo, ile hali ya uzalendo ni kama imepungua. Sasa tujiulieze, imepungua kwa kiasi gani, hasa wale watu kwenda kujitolea? Wasomi wetu wanaomaliza sasa hivi wengi wapo mitaani, lakini bado tunalalamika tuna uhaba wa walimu na watumishi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ifanyike *program* maalum ya kuhakikisha kwamba watu wanajitolea na wale wanaojitolea ndiyo wawe wa kwanza kuajiriwa. Kwa sababu wapo watu ambao wanajitolea, nafasi za kazi zinatangazwa, lakini wale wanaojitolea wanaachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani tungetengeneza utaratibu mzuri kwamba wale wanaojitolea, basi ndiyo wawe wa kwanza kuajiriwa kwa sababu wameonyesha uzalendo wa moja kwa moja kuanza kazi mwaka wa kwanza, miaka miwili, lakini kazi inapotangazwa, wanaachwa. Nadhani siyo jambo sahihi, maadam tu wana zile sifa ambazo zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao watu wanaoitwa uthibiti ubora. Kuna malalamiko makubwa sana kwenye uthibiti ubora hasa wa elimu. Zamani hawa watu tulikuwa tunawaita Wakaguzi. Hawa watu wanaoenda kukagua shule, maana yake wanakagua shule; na ile kazi ni kubwa. Ukijaribu kuangalia kwenye *level* ya wilaya, yuko Mthibiti Ubora Mkuu wa Wilaya na wapo Maafisa Elimu. Hawa watu bado wanalalamikia masuala ya nyongeza, zile fedha za nafasi; wanaita fedha za nafasi, kitu cha namna hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Serikali ingejaribu kuangalia uwezekano wa hawa watu, yale malalamiko ambayo wanasema kwamba wanaonekana kama ni *second class,* yaondoke ili waweze kuwa sawa na wenzao na waweze kufanya kazi zile kiufanisi. Kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa, kuna uhaba mkubwa wa magari, kuna uhaba mkubwa wa vifaa na umbali wa maeneo wanayokwenda. Kwa hiyo, wanajikuta kwamba wanafanya kazi kubwa na ambayo kwa kweli wanahitaji kupewa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ahsante kwa nafasi na ninaunga mkono hoja zote zilizotolewa hapa na Wenyeviti wote wa Kamati, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba na Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kusimama katika Bunge lako hili na kupata fursa ya kuchangia taarifa mbalimbali kutoka kwenye Kamati ambazo zimewasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuingia Bungeni, Kamati yangu ya kwanza ilikuwa Kamati ya UKIMWI, lakini baadaye nilienda kuwa Mjumbe katika Huduma za Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, mimi ni kama Mjumbe Mstaafu kwenye hizo Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza sana sana kwa kazi nzuri ambazo zinafanyika. Nimeanza kusema kwamba nilikuwa Mjumbe kwenye hizi Kamati, niliona kule mwanzo jinsi tulivyokuwa tunapata shida kwenye baadhi ya mambo, lakini naona baada ya kupitia taarifa hizi, kwa kweli kwa sasa yako maeneo ambayo tunafanya vizuri sana, sina budi kupongeza kwa Wenyeviti wa Kamati, Wajumbe wa Kamati na hata Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la ujenzi wa Vituo vya Afya. Binafsi naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya. Wako Wajumbe wamesema tuna tabia ya kupongeza sana halafu baadaye tunalaumu sana. Kama binadamu, kunapokuwa na jambo zuri ni lazima usime, lakini hakuna mazuri yasiyekuwa na changamoto. Tunaeleza changamoto kwa ajili ya kuishauri Serikali ili iendelee kufanya vizuri vile ambavyo imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kama mwanamke, lakini siyo tu mwanamke, ni mwanamke ambaye nimeshawahi kuingia leba, nimeona matatizo ambayo tumekumbana nayo huko nyuma kupita maeneo ya uzazi na leo jinsi mambo yanavyokwenda vizuri. Kwa kweli naomba nipongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Serikali imeweza kujenga Vituo vya Afya 350. Katika Vituo vya Afya hivyo, katika Mkoa wangu wa Ruvuma tumepata Vituo vya Afya saba. Vituo hivyo saba ni pamoja na vilivyopo katika Wilaya ya Tunduru, Kituo cha Afya Matemanga, Mkasale na Mchoteka. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Kituo cha Afya Matemanga ambacho kwa sasa tayari kimeanza kutoa huduma ya upasuaji, nafikiri ndiyo lengo la Serikali kukaribisha huduma ili akina mama wanapopata dharura ya upasuaji, waweze kupata hiyo huduma kwa haraka sana. Naomba sana niipongeze Serikali kwa hiki ninachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza viongozi ambao wameshiriki kwa namna moja au nyingine, akiwepo Diwani wa Kata ile ya Matemanga; amejitahidi sana kufuatilia kwa Serikali, amepiga kelele na hatimaye tumefanikwa, tuna uwezo sasa katika kituo kile kufanya upasuaji wa akina mama wajawazito. Vile vile wanapasuliwa akina baba wenye matatizo ya ngiri na huduma nyingine. Kwa kweli nawapongeza sana na ninawatakia kila heri kwa namna moja au nyingine wale ambao wamehusika katika kufanikisha zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumze suala la mikopo ya asilimia 10. Ni kweli kupitia Halmashauri zetu na kupitia mapato ya ndani, zipo Halmashauri ambao zinafanya vizuri lakini zipo ambazo mpaka sasa bado zinatekeleza jambo hili kwa kusuasua. Naomba nitumie nafasi hii kupongeza Halmashauri ambazo zinafanya vizuri kupitia hii asilimia 10 kwa lengo la kukopesha akina mama, vijana na walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiwasaidia akina mama wajasiriamali wadogo wadogo kuweza kuinua mitaji yao. Kwa kweli jambo hili ni jema. Naiomba Serikali, kwa zile Halmashauri ambazo hazitekelezi vile ambavyo inakusudiwa, ni lazima kuchukua hatua kuona kwamba kila Halmashauri inatekeleza ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la walemavu. Katika kutekeleza hili jambo kuna miongozo ambayo inatolewa na Wizara, wanapeleka kwenye Halmshauri kwa ajili ya kuziagiza Halmashauri zitoe pesa kwa kufuata miongozo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwenye suala la walemavu. Naomba niishauri Serikali kwenye suala la walemavu ambalo lina shida kidogo. Katika kupitia ile miongozo, inawataka pia walemavu nao wapate ile mikopo kupitia vikundi vya watu watano watano. Ninaamini kabisa kwamba tunapozungumza vikundi, viwe ni vya watu walioshibana ili waweze kuchukua mkopo na kulipa, lakini yapo maeneo mengine walemavu wanashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kupitia maelekezo yanayotolewa, lingetolewa kabisa eneo maalum la kumtaka hata mlemavu mmoja mmoja aweze kupata mikopo. Kwa sababu maeneo mengine wanashindwa. Unaweza kwenda kwenye kijiji pengine wanatakiwa watano watano, lakini wakakosekana idadi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana kupitia Serikali yangu na sina shaka ni Serikali sikivu; kwa kuwa tuna lengo la kuwasidia walemavu, basi kuna vitu ambavyo tunatakiwa

tuviangalie upya ili tulegeze masharti tuweze kuwasaidia, tuhakikishe na wale walemavu wananufaika na hii huduma na mikopo ili iweze kuwaendeleza katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambao naomba nilizungumze ni suala la ikama ya watumishi. Tunafahamu kwamba tuna tatizo la ikama ya watumishi katika idara mbalimbali, lakini naomba nizungumze kwenye suala la Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya Kata. Kwenye Halmashauri zangu nane zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma, naomba nitolee mfano kwenye Halmashauri moja ambao wana uhitaji wa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii 39, lakini mpaka sasa wapo 13. Hata wale 13, wengine wamepelekwa kwenye Idara nyingine kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii wana kazi kubwa sana. Kazi mojawapo ni kuhakikisha miradi ile ya maendeleo inayokwenda kwenye maeneo wanatoa ushauri mbalimbali. Hata hii mikopo tunayozungumza, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya Kata ndio wanaotakiwa waifanye hii kazi ya kuleta uhamasishaji kwa vikundi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii mikopo inanapotolewa wakati mwingine, vikundi vingine vinashindwa, vinasuasua katika kufanya marejesho; na dhamira ya Serikali itoe mikopo na hatimaye watu weweze kurejesha mikopo. Kwa hiyo, wenye kuweza kuleta hamasa ni wale Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Utumishi alitembelea katika Halmashauri yetu, aliona mazingira yaliyopo kuhusiana na suala la watumishi. Naomba sana nisisitize kwenye eneo hili kwamba watumishi waliopo ni wachache. Unaweza ukaona na pia Wizara husika inaweza ikaona. Kama wanatakiwa 39 halafu unakuta kuna 13, lakini bado hata 13 wenyewe wameenda katika Idara nyingine katika kusaidia kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niipongeze sana Serikali yangu na Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika. Tunawatakia kila heri, wafanye kazi vizuri ili CCM iendelee kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba Profesa, atafuatiwa na Mheshimiwa William Tate Ole Nasha na Mheshimiwa Ummy Mwalimu ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami niungane na Wabunge wenzangu kuzipongeza Kamati zote zilizohusika; Kamati ya Afya, Kamati ya Elimu, Kamati ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo kwenye suala dogo tu la elimu. Asilimia 90 ya Watanzania wanaopeleka watoto wao shule, shida yao kubwa ni mtoto kumaliza shule na kupata ajira. Naona kwenye majumuisho yote, sioni mahali panapoongelewa suala ajira. Suala hili la ajira ni lazima tuendelee kulijadili kwa mapana makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwona Mheshimiwa Waziri anaendelea kufunga vyuo vingi ambavyo havikidhi mahitaji ya kielemu. Ushauri wangu, badala ya kuvifunga vyuo, Mheshimiwa Waziri alete Muswada humu Bungeni ili mtu akitaka kufungua chuo au kusajili wanafunzi ahakikishe asilimia 80 ya wanafunzi wamepata ajira ndiyo a-*qualify* kupata leseni ya chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *qualification* ya chuo isije ikawa majengo kwa hali ilivyo sasa hivi. Mtu kama aweza kutoa ajira asilimia 80, yeye mwenye chuo ndio akatafute ajira ili hata kama mtu ana chuo chini ya mti, watu wetu wanapata ajira, apewe leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sasa hivi ni kweli kuna utapeli mkubwa sana kwenye vyuo. Watu wetu wanalima, wanapika gongo, wanachimba madini kwenye matope, wanampatia mtu wa chuo kweli anawapa karatasi. Kama sheria itakuja hapa kwamba ili wewe uanzishe chuo u-*confirm* kwetu kwamba wanafunzi unaowachukua lazima wape kazi. Wasipopata kazi, ushitakiwe kwa kesi ya utapeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Mheshimiwa Waziri ataleta huo Muswada Bungeni, unaweza ukatupunguzia mgogoro na watakuja watu wengi sana kufungua vyuo ili kusudi *qualification* ya chuo isije ikawa majengo. Hata kama mtu atasoma kwenye jengo zuri, kama hakupata kazi inamsaidia nini? Waheshimiwa akina Nelson Mandela na akina Mugabe wamesoma magerezani, lakini wamekuja kuwa viongozi leo na wote tunawatukuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hana sababu yoyote ya kugombana na wenye vyuo; alete Muswada Bungeni, tupitishe Muswada, mtu yeyote anayetaka kuanzisha chuo; Waganga wa Kienyeji wanafundishwa Uganga, watu wanaendelea vizuri na Waganga tunawaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaye humu Mheshimiwa Karamagi, Waziri wa Nishati, ni Mganga wa Mifupa. Alisoma chuo gani? Ni Mganga wa Mifupa! Kwa hiyo, nakuomba … *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI**: Mheshimiwa Kalemani.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Karamagi. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Naamini ulimaanisha Mheshimiwa Kalemani, siyo?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kalemani, yah, yah, ni Mheshimiwa Kalemani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kalemani ni Mganga wa Mifupa na anatibu na anaponyesha, lakini hakusoma kwenye chuo chenye majengo, alisomeshwa kwenye Chuo cha Waganga wa Kienyeji na ni Mganga. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana wenzetu hawa wa mitaala ya shule; watu wanaikwepa *VETA* sasa hivi, naona Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani wanazungumzia suala la *VETA,* wananchi hawaitaki *VETA* kwa sababu *VETA* unaenda kujifunza kupaka rangi miaka mitatu, inawezakana kweli kupaka rangi miaka mitatu? Haiwezekani! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kujifunza kupaka rangi miaka mitatu. Mtu kama ameelewa kupaka rangi na soko halihitaji cheti, kwa nini siku nne asiondoke akaendelee na shughuli za zake? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri afungue uwazi, watu wote watakubali. Kwa mfano, kutengeza simu; mtu aruhusiwe kutengeneza simu, akishafahamu siku

nne, mruhusu aende akaendelee na shughuli zake. Maana soko haliulizi cheti. Hakuna mtu anaenda kutengenezewa simu kwa kuulizwa umesoma wapi na cheti kiko wapi? Unapeleka simu yako wanakutengenezea. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu atusaidie sana ili kupunguza huu mgogoro. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la hospitali, tunaishukuru sana Serikali kwa hospitali, zahanati kila kitu kipo. Tatizo kubwa lililopo ni kwenye matibabu hasa *X-Ray* na vitu vingine. Ukienda benki kuuliza *statement* au kuuliza *balance* ya pesa, hawakuchaji gharama ya kompyuta, kwa sababu ile kompyuta ndiyo *investment* ya benki. Sasa inawezekanaje nikienda hospitali unanichaji gharama ya *X-Ray?* Kwa hiyo, *X-Ray* ni *investment* ya hospitali, maana inamsaidia Daktari kujua ugonjwa wangu, haiwezi kuwa *package* ya kunichaji mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea, wewe ukifika unaumwa mle ndani, hawa wana *X-Ray* karibu nane; kuna *Ultrasound* na nyingine. Unapelekwa zote sehemu kumi, halafu unaletewa *bill* unaambiwa ni shilingi 300,000/= halafu unaambiwa nenda kanywe maji mengi. Inawezekana kweli! Haiwezekani na hakuna mtu anaweza akambishia Daktari. Nani humu anaweza akambishia daktari? Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Afya na Kamati yako, tunaomba mtengeneze mamlaka kama *EWURA* ambayo itadhibiti bei za dawa na bei za vipimo. Haiwezekani sisi tunadhibiti mbolea, tunadhibiti mafuta lakini hatuna mamlaka inayodhibiti bei ya vipimo na bei ya dawa. Haiwezekani! Maana yake sasa hivi ni tatizo kubwa kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli jamaa zetu hapa walikuwa wanalalamika kuhusu suala la maiti; kuna matatizo makubwa sana. Mtu amefariki, acha ile *issue* ya *bill,* kwa sisi kama Waislamu, ukifika pale wanakwambia tumeshaihudumia maiti, tunakudai shilingi 300,000/=. Sasa unashangaa, sisi tunataka kuzika leo, wanakupa *bill* kwamba wameshaihudumia maiti. Sasa wewe hujui umehudumiwa nini? Kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Afya, tunaomba sana sana, hasa sisi Wabunge ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Afya ajaribu sana kufikiria suala hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa ni usajili wa Zahanati. *Medical Assistant* akitaka kusajili leo Zahanati, shida anayopata matokeo yake wanazifunga. Daktari aliyestaafu akitaka kusajili hospitali, anashindwa; lakini Mganga wa Kienyeji anasajili ndani ya dakika kumi na anaruhusiwa kulaza wagonjwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inaingiaje akilini? Wote humu mnafahamu, mmesoma na Madaktari wamo, kweli Mganga wa Kienyeji anasajili dakika kumi, *Medical Assistant* au daktari bingwa mstaafu hawezi! Anapata shida ngumu sana na wote wanazifunga. Leo watu wa mionzi wanazunguka wanaendelea kufunga Zahanati, lakini Waganga wa Kienyeji wanaendelea kulaza wagonjwa. Itawezekanaje? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli ni kitu ambacho kweli kinaingia akilini! Tunaomba sana Kamati ya Mheshimiwa Serukamba, afikirie kabisa shida ya wananchi wanayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaelewa kwa nini alitunukiwa Uprofesa na Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo mmesikia hapo mawazo jamani, mawazo mazuri kabisa hayo!

Vyuo visifunguliwe tu vitoe vyeti. Huyu ni mwajiri mkubwa, hajasema yeye anaajiri watu wangapi; na kasema haulizi vyeti. Kwa hiyo, anaweza akaanzisha chuo naye. *(Makofi)*

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, wanaitwa kwenye kikao sasa, Mheshimiwa Spika yuko tayari.

Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja za Kamati zote mbili. Naomba nianze kwanza kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote mbili pamoja na Wajumbe wao kwa kuwasilisha ripoti nzuri. Niseme mapema kabisa kwamba tunapokea ushauri wote ambao wameutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niruhusu niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia Hoja za Kamati zote mbili na kutoa ushauri, nao pia napenda niwafahamishe kwamba Wizara yangu itachukua ushauri wote na kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu masuala machache ambayo yameibuliwa katika mjadala. La kwanza kabisa, Kamati ya UKIMWI imetushauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Technolojia kujenga mabweni mengi zaidi kama moja ya njia za kuwasaidia watoto wa kike wasiweze kupata maambukizi ya UKIMWI. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kati ya mwaka 2016 hadi mwaka huu, Serikali imejenga mabweni 333 na tunaendelea kujenga mengine ikiwa ni sehemu ya kuwasaidia watoto wa kike waweze kusoma bila kuwepo na changamoto zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imetushauri na imezungumza kwa mapana na marefu pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kushuka kwa Bajeti ya Sekta ya Elimu. Takwimu ambazo zipo zikitafsiriwa vibaya zinaweza zikaonesha kwamba bajeti ya elimu imeshuka katika miaka ya hivi karibuni, lakini bajeti ikisomwa katika muktadha sahihi ukweli wa mambo ni kwamba bajeti imeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Wizara ya Sekta ya Elimu kwa sasa ni bajeti ambayo ni halisia na imejikita katika mahitaji halisi ya Watanzania katika Sekta ya Elimu. Baadhi ya bajeti za huko nyuma zilikuwa zimejaa makokoro mengi, huko ndiko kulikuwa na fedha za kusafiri kiholela kwenda nje, fedha za mikutano na warsha ambazo hazina tija, fedha za chai ambazo hazisaidii chochote na fedha ambazo zimewekwa ajili ya upigaji. Kwa hiyo, kilichofanyika ni kwamba bajeti ile imetengenezwa katika uhalisia na hivyo kuweza kukidhi mahitaji halisi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika kuangalia tu bajeti yenyewe, bajeti ya Sekta ya Elimu haiwezi ikawa imeshuka kwa sababu kuanzia mwaka 2016 Serikali inatekeleza Mpango wa Elimu bila Malipo. Mpango ambao Serikali inatumia shilingi bilioni 23.85 kwa mwezi. Kwa hiyo, katika miaka minne tu pekee Serikali imetumia zaidi ya shilingi trilioni moja kwenye *item* moja ya elimu bila malipo. Katika hali ya kawaida haiwezekani bajeti ambayo ina ingizo jipya la shilingi trilioni moja ikaonekana kwamba imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata tukiangalia baadhi ya matumizi mengine ya kawaida; mwaka 2015/2016, bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilikuwa ni shilingi za Kitanzania bilioni 327. Leo hii tunavyozungumza, ni shilingi bilioni 450. Kwa hiyo, kuna ongezeko la karibia shilingi bilioni 100. Kwa hiyo, ukiangalia tu *items* hizo mbili, kwa vyovyote vile siyo uhalisia

tukizungumza kwamba bajeti imeshuka. Kilichofanyika ni kwamba tumefanya *realistic budgeting* na kujaribu kubana matumizi na kuondoa matumizi ambayo hayana msingi, huku tukiongeza fedha kwa ajili ya maeneo ambayo ni ya kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kiuhalisia bajeti ya Sekta ya Elimu imeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamependekeza kwamba wigo wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu upanuliwe ili wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya kati au vyuo vya *NACTE* nao waweze kunufaika. Wizara yangu inabeba mapendekezo haya, lakini nataka nitoe taarifa tu, ifahamike kwamba pamoja na kwamba kwa sasa inaweza ikaonekana kwamba wanafunzi wa vyuo vya kati hasa vyuo vya ufundi wanalipa gharama au wanalipa *tuition* kuweza kuingia kwenye vyuo hivyo, hali halisi ni kwamba kwa kweli wanalipa *token* na bado gharama nyingine zote zinabebwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwanafunzi anayesoma kwenye Chuo cha Ufundi kwa mfano *Arusha Technical College*, analipa ada ya kama shilingi 140,000/=, lakini akienda kwenye mazoezi ya viwandani, Serikali inampa shilingi 500,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona. Bado malazi yake, chakula na gharama nyingine zinabebwa na Serikali. Kwa hiyo, hata kama hawapati mikopo, lakini siyo kwamba Serikali haiwasaidii kusoma. Kwa hiyo, bado Serikali inabeba jukumu la kuhakikisha kwamba vijana hawa wa vyuo vya ufundi na vyuo vya kati nao wananufaika na msaada wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na pendekezo vilevile ambalo limetolewa la kuboresha vyuo vya ufundi kwa ujumla wake na kufanya maboresho ya sera na sheria. Pendekezo hili limepokelewa, lakini naomba tu nitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imechukua jitihada kadha wa kadha kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu ya ufundi. Kwa wale ambao wameenda kwa mfano kwenye, Chuo cha Ufundi Arusha hivi karibuni, ukifika pale Serikali imeweza kuweka vifaa vya kisasa kwenye karakana, vyenye thamani ya shilingi bilioni 15; na ni vifaa ambavyo havipatikana katika nchi nyingine yoyote ya Afrika isipokuwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hilo, Serikali sasa imeanza ujenzi wa chuo kipya cha ufundi cha Dodoma, ambacho kitakuwa na hadhi sawa na *DIT* na *Arusha Technical College*. Wote ni mashahidi kwamba Serikali kwa sasa inajenga vyuo 46 vipya vya wilaya na vya mikoa vya VETA. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge nyie wenyewe ni wanufaika. Serikali imetenga shilingi bilioni 100 na ujenzi uko katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wote ni mashahidi, Serikali imefanyia ukarabati mkubwa vyuo 54 vya wananchi vya *FDCs* ili viweze kuwa katika hali bora zaidi. Kama vile haitoshi, Serikali imejipanga kununua vifaa vya vyuo hivi vya ufundi vyenye thamani ya shilingi bilioni 26 kimsingi ili elimu yetu ya ufundi iwe ya kisasa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imependekeza iundwe Tume ya Elimu ili kuweza kupendekeza namna ya kuboresha elimu. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa sasa Wizara imeanzisha mkakati wa kuhuisha Sera ya Elimu. Kwa hiyo, tunategemea kwamba Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wengine watahusishwa katika zoezi hilo. Kwa hiyo, naomba mshiriki kikamilifu ili muweze kutoa mawazo ya namna gani ya kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini siyo kwa umuhimu, kulikuwa na hoja kwamba shule za binafsi haziwezi kupata vitabu kutoka taasisi ya elimu. Naomba nilitaarifu

Bunge lako Tukufu kwamba shule binafsi zinaweza zikapata vitabu kwa kununua kwenye maduka maalum ambayo yako kila mkoa. Kwa hiyo, naomba niwafahamishe kwamba inawezekana kabisa kupata vitabu vile na vyenyewe vya kwao havijaandikwa kwamba haviuzwi. Vile ambavyo vimeandikwa "haviuzwi" ni vile ambavyo vinatolewa kwenye Shule za Umma; lakini kila mkoa kuna duka mahususi ambalo Taasisi ya Elimu Tanzania imetenga kwa ajili ya kuuza vitabu kwa shule binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ummy Mwalimu, atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe na Mheshimiwa Jenista Mhagama, ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kuzipongeza Kamati zetu mbili; Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Kamati ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya inayoongozwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba tumepokea maoni na ushauri wa kamati na pia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika michango yao, lengo letu likiwa ni kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na afya bora ili kuwawezesha kushiriki katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda lakini pia katika kuboresha maisha yao. Kwa kweli tunazipongeza Kamati, wametoa maoni na ushauri mkubwa na kamati hizi zimekuwa msaada mkubwa kwetu sisi Wizara katika kuboresha huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni makubwa ambayo yametolewa na Kamati, suala la kwanza ni kwamba tuhakikishe tunaongeza watumishi katika sekta zote mbili; Sekta ya Afya na Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Ni kweli tunakubaliana na maoni na ushauri wa Kamati, lakini niseme kwa nini tunao upungufu mkubwa wa Watumishi wa Afya? Ni kwa sababu ya uwekezaji mkubwa ambao tumeufanya wa ujenzi wa Vituo vya Afya, ujenzi wa Hospitali za Wilaya, ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa sita pamoja na Hospitali Maalum. Kwa hiyo, kadri tunavyopanua miundombinu ya kutoa huduma za afya ndivyo mahitaji ya rasilimali watu yanavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, Wizara yangu pamoja na ya kaka yangu Mheshimiwa Kapt. Mstaafu George Mkuchika, tumekaa tukabainisha mahitaji halisi ya ongezeko la Watumishi wa Afya, tumeandaa mpango wa miaka mitano na tunajua ni kiasi gani tunahitaji ili tuweze sasa kuhakikisha vituo vyetu vyote vya kutoa huduma za afya vinakuwa na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejipanga, ikifika mwaka 2022 tupunguze uhaba wa Watumishi wa Afya kutoka asilimia 52 iliyopo hadi asilimia 30. Nami naamini hili jambo linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile umetoka ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwamba tutumie watumishi wa kujitolea *(volunteers);* tumeanza katika Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa tumeanza katika Hospitali zetu za Kitaifa. Nikitoa mfano, hospitali ya Dodoma, kila mwezi inatumia shilingi milioni 35 kwa ajili ya watumishi wanaojitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, changamoto ipo katika Vituo vya Afya na Zahanati, kwa sababu wao hawana makusanyo ya kutosha. Hawa watu watajitolea, wanahitaji posho ya kujikimu, wanahitaji usafiri. Hawawezi wakajitolea watoto wetu bila kuwapa motisha *(incentive)* ili waweze kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwathibitishie Kamati na Waheshimiwa Wabunge, kadri tutakavyopata Watumishi wa Afya, tutaweka kipaumbele kwenye huduma za afya ya msingi, kwenye Zahanati, kwenye Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya. Amesema vizuri kaka yangu Mheshimiwa Ndassa *(Senator)*, kadri tutakavyoboresha huku chini, ndivyo tutakapopunguza mzigo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni la ugharamiaji wa huduma za afya *(health care financing)* na hili limegawanyika katika maeneo makubwa mawili. Kamati inatushauri tuongeze bajeti ya fedha za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tuseme, suala la afya ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Serikali ya Awamu ya Tano inajali na kuthamini afya za Watanzania. Kwa sababu ya msingi bila wananchi kuwa na afya bora, hatutaweza kufikia Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata ukiangalia, nadhani kuna sintofahamu; tutofautishe bajeti ya Wizara ya Afya na Bajeti ya Sekta ya Afya. Bajeti ya Sekta ya Afya inapitia pia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inapitia katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambapo kuna Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali ambao ni Watanzania hawa hawa wanapata pia huduma za afya. Kutokana na jambo hili, Serikali ya Awamu ya Tano tukiiangalia, tumeongeza bajeti ya Sekta ya Afya kutoka shilingi trilioni 1.2 mwaka 2013/2014 hadi shilingi trilioni 1.8 mwaka 2019/2020. Sisemi kwamba fedha hizi zinatosha, lakini unaiona dhamira yetu ya dhati ya kutaka kuboresha huduma za afya. Matokeo chanya yameanza kuonekana, hatujisifii tu kwamba tumejenga majengo nilikuwa Kome kwa rafiki yangu Mheshimiwa Tizeba, mama mjamzito sasa hivi anajifungulia Kome bila ya kuvuka kivuko kwenda Sengerema kujifungua, rafiki yangu Mheshimiwa Allan Kiula Mkalama kituo cha afya mama mjamzito anapata huduma za uzazi za dharura pale pale, kwetu sisi Awamu ya tano haya ni mafanikio makubwa sana ya kuokoa maisha ya mama mjamzito lakini ya kuokoa maisha ya watoto wa changa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni Mtulia amesema miaka minne iliyopita tulikuwa tunapeleka wagonjwa zaidi ya 600 kwa mwaka nje ya nchi, kwetu sisi siyo suala la kupunguza gharama sasa hivi tumetoka 600 mpaka 53 maana yake nini? Wananchi wengi zaidi wanapata huduma za upasuaji wa moyo ndani ya nchi, ukipeleka India utapeleka 600 ukifanya ndani ya nchi unafanya zaidi ya watu 3,000; kwa hiyo siyo suala la gharama lakini ni suala la kuhakikisha hata Mtanzania masikini anapata huduma bora za matibabu ya kibingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye hili niahidi kwamba Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya kadri uchumi wetu utakavyoruhusu kwa sababu tunavyo vipaumbele vingi, tunavipaumbele vya maji, tunavipaumbele vya umeme, vya kilimo, lakini tutajitahidi kuongeza kuongeza bajeti kadri hali ya kiuchumi itakavyo ruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la ugharamiaji wa huduma za afya, liko suala la wananchi kumudu gharama namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti Peter Serukamba na kamati yake kwa mara ya kwanza wameona mzigo mkubwa ya misamaha ambayo hospitali zetu zinabeba. Kwa hiyo tunavyokaa tukalaumu huduma mbaya na sisi ndiyo maana Wizarani tumesema tuje sasa na takwimu, misamaha kwa kila hospitali ni shilingi ngapi? Na hii ndiyo inajibu hoja mwananchi maskini sera inataka mwananchi kuchangia huduma za afya isipokuwa makundi matatu, lakini kama mtu hana uwezo tumeweka utaratibu wa kuchangia na ndiyo maana nikisoma haraka haraka, Kagera katika kipindi cha mwaka jana wametoa misamaha

ya shilingi milioni 170, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa misamaha shilingi milioni 391, Mtwara Ligula misamaha shilingi 67 na Mbeya shilingi milioni 88.

Mheshimiwa Spika, nimesema Dodoma na Kamati imesema kwa hiyo ili suala la msamaha sisi ni jukumu letu kila Mtanzania apate huduma bila ya kikwazo cha fedha, lakini tumeangalia muarobaini wa kwenda nalo mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo kama ilivyoshauri Kamati ni kuhakikisha tunakuja na bima ya afya kwa kila mtu ili aweze kupata huduma, siyo kwamba tumekaidi ushauri wa Kamati na Bunge, bado tupo katika taratibu na majadiliano ndani ya Serikali lazima tufanye-*actuarial study* (tathimini ya uhakika) kama kila mwananchi awe na bima je wachangie shilingi ngapi, wapate huduma katika hospitali za binafsi na hospitali za umma. Kwa hiyo siyo jambo la hararaka tumeelekezwa ebu tufanye tathmini ya kina tusije tukaanzisha bima kesho baada ya wiki mbili wananchi wanakosa huduma kwa sababu mfuko umefilisika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la maendeleo ya jamii, tumepokea ushauri wa Kamati kuhusu kuboresha mitaala/kufanya *review* ya mitaala ya vyuo vyetu vya maendeleo ya jamii kwamba imepitwa na wakati tunalipokea na tutalifanyia kazi.

Lakini labda ;ingine la kusema amelisema vizuri Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Mbunge *the way forward* tusiwe pia ni taifa la kulilia tiba tiba, tiba sisi kama Wizara tumeona ipo haya sasa Serikali, jamii na wadau tukawekeza kwenye huduma za kinga, watu wanaumwa kwa sababu hawana vyoo, watu wanaumwa kwa sababu hawazingatii lishe bora, watu wanaumwa kwa sababu hawafanyi mazoezi, hawazingatii ulaji wa vyakula unaofaa wanavuta sigara, wanakunywa pombe kupita kiasi. Kwa hiyo,ili kupunguza mzigo wa fedha wa gharama za kutoa huduma za afya lazima wote kwa pamoja twende katika huduma za kinga badala tu ya kuwekeza katika huduma za kinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la Kamati ya UKIMWI ya Mheshimiwa Mukasa na mimi nimpongeze kwa kweli amekuwa ni msukumo mkubwa sana kwetu sisi Serikali kuhakikisha tunachukua hatua za kuhakikisha tunatokomeza virusi vya UKIMWI na UKIMWI ifikapo mwaka wa 2030 na inawezekana. Kwa hiyo, 90 ya kwanza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kw amuda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA , WAZEE NA WATOTO:** Ya pili au ya kwanza?

**NAIBI SPIKA:** Ni ya pili Mheshimiwa, lakini malizia dakika moja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Kwa hiyo, kwenye 90 ya kwanza nataka tu *clarify* sasa hivi asilimia 77 ya Watanzania wanoishi na virus vya UKIMWI tayari wanafahamu kwamba wanayo maambukizi ya UKIMWI na sasa hivi asilimia 98 ya wanaoishi na virusi vya UKIMWI tumewaingiza katika utaratibu wa dawa na asilimia 88 virusi tayari vimefubazwa. Kwa hiyo, tunaenda vizuri Waheshimiwa Wabunge sina shaka kwamba tutafika lengo la kutokomeza UKIMWI Tanzania ikifika mwaka 2030 sambamba na kutokomeza kifua kikuu.

Mheshimia Naibu Spika, baada ya kusema hayo nawapongeza Kamati na ninaunga mkono hoja na Wizara tutatelekeza maoni na ushauri wa Kamati pamoja na wajumbe ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa ajiandae kwa ajili ya kuja kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa nianze kwa kuunga mkono hoja na vilevile kuwapongeza sana viongozi wa Kamati yangu na Wajumbe kwa kazi kubwa wanayofanya ya kutushauri Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tumeanza vizuri mwaka huu na kama alivyosema Mheshimiwa Mtulia nyota wetu wa soka ambaye vilevile nahodha wa timu ya Taifa akatufungulia milango, akawafungulia milango vijana wetu Watanzania kuingia kwenye ligi ya heshima duniani, kubwa ya *EPL* ila tu niombe Watanzania najua mmehamasika sana tujiebushe na kauli zisizo na staha kwenye mitandao ya michezo inayotumiwa na wengi, badala ya kumsaidia Samatta hatumsaidi bali tunamjengea uwasama kijana wetu na wenzake huko ughaibuni nawaomba sana hasa katika kutumia mitandao na bahati mbaya sana wanaowatafsiria wenzetu huko Aston Villa siyo Watanzania, ni wenzetu ambao hawatutakii nia njema ni Kiswahili watapotosha tu, kwa hiyo, hebu tujihadhari sana na mihemuko iliyopitiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaeleza tu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tuna wachezaji 22 wanaocheza nje nchi ambao tukiwahitaji wakati wowote wapo tayari kuisaidia timu ya Taifa bila kumsahau kinda wetu Kelvin John ambaye sasa hivi yupo kwenye *football academy* ya Uingereza na timu nyingi kwa kweli zinamtolea macho sasa hivi.

Leo tumempokea hapa Bungeni Salim Mtango wa Tanga kwa kubeba mkanda wa *UBO* wa dunia na mwenzake vilevile Mchanje Yohana wa Tanga huko huko naye amebeba mkanda wa *UBO* nawapa pongezi sana tena sana. Sasa hivi Tanzania tuna jumla ya mikanda 12 ya Kimataifa. Kwa hiyo, tunafanya vizuri sana kwa ndondi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rashid Shangazi namshukuru Mbunge wa Mlalo amelalamikia usikivu hafifu wa *TBC* maeneo kadhaa ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii kuelezea tu kwamba mara baada ya Uhuru Baba wa Taifa alihakikisha nchi hii inajenga minara minane ya masafa ya kati dhidi ya *(medium wave)* na hiyo minara kwa kweli, ni kama iliweza kujitosheleza nchi nzima ilikuwepo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Kigoma, Dodoma vilevile Mbeya, Songea na Nachingwea, lakini teknolojia ya mawasiliano inakwenda kwa kasi sana, mitambo ya *medium wave* ilianza kupoteza/kuondoka kabisa katika teknolojia ikaingia mipya kabisa ambayo kwa kweli kusikia inafurahia lakini ina matatizo pia kwa upande hasa sehemu ambayo kuna vizuizi kama milima, tukaingia huu teknolojia ya *frequency modulation (fm)* na mitambo ile kwa sababu imekosa watengenezaji waliacha kabisa ikakosa kwakweli vipuli kwahiyo nchi ikaingia kwenye mtikisiko mkubwa sana wa jinsi gani tutatoka huko ndiyo tukaanza kutumia kuweka sehemu mbalimbali za nchi mitambo ya *fm.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kwa mfano katika muda mfupi uliopita Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia usikivu wa TBC ulikuwa asilimia 54 tu sasa tunaelekea kwenye asilimia sabini na kitu, tumekwenda Wilaya za mpakani Rombo, Longido, Tarime, Kibondo na Nyasa, lakini huwezi tu ukaweka ukaacha inabidi urudie tena kuangalia kwa sababu mawimbi haya yana tabia ya kuhama kutokana na *topography.*

Kwa hiyo, tumepita hivi karibuni tumeenda Tanga kuangalia mitambo yetu tukakuta kweli bado tuna matatizo baadhi ya sehemu kutokana na mitambo yetu kukosa nguvu, sasa iliyoko sehemu ya Mnyuzi sehemu kama Mkinga na Kilindi inabidi turudie na ninawahakikishia

Wabunge kutoka Mkoa wa Tanga kwamba eneo hilo tumeliona Mkinga na Kilindi kuna matatizo.

Vile vile tulikwenda Lushoto tumeona kuna mitambo pale lakini hata tukiikarabati na tutaikarabati ndani ya miezi mitatu ijayo bado Bumbuli na Mlalo wanatatizo ambalo wanahitaji kwa kweli kulifanyia kazi na tunawahakikishia ndani ya mwaka huu tutatatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kilimo cha Mabungo ambacho kipo Moshi vilevile mtambo wetu vimeshika sana nguvu yake inahitaji ukarabati, vipuri vyote vimeshafika, lakini hata tukisha karabati bado Rombo itaendelea kupata matatizo kutokana na milima milima sehemu ile, Rombo inahitaji kwa kweli tuifanyie kazi zaidi pamoja na kwamba Rombo hapo hapo tuna mitambo mipya inabidi tuongeze mitambo mingine ni kama ambavyo tutakavyofanya Longido ambako tuna mitambo tayari Namanga, tuna mipambo *Longido DC* lakini mitambo *Longido DC* lakini bado lazima tuongeze mitambo mingine kutokana na *topography* ta eneo hilo, tumeenda Manyara, tumeenda Singida hali iko hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu mwaka huu wa fedha tunaweka mitambo Unguja na Pemba kwa bajeti mliopitisha hapa, tunaweka mitambo Simiyu na vilevile tunaboresha usikivu Songwe na Ludewa kwa Mheshimiwa Ngalawa. Vilevile, kwa ushirikiano kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tutaweka mitambo Kilwa, tutaweka Itigi, Ruangwa, Kilombero na bila kusahau Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa kuona juhudi za Wizara katika kuboresha matangazo ya *TBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Huduma za Jamii imelalamikia ubovu wa miundombinu ya michezo; napenda kusisitiza kwamba ndugu zangu kwa kweli ni jukumu letu sote si jukumu la Serikali peke yake Wizara, Taasisi, Mashirika ya Umma, sekta binafsi na hata sisi Waheshimiwa Wabunge unaweza ukajenga hata kiwanja cha *volleyball* kwa kutumia pesa ya Mfuko wa Jimbo au kiwanja cha *netball*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni wajibu wetu wote tusisubiri tu Serikali peke yake na wito huu tumeshautoa na umepokewa kweli na mikoa mingi, tunashukuru sana Mkoa wa Arusha ambao umetoa agizo, umeazimia kwamba kila Halmashauri itajenga viwanja vya michezo na wao Jiji la Arusha wameamua wameanza nimeenda kuangalia kiwanja cha Ngarenaro, ni kiwanja changamani kuna *netball,* kuna *basketball*, kuna mchezo wa soka pale kiwanja kizuri kimemalizika kwa asilimia 80 wanajenga kwa jumla ya shilingi milioni 360. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeenda sehemu inaitwa Sinoni, kuna Mtanzania pale anaishi Marekani amekumbuka nyumbani, amejenga kiwanja kizuri sana kina taa mpaka za usiku kwa ajili ya watoto kwa shilingi milioni 126; hawa vijana wa kutolewa mfano kuliko vijana wenzetu wengi wanaokaa nje muda mwingi wako kwenye mitandao ya kijamii. Unafuatiwa Mkoa wa Dar es Salaam, nilishasema naipongeza *Simba Sports Club* wanajenga viwanja viwili, kimoja cha nyasi na kingine kiwanja cha nyasi bandia huko Bunju. Vilevile Manispaa ya Kinondoni inajenga uwanja wa kisasa Mwenge kwa shilingi bilioni 2.7 na ukamilika mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijawatendea haki Manispaa ya Songea Mjini kwa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, wametenga eneo la ekari 50 katikati ya Kata ya Lirambo na Peramiho kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha gofu. Sasa hapa tutaona ndugu zetu wa Songea hiyo gofu watakapoanza kujifunza, lakini kwa kweli nina uhakika kutokana na uzuri wa eneo lenyewe na hakika nchi nyingi zitakimbia kuja kufanya mchezo kule wa gofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii vilevile kuwatahadharisha wana Tanga wanaonisikiliza saa hizi wanaovamia eneo la *TFF* la Mianjani ambako kutajengwa *training center* yenye viwanja na vilevile hosteli. Naomba niwasisitizie kwamba hawatalipwa fidia, kuna mtu anawadanganya danganya sehemu za ardhi/ofisi zetu hizi kwamba hebu jengeni mtalipwa fidia, fidia haitalipwa, nataka niwahakikishie hilo na ujenzi utaanza muda si mrefu kutoka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kubenea amelalamikia anauita ushabiki wa *TBC,* nilitaka nisisitize tu kwamba Mheshimiwa Kubenea kupitia kwako kwamba *TBC* ni chombo la Serikali, hilo haliwezi kubadilika na *TBC* inachokifanya siyo tofauti na vyombo vingine vya Serikali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* iko pale kuelezea kwa kinagaubaga utekelekezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo za Serikali ambavyo hivi vitu haviwezi kupata nafasi kwenye vyombo vya habari binafsi ambavyo vinaangalia zaidi faidi *at the end of the day. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine wengine hawana habari, *BBC* mnayoiona kila siku msije mkafikiri iko pale kwa msaada hapana. *BBC* leo iko pale kwa umri wa miaka 98 haijawahi kuzimwa hata siku moja, iko pale kwa maslahi ya Serikali ya Uingereza, sio inatusaidia na sisi tupate taarifa iko pale kwa maslahi. *VOA* huu mwaka wa 78 haijawahi kuzimika inatangazwa kwa lugha 47, *BBC* lugha 40, wafanyakazi zaidi ya 3500 kila chombo kwa ajili ya nini. Kama ingekuwa kuwatangazia Waingereza wenyewe si ingekuwa kiingereza peke yake hivi ni vitu vya kimkakati kila nchi inafanya, msiishambulie *TBC* bila sababu, kuna Serikali inafannya vitu, lazima vitangazwe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijui nimesikia kengele? Ooooh!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nimuite Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Masuala ya UKIMWI aje ahitimishe hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Kwanza kabisa napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa michango yenu mizuri ambayo imelenga kuboresha katika vita hii ya kupambana na masuala ya UKIMWI, dawa ya kulevya lakini pia na kifua kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza sana Mawaziri kwa kufafanua. Suala la UKIMWI ni suala mtambuka kwa hiyo, liko katika sekta zote, kwa hiyo basi Wizara kama ya Michezo ikiboresha mambo yake Wizara ya Elimu ikiboresha mambo yake, hata changamoto zile ambazo zinasababisha watu kupata UKIMWI zinapungua. Kwa hiyo, tunawashukuru Mawaziri kwa juhudi zenu katika kuboresha mambo ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Waziri, Ummy Mwalimu kwa kutufafanulia kutupatia *data* ya hivi karibuni ya kuhusu suala la 90, 90 ambalo watu wengi wamezungumzia. Kwa hiyo, tunashukuru, lakini tunaomba juhudi hizi ziendelee

kufanyika ili kwa sababu mwaka huu 2020 ndio mwaka ambao tunatakiwa tufikie 90, 90 zote tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wabunge ambao wamechangia hoja walikuwa sita, kwa sababu ni wachache naomba kuwataja majina; Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Mboni Mhita, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, lakini na Waheshimiwa wengine wakati wanaanza pia waliipongeza Kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Wabunge ambao wameonesha hoja zao mingi kabisa ilikuwa imejikita kwenye maeneo yafuatayo; suala la 90-90-90 limezungumzwa, suala la kuhakikisha kwamba Serikali inatafuta vyanzo vya uhakika ambayo Kamati pia imezungumza, imejitokeza. Pia imejitokeza wamechangia kwamba watu waweze kupima ili waweze kutumia dawa ili tuweze kufikia 90-90; lakini pia jambo lingine lilizongumzwa na wachangiaji ni kuharakisha utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya miaka 15 ambayo inamruhusu sasa kupima bila ridhaa ya mzazi ili hasa tuweze kufikia 90 ya kwanza ile ambayo ni muhimu sana kwa 90 pili na ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mchango mwingine ulijikita kwamba elimu zaidi sasa iendelee kutolewa ili watu waelewe zaidi masuala ya UKIMWI, *TB* na madawa ya kulevya. Pia kuna mchangiaji mwingine ambaye amesema basi Serikali iangalie namna ya kutoa msamaha wa kodi kwa *NGOs* zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI, *TB* na madawa ya kulevya ingawa wakati tumekutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitufafanulia kuhusu jambo hili. Zipo *NGOs* kwa kufuata utaratibu maalum wanaweza wakapata huo msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Waheshimiwa wengine Wajumbe wamepongeza Kamati kwa kazi nzuri. Kwa hiyo, hakukuwa na mambo mengi sana ambayo yamejitokeza, sana sana wachangiaji wengi wamepongeza Kamati kwa kazi nzuri na *issues* ambazo zimetokea wamezizungumza zote ziko kwenye Kamati. Niwashukuru kwamba na wenyewe wameona na wanapongeza juhudi ya Serikali katika kupambana na suala hili la UKIMWI, madawa ya kulevya pamoja na *TB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwa kuhitimisha kwamba magonjwa haya kwa kweli ni hatari hasa upande wa UKIMWI kwa sababu hata kama Serikali itaweka trilioni za fedha kama hatutabadili tabia zetu bado ugonjwa huu hatutaweza kufikia lengo la 2030. Kwa hiyo tubadili tabia tuweze kulindana ili kuweza kufanikisha kutatua changamoto hii ambayo inatukumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi, baada ya kusema haya nahitimisha hoja yangu na naomba kutoa hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibu wetu wa kikanuni sasa nitawahoji.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda, kwa hivyo mapendekezo na maazimio yaliyoko kwenye taarifa ya kamati hii yanakuwa ni Maazimio ya Bunge na upande wa Serikali uyachukue na uyafanyie kazi.

Nimuite Menyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba ahitimishe hoja yake.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wamejadili vizuri ripoti yetu, wamechangia Wabunge 22 na wajumbe watano wameandika kwa maandishi, kwa sababu ya muda nitaomba nisiweze kuwataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Wizara ya Afya; nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge wote jambo moja ambalo nadhani Serikali mtakubaliana na Waheshimiwa Wabunge moja, ni kuhusu watumishi wa afya. Umefika wakati, tumewekeza fedha nyingi sana kwenye vituo vya afya, kwenye zahanati, hospitali za mikoa, hospitali za wilaya na hospitali za kikanda. Uwekezaji huu ili uweze kuwa na maana ni muhimu sana kuwa na wafanyakazi, niwaombe Serikali mpo hapa tujitahidi sana tupate wafanyakazi kwenye Idara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo wengi wamelisema na sisi kwenye mapendekezo yetu tumeliweka ni jambo la bima ya afya. Mimi nawaomba sana Serikali kama kuna jambo, na Mheshimiwa Spika alisema tutakuwa tumeleta ukombozi kwa Watanzania ni kuleta Sheria ya Bima ya Afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili naomba sana watu wa Serikali tusipate kigugumizi kuleta sheria hii. Kamati yangu ilikwenda Rwanda, Rwanda kila Mnyarwanda ana bima ya afya, lakini kwa sababu wanajua kuna watu maskini wameweka *social stratification,* wamewagawa watu. Katika wote kuna asilimia karibu nne hawana uwezo kabisa, hao Serikali inawalipia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu ukilipiwa na Serikali hutakiwi hata kuwa na *bank account*, *so* lazima wajue kweli wewe ni maskini kweli kweli. Kwa hiyo, mimi naomba sana Serikali suala hili la bima kwa wote, na mimi nasema siyo suala la *NHIF,* ni suala la bima ya afya kwa wote. Ukiipata kwenye *private sector* sawa, ukiwa nayo kwenye Mfumo wa Serikali sawa, cha msingi kila Mtanzania awe na bima ya afya.

Mimi naomba sana Serikali mlete, na hii mtakuja jambo la misamaha, kuna Wabunge wamesema habari ya maiti kukataliwa, lakini jamani gharama za matibabu ni kubwa sana. Ni kweli wanasamehewa watu wengi, ni kweli Serikali haipeleki ruzuku, kwa hiyo kinachotokea sasa hizi hospitali hazitoweza kutoa huduma bora katika mazingira ambayo bajeti yake haifai. Kwa hiyo niwaombe wenzangu Serikalini jitahidini sana ili kupambana hili la misamaha lazima tulete bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya pia kuna suala la kinga na lishe, nadhani imefika wakati tuwekeze fedha nyingi kwenye kinga pamoja na lishe, tutaokoa magonjwa mengi sana. Ili tuweze kuwekeza kinga lazima turudi kwenye *drawing board,* tuajiri watu wa *social workers* waende huko vijijini, hawa ndiyo watasaidia katika haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo wamechangia watu wengi ni kwenye elimu, mimi nataka niseme kidogo kwenye elimu na nina mambo makubwa mawili/matatu; moja, leo dunia inaenda kwa kasi sana, yuko mwanazuoni mmoja anasema; "*we stand on the blink of*

*technological revolution will fundamentally alter the way we live, work and relate to one another*".

Kwa nini nimesema hivyo, leo tunakwenda kwenye *fourth industrial revolution,* tunakwenda kwenye dunia ya teknolojia, kwa hiyo, lazima Wizara ya Elimu turudi tuangalie elimu tunayotoa inaweza kwenda kupambana na mabadiliko haya makubwa ya kiteknolojia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri hapa anasema wanatafuta utaratibu kuowesha mitaala, kuangalia mambo ya, jamani! Bado mimi kama Mwenyekiti na Kamati yangu tunaomba Serikali muendelee kutafakari umuhimu mkubwa kuhakikisha tunapitia mfumo upya wa elimu. Tuje na mfumo ambao kuanzia *kindergarten* mpaka *university,* tuangalie je, elimu tunayofundisha, mitaala, uwekezaji, fedha vinajibu matakwa ya sasa? Kama hatuhangaiki na hilo tutapata taabu sana huko tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la kuboresha elimu, mimi ningeomba sana watu wa Wizara ya Elimu ili kuboresha elimu kunaendana, unaposema tunaboresha elimu lazima hiyo kazi ifanywe na shule za umma na shule za *private*. Lazima watu binafsi watusaidie kwenye kuboresha elimu yetu, lakini naomba sana Serikali mtafakari, umefika wakati suala la shule za binafsi, kwamba usimamizi wa shule zote liwe chini ya Wizara ya Elimu, tuondoe TAMISEMI. Kwa sababu TAMISEMI naye ana shule kwa hiyo TAMISEMI kuna *conflict of interest,* kwa hiyo, kuna maamuzi atafanya TAMISEMI kwa sababu anajua anapendelea shule zake. Kwa hiyo, ili kuondokana na hilo jambo mambo yote ya usimamizi wa elimu Tanzania yarudi Wizara ya Elimu, lakini watoa elimu watakuwepo wa binafsi, itakuwepo TAMISEMI kwa maana ya shule za umma. Mimi nadhani hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia nyingine ni kuhakikisha kuwa tuna *quality* na *access,* lakini hayo yote yatapatikana kama hatutafanya vurugu kwenye shule hizi za binafsi, lakini pia tuangalie uwezekano wa kutoa kodi kwenye shule za binafsi ili tuweze kuzisaidia.

Pia kuna suala la walimu wa sayansi ni jambo kubwa limesemwa na Wabunge wote, tuangalie pia mitaala ya vyuo vya ufundi na mMimi nasema jamani tumesema tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda unahitaji ….. *education so* lazima tuangalie upya; je, mitaala yetu ya ufundi inajibu huko tunakotaka kwenda? Kuna shule zinapoteza hawa walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la *TBC*. *TBC* ni muhimu sana, lazima tuendelee kuwekeza ili *TBC* ndiyo *pride* ya Tanzania, ndiyo *pride* ya Serikali.

Kwa hiyo, lazima tuwekeze kwenye chombo hiki cha kwetu cha Watanzania. Pia na vyombo vya binafsi lazima tuendelee kuvisaidia ili vitusaidie kutoa elimu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sana naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge nitawahoji.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendelo ya Jamii katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, kwa hiyo, waliosema ndiyo wameshinda.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa namna mlivyoshiriki mjadala wa hizi kamati mbili, lakini pia tuwashukuru wenzetu wajumbe wa hizi kamati mbili kwa kazi nzuri waliyoifanya. Nadhani ninyi nyote ni mashahidi kwamba wamefanya kazi nzuri, lakini pia wameweza kushauriana na Serikali kufikia hapo ambapo tunaweza sasa kupongeza.

Kwa hiyo ushauri wao kwa Serikali maana yake Serikali inaufanyia kazi na kwa yale waliyoyasema humu, waliotuletea kama mapendekezo na maazimio sasa yameshakuwa maazimioa ya Bunge.

Kwa hiyo, upande wa Serikali Ichukue mapendekezo ambayo kamati zimetoa kwenye hizi taarifa zake lakini pia yale ambayo waliyaleta kama Bunge liazimie kwa hoja hizi zote mbili kwa huko kuwahoji na Bunge kuafiki maana yake yamekuwa maamuzi ya Bunge upande wa Serikali uweze kuyafanyia kazi. Sisi tunawatakia kila la kheri na tunaamini hizi Kamati zitaendelea kutoa ushirikiano kwenu lakini na ninyi mtaendelea kutoa ushirikiano kwa hizi Kamati zinazofanya kazi kwa niaba yetu sisi sote. Kwa hiyo tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hayo maazimio.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge, Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo wanatangaziwa kwamba badala ya kukutana leo saa mbili usiku na Wizara ya Katiba na Sheria, sasa watakutana kesho saa mbili asubuhi. Badala ya saa mbili usiku wakutane saa mbili asubuhi, kwa hiyo saa mbili asubuhi ndiyo watakutana na Wizara badala ya usiku huu na wale ambao hawapo tuangalie namna ya kuwasilisha hizi taarifa ili wasije wakaja hiyo saa mbili halafu wakaja kuambiwa imeahirishwa baada ya kufika maeneo ya Bunge. Kwa hiyo, wale tupeane taarifa wasije wakaja hapa wakakuta hakuna wenzao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka saa tatu kamili asubuhi kesho.

*(Saa 1:33 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 7 Februari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*